**16 MEI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 16 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Halima Mdee.

Na. 332

### Uwekezaji unaofanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza: -

Je, tangu kuanzishwa kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni kiasi gani cha fedha kimewekezwa na nini faida na hasara za uwekezaji huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 kwa hesabu zilizokaguliwa na *CAG,* thamani ya uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ilikuwa imefikia jumla ya shilingi trilioni 14.4 ambapo Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* ulikuwa umewekeza jumla ya shilingi trilioni 6.03, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF)* ulikuwa umewekeza jumla ya shilingi trilioni 7.49 na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF) Workers Compensation Fund* ulikuwa umewekeza jumla ya shilingi bilioni 521.94.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya uwekezaji huu ni kulinda thamani ya michango ya wanachama na kuhakikisha Mifuko inakuwa endelevu ili kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kulipa mafao. Aidha, uwekezaji huu huchangia na kuongeza ajira, mapato ya Serikali kupitia kodi na kuchochea shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo katika uwekezaji wowote kuna vihatarishi *(risk)* ambavyo vinaweza kusababisha hasara kwa baadhi ya uwekezaji. Hasara zilizojitokeza kwa uwekezaji uliofanywa na Mifuko ni pamoja na kutolipwa kwa wakati kwa mikopo iliyotolewa kwa wanufaika mbalimbali na baadhi ya miradi kutofanya vizuri ikilinganishwa na matarajio yaliyokuwepo wakati wa kubuni miradi hiyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu lilikuwa linasema faida na hasara ya uwekezaji. Umeniambia kiasi cha uwekezaji kilichowekezwa lakini hujaniambia faida na hasara ya kifedha. Kwa sababu inasemekana kwamba uwekezaji unafanywa kwenye maeneo yasiyokuwa na tija. Kwa hiyo, naomba nijibiwe swali la faida na hasara ya kifedha. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, moja ya miradi mipya ni mradi wa Mkulazi kwa ajili ya uzalishaji wa Sukari. Pia, kwa mujibu wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambae wewe umemrejea anasema, Mipango duni ya utekelezaji wa mradi huu mpya ambao fedha za mifuko zinatumika, umesababisha gharama ya uwekezaji kuongezeka kwa bilioni 79, moja, hasara ya miaka ya miwili mfululizo ya bilioni 20.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, uliza swali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, unadhani mna matatizo gani linapokuja suala la uwekezaji kwa kutumia fedha za mifuko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuhusu swali lake la kwanza kuhusiana na faida na hasara lilikuwa linauliza tangu kuanzishwa kwa mifuko ni kiasi gani cha fedha kimewekezwa na lakini eneo la pili, lilikuwa linauliza katika kila mfuko nini faida na hasara za uwekezaji? Kwa hiyo, ilikuwa ni faida na hasara sio fedha. Hata hivyo, tumeeleza kwenye eneo la fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la fedha miradi ambayo imewekezwa nimeeleza kwenye swali la msingi kwamba ni zaidi ya shilingi trilioni 14. 4 ambayo imewekezwa katika mifuko miwili kwa maana ya *PSSSF* zaidi ya shilingi trilioni 7.4 lakini pia kwenye *NSSF* ni trilioni 6.3. Sasa kwa fedha ambazo ni hasara haiwezi kuwa *counted* ni hasara kwa sababu uwekezaji ule ni endelevu na umeendelea kuwa wanaendelea kulipa kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika *principle* za uchumi ni sawa na kupwa na kujaa kwa bahari. Wakati wa uwekezaji tunaofuata ni mwongozo unaotolewa na Benki kuu ya Tanzania ambayo inaeleza maeneo ya uwekezaji. Pili, inaeleza namna gani ambayo watakwenda kuwekeza pamoja na ukomo wa kiwango cha kuwekeza fedha hizo. Kwa hiyo, hiyo unaweza ukaja ukaiona katika miradi na mingine imekuwa inawekezwa ikiwa ni inatoa huduma kwa wananchi. Kwa mfano; daraja la kigamboni na majengo mengine ambayo ni ya mifuko hii yameendelea kupata fedha kulingana na hali ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye swali lake la pili ambalo ameuliza kuhusu uwekezaji kwenye mfuko wa Mkulazi na ameeleza kuhusiana na Taarifa za *CAG*. Msingi ni ule ule kwamba Mkulazi kwa sasa hatujaanza uzalishaji lakini katika maeneo yale yaliyoainishwa utakumbuka vizuri wakati wa Uwekezaj*i BOT* inatoa kanuni na miongozo na inaeleza maeneo ya uwekezaji na tatu inaeleza hadi ukomo wa uwekezaji. Sasa, katika uwekezaji huo kwa sasa katika kiwanda cha Mkulazi hakijaanza uzalishaji…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, umeshamjibu vizuri, umemjibu vya kutosha, ahsante.

Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Leah Komanya.

Na. 333

**Mashine za *POS* ambazo hazikuwa hewani 2018 -2021**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza: -

Je, mashine ngapi za kukusanya mapato zilibainika kutokuwa hewani na hazikutambulika na Halmashauri mwaka 2018/2019, 2019/2020 na 2020/2021?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 kulikuwa na mashine 14 za kukusanyia mapato *(POS)* katika halmashauri mbili, mwaka 2019/2020 kulikuwa na mashine 1,469 za kukusanyia mapato *(POS)* katika halmashauri 54 na mwaka 2020/2021 kulikuwa na mashine 1,355 katika halmashauri 46 ambazo hazikuwa hewani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imefanya maboresho ambapo matumizi ya mashine za kukusanyia mapato kupitia mfumo wa *LGRCIS* yatakoma ifikapo tarehe 30Juni, 2023 hivyo kuanzia tarehe 1 Julai, 2023 hakutakuwa na *POS* zitakazokuwa *offline* zaidi ya saa 24.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah.

**MHE. LEAH. J. KOMANYA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maboresho yaliyofanywa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa kuwa changamoto kubwa ya mkaguzi wa nje *CAG* katika *POS* ilikuwa ni matumizi ya fedha mbichi na kusababisha kushuka kwa mapato ya hamashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kufahamu je, mfumo mpya wa *TAUSI* unakwenda kukabiliana nayo vipi hii chanagamoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakusanya mapato wengi hawana taaluma. Nilitaka kujua mkakati wa Serikali wa kuajiri wahasibu wa kutosha katika halmashauri zetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la kwanza nianze kwa kusema changamoto kubwa ambayo ilikuwepo kwenye halmashauri zetu na hizi *POS* kuwa ziko *offline* ilikuwa ni uadilifu wa watumishi wetu. Tayari Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilichukulia hatua wale wote waliopatikana na hatia ya kucheza na *POS* hizi na hivyo kupotezea mapato halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna *Dashboard* hivi sasa katika mfumo mpya wa *TAUSI* ambapo katika halmashauri zote, Mkurugenzi ana uwezo wa kuona mapato yaliyokusanywa kwa wakati huo na kama kuna POS yoyote itakwenda *offline* basi nayo Mkurugenzi ataona. Hata hiyo, dashboard ile ile iko Mkoani na vilevile Ofisi ya Rais, TAMISEMI tuna uwezo wa kuona. Kwa hiyo, tumefanya maboresho makubwa sana na kuanzia tarehe 1 Julai ndio mfumo pekee ambao utatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali la pili; la taaluma, Kuajiri watu wenye taaluma ya uhasibu. Hili tunalipokea na kadri ya uwezo wa Serikali wa kibajeti tutaajiri watu kuendana na taaluma ya uhasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi. Kwa kuwa Serikali imekuja na

mfumo mpya wa kukusanya mapato unaojulikana kama *TAUSI,* nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba madiwani wote wanapata elimu ya huu mfumo? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali kwenye mfumo huu wa *TAUSI,* kwanza ni Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilitoa *technical specification* kwa halmashauri zote za aina ya *POS* ambazo zinatakiwa kununuliwa ambazo zitaendana na mfumo huu. Kadri tunavyokwenda tunatoa mafunzo kwa wale wanaohusika na *POS* hizi kule kujua ni namna gani wanatumia *POS* hizi ambazo zinaendana na mfumo huu wa *TAUSI.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Geoffrey Mwambe.

Na. 334

**Taa za barabarani**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itasimika taa kwenye barabara za mitaa Mji wa Masasi ili kuongeza usalama, kupunguza uhalifu na kuhamasisha shughuli za biashara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Geoffrey

Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa uhitaji wa taa za barabarani katika Halmashauri ya Mji wa Masasi kutokana na kukua kwa shughuli za kimaendeleo, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa wedha wa 2022/2023, Serikali kupitia *TARURA* - Wilaya ya Masasi imetenga shilingi milioni 192 kwa ajili ya kusimika taa 48 kwenye barabara za Mji wa Masasi ambazo zitawekwa kwenye barabara za *TANESCO* - Yatima na Barabara ya Mkapa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa ningependa kujua kwamba Serikali inafikiriaje kwa halmashauri ambazo hazina uwezo mkubwa kimapato wa kuweza kugharamia uwekaji wa taa barabarani kupitia ruzuku inayotolewa na *REA* kwamba halmashauri hiyo ikapata ruzuku asilimia 75 mpaka 100 ukilinganisha na asilimia 50 ya sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni kwamba, sasa hivi tunajua tunafanya juhudi kubwa ya kujenga barabara za mijini hususani pale Masasi na kwenye majimbo ya wenzangu. Kwa nini TAMISEMI sasa isiamue kufungamanisha fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya ujenzi wa barabara na fedha kwa ajili ya uwekaji wa taa ili Mkandarasi anayepewa kujenga zile barabara pale mjini anamalizia na kuweka taa moja kwa moja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwambe, la kwanza hizi Halmashauri ambazo haazina uwezo kupata ruzuku ya *REA*. Hili tunalichukua kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI na tutahakikisha tunakaa taasisi yetu ya *TARURA* kwa kushirikiana na taasisi ya *REA* ambayo iko chini ya Wizara ya Nishati kuona ni namna gani tunaweza kufanya kazi ka Pamoja na kutoa hiyo ruzuku iende kwenye barabara hizi kwenye miji ambayo haina uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, kwa sasa barabara zote zinazojengwa na *TARURA* nchini kote hasa zile zinazopita kwenye Katikati ya miji zinawekewa taa. Pia, kama Masasi kule hawajaanza naamini wakimaliza tu katika ujenzi wa barabara hizi taa zitaanza kufungwa kama nilivyokuwa nimesema kwenye majibu yangu ya msingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrimi.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mji wa Mugumu kama unakuwa kwa kasi na shuguli za maendeleo wakati wote zinaendelea.

Je, ni lini sasa Serikali itatusaidia kuhakikisha tunapata taa za barabarani katika mji wa Mugumu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kuweka taa katika mji wa Mugumu kwenye barabara zinazokamilika. Mheshimiwa Mbunge ni shahidi kuna barabara inayozunguka Soko kuu la Mugumu ambayo inakamilika muda si mrefu na barabara ile itakapokamilika taa zile zitafungwa kama

nilivyosema awali kwamba sasa *TARURA* katika barabara zote zinazojengwa katikati ya miji ni lazima ziwekewe taa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri, alipokuja Katibu Mkuu wa CCM, Kiteto alituahidi taa za barabarani pale mji wa Kibaha na tumeleta maombi. Ni lini Serikali itatuletea hizi fedha tuweke taa za barabarani pale mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amesema ilikuwa ni ahadi ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi ambae Serikali hii ndio inatekeleza Ilani yake ya uchaguzi, tutakaa na wenzetu wa *TARURA* ambao ni taasisi iko chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuona wamejipangaje katika kutekeleza uwekaji wa taa hizi kama ambavyo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inavyotaka.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

Na. 335

**Bei ya kahawa kuamuliwa kwa nguvu ya soko**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:--

Je, ni lini Serikali itaachia bei ya zao la kahawa kuamuliwa kwa nguvu ya soko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bei ya kahawa duniani hutegemea mwenendo wa bei katika masoko ya rejea ya kahawa duniani ambayo ni soko la bidhaa la New York *(ICE)* kwa kahawa za arabika na *euronest LIFFE* ya London kwa kahawa aina ya robusta. Mabadiliko ya mwenendo wa bei katika masoko hayo huchochewa na kiasi cha kahawa kilichozalishwa duniani na mahitaji kwa wakati husika.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya mwenendo wa bei ya kahawa katika masoko rejea yana athari za moja kwa moja kwenye bei za kahawa katika masoko ya kahawa hapa nchini na duniani kwa ujumla. Hivyo, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi yanayoleta ushindani wa kutosha ili kuchochea bei ya kahawa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nina maswali mawili ya nyongeza. Ningependa kupata kauli ya Serikali, kule kwetu Muleba wakulima wanafukuzwa wanakamatwa wakisafirisha kahawa kutoka kata moja hadi kata nyingine na katika tarafa hadi tarafa nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; nilitaka kujua kahawa ni mali ya nani? Ni mali ya Serikali au ni mali ya mkulima? Na ni lini ile hadhi inabadilika? Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge Dkt. Kikoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kauli ya Serikali ni marufuku kwa wakulima wa kahawa walioko katika eneo moja kukamatwa na kuzuiwa kufanya biashara yao kwa sababu biashara hii inafanyika kwa mujibu wa Sheria Na. 23 ya mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, zao la kahawa kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge, katika hali yake ya kawaida Serikali inafanya uratibu lakini mazao haya ni ya wakulima. Najua alikuwa anaelekea wapi, lakini lengo kubwa la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunasimamia na kumfanya mkulima wa kahawa aweze kunufaika. Kwa hiyo kama Serikali tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira wezeshi ili mkulima wa kahawa aweze kunufaika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnada wa Kahawa wa Songwe ni tofauti kabisa na mnada wa kahawa uliopo kule Kagera. Mazingira ya pale Songwe siyo rafiki, hauko wazi na kuna uhuni mwingi unaofanywa na baadhi ya wanunuzi kwa kushirikiana na watu wa bodi kuchezesha bei ya kahawa kwenye mnada ili wakulima wasipate bei inayostahili.

Je, kwa nini Serikali isiboreshe mazingira ya mnada wa kahawa wa Songwe ufanane kama mnada wa kahawa wa Kagera ambao uko wazi *fair* na hakuna uhuni wowote unaoweza kufanyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge George Mwenisongole, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kagera inalimwa robusta, Songwe inalimwa arabica. Haya ni *variety* mbili tofauti. Ukienda kwenye soko ili uweze kuuza kahawa ya arabica lazima pia ionjwe ndio unapata radha na *quality* inayokwenda ku-*determine* bei. Tumesikia hoja ya Mheshimiwa Mbunge naelekeza bodo ya kahawa kuhakikisha kwamba wanaweka mazingira wezeshi ili pia mkulima wa Songwe aweze kunufaika na bei ya kahawa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bilakatwe.

**MHE. INNOCENT M. BILAKATWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Zao la kahawa limevamiwa na ugonjwa wa mnyauko.

Je, Serikali iko tayari kuongeza miche yenye ubora ili zao hili muhimu lisije likafutika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa; na katika bajeti yetu ya mwaka 2023/2024 tumeongeza miche kufikia miche milioni 20 ili wakulima waweze kupata miche bora ambayo pia itakuwa na ukinzani wa magonjwa ambayo yanaathiri zao la kahawa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyohiyo Mheshimiwa Francis Mtinga.

Na. 336

**Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Bonde la Dominiki – Mkalama**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga miundombinu ya Umwagiliaji ikiwemo kuchimba visima virefu katika Bonde la Dominiki, Kata ya Mwangeza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Dominiki lipo katika Kata ya Mwangeza Halmashauri ya Mkalama. Bonde hili ni kati ya maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji yaliyobainishwa na kutambuliwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ndani ya Halmashauri ya Mkalama. Bonde la Dominiki lina takribani hekta 800 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo kwa sasa wakulima wa bonde hili hutegemea kilimo cha mvua. Hii ni kutokana na kutokuwa na uwekezaji wa aina yoyote ya miundo mbinu ya umwagiliaji na chanzo cha kudumu cha maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mpango na bajeti ya mwaka 2023/2024 imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili

kupata gharama halisi za kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji katika Bonde hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri sana ya Serikali yanayotia moyo; hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Mkalama inategemea sana vitunguu kwa mapato yake ya ndani.

Je, Serikali haioni haja ya kwamba mpango huu mzuri ufanyike kwa mtindo wa *build and design* ili uweze kwenda kwa haraka zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa pale Mwangeza kuna mradi wa *ASDP two* ambao ulibomoka;

Je, Serikali haioni sasa haja ya kuukarabati mradi huo haraka ili wananchi wa pale mwangeza waendelee kupata umwagiliaji wakati wakisubiri hili bonde la vitunguu kufanyiwa *design?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi yote ya umwagiliaji ambayo tumeipita nchi nzima utaratibu unaofanyika hivi sasa ni kuhakikisha kwanza tunaanza na upembuzi yakinifu na baadaye ndipo unakuja usanifu wa kina na kisha twende kwenye ujenzi. Hii ni kwa sababu tulipata changamoto ya miradi mingi sana ya miaka iliyopita

ambayo haikupitia hatua hii na hivyo imekuwa ikibomoka kwa haraka sana. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba miradi hii inakuwa endelevu na ya kudumu ili wakulima waweze kunufaika. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge wavumilie taratibu hizi zikamilike mradi huu utajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la kuhusu Mwangeza. Katika kiambatisho cha saba katika jedwali lile la bajeti yetu eneo la Mwangeza ni kati ya maeneo ambayo yanakwenda kufanyiwa upembuzi yakinifu na baadaye pia tutajenga skimu na kukarabati ili wakulima waweze kupata fursa ya kushiriki katika kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo ni eneo ambalo lipo ndani katika mipango ya Serikali tayari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Jimbo la Kalenga lina skimu 19 za umwagiliaji ambazo miundombinu yake yote ni chakavu.

Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba miundombinu hii inaboreshwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti yetu ya mwaka 2023/2024 tumetenga maeneo zaidi ya 80 ambayo yanakwenda kufanyiwa ukarabati zikiwemo skimu zilizo katika Jimbo la Kalenga. Kwa hiyo nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, anaweza kupitia akaangalia orodha yetu na akaona kama maeneo yao yapona aweze kujiridhisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii; je, ni lini Serikali itajenga bwawa na mifeji kwa ajili ya umwagiliaji katika Kata za Shambalaiguruka na Majengo kwa lengo la kupunguza athari za mvua na mafuriko ya Mto Nduruma na Mto Chiplepa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti yetu inayokuja tumetangaza kwamba tunaenda kujenga mabwawa 100 ambayo yatagusa takriban maeneo yote nchi nzima. Hivyo katika wilaya ya kwake Mheshimiwa Mbunge tunakwenda kuangalia maeneo ambayo amaeyataja. Kama si hayo basi tutaichukua kama sehemu pia ya kuifanyia kazi ili katika wakati mwingine ujaotuweze kuyajenga pia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, kwa niaba.

Na. 337

**Mafao ya Wastaafu wa Jeshi la Polisi Zanzibar**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. KASSIM HASSAN HAJI** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kubadili utaratibu wa malipo kwa wastaafu wa Jeshi la Polisi wa Zanzibar ili kuondoa usumbufu wanaoupata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa Mwanakwerekwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, awali utumishi wa Askari Polisi ulikuwa kwenye masharti ya pensheni na bakshishi. Askari ambaye hakuwepo kwenye masharti ya pensheni alifanya kazi kwa mkataba wa miaka 12 kwa kujaza mkataba wa kipindi cha kila baada ya miaka mitatu kumalizika. Kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322, askari kwa hiari yake mwenyewe baada ya mkataba alipaswa kufanya chaguo la ama kuendelea na utaratibu wa ajira ya mkataba na kwa malipo ya bakshishi ambao ukomo wake wa utumishi ni miaka 21 au kuingia kwenye utaratibu wa ajira ya malipo ya pensheni na kulipwa mafao ya uzeeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Jeshi la Polisi limefanya maboresho kwa kuondoa utaratibu wa mkataba wa miaka 12 na kuwa miaka sita pamoja na kuondoa chaguo. Na baada ya mkataba kumalizika askari wote wanaingia kwenye ajira ya kudumu yaani pensheni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali lakini ni ukweli usiopingika kwamba maslahi ya watumishi wa idara hii ya Jeshi la Polisi bado yanahitaji maboresho.

Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuboresha maslahi ya Askari Polisi ili sasa watakapokuwa wanastaafu waweze kupata mafao ambayo yana endana na hali halisi ya maisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashidi Shangazi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuangalia maslahi ya askari wa vyombo vya usalama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameamua kuunda Tume ya Haki Jinai ambayo pamoja na mambo mengine inakwenda kuangalia vilevile eneo hili la maslahi ya askari. Kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo Mheshimiwa Rais ni katika mambo ambayo anayapa uzito mkubwa sana, na tusubiri pale ripoti ya Tume itakapomaliza ili tione sasa utekelezaji wake utakuwa vipi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kati ya mwezi wa nne mpaka ninavyozungumza sasa mauaji yamefanyika katika mji wa Sirali ni uporaji wa mali…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara swali la msingi ni wastaafu na malipo yao.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Wizara ya Mambo ya Ndani.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo una chomekea hapo hapo, haya tuendelee.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, enhee naomba uniruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Endelea

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimesema kati ya mwezi wa nne mpaka mwezi wa tano kuna mauaji yamefanyika katika Mji wa Sirali wameua mtu pale Kubiterere Mwema wameua mtu katika Kata ya Pemba, wamepiga risasi pale Kiru kwenye kata yangu, na juzi walimuua daktari katika Kituo cha Afya cha Kilende Nyamungo. Kuna kata nane watu wanapigwa risasi hadharani, na hali hiyo haijafuatiliwa.

Ningeomba nijue kauli ya Serikali wanachukua hatua gani za dharura ili kurejesha amani katika Jimbo la Tarime na hasa Mji wa Sirali ambao ni mji wa mpakani na biashara kwa kweli imekuwa hali siyo nzuri sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kama una majibu kama huna unatafuta takwimu unaweza ukalijibu siku nyingine au mtakutana *canteen.* Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waitara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza jambo la kwanza na la muhimu ambalo ningependa Watanzania ambao wanatusikiliza hapa walifahamu ni kwamba hali ya usalama katika nchi yetu ni imara. Matukio ambayo yoyote yanayotokezea katika nchi yetu ya uhalifu wa aina yoyote unaofanywa na mtu yoyote hakuna hata tukio moja ambalo linatokea na polisi ama vyombo vya usalama visifanikiwe kulidhibiti.

Kwa hiyo, mauaji ya aina yoyote ambayo yamekuwa yakitokezea nchini aidha hatua zimeshachukuliwa ama zinaendelea kuchukuliwa. Wako ambao waliohusika wameshapelekwa katika vyombo vya sheria wako ambao uchunguzi unaendelea kufanyika. Na hata suala la jimbo lake, kwa sababu ametoa takwimu, sasa sina hakika kwa

aina yake ya kusema ni nani na kwa hiyo siwezi nikamjibu hapa kumwambia tukio hili liko katika hatua gani. Nimhakikishie tu kwamba hakuna sehemu yoyote katika nchi hii ikiwemo katika jimbo la Mheshimiwa Waitara ambapo kutatokea uhalifu wa aina yoyote na vyombo vyetu vya usalama vikiwemo jeshi la polisi vishindwe kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Mbunge, kama ana jambo mahsusi katika jimbo lako ambalo unahisi mpaka sasa hivi hajaridhishwa na hatua iliyochukuliwa naomba, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maswali unipatie taarifa hizo ili tuweze kuzifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu sahihi.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Nyoka.

Na. 338

**Ujenzi wa barabara ya Mletele hadi Namanditi – Ruvuma**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kujenga Barabara ya Mletele - Msamala – Mkuzo hadi Namanditi kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Barabara ya Mletele – Msamala – Mkuzo hadi Namanditi *(Songea Bypass*) yenye urefu wa kilometa 14 umejumuishwa katika mradi wa ujenzi wa Barabara ya Makambako hadi Songea yenye urefu wa kilometa 280. Sehemu ya kutoka Songea – Rutikira (km 97) ambao unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia chini ya mradi wa *Tanzania Transport Integration Project (TanTIP)*. Maandalizi kwa ajili ya kutangaza zabuni za kumpata mkandarasi wa ujenzi yanaendelea, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika kutokana na ahadi mbalimbali za viongozi wa Serikali, tangu Serikali ya Awamu ya Tatu, yaani mika 23 mpaka sasa uthamini wa maeneo hayo tayari umeshafanyika zaidi ya mara tatu. Sasa naombe nijue;

Je, ni lini wananchi wa maeneo haya watalipwa fidia ili waweze kupisha ujenzi wa barabara hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali jingine, kulingana na uwingi wa malori kulazimika kupita katikati ya mji wa songea hivyo kulazimisha msongamano ajari na uchafuzi wa mazingira.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara ile ili kuweza kupunguza adha inayowakuta wananchi wa Mkoa wa Ruvuma hususani wakazi wa Songea Mjini, kuzingatia kwamba bajeti ya Serikali ya Wizara hii bado haijapitishwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda

kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tathmini tumekwisha kufanya mara tatu, na hii ni kutokana na sheria ya tathmini; kwamba inapofika baada ya miezi sita na kama hakuna malipo yamefanyika inatakiwa tathmini ile iweze kufanyika tena, vinginevyo ilipwe kwa fidia.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi ambao wataathirika katika ujenzi huu ni kwamba tayari sasa tathmini imekamilika, hii ya mwisho, na daftari lipo kwa Mthamini Mkuu wa Serikali ili aweze kusaini na hatimaye Serikali itafute fedha kwa ajili ya kulipa fidia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kweli tunatambua umuhimu wa barabara hii na ndiyo maana kwa kushirikiana na Benki ya Dunia Serikali imepata mkopo kwa ajili ya ujenzi katika kipande hiki cha Songea - Lutukila na tupo katika hatua za manunuzi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, mara baada ya manunuzi kukamilika tunaanza kujenga, na iko ndani ya mwaka huu wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Dkt. Ritta Kabati.

Na. 339

**Kutenga fedha kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa barabara**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa barabara ya Dodoma – Iringa katika Mlima wa Nyang'oro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa ujenzi na uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2022/2023, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 250 kwa ajili ya kazi ya kufanya uchunguzi wa miamba na udongo unaomomomonyoka katika eneo la Nyang'oro katika Barabara ya Dodoma kwenda Iringa ili kujua tabia za miamba na udongo huo na kuja na mapendekezo ya kitaalam ya jinsi ya kuzuia kumomonyoka huo. Tathmini za zabuni ya kumpata mshauri *(consultant)* wa kufanya kazi hiyo iko hatua za mwisho na Mkataba utakuwa umesainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023. Baada ya taarifa ya kitaalam kutolewa, Serikali itatenga fedha za kutekeleza mapendekezo ya kuzuia mmomonyoko huo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, lakini nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake japokuwa hali ni mbaya sana wakati wa mvua katika lile eneo naomba wajitahidi kufanya haraka sana.

Naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza; kwa kuwa barabara ya Kinyanambo C - Mapanda mpaka Ukami na Kinyanambwa A Saadani – Igoma katika Jimbo la Mufindi

Kaskazini ni ya kiuchumi na pia ni ya ahadi ya Mheshimiwa Rais; je, ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami?

Swali la pili, barabara ya Iringa – Kilolo - Idete ni ya mkoa na Serikali iliahidi muda mrefu sana kuiunganisha na mkoa wa Morogoro kupitia kata ya Idete, Itonya, Muhanga mpaka Mungeta; je, ni lini ahadi hiyo itatimia kwa sababu uchumi wa mkoa wa Morogoro na Iringa uweze kukua kwa urahisi zaidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala hili la barabara ya Kinyanambo C-Mapanda mpaka Ukome. Ni ahadi ya viongozi wetu wa kitaifa na ahadi zote za viongozi wa kitaifa sisi Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tutahakikisha tunazitekeleza na tunaziweka katika vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2023/2024, hususani kwenye barabara hii ya Kinyanambo C -Mapanda-Ukoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, barabara hii ya Iringa – Kilolo – Idete kipande cha Ipogolo – Kilolo chenye kilomita 33 ni barabara ambayo inafadhiriwa na Benki ya Dunia na mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao, wapo katika hatua za manunuzi na kilometa 67 zilizobaki nazo zimekwishafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wa maeneo haya kwa sababu unaunganisha kati ya Mkoa wa Iringa pamoja na Morogoro kwamba inakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulipitisha bajeti hapa ya kujengwa kipande cha Haydom mpaka Labay kwa kiwango cha lami na bajeti ya Waziri bado hatujapitisha.

Je, ni lini atasaini mkataba ule ili barabara ile ijengwe kipande hiki nilichosema kwa kiwango cha lami au tuje na sarakasi kwa namna nyingine tena kwenye bajeti hii ya Jumatatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwenye mwaka huu wa fedha tunatakiwa tujenge barabara hii aliyoitamka Mheshimiwa Mbunge na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha kwa sababu mwaka wa fedha wa Serikali ni mpaka tarehe 30 Juni, nina hakika tutakuwa tumesaini barabara hii ili mkandarasi aanze kufanya kazi pale. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Martha Festo Mariki.

Na. 340

**Ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga kwa kiwango cha lami**

**MHE. MARTHA F. MARIKI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga barabara ya Kibaoni – Majimoto hadi Inyonga kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Majimoto hadi Inyonga yenye kilometa 162. Hadi sasa jumla ya kilometa 9.3 zimejengwa kwa kiwango cha lami sehemu ya Inyonga kilometa 4.2 na Majimoto kilometa 2.6 na Usevya kilometa 2.5 ambapo ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Mpimbwe. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa sehemu iliyobaki, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, wananchi wa Mkoa wa Katavi hususan wa eneo hili wamekuwa wakizunguka umbali mrefu kupitia Eneo la Mpanda mpaka Inyonga kutokana na kwamba barabara hii kipindi cha masika imekuwa haipitiki kabisa.

Swali la kwanza; je, Serikali haioni sasa umuhimu wa haraka wa kufanya ujenzi wa barabara hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali inafanya ujenzi wa Barabara ya kutoka Mpanda – Uvinza mpaka eneo la Lulafe. Je, ni lini Serikali itakamilisha kilometa zilizobaki

mpaka Uvinza ili tuweze kuunganishwa na wananchi wa Mkoa wa Kigoma kwa ujenzi wa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii aliyoitamka ni kilometa hizo 60 ambazo zinahitaji kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini Serikali iliona umuhimu kwanza kwa kuanza ujenzi wa Daraja la Kavuu ambalo lilikuwa la chuma sasa tunakwenda kuweka zege na kazi hii inaendelea. Katika mwaka wa fedha sasa tutakamilisha hizo kilometa zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kwa Barabara hii ya Mpanda – Uvinza; barabara hii ipo na mkandarasi anaitwa *CHICO* na tayari tumeanza ujenzi wa kiwango cha lami kilometa 25 na tunategema kwamba mkataba huu utaisha baada ya mwaka mmoja na miezi sita. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa maeneo hayo yote, kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaendelea kutekeleza mradi huu na utakamilika kwa wakati, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, barabara ya Kwa Sadala – Isuke kilometa 15 imekuwa ni ahadi ya muda mrefu kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami na hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais; je, ni lini sasa barabara hii ya Kwa Sadala – Isuke kilometa 15 itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na barabara hii ya Kwa Sadala – Isuke na kwa kuwa ni ahadi za viongozi wetu wa Kitaifa kama nilivyokwishajibu swali la Mheshimiwa Martha kwamba, ahadi zote za viongozi wa Kitaifa, sisi Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tumeziweka katika mpango wa bajeti ijayo. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge apitishe bajeti itakayosomwa hapa tarehe 22 na 23 ili barabara hiyo iwe sehemu ya utekelezaji huo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe, jiandae Mheshimiwa Stella.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Chombe – Igonda – Kaoze mpaka Ilemba? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii aliyoitamka Chomba – Igomba…

Mheshimiwa Naibu Spika, Ikupa, *sorry,* Stella Ikupa.

**NAIBU SPIKA:** Hapana Bupe, Mheshimiwa Bupe. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Bupe, *okay sorry*. Mheshimiwa Bupe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii aliyoitamka kadri Serikali itakavyopata fedha, tutakwenda kuitekeleza barabara hii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Wananchi wa Mkoa wa Songwe wana changamoto wanapokwenda kuhitaji huduma kutoka mkoani imewalazimu kwenda kupitia Mkoa wa Mbeya na kuanza usafiri kuelekea Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Barabara kutoka Mloo – Isasa – Magamba mpaka Mkwajuni ili kurahisha huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Songwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyotamka Mheshimiwa Mbunge iko katika mpango wa Serikali wa kujenga na sasa tunatafuta fedha ili tuanze ujenzi wa barabara hii, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

Na. 341

**Hitaji la Kivuko – Reli ya Bandari ya Isaka**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga vivuko ili kuweza kupita magari, pikipiki na baiskeli katika Reli ya Bandari Isaka - Msalala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kuimarisha usalama katika maeneo yote ya makutano ya reli na barabara kuu kwa kujenga madaraja au kuweka mageti ya kisasa yanayojifungua na kujifunga yenyewe ili kuzuia watumiaji wa barabara kupita pale treni inapopita kwenye makutano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuweka mageti hayo katika makutano yote ya reli na barabara yaliyopo kwenye barabara kuu yakiwemo makutano ya Isaka. Kwa sasa Serikali imeweka walinzi eneo hilo kwa saa 24 ili kuhakikisha usalama wa watumiaji wa barabara hiyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya vivuko ambavyo vinasababisha mkwamo wa kutoka kitongoji kimoja kwenda kingine. Kuna changamoto kubwa sana kutoka Kijiji cha Itogwamolo kwenda Kijiji cha Bandari, lakini hivyo hivyo kutoka kitongoji cha Shilabela kwenda Isaka Stesheni na hivyo hivyo kutoka kwenye Kata ya Isaka kwenda ya Jana. Sasa swali langu la kwanza; ni lini Serikali itaweza kutenga fedha ili iweze kujenga vivuko vitakavyowawezesha wananchi kufika kwenye maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa katika eneo la Isaka hasa kwenye suala la bandari.

Je, ni lini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakuja kwenye Kata ya Isaka ili aweze kufanya mkutano wa hadhara awasikilize wananchi wa Isaka kero kubwa ambayo inayozuka katika maeneo haya ya bandari, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa karibu sana masuala ya kivuko katika eneo hili. Serikali itaanza ujenzi katika vijiji hivyo alivyovitamka vyote, hususan katika Kijiji cha Isaka na Isakajana, Isaka Stesheni na Kitongoji cha Shilabela na Kijiji cha Itogwa hadi Kijiji cha Bandari. Tutaanza ujenzi wa kuunganisha vijiji hivi tarehe 27 ya mwezi huu wa tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwenda kukagua, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na yeye, mara baada ya kuanza ujenzi tutaenda kukagua eneo hili pamoja na eneo la Stesheni ya Kisaka, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri pamoja sio sekta yako, lakini umejibu vizuri sana, ahsante sana.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa George Ngassa. *(Makofi)*

Na. 342

**Kauli ya Serikali kwa wateja waliolipa shilingi elfu ishirini na saba**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya wateja waliolipia shilingi 27,000 ambao wanatakiwa kulipa fedha zaidi ili kuunganishiwa umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uunganishaji umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 kwa maeneo yote ya mjini na vijijini, wateja wengi sana walijitokeza na bei ziliporudi za awali, wateja takribani 80,000 walibaki bila kuunganishiwa umeme na walikwishalipia huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Serikali uliotekelezwa na *TANESCO* ulikuwa ni kuwaunganishia umeme wateja wote waliolipia shilingi 27,000 bila kuongeza malipo yoyote. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023, wateja wote waliolipia shilingi 27,000 kabla ya Januari, 2022 walikwishaunganishiwa umeme bila kulipa gharama za ziada, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwanza nimpongese Meneja wa *TANESCO* wa Wilaya ya Igunga kwa hatua kadhaa ambazo ameendelea kutupa ushirikiano katika kutatua tatizo hili kwa niaba ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; pamoja na changamoto hii ya malipo ilijitokeza, lakini pia kumekuwa na changamoto ya kukatika umeme mara kwa mara pake katika Mji wa Igunga hususan mjini kati pale, maeneo ya Mwamashimba, Igulubi, Nanga, Bukoko, Ikumba na Ikunungu. Je, nini kauli ya Serikali au Serikali ina mpango gani wa kutatua hii changamoto ya dharura ambayo inaathiri shughuli za kiuchumi za wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ukiangalia katika utekelezaji wa mipango hii ya Serikali pale katika jimbo letu. Kulikuwa na mpango pia wa Serikali kuongeza nguvu kwa kujenga kituo cha kuzalisha umeme. Je, Serikali ina mpango gani katika hili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mbunge Ngassa kwa sababu ni mfuatiliaji mzuri sana wa miradi ya maendeleo katika jimbo lake. Kuna wakati hata mimi alinichukua kutoka Wizara ya Madini kwenda kumsaidia changamoto za wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala lake la kwanza, napenda kumjulisha kwamba Serikali imeanza kutekeleza Mradi wa Gridi Imara wenye thamani ya shilini bilioni 500 ambao utakwenda kujenga kwanza vituo vya kupooza umeme katika kila wilaya; pili kujenga njia ya kusafirishia umeme; na tatu kufanya marekebisho makubwa kwenye njia ya umeme ili umeme nchini uwe wa uhakika, lakini pia

Bwawa la Nyeyere litakapokamilika nadhani hiyo adha ya kukatika kwa umeme itakuwa ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, kuhusu hawa wananchi ambao anasema waliahidiwa kuunganishiwa umeme, ni kwamba Wizara ya Nishati inaendelea na mchakato na mchakato huo utakapokamilika watafahamishwa, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili Mheshimiwa Shangai, kwa niaba, Mheshimiwa Zaytuni.

Na. 343

**Kukiondoa Kijiji cha Ngaresero kwenye eneo la Pori Tengefu la Pololeti**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaondoa Kijiji cha Ngaresero kwenye eneo la Pori Tengefu la Pololeti baada ya kujumuishwa kimakosa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshiwa Naibu Spika, Kijiji cha Ngaresero hakipo katika Pori la Akiba Pololeti ila kipo Kata ya Ngaresero, Tarafa ya Sale. Kijiji hicho ni mojawapo ya vijiji ambavyo vipo ndani ya Pori Tengefu Ziwa Natron. Kulingana na Sheria ya Ardhi

Namba 4 ya mwaka 1999 na marekebisho yake ya mwaka 2019, ardhi ya Pori Tengefu Ziwa Natron ipo kwenye kundi la ardhi ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori Tengefu Ziwa Natron ni moja kati ya maeneo yaliyotolewa maelekezo na Baraza la Mawaziri kuwa lipandishwe hadhi. Hivyo, wakati wa utekelezaji wa maelekezo hayo, wananchi wa kijiji cha Ngaresero watashirikishwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri Kijiji hiki cha Ngaresero bado kina changamoto kubwa na ndio msingi wa swali la Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kuambatana na mimi pamoja na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro kwenda kujionea hali halisi ya kijiji hiki? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwashukuru na kuwapongeza Wabunge wa Mkoa wa Arusha hususan katika Jimbo hili la Ngorongoro na Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Zaytun. Kama ambavyo Serikali imeendelea kutatua migogoro mbalimbali, mgogoro huu tutaenda kuushughilikia ili tukae na wananchi, tuweze kufikia muafaka na hatimaye pori hili liweze kufikia hadhi iliyotarajiwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Esther Malleko.

Na. 344

**Serikali kuboresha Uwanja wa Ushirika Moshi**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha Uwanja wa Ushirika Moshi ili kukuza utalii wa michezo nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Maleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kinamiliki viwanja mbalimbali vya michezo ambavyo ni uwanja wa mpira wa miguu, pete, wavu, kikapu na riadha. Viwanja hivyo ni miongoni mwa miundombinu iliyojengwa na Serikali ili kuendeleza michezo na burudani kwa jumuiya ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa viwanja hivyo vipo katika hali nzuri na vinaendelea kutumika kulingana na malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Chuo kina utaratibu wa kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ukarabati wa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, pamoja na Serikali kutenga fedha za ukarabati kila mwaka, lakini vyumba vya kubadilishia wachezaji ni chakavu, pia chumba cha marefarii kipo karibu sana na chumba cha timu pinzani ambayo inaleta wakati mwingine sintofahamu. Je ni lini sasa Serikali inaweza kutatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je nini mpango wa Serikali kuongeza nguvu katika kujenga Uwanja wa Majengo ambao unajengwa kwa fedha za ndani ili uweze kukamilika mapema? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Malleko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishaeleza katika majibu ya swali la msingi kwamba ni wajibu wa Serikali kupitia Chuo chetu cha Ushirika kwa maoteo ya bajeti kwa ajili ya ukarabati. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge na nilithibitishie Bunge lako Tukufu tutaendelea kufanya hivyo na hivi sasa tutatupia macho maeneo hayo aliyoyataja katika vyumba hivyo vya kubadilishia nguo pamoja na hiki chumba cha marefarii, tutafanya hayo marekebisho labda katika bajeti ijayo ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, anataka kufahamu vile vile mkakati wa Serikali kuhusiana na Uwanja huo wa Majengo. Naomba nimthibitishie Mbunge kwamba uwanja huo tunafahamu kwamba uko chini ya Manispaa ya Moshi. Kwa hiyo tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI, lakini vile vile Wizara yenye dhamana ya michezo kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mbunge wa Segerea, Mheshimiwa Bonnah hajapata majibu na anasumbuliwa sana na wananchi kuhusu Uwanja wa Sigara Tabata, Jimbo la Segerea. Hebu nenda kalifuatilieni hili, mtuambie nani anayemiliki ili mumsaidie Mbunge aweze kuwaambia wananchi wake.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, tumelipokea.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mbogo.

Na. 345

**Uhitaji wa maji Kijiji cha Nkundi – Nkasi Kusini**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Mradi wa Maji katika Kijiji cha Nkundi – Nkasi Kusini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Nkundi kinapata huduma ya maji kupitia Mradi wa Maji wa Bwawa la Kawa uliojengwa mwaka 2016. Hata hivyo, huduma ya maji kwenye kijiji hicho ilisimama kutokana na changamoto za kiuendeshaji zilizosababishwa na gharama za kusukuma maji kulingana na

uwezo wa wananchi. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali imechukua hatua ya kuunganisha Chombo cha Watumiaji Maji Ngazi ya Jamii *(CBWSO)* cha kijiji hicho na vijiji vingine viwili vya Kipande na Kantawa ili kumudu gharama za uendeshaji. Tayari maji yameanza kusukumwa na kazi inayoendelea sasa ni kukarabati mabomba kwenye maeneo yaliyopasuka. Baada ya kazi hiyo, wananchi 4,540 wa Kijiji cha Nkundi wataendelea kupata huduma ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo, jiandae Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kijiji cha Londokazi, Kalundi na Ntalamila wana changamoto kubwa sana ya maji.

Je, ni lini Serikali itakwenda kuchimba visima ili kuondoa adha hiyo ya maji?

Swali la pili, Jimbo la Nkasi Kusini vipo vijiji karibia 20 mwambao mwa Ziwa Tanganyika ambavyo hakuna barabara na hata hii miradi ya maji na vifaa vinashindwa kufika kule, kwa hiyo wananchi wanaendelea kuteseka wanakunywa maji ya kwenye visima pamoja na mifugo. Je, ni lini na ni mpango gani Serikali kwa kushirikiana na *TARURA* waweze kuchonga maeneo hayo ili vifaa vya miradi ya maji iweze kufika katika vijiji hivyo ambavyo ni Msamba, Kilambo cha Mkolechi, Izinga, Mbwiza, Lyela, Kasanga, Kasapa, Lupata, Lyapinda, Ninde, Kapumpuli na Kilabu cha Mkolechi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vincent Mbogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa visima sasa hivi tayari gari liko kwenye mkoa wako na tutakuja kuchimba visima kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha. Vifaa vyetu kupitika katika barabara ambayo ni mbovu tutafanya mawasiliano na Wizara husika tutahakikisha mitambo ile inafika kwenye vijiji hivi na vijiji hivi vinaweza kuchimbiwa visima ili waweze kupata maji safi na salama na kufaidi ile azma ya Mama kumtua ndoo Mama kichwani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Eric, jiandae Mheshimiwa Oliver.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Mradi wa maji kutoka Kijiji cha Lumea, Kalebezo hadi Nyehunge ulijengwa chini ya kiwango, mabomba yanapasuka na kusababisha maji kukatika. Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kuahidi kwamba atautembelea mradi huo ili ikiwezekana kuufanyia ukarabati na marekebisho upya.

Je, yuko tayari kutembelea mradi huu ili kujionea yanayoendelea?

**SPIKA:** Sasa atembelee peke yake au utamchukua maana hukuwa muwazi? Muambatane pamoja au siyo?

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *yah* kuambatana naye.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa

Eric Shigongo kuhusiana na mradi huu ambao tayari Mheshimiwa Mbunge tumeongea mara kadhaa alipofika Wizarani, niseme kwamba niko tayari na tutakwenda kuhakikisha maeneo yote ambayo yalipata uharibifu tunayafanyia kazi kwa haraka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver, jiandae Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mradi wa Maji Kyerwa Nyaruzumbula mpaka Kamuli utaanza lini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu tayari tuna mkandarasi wakati wowote mradi utaanza kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ni lini mabomba yaliyosambazwa katika Kata mbalimbali ya Jimbo la Mbagala yataanza kutoa maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chaurembo, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mabomba yaliyosambazwa lazima mwisho wa siku yatoe maji, miradi yetu sisi inapokamilika lazima mwisho wa siku itoe maji. Hivyo nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge maeneo yote ambayo tumeshasambaza unafahamu kazi nzuri ya *DAWASA* inayoendelea kufanyika, kuna matenki makubwa yameshakamilika na sasa hivi yamebakia kwenye hatua za mwisho kabisa ili yaweze kufikia maeneo yote ambayo tayari yana mtandao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Upo Mradi wa Mwabusiga katika Kata ya Kishapu wenye thamani ya shilingi milioni 314, mradi wa maji ya Ziwa Victoria. Mradi huu unatekelezwa chini ya mpango wa *force account* na uko katika Mfuko ule wa Maji na bahati mbaya kabisa fedha sasa hazijaja. Ziko taratibu za ununuzi wa mabomba na vifaa vingine ambavyo vinahitaji fedha. Sasa lini Serikali itakwenda kuleta fedha na ukizingatia mwaka wa fedha sasa tunakwenda kuumalizia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi huu suala la fedha kila mwezi tunakuwa na mgao. Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa naomba tuonane ili mgao unaofuata mwanzoni mwa mwezi Juni tuweze kuupatia fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Shonza.

Na. 346

**Ahadi ya Kupeleka Mradi wa Maji – Tunduma**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, lini ahadi ya kupeleka mradi mkubwa wa maji Tunduma utatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la maji linaloukabili Mji wa Tunduma na hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali inakarabati miradi ya Uhuru, Nyerere, Ipito, Tunduma na miundombinu ya maji safi Mjini Tunduma. Ukarabati huo unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2023 na kunufaisha wakazi 37,853 katika Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali itaanza kutekeleza mradi mkubwa wa maji kupitia chanzo cha Mto Momba na kwa sasa taratibu za kuajiri Mkandarasi zinaendelea. Kukamilika kwa mradi huo kutaondoa tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na hasa

*commitment* ambayo Mheshimiwa Waziri aliweka wakati akihitimisha bajeti yake. Niseme kwamba wananchi wa Mji wa Mlowo, Mji wa Vwawa pamoja na Tunduma ambao ndiyo wanufaika wakubwa wa huo mradi tunaishukuru sana Serikali na tunaamini kwamba mwaka ujao wa fedha mradi huo utaanza, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni waliopo Jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Spika, Ndugu Penina Mulindo - Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Sauti ya Matumaini *(SAMAF)*. Haya simama wakuone. Umesimama eeh? *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Ndugu Mary Geofrey Mashina - Mwenyekiti wa *SAMAF,* ahsante; Ndugu Janeth Jovin – Mhazini, Ndugu Beatrice Shayo - Afisa Miradi, Ndugu Tatu Mohamed - Katibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mmeliona Jeshi kubwa hilo? Ahsanteni. *(Makofi/ Kicheko)*

Wageni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu; Profesa Carolyne Nombo - Katibu Mkuu; Profesa James Mdoe - Naibu Katibu Mkuu; Dkt. Frankline Rwezimula - Naibu Katibu Mkuu; Dkt. Lyabwene Mtahabwa - Kamishna wa Elimu; Profesa Penina Mrema - Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo ya Mwalimu Nyerere; Profesa John Kondoro - Mwenyekiti wa Bodi ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Ndugu Ndemfoo Tarimo, Naibu Katibu Mtendaji Utawala na Fedha *UNESCO Tanzania;* Profesa Yunusi Mgaya Mkurugenzi Mkuu wa *NIMRI;* karibuni sanna. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wameambatana na Wakurugenzi Wakuu wa Idara pamoja na Taasisi zilizo chini ya

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Wakuu wa Idara wote na wadau wa maendeleo katika elimu, ahsanteni na hongereni kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

YUpo Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa akiambatana na Wenyeviti wa Jumuiya ya Wazazi wa Mikoa pamoja Mratibu wa Viongozi Jumuiya ya Wazazi Makao Makuu Dodoma, karibuni, sana. Ahsanteni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wawili wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, familia yake wakiongozwa na dada yake Theodora Mkenda. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Profesa Mkenda kutoka Rombo wakiongozwa na Ndugu Themistockles Massawe, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Omari Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Ndugu Saada Mtembeji, mke wa Mheshimiwa Omari Kipanga, karibu; Ndugu Samiri Kipanga mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri. Haya tumemuona ahsante. *(Makofi)*

Ipo pia Kamati ya Siasa kutoka Wilaya ya Mafia wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Ndugu Kurwa Milonge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni 103 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo, wanafunzi wa Kiwanja cha Ndege kutoka Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo kutoka Wilaya ya Maswa, karibuni. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Hussein Amar, wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Rashid Shangazi kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Maafisa Habari kutoka Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni 42 wa Mheshimiwa Latifa Juwakali, wanafunzi kutoka Chuo Kikuu Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Priscus Tarimo kutoka Jijini Arusha na nchini Denmark, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Katibu Mtendaji *Elveron Hope Foundation* kutoka Ilemela Mwanza, karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Eric Shigongo kutoka Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Elimu ambao ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa ameandamana na baadhi yao tumeshawatangaza.

Wapo pia walimu wawili ambao wamejipambanua kwa bidii, hamasa na mbinu za kufundishia ambao ni wageni wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Wapo pia Rais na viongozi wa *TAHLISO*, wanafunzi wawakilishi kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Wapo Madiwani wawili kutoka Rombo. *(Makofi)*

Yupo Rais wa *Tanzania Academy of Science,* Profesa Mgonja, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni viongozi 20 Vyama vya Siasa kutoka Mkoa wa Dodoma na wawakilishi watatu wa Benki ya *ABSA* iliyokuwa ikitambulika kama *Barclays,* karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Katibu.

**MHE. JOSEPH K MUSUKUMA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo. Mheshimiwa Musukuma.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukupongeza kwa kazi kubwa ambayo umeifanya jana kwa wananchi wako wa Kariakoo na Jimbo lako unaloliongoza, umeonesha uzalendo mkubwa, walipokuwa na matatizo umelia nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 54(1), unasoma na kifungu (3). Liko suala linaloendelea kwa sasa halina tofauti kubwa sana na suala lililotokea Kariakoo. Mwaka 2022/2023 tulipitisha kodi kubwa sana ya vileo na viburudisho vingine, lakini kwa hali iliyopo sasa sehemu zote ambazo zinafanya biashara ya klabu na *open bar* zimefungwa. Nimefanya utafiti wangu jana kwenye Jimbo lako peke yako Dar es Salaam una klabu karibia 12 zimefungwa, nimemsikiliza Waziri wa Afya jana wakati

anahitimisha alitueleza Watanzania tusijifungie ndani tutafute vitu vya ku-*refresh* vichwa vyetu tunapokuwa tumepata muda wa kupumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakusanya pesa nyingi sana na tulizi-*budget* kwenye bajeti iliyopita kutokana na vileo, vileo haviuzwi viwandani vinauzwa na hivi vilabu tulivyovifunga na vinywaji vingine. Sasa nilitaka kupata mwongozo wako ikikupendeza tutajadili na Wabunge nitatoa hoja tujadili kwa sababu nimejaribu kuangalia kwako kuna klabu 12, Mwanza kuna klabu tano, Mbeya kwa Spika kuna klabu nne zimefungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapoteza mapato makubwa na sioni sehemu ambayo tukiendelea kupoteza haya mapato tutayakusanya kutoka kwenye chanzo gani? Kwa hiyo, nilikuwa naomba mwongozo wako ikikupendeza basi nitatoa hoja ili Wabunge tujadili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 76 lakini ninajielekeza Kanuni ya 52(1) lakini vilevile na (4) ambapo inahusu kujibiwa maswali kikamilifu pale ambapo tunaleta maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi nilikuwa na swali namba 332 ambapo swali langu lilitaka kujua kiasi ambacho Mifuko ya Hifadhi imewekeza kwa mantiki ya kila Mfuko, faida na hasara ya uwekezaji huo. Mheshimiwa Naibu Waziri wakati ananijibu ametaja vizuri kabisa kiasi ambacho kimewekezwa na mifuko mbalimbali ambayo ni shilingi trilioni 14.04, lakini ilipokuja faida na hasara amezungumza maneno tu na huwezi kuwekeza fedha halafu ukajibu maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya maswali tunawapelekea muda mrefu sana na mimi nina amini wana majibu, lakini vilevile swali la nyongeza vilevile halikujibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba Mwongozo wako unaweza ukaenda kurejea *Hansard* vilevile ili basi kama utaridhika kwa Kanuni ya 52(4) utoe maelekezo ili haya majibu yajibiwe vizuri kwa sababu ni fedha za watumishi wa nchi hii, kwa hiyo wana haki ya kujua uwekezaji wao unalipa vipi na kwa tija ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mwongozo katika hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima hebu soma Kanuni ya 52(4) inasema nini? Umesema una-*quote* 52(4), inasema nini?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, 52(1) inasema...

**NAIBU SPIKA:** Umesema (4).

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema 52(1) na (4) naomba unisikilize vizuri. Nimesema 52(1) kuhusiana na swali kujibiwa kikamilifu, na Kanuni ya 52(4) ni mamlaka yako wewe sasa, busara yako itakavyokutuma ukisikiliza swali ukapata jibu.

**NAIBU SPIKA:** Hakuna 52(4) Mheshimiwa Halima, kuna 53(4) siyo 52(4) tazama Kanuni yako vizuri.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, 52(1) na (4) Kanuni hii hapa.

**NAIBU SPIKA:** Moja na mbili.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni mpya Bosi wangu mimi nimepewa hiyo. Kuhusu maswali kujibiwa kikamilifu 52(1) au nikusomee na (4) hii ni Kanuni ambayo mimi nimepewa. Sasa kama Kanuni ya Mjumbe inakuwa tofauti na kanuni ya Bosi itakuwa hatari sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima unajua…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, 53(1) na (4).

**NAIBU SPIKA:** Aah! Kaa chini hamna cha samahani, kaa chini. Maana mmecheka hapa na mkasema Kanuni mpya, mmekifanya Kiti kama hapa kina matatizo.

Mheshimiwa Halima nimekuambia hakuna Kanuni ya 52(4) hizi Kanuni sisi tunalala nazo na ukasema iko kwenye Kanuni ya 52(4) Kanuni mpya ambayo hakuna. Sasa unanyanyuka unataka kuniambia hakuna. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 53(1) na (4).

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kiti chako kinatakiwa kitumie tu busara.

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini.

Mheshimiwa Halima Mdee amejichanganya na Kanuni, pamoja na hayo anaweza kuwa na swali la msingi kwa sababu anataka majibu yake hakuridhika nayo, lakini Kanuni zetu ziko wazi. Pale ambapo hujaridhika, Kiti kinaweza kutoa mwongozo kwa jibu lijibiwe tena au wewe unaweza kupeleka malalamiko yako kwa Katibu na ukapewa Mwongozo na Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Mwongozo wa Mheshimiwa Musukuma kuhusu masuala ya makelele, hayo huko ni mjadala mkubwa sana Kitaifa na hata hao wenyewe wanywaji hulalamikia makelele hayo hayo saa nyingine, kwa hiyo, mimi nimpe sasa nafasi Waziri wa Mazingira ili aweze kuyatolea ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa busara zako za kuendesha vizuri Bunge hili katika kumsaidia Mheshimiwa Spika. Ni kwamba, nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria ambazo sisi Wabunge ndio tunazitunga, kanuni na miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Mazingira Sura namba 191 na vifungu vyake, inaanisha masuala mbalimbali ya kutunza mazingira. Kama tunavyokumbuka ni kwamba mwaka 2021 Wizara takribani nane tulikutana baada ya Watanzania wengi kulalamika ikiwepo Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Wizara ya Mambo ya Ndani, ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa; Wizara ya Afya; Wizara ya Sanaa na Habari kipindi kile ikiwa pamoja; tulikuwa tukijadili jambo hili mwisho tukatoka na mwongozo wa kutoa maelekezo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari yake ilionekana, kuna watoto wengine wanapoteza usikuvu kabisa na wanakuwa viziwi; kuna wagonjwa wengine ambao wako ndani, na wengine wanafariki. Kwa hiyo, maelekezo kwa mujibu wa sheria ni kwamba, kila eneo lina utaratibu wake wa kuendesha biashara. Sasa katika eneo hilo, maeneo ya kumbi za starehe yameainishwa. Kwa mfano, *night clubs* ambazo zina *soundproof,* huko watu wanaweza wakapiga muziki kwa kadiri wenyewe wanavyohitaji, hawawezi kuathiri watu wengine katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine ya *bar,* kuna utaratibu wake na zile *sound detectors.* Ndiyo maana hivi karibuni katika utekelezaji wa sheria hiyo, taasisi yetu ya *NEMC* kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ilikuwa ikiwafuatilia watu katika maeneo mbalimbali wanaokiuka sheria. Katika zoezi hili, takribani *bar* zipatazo 89 zilisimamishwa kutoa huduma yake. Asubuhi yake nikatoa maelekezo ya jinsi gani kuratibu kwa sababu sehemu nyingine kulikuwa na *integration* ya kazi nyingine, kwa mfano, uuzaji wa chakula na masuala mengine. Tukatoa mwongozo, na ninashukuru karibu nyumba zote kwa mfano hapa Dodoma kuna *bar* tano zilifungiwa, lakini mpaka leo wote wameshatii utaratibu wa kiserikali na kukubali na kufanya *commitment* kwamba wanaenda kutekeleza sheria hiyo ya Serikali. Kwa hiyo, leo hii *bar* zote za Dodoma, mpaka jana ilibakia *bar* moja, leo hii zote zimepewa *go ahead,* zote zimefunguliwa na zinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika Mwanza zilikuwa sita, Dar es Salaam zilikuwa ndiyo nyingi na mpaka jana zilikuwa 31. Nyingine walikuwa na stoo tu za kuuzia vinywaji. Japo ana stoo za kuhifadhia lakini anaamua kufungua sehemu ya muziki hata bila kibali. Kwa hiyo, nashukuru sana Taasisi yetu ya *NEMC,* imeweza kufanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yetu kubwa ni kwamba tukifanya *compliance* ya sheria na kanuni, nadhani hatutakuwa na shida. Ndiyo maana leo hii hapa Dodoma, ukienda hata *Club 84,* hakuna changamoto yoyote, na hakuna anayolalamika na *Club 84* kwa sababu iko na madhari hiyo. Hapa Dodoma kuna La patrona, juzi juzi walipata changamoto hiyo, lakini ni miongoni mwa watu sasa hivi wameingia katika utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kweli kulikuwa na malalamiko, lakini kubwa zaidi ni kwamba tuliomba wenzetu wakubali kutekeleza sheria na kanuni. Hata hivyo,

nawashukuru sana wenye biashara hizo, kwa taarifa niliyoipata mpaka jana usiku wengi wame-*comply* na wameandika *commitment letter* kweli na kukubali kwamba walikuwa wanafanya kinyume na sheria, na wameweza kununua *sound detectors.* Imani yangu kubwa, zoezi hili tunaendelea nalo na kwamba hizi *bar* zote zitafunguliwa kwa sababu wote wamekubali kutii sheria na kuandika *commitment letter* na mwisho wa siku tutawalinda Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba hatuwezi kujua ni akina mama wajawazito wangapi wamepoteza ujauzito kwa ajili ya kelele zilizopitiliza. Hatujui baba au mama, watu wangapi wamefariki kutokana na *sound* zilizopitiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namfahamu sana *Comrade* Musukuma, ana nia njema lakini katika nia njema hiyo, ndiyo maana Serikali tumeamua kuweka utaratibu mzuri, na ndiyo maana sehemu zote zinafungulia, biashara inaendelea lakini kwa kutekeleza sheria na kanuni tulizojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa, kuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Mkenda ambao ni John Faustine Mkenda, ni mdogo wake. Kwa hiyo, walitaka tuwatangaze, karibuni. Samahani Mheshimiwa hatukuwahi kutangaza, karibuni sana.

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2023/2024**

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Elimu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Fungu 18 - Tume ya Taifa ya *UNESCO*, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Fungu 46 na Fungu 18 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Taifa ya *UNESCO* kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na kutimiza miaka miwili tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu. Katika kipindi hicho ametuongoza vyema na kutuwezesha kupata maendeleo na mafanikio makubwa kutokana na miongozo anayotupatia ambayo imetusaidia sana katika kusimamia na kuendeleza Sekta ya Elimu, Sayansi

na Teknolojia. Aidha, namshukuru kwa kuniamini mimi pamoja na Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuendelea kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wao mahiri katika kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge, na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nawe Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa uongozi wenu mahiri wa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, natumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini; na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile; Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo; Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko Mbunge na Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wote wa Kamati. Aidha, naomba niwashukuru kwa kupokea, kuchambua na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2022/2023 na kuishauri vema Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua na kuthamini sana mchango wa Kamati katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Elimu inachangia katika utekelezaji wa Mpango wa III wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano kwa kuandaa rasilimali watu yenye ujuzi, maarifa na stadi zitakowezesha kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, napenda kuishukuru familia yangu hasa mke wangu Beatrice kwa kuendelea kuwa karibu yangu na kunitia moyo na kuniwezesha kufanya kazi kwa juhudi na ari kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya utelekezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Fungu 46 na Fungu 18 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, na Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Bunge lako tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi 1,555,827,466,796.00 kwa ajili ya Fungu Namba 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo shilingi 533,456,916,000.00 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,022,370,550,796.00 zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO* - Fungu 18 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha shilingi 2,709,163,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha shilingi 1,176,870,000.00 za mishahara na shilingi 1,532,293,000.00 za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 Wizara kupitia Fungu 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya shilingi 642,667,620,483.06 ambapo kiasi cha shilingi 8,680,995,000.00 kilipangwa kukusanywa na idara na vitengo na shilingi 633,986,625,483.06 zilipangwa kukusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli hayo ni kutokana na ada, malipo ya

ushauri elekezi, huduma za Uthibiti Ubora wa Shule na utoaji wa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2023 Wizara imekusanya shilingi 400,139,396,734.49 sawa na asilimia 62 ya makadirio ambapo shilingi 8,116,780,685.14 zimekusanywa na idara na vitengo na shilingi 392,022,616,049.35 zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya shilingi 533,456,916,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, matumizi ya mishahara ni shilingi 500,196,732,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2023, Wizara imepokea jumla ya shilingi 410,266,920,334.60 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46, ambazo ni sawa na asilimia 76.91 ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya *UNESCO* – Fungu 18 Wizara imepokea jumla ya shilingi 1,976,133,163.28 sawa na asilimia 73 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,022,370,550,796.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni shilingi 840,906,789,796.00 na fedha za nje ni shilingi 181,463,761,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili, 2023, Wizara imepokea jumla ya shilingi 1,063,782,313,215.36 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 104.05 ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo shilingi 880,846,253,860.91 ni fedha za ndani na shilingi 182,936,059,354.45 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la kiasi cha fedha za ndani kilichopokelewa kinajumuisha kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya ununuzi wa vishikwambi vya walimu, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, na wathibiti ubora wa shule; na fedha kwa ajili ya Bodi ya Mkopo kilichoongezwa ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wa elimu ya juu. Aidha, ongezeko la kiasi cha fedha za nje kilichopokelewa kinajumuisha fedha zilizopatikana kutokana na matokeo ya kutekeleza kwa ufanisi wa viashiria vya miradi ya Lipa Kulingana na Matokeo *(Programme for Results)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapitio ya sera na mapitio ya mitaala, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023, ulijielekeza katika kutekeleza maeneo ya kimkakati ikiwa ni pamoja na kuongeza fursa na kuimarisha elimu ya ufundi nchini; kuhimiza uandishi, uchapishaji na uchapaji wa vitabu hapa nchini; kuongeza wigo wa shule za ufundi; na kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo katika taasisi za Elimu ya Juu kwa kuanza kujenga kampasi za vyuo zenye kujielekeza katika mafunzo kwa vitendo katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maeneo hayo ya kimkakati ulieenda sambamba na utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo:-

(a) Kuhuisha Sera, Mitaala, Sheria na Miongozo ya Utoaji wa Elimu na Mafunzo Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Mitaala katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Juu kwa lengo la kuleta mageuzi ya elimu nchini na kuwapatia wahitimu ujuzi na maarifa stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhuishaji wa Sera unahusisha mabadiliko katika mfumo wa elimu ili kuwawezesha wahitimu kujiamini, kujiajiri na kuajirika katika mazingira ya utandawazi na kukidhi mahitaji ya soko. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imefanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ili kubaini utoshelevu wa sera hiyo na kuandaa taarifa ya mapitio ambayo imewezesha maandalizi ya Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 - Toleo la Mwaka 2023 ambalo limejielekeza katika utoaji wa elimu ya amali. Elimu ya amali maana yake ni elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi katika ngazi zote za elimu na mafunzo. Vilevile imefanya mapitio ya mitaala ili kubaini utoshelevu wake na kuandaa taarifa ya mapendekezo ya mitaala kulingana na maelekezo ya sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa Sera ya Elimu na Mafunzo, Toleo la 2023 na Mitaala ya Elimu inapata maoni ya wadau wengi, kabla ya uidhinishwaji wake, Wizara imeendesha Kongamano la Kitaifa lililofanyika kuanzia tarehe 12 hadi 14 mwezi Mei, 2023, hapa mkoani Dodoma. Katika Kongamano hilo, zaidi wa Wadau wa Elimu 1,450 walishiriki wakiwemo wanafunzi, walimu, wahadhiri, wakufunzi, wazazi, wadau wa maendeleo, na viongozi mbalimbali ikiwa ni pamoja na viongozi wa dini, siasa na jamii. Vilevile Wizara inaendelea kupokea maoni hadi tarehe 31 Mei, 2023. Aidha, mwezi Juni, 2023 Wizara itaanza taratibu za kuomba idhini ili kuwezesha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa Elimu ya Awali, Msingi na Elimu ya Ualimu inatolewa kwa kuzingatia viwango na ubora stahiki, Serikali imeandaa miongozo kama ifuatavyo:-

(i) Mwongozo wa Kitaifa wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali Tanzania Bara kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu ya awali kwa kuzingatia viwango vya ubora pamoja na kiongozi cha kutekeleza mwongozo huo;

(ii) Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo Shikizi vya Shule ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika vituo shikizi nchini; na

(iii) Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji na Utekelezaji wa Shughuli za Ushirikiano wa Wazazi na Walimu katika Elimu ya Awali na Msingi Tanzania Bara kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya wazazi na walimu katika kutoa huduma stahiki kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza fursa za elimu kwa wote. Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanaandikishwa wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum. Aidha, inaendelea kuhakikisha kuwa wanafunzi waliopata fursa za masomo wanashiriki kikamilifu katika masomo na kuhitimu. Azima hiyo, imefikiwa kwa kutekeleza afua mbalimbali zikiwemo usajili wa jumla ya asasi 683 zilizokidhi vigezo kati ya 684 zilizoomba kwa mchanganuo ufuatao:-

(1) Shule za Awali pekee 26 zisizo za Serikali, na Shule za Awali na Msingi 309;

(2) Imesajili jumla ya wanafunzi 22,802; wanawake 11,641 na wanaume 11,161 katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali; na

(3) Imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu uandikishwaji na umuhimu wa Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kupitia vyombo ya habari, mitandao ya kijamii na maadhimisho ya Siku ya walemavu duniani, Wiki la Elimu Jumuishi, Siku ya Fimbo nyeupe kwa wasioona, Siku ya Braille duniani, na Siku ya watoto wenye *Down Syndrome* na *rare disease*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutoa fursa kwa wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali, Serikali imewezesha kuwarejesha wanafunzi 1,967. Kati ya hao, wanawake 1,046 na wanaume 86 katika mfumo rasmi wa elimu. Vilevile, imedahili jumla ya wanafunzi 23,263, yaani wanawake 15,006 na wanaume 8,257 katika mikoa 26 ambao wanapata Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala *(Alternative Education Pathway)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mamlaka ya Elimu Tanzania imetekeleza yafuatayo:-

(i) Imewezesha ujenzi wa shule mpya za msingi 40; madarasa 174 katika shule za msingi 70; mabweni manne katika shule za msingi tatu; nyumba za walimu 53 katika shule za msingi 53; mabweni manne katika shule za msingi nne; matundu ya vyoo 6,634 katika shule za msingi 472 na ofisi moja. Aidha, imewezesha ukarabati wa shule kongwe 45 za msingi; na

(ii) Imewezesha ukamilishaji wa ujenzi wa shule mpya za sekondari 231 za Kidato cha Kwanza hadi cha Nne zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa kila shule, shule 10 za Kidato cha Tano na Sita kwa wanafunzi wa kike kati ya shule 26 zinazotarajiwa kujengwa kwa kila mkoa zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kila shule. Aidha, imewezesha ujenzi wa madarasa 46 katika shule za sekondari 46; mabweni 72 katika shule za sekondari 54; nyumba za walimu 19 katika shule za sekondari 18; maabara 26 katika shule za sekondari 14, maktaba nne, mabwalo 22, ofisi sita; vilevile, imewezesha upanuzi wa shule kongwe 18 na ukarabati wa shule kongwe 16 za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia Walimu Tarajali na kuboresha miundombinu katika Vyuo vya Ualimu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Imeendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga Mhonda na Dakawa ambapo ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji. Vilevile naendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Vyuo vya Ualimu vitano ambavyo ni Mamirevi, Vikindu, Songea, Singachini na Katoke. Ujenzi na ukarabati huo upo katika hatua za ukamilishaji. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutaimarisha mazingira ya utoaji wa elimu ya walimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Ualimu;

(ii) Imekamilisha ukarabati wa Chuo cha Ualimu Butimba na kuendelea na ukarabati wa maabara ya Sayansi na TEHAMA katika vyuo sita vya ualimu ambavyo ni Chuo cha Ualimu Morogoro, Mpwapwa, Tukuyu, Kasulu, Patandi na Dakawa. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Serikali imenunua na kusambaza viti mwendo 253 kwa wanafunzi wa shule za msingi 200 na sekondari 53 wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuwawezesha kumudu mazingira ya shule nyumbani.

(c) Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kufanya tathimini ya jumla katika asasi 6,316 ambapo shule zilipewa ushauri wa kitalamu na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile imekamilisha ujenzi

wa ofisi tano za Udhibiti Ubora wa Shule katika Halmashauri za Wilaya ya Pangani, Ubungo, Njombe, Bunda, Tarime kwa lengo la kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujenga umahiri wa walimu na wakufunzi katika ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kuimarisha usimamizi wa shule na vyuo vya ualimu, Serikali imetekeleza yafuatayo:-

(i) Imeandaa moduli 12 za Mafunzo Endelevu kwa Walimu kazini (MEWAKA) wa Elimu ya Awali na Msingi na imetoa mafunzo kwa walimu 26,657 wanaofundisha elimu ya awali na msingi kupitia vituo vya walimu na shule teule;

(ii) Imetoa mafunzo kuhusu elimu ya stadi za maisha zinazolenga afya ya uzazi, VVU na UKIMWI na Jinsia kwa walimu 25,700;

(iii) Imetoa mafunzo kuhusu mbinu bora ya ufundishaji kwa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa vitendo kwa walimu wa sekondari 15,282.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha ufundishaji wa masomo ya Amali. Amali ni elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa ajili ya msingi na sekondari na kwa ajili ya maandalizi ya utekelezaji wa Sera na Mtaala Mpya Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(i) Imeanza maandalizi ya Elimu ya Ualimu wa Ufundi kwa kubainisha vifaa na mashine zinazoitajika katika mafunzo hayo;

(ii) Imeanza maandalizi ya utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Ualimu wa Ufundi na kubainisha Vyuo vya Ualimu 10 ambavyo vitatekeleza mtaala huo. Vyuo hivyo ni Kitangali, Ndala, Nachingwea, Kleruu, Mtwara Ufundi, Mpwampwa, Korogwe, Dakawa, Bunda na Kabanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha upatikanaji wa vitabu kwa wanafunzi katika elimu ya awali, msingi na sekondari ili kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi, Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(i) Imeendelea na uchapishaji wa vitabu 2,000,000 vya masomo ya Sayansi na Hisabati kwa ajili ya kusambaza katika Halmashauri zenye mpungufu mkubwa;

(ii) Imechapa na kusambaza nakala 12,307,578 za vitabu kwa mchanganuo ufuatao; nakala milioni 2.5 za vitabu vya hadithi vya Elimu ya Awali; nakala milioni 3.8 za vitabu vya hadithi vya darasa la kwanza na la pili nakala; milioni 4.12 za vitabu vya kiada darasa kwanza na pili na nakala; milioni 1, 687,140 za vitabu vya kiada vya darasa la tatu, la nne na tano na nakala; 17,104 za vitabu vya maandishi yalikuzwa darasa la tatu, la nne na tano kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na nakala 640 za vitabu vya kiada vya maandishi ya breli kwa ajili ya watoto wa elimu ya awali wasiyoona na nakala; 904 za maandishi yaliyokuzwa kwa wenye uoni hafifu;

(iii) Imechapa na kusambaza nakala 525,000 za vitabu vya kiada vya masomo ya *Mathematics, Agriculture, English, Baseline Orientation course, Biology, Chemistry, Book keeping, Civics, English Food and Human Nutrition's, French, Geography, History, Information and Computer Studies*, Kiswahili, *Economics, Music, Physics, Textiles and Theatre Arts* kwa kidato cha kwanza na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitabu vyote vilivyochapwa na kusambazwa vinapatikana katika Maktaba Mtandao ambapo wanafunzi na walimu wanaweza kuvipata bila gharama yoyote ya kuunganishwa kwa mtandao *(zero rate)* na hivyo kurahisisha upatikanaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imesimamia utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi bunifu ambapo Mgeni Rasmi katika halfa hiyo alikuwa ni Rais Mstaafu wa Msumbiji, Mheshimiwa Joaquim Chissano. Tuzo hiyo imeusisha mashindano ya waandishi wa riwaya na mashairi ambapo jumla ya Miswada 283 ilipokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tuzo hiyo mshindi wa kwanza aidha, wa riwaya na mshindi wa kwanza wa ushairi kwa kila nyanja walizawadiwa jumla ya shilingi 10,000,000 ngao, cheti pamoja na vitabu vyao kuchapwa na kusambazwa kwa gharama ya Serikali. Mshindi wa pili alizawadiwa shilingi 7,000,000 na cheti na mshindi wa tatu shilingi 5,000,000 na cheti kwa kila nyanja. Vilevile, tuzo hiyo itasaidia kuongeza idadi ya vitabu vilivyoandikwa na watanzania badala ya kutegemea vitabu vinavyotoka nje ya nchi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukuza ujuzi na uandishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini pamoja na kutambua kuibua, kukuza vipaji vya uandishi na kueneza hali ya usomaji Serikali imeratibu mashindano ya uandishi wa insha kwa wanafunzi 1,116 kwa shule za sekondari ambapo washindi watano waliyopatika kwa ajili ya kushiriki katika mashindano hayo ngazi ya kikanda kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kutoa huduma ya maktaba nchini kwa ajili ya kupata maarifa na taarifa mbalimbali Serikali kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imesambaza nakala za vitabu 21,200 katika maktaba za mikoa 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la upimaji na tathimini ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu Serikali kupitia Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania imetekeleza yafuatayo: -

(i) Imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa mwaka 2022 kwa wanafunzi 1,592,600 ambao ni sawa na asilimia 92 ya wanafunzi waliyosajiliwa kufanya upimaji wa darasa la nne;

(ii) Imeendesha mtihani wa kumaliza elimu ya msingi wa Mwaka 2022 kwa watainiwa 1,350881 ambao ni sawa asilimia 97.59 ya watahiniwa waliyosajiliwa;

(iii) Imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili wa mwaka 2022 kwa wanafunzi 635,130 ambao ni sawa na asilimia 92 waliyosajiliwa;

(iv) Imeendesha mtihani wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2022 kwa wanafunzi watahiniwa 522,217 ambao ni sawa na asilimia 97.66 ya watahiniwa;

(v) Imeendesha mtihani wa maarifa QT kwa watahiniwa 9,557 kati ya watahiniwa 12,110 waliyosajiliwa kufanya mtihani ambapo watahiniwa 4,059 sawa na asilimia 42.47 walifaulu na ;

(vi) Imeendelea na utaini wa Mtihani wa kidato cha sita 2023 kwa watahiniwa 106,946 waliyosajiliwa na Mitihani wa Ualimu kwa watahiniwa 8,900 waliosajiliwa. Mitihani hiyo ilianza kufanyika tarehe 2 Mei, 2023.

(d) Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Utoaji wa Elimu na Mafunzo katika Ngazi Zote za Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa mafunzo kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu *(Education Sector Development plan)* na Mpango Mkakati wa Wizara *(strategic plan)* kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kuimarisha usimamizi wa elimu nchini Wizara imesambaza jumla ya vishikwambi 4,067 kama

ifuatavyo: - Vishikwambi 1,352 kwa wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu, Vishikwambi 305 kwa wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vishikwambi 730 kwa wakufunzi wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vishikwambi 1,680 kwa Wadhibiti Ubora wa Shule Ngazi za Kanda na Halmashauri. Aidha, imekabidhi vishikwambi 274,812 Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mtaa na Vishikwambi 6,600 kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar ili visambazwe kwa walimu wa shule za msingi na sekondari, maafisa elimu ngazi za mkoa, halmashauri na kata.

(e) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (mafunzo ya amali).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za mafunzo ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(i) Imedahiri jumla ya wanafunzi 1,23,352 katika Ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada kwa fani mbalimbali na;

(ii) Imesajili vyuo 127 katika Bodi za Masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi katika taasisi za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu. Katika kufikia azma hiyo Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(i) Imetoa mafunzo kuhusu upimaji na ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri kwa wanafunzi 1,206 wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji na;

(ii) Imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 1,980 wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa lengo la kuimairisha utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa wadau.

(f) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu, Serikali imeongeza fursa za elimu na mafunzo ya elimu ya juu nchini kwa kudahili jumla ya wanafunzi wa elimu ya juu 113,383 ambapo wanawake ni 49,188 na wanaume ni 64,195 sawa na asilimia 88 ya waombaji kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imeendelea kuimarisha huduma ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa lengo la kuongeza wigo wa upatikanaji wa mkopo kwa wanafunzi wenye sifa na mahitaji. Katika kufika azma hiyo Serikali imetoa jumla ya shilingi 652,763,079,647 kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ya Elimu ya Juu kwa wanufaika 202,877 ambapo shilingi 552,176,491,647 zimetolewa kwa wanafunzi wanaosoma ya nchi na shilingi 586,388,000 kwa wanafunzi wanaosoma nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kupitia Samia *Scholarship* Serikali imetoa ufadhili wa shilingi 2,754,370,430 kwa wanafunzi 593 wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi katika kidato cha sita ambao wanaendelea kusoma masomo ya Sayansi, Teknolojia ya Uhandisi, Hisabati au Afya na Sayansi Shirikishi, *(Science Technology, Engineering Mathematics and Allied sciences)* katika ngazi ya shahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa mikopo ya elimu kwa wanafunzi ambapo Benki ya *NMB* imezindua huduma hiyo kwa wanafunzi kupitia mzazi au mlezi au mwanafunzi mwenyewe kama ana miamala kwenye benki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 shilingi bilioni 200 zimetengwa na mkopaji anaweza kukopa kuanzia shilingi 200,000 hadi shilingi 10,000,000 kwa marejesho ya riba nafuu ya asilimia 9.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kuishukuru uongozi wa Benki ya *NMB* na kutoa rai kwa taasisi nyingine za kifedha pamoja na wadau mbalimbali wa elimu nchini kuunga mkono Serikali katika jitihada za kutoa mikopo ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo ya elimu nchini. Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na nchi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha watalam wetu wanapata uzoefu na ujuzi wenye kuendana na mahitaji ya kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuwezesha mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi wa Taasisi za Elimu ya Juu kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na utendaji kazi. Aidha, katika kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kuongeza fursa za mafunzo katika taasisi za elimu ya juu, sayansi na teknolojia Serikali vilevile imeongeza uwekezaji.

(g) Kuimarisha matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchochea maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu nchini kwa lengo la kuchangia maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Katika kufikia azma hiyo Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(i) Imetoa mafunzo kwa wabunifu wachanga 83 na rasilimali fedha kwa wabunifu 27 walioibuliwa katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ya 2022 kwa lengo la kuendeleza ubunifu na teknolojia ili zifikie hatua ya ubiasharishaji na;

(ii) Imetambua teknolojia mpya 27 zilizozalishwa nchini na hivyo kufanya jumla ya teknolojia zilizotambuliwa nchini hadi sasa kufikia 506. Lengo la utambuzi huo ni kuwa na kanzidata ya kitaifa kwa ajili ya rejea kuhusu taarifa za teknolojia na ubunifu zilizozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kubidhaisha teknolojia na ubunifu kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali za kijamii na kuongeza ufanisi katika kuchangia maendeo ya nchi. Katika kufikia azma Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(i) Imeendeleza ubunifu wa *PPH water meter* kwa kutengeneza na kufunga *meter* 20 kwa majaribio katika wilaya 10 za mikoa mitano hapa nchini;

(ii) Imewezesha kampuni changa mbili za teknolojia na ubunifu ambazo ni *Smart* Darasa na Dawa Mkononi kushiriki katika shindano la ubunifu ambalo lilifanyika nchini Afrika ya Kusini lenye lengo la kuendeleza ubunifu. Aidha, shindano hilo lilishirikisha waanzilishi 13 kutoka Namibia, Afrika Kusini, Botswana na Zambia ambapo ubunifu wa Dawa Mkononi kutoka Tanzania uliibuka mshindi namba mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kapitia Tume ya Nguvu za Atomiki imeendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya mionzi ya nyuklia hapa nchini.

(h) Kuimarisha na Kuendeza Tatifi na Matumizi ya Matokeo yake katika Ajenda ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa utatifi na matumizi yake katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii na kuchangia maendeleo ya nchi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa ndani wa kufanya utafiti na kutumia matokeo ya utafiti kwa kutoa machapisho 1,836 kupitia taasisi za elimu ya juu katika

majarida ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kuchangia katika kuvitangaza vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kadhalika imeendelea kuanzisha, kuratibu na kusimamia miradi mbalimbali ya utafiti na ubunifu katika taasisi za Elimu ya Juu na Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuongeza maarifa na kutatua changamoto katika jamii. Azma hiyo imefikiwa kwa kufanya miradi ya tafiti 418 katika Vyuo Vikuu, Vyuo Vikuu Vishiriki na Taasisi za Utafiti na Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhamasisha watalamu, kuandika na kuchapisha kazi zao tutafiti Serikali imeandaa Mwongozo wa utoaji Tuzo kwa Watafiti watakoa chapisha utafiti wao katika majarida yenye hadhi ya Kimataifa *(High Impact Factor Journals)* katika Fani za Sayansi Asilia na Tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumum ya Tume ya *UNESCO* (FUNGU 18). Mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO* imetekeleza yafuatayo: -

(i) Imetoa mafunzo kwa washiriki 23 kutoka vyombo vya habari vya wakilishi wa Serikali kutoka Idara ya Habari Maelezo na wanachuo kutoka Chuo Kikuu cha SUZA kuhusu nafasi ya vyombo vya habari katika kukuza utawala wa haki na sheria na;

(ii) Imeratibu mafunzo dhidi ya mapambano ya matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za mbinu haramu michezoni kwa kushirikiana na Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo ambapo washiriki 230 wakiwemo wakufunzi, viongozi wamichezo na michezo na watunga Sera walishiriki na;

Mwisho imeendelea kufanya utambuzi wa taasisi zilizokidhi vigezo vya kujiunga na mitandao ya elimu ya *UNESCO*, vilevile imehuiwisha mikataba minne iliyohusisha elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kina ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Kina inapatikana katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 6 mpaka 54 ambao naomba uingie katika kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2023/2024. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vitano vyenye lengo la kuongeza ubora wa elimu, kuwezesha vijana wa kitanzania na kupata maarifa, ujuzi, kujiamini, kujiajiri na kuajirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo: -

(i) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu na kuanza utekelezaji;

(ii) Kuongeza fursa na ubora wa mafunzo ya amali, amali ni ufundi na ufundi stadi katika elimu ya sekondari na vyuo vya mafunzo ya amali;

(iii) Kuongeza fursa na ubora wa elimu ya msingi na sekondari;

(iv) Kuongeza fursa na ubora wa elimu ya juu na;

(v) Kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda hapa nchini.

(a) Kukamilisha Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 na Mitaala ya Elimu pamoja na kuanza utekelezaji wake ili

kuimarisha maarifa na ujuzi kwa wahitimu wa ngazi zote za elimu. Aidha, Serikali itafanya mapitio ya Sheria ya Elimu na sheria mbalimbali za Taasisi za Elimu ili kuendana na sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la 2023.

(b) Kuongeza Fursa na Ubora wa Mafunzo ya Amali (Ufundi na Ufundi Stadi) kwa Sekondari na Vyuo vya Kati vya Amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha mafunzo ya Amali kwa shule za sekondari na vyuo vya ualimu kwa kukabarati wa shule za sekondari za ufundi na kuzipatia vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Aidha, itaboresha vyuo vya ualimu kumi kwa kujenga karakana na kuweka mitambo na vifaa katika vyuo hivyo ambavyo ni Kitangali, Ndala, Nachingwea, Kleruu, Mtwara Ufundi, Mpwapwa, Korogwe, Dakawa, Bunda na Kabanga kwa lengo la kuimarisha utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi (Elimu ya Amali) kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile chuo cha ualimu Mtwara kawaida na Mtwara ufundi vitawezesha walimu taraji kupata mafunzo ya Shahada ya Amali kwa kutumia wahitimu wa vyuo vya ufundi *TET* na Vyuo vya Ualimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuongeza fursa za Elimu ya Amali kwa kuendelea kusajili na kudaili wanafunzo katika Vyuo vya Mafunzo ya Amali. Aidha, katika kuongeza idadi ya walimu wa ufundi Serikali itadaili wanafunzi 660 katika chuo cha ualimu wa mafunzo ya ustadi Morogoro – *MVTTC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwajengea umahiri walimu wa vyuo vya mafunzo ya amali, vyuo vya maendeleo ya wananchi ili kuinua ubora wa mafunzo Serikali itatoa mafunzo kwa wakufunzi 1,450 kuhusu ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri kwa lengo la kuwa na walimu mahiri

watakao toa mafunzo kwa wanachuo ili waweze kujiajiri na kuajirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi 64 katika kila wilaya ambazo hazina vyuo hivyo, pamoja na ujenzi wa Chuo cha Mkoa wa Songwe; na itaanza kutoa mafunzo ya amali katika vyuo 29 vilivyokamilika. Vilevile, itakamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya Chuo cha Ufundi Dodoma ambapo kukamilika kwa awamu hii kutawezesha kudahili wanafunzi 1,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, si kuwezesha ongezeko la fursa na ubora wa elimu ya msingi na sekondari tu, Serikali pia itaendelea kuongeza fursa za Elimu kwa kutoa ithibati kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kusasajili shule za msingi na sekondari takribani 560. Aidha itaanza kusajili shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa mfumo wa kielektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutoa fursa za elimu na mafunzo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kununua na kusambaza zana na vifaa saidizi kwa walimu tarajali na walimu na wakufunzi wenye mahiutaji maalumu. Aidha Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kubaini na kukuza vipaji vya uandishi unaozingatia ubunifu kwa lengo la kujenga tabia ya kujisomea, kuhifadhi historia, mila na desturi za jamii pamoja na kuimarisha vipaji vya sanaa na michezo. Katika kufikia azma hiyo Serikali itatekeleza yafuatayo: -

(i) Itasimamia utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere; Nashukuru Profesa Mramba yupo hapa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mwalimu Nyerere; ya uandishi bunifu yenye lengo la kuwatambua na kuwazawadia waandishi mahiri katika nyanja za riwaya, hadithi fupi na ushairi na maeneo mengine yatakayoibuliwa kwa lengo la

kukuza kazi za uandishi bunifu, uchapaji na kuongeza idadi ya machapisho katika shule na maktaba zetu hapa nchini.

(ii) Itaendelea kuratibu mashindano ya uandishi wa insha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ili kukuza stadi za uandishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha uthibiti ubora wa elimu katika ngazi ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, Serikali itatekeleza yafuatayo: -

(i) Itaimarisha mfumo wa udhibiti bora wa shule kwa kufanya ugatuaji kutoka ngazi ya kanda kwenda ngazi ya mikoa ili kusogeza huduma karibu na wadau na kuzifikia asasi nyingi; na

(ii) Itafanya tathmini ya jumla ya shule na asasi 6,700 katika maeneo kadhaa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha kujifunzaji na kuongeza ufaulu wa wanafunzi Serikali itaendelea kuwajengea uwezo walimu wanaofundisha katika shule za msingi na Sekondari pamoja na wadhibiti ubora wa shule kwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Itatoa mafunzo kwa walimu 10,000 wa masomo ya Sayansi na Hisabati katika shule za sekondari kidato cha kwanza mpaka cha nne.

(ii) Mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 4,500 wa shule za sekondari 1,300; na mafunzo kuhusu programu ya shule salama kwa wakuu wa shule za sekondari na wadhibiti ubora wa shule 1,378; mafunzo kuhusu unasihi na ulinzi wa mtoto kwa walimu 3,370 wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu; mafunzo kuhusu ufundishaji wa moduli za masomo 18 hatua ya kwanza na pili kwa walimu 600 kutoka katika vituo

154 vya elimu kwa njia mbadala kwa lengo la kuongeza umahiri na urahisishaji ufundishaji na ujifunzaji;

(iii) Itaendelea pia kuwajengea uwezo walimu 12,000 wa shule za msingi katika upimaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu katika mikoa 10 iliyokuwa na wastani wa chini wa stadi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari kwa kuchapa na kusambaza vitabu vya kiada katika maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la awali, darasa la kwanza, la tatu, sekondari, kidato cha kwanza na elimu ya ualimu kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na vitabu vya nukta nundu kwa ajili ya wanafunzi wasioona.

Mheshimiwa Naibu spika, katika kuongeza idadi ya vitabu vya ziada na rejea vitakavyosaidia walimu na wanafunzi kukuza uelewa wa mada mbalimbali Serikali itatathmini vitabu vya ziada na rejea kutoka kwa waaandishi binafsi. *Either* itawezesha uchapaji wa vitabu wa viongozi mbalimbali wa kitaifa kwa lengo la kukuza uzalendo na maarifa kwa wanafunzi. Vitabu hivyo ni pamoja na kile cha Maisha ya Benjamin William Mkapa, kitabu cha Maisha ya Ally Hassan Mwinyi kitabu cha Mwalimu Julius Nyerere, majuzuhu yale matatu, *38 Reflections on* Mwalimu Nyerere na kitabu cha Abdurazack ambacho kimetafsiriwa Kiswahili kinachoitwa Peponi. Kwa hiyo tutakuwa tunavichapisha vitabu hivyo na kuvisambaza kwa maktaba kwa gharama yetu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu na kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya elimu, msingi, sekondari na elimu ya juu Serikali kupitia Wizara na taasisi zake itatekeleza yafuatayo: -

(i) Itawezesha ujenzi wa vyumba 90 vya madarasa, matundu ya vyoo 360, mabweni 10 ya wasichana, nyumba 36 za walimu na maabara 20 za sayansi. Vilevile itawezesha ujenzi wa miundombinu katika shule 10 za wanafunzi wenye mahitaji maalum kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania; na

(ii) Itakarabati miundombinu ya maabara za kilimo, sayansi, lugha na sayansi kimu katika vyuo vya ualimu saba ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo. Aidha, itaendelea kuunganisha vyuo vya ualimu 11 katika Mkongo wa Taifa kwa ajili ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa jengo la maktaba ya Taifa Makao Makuu Dodoma ambalo pia litatumika kuhifadhi nyaraka na machapisho kwa lengo la kutunza historia, maarifa, maadili, mila na desturi za Mtanzania. Vilevile itajenga maktaba ya Mkoa wa Singida ambayo itawezesha upatikanaji wa huduma za maktaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kukuza na kuendeleza kisomo na elimu kwa umma kwa kuanzisha madarasa 1,000 ya kisomo yanayolenga kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya watu wazima. Aidha, itaendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea ujuzi vijana 12,000 kupitia Mpango wa Elimu Changamani kwa Walio Nje ya Shule ya awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha uongozi na usimamizi wa elimu nchini, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu itatoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na usimamizi wa elimu kwa walimu wakuu 6,500 wa shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania litaendesha mitihani na upimaji wa kitaifa wa darasa la nne kwa wanafunzi 1,815,792 na mtihani wa

kumaliza elimu ya msingi kwa watahiniwa 1,537,171; mtihani wa upimaji wa kitaifa wa kidato cha pili kwa wanfunzi 691,078 na kitado cha nne kwa watahiniwa 610,330, na mtihani wa maarifa kwa watahiniwa 8,500. Pia mtihani wa kidato cha sita kwa watahiniwa 94,920 na mtihani wa ngazi ya cheti na stashahada ya ualimu kwa watahiniwa 8,505.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuongeza fursa na ubora wa elimu ya juu. Serikali itaratibu na kuongeza fursa za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Itadahili wanafunzi 135,000 kwa mwaka wa kwanza wanaotarajiwa kuomba udahili katika vyuo vya elimu ya juu kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada ya Awali na Umahiri;

(ii) Itatoa nafasi 100 za ufadhili wa masomo kutoka nchi rafiki na mashirika mbalimbali nje ya Bara la Afrika kwa wanfunzi wa elimu ya juu.

(iii) Itaongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka wanafunzi 202,877 hadi 210,169, na itaendelea kutoa fursa za elimu ya juu kwa wanafunzi wenye ufaulu uliojipambanua kutoka wanafunzi 592 hadi 1,200 kupitia Samia *Scholarship*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaboresha mafunzo ya udaktari nakuongeza utoaji wa huduma katika vitengo mbalimbali vya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, ikiwemo Shule ya Meno na kuendelea na mradi wa ujenzi wa Kliniki ya Uporoto kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kufundishia, utafiti na kutoa huduma za tiba kwa jamii. Vile vile itaimarisha miundombinu ya kufundishia katika kituo cha umahiri cha magonjwa ya moyo na mishipa ya damu Kampasi ya Mloganzila.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza ufanisi na utendaji wa kazi kwa watumishi katika sekta za elimu ya juu nchini. Serikali itaendelea kutoa ufadhili wa wanataaluma na wataalamu 1,197 wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itandelea kuimarisha miundombinu ya taasisi za vyuo vikuu ili kuboresha mazingira ya kujifundishia na kujifunzia kwa kujenga kampasi mpya 14 za vyuo vikuu katika mikoa ambayo ilikuwa haina kampasi kama hizo. Kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya sayansi teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza maaraifa na kutatua changamoto mbalimbali katika jamii Serikali itafanya tafiti katika maeneo 177 ya elimu, lugha, kilimo, biashara, uvuvi, mifugo, tiba, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano, maliasili, sayansi, teknolojia, watu wenye mahitaji maalumu, kilimo na chakula na uongozi wa bisahara. Vile vile itaendelea kutoa huduma ya ushauri wa kitalamu katika nyanja mbalimbali. Aidha itaandaa machapisho 1,806 kwa lengo la kueneza matokeo ya tafiti hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuwatambua wabunifu, kuwaendeleza na kubiasharisha ubunifu wao, pamoja na kuendeleza miradi mbalimbali ya ubunifu kwa lengo la kukuza utaalamu asilia kwa kuendeleza teknolojia zilizozalishwa na wabunifu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha matumizi salama ya mionzi ya nyuklia nchini, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za *Atomic* itaendelea kudhibiti matumizi ya mionzi nchini kwa kukagua vituo 900 vyenye vyanzo vya mionzi ili kuhakikisha usalama wa wagonjwa, wafanyakazi na jamii. Aidha itapima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,110 wanaofanya kazi kwenye mazingira yenye

vyanzo vya mionzi. Vile vile itafatilia hali ya usalama wa hewa katika anga kupuitia vituo 1,045.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa *UNESCO* fungu 18. Serikali kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO* itaendelea kuratibu, kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya *UNESCO*. Vilevile itatoa elimu kwa taasisi na mamlaka za Serikali kuhusu mkataba wa 2001 wa urithi wa chini ya Bahari *(Underwater Heritage)* ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko mbioni kuridhia. Aidha itafuatailia na kutathmini maeneo mapya ya urithi yaliyopendekezwa na wadau ili kuongeza meneo zaidi ya urithi wa dunia nchini yatakayotambuliwa na *UNESCO* kwa lengo la kuongeza vituo na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Natumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa maarufu kama *QS* Omari Juma Kipanga, Mbunge, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majikumu yangu na kufikia malengo ya Wizara. Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu Mkuu, Profesa Carolyne Ignatius Nombo, Naibu Makatibu Wakuu, Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Franklin Jasson Rwezimula kwa kunipa ushirikiano mkubwa. Vilevile, namshukuru sana Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote wa Wizara kwa juhudi na kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru pia viongozi wa vyama vya wafanyakazi, watumishi wa Wizara na taasisi zake, walimu, wanafunzi, na wadau wote wa rlimu kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki na menejimenti za shule, vyuo na taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kutoa shukrani za pekee kwa ndugu zangu wa Rombo ambao wamenifanya kuwa Mbunge na kuendelea kuniunga mkono, na wanavyoona huku tunachapa kazi na wameendelea kuniunga mkono, ahsante sana Rombo. Vilevile nawashukuru washirika wa maendeleo na wadau wote wa elimu ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa mopango wa miradi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo; Serikali ya Misri, Msumbiji, Morocco, Namibia, Tunisia, Mauritius, Comoro, Ethiopia, Zimbabwe, Algeria, Afrika Kusini, Malawi, Umoja wa Falme za Kiarabu, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Finland, Hungary, India, Indonesia, Italia, Israel, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Malaysia, Netherland, New Zealand, Norway, Palestine, Romania, Saudi Arabia, Sweden, Thailand, Ufaransa, Urusi, Uswisi, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani na Venezuela. Aidha natambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kushukuru mashirika ya kitaifa na kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za elimu, sayansi na teknolojia ambayo ni pamoja na; *Swedish International Development Agency (SIDA),* Umoja wa Nchi za Ulaya, *Foreign, Commonwealth and Development Office,* Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, *Global Partnership in Education*, *United Nations International Children's Emergency Fund*, *United Nations Development Programme*, *United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO), United States Agency for International Development (USAID),* Benki ya Dunia, *Inter University Council for East Africa*, *Human Development Innovation Fund*, *Deutscher Akademischer Austauschdienst (DAAD), British Council*, *Campaign for Female Education, Commonwealth Secretariat*, *Aga Khan Education Services*, *Japan International Cooperation Agency (JICA),* Karibu Tanzania *Organization (KTO), Korea*

*International Cooperation Agency (KOICA), Water Aid, Plan International,* Tanzania *Education Network*/Mtandao wa Elimu Tanzania *(TEN/MET), Mo Foundation*, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) na *Christian Social Services Commission (CSSC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2023/2024. Ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,675,753,227,000 kwa mchanganuo ufuatao: -

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi 537,880,762,000…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hiyo 327, hiyo ili iwekwe vizuri kwenye *Hansard*, hiyo *figure* ya kwanza isome vizuri. Ya trilioni moja bilioni mia sita isome tena.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie. Ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,675,553,327,000 kwa mchanganuo ufuatao: -

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi 537,880,762,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara ambapo shilingi 500,957,569,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 36,923,193,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, shilingi 1,137,872,565,000 zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ambapo shilingi 979,083,678,000 ni fedha za ndani na shilingi 158,788,887,000.00 ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya *UNESCO* (Fungu 18) tunaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,733,888,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya hizo mishahara ni shilingi 1,124,980,000 na matumizi mengineyo ni shilingi 1,608,908,000)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba Taarifa nzima ya hotuba yangu iingie katika kumbukumbu za Bunge, na kwa heshima kubwa sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya bajeti ya Fungu 46 na Fungu 18 yenye jumla ya shilingi 1,678,487,215,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani yangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara www.moe.go.tz na naomba yote iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

## HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF F. MKENDA (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASLISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya FUNGU 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na FUNGU 18 - Tume ya Taifa ya UNESCO, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa mwaka wa fedha 2022/23. Aidha, naliomba

Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Taifa ya UNESCO kwa mwaka wa fedha 2023/24.

3. **Mheshimiwa Spika,** natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na kutimiza miaka miwili tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu. Katika kipindi hicho ametuongoza vyema na kutuwezesha kupata maendeleo na mafanikio makubwa kutokana na miongozo anayotupatia ambayo imetusaidia sana katika kusimamia na kuendeleza Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, namshukuru kwa kuniamini mimi pamoja na Mheshimiwa Omary Juma Kipanga (Mb) Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuendelea kuongoza Wizara hii.

4. **Mheshimiwa Spika,** natumia fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein
Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri katika kuliongoza Taifa letu.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) kwa uongozi wenu mahiri wa kuliongoza Bunge letu tukufu. Aidha, natumia nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga,

Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa jimbo la Babati Vijijini, na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa jimbo la Mufindi Kusini, kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda nimshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mb), Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote wa Kamati. Aidha, naomba niwashukuru kwa kupokea, kuchambua na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2022/23 na kuishauri vema Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2023/24. Natambua na kuthamini sana mchango wa Kamati katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Elimu inachangia katika utekelezaji wa Mpango wa III wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano 2021/22 – 2025/26 kwa kuandaa rasilimaliwatu yenye ujuzi, maarifa na stadi zitakowezesha kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu.

7. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu hasa mke wangu Beatrice kwa kuendelea kuwa karibu yangu na kunitia moyo na kuniwezesha kufanya kazi kwa juhudi na ari kubwa.

8. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya utelekezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

## B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2022/23

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

9. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha Shilingi **1,555,827,466,796.00** kwa ajili ya FUNGU namba 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo Shilingi **533,456,916,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **1,022,370,550,796.00** zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - FUNGU 18 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi **2,709,163,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha Shilingi **1,176,870,000.00** za mishahara na Shilingi **1,532,293,000.00** za matumizi mengineyo.

### Ukusanyaji wa Maduhuli

10. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara kupitia FUNGU 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya Shilingi **642,667,620,483.06** ambapo kiasi cha Shilingi **8,680,995,000.00** kilipangwa kukusanywa na idara na vitengo na Shilingi **633,986,625,483.06** zilipangwa kukusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli hayo ni kutokana na ada, malipo ya ushauri elekezi, huduma za Uthibiti Ubora wa Shule na utoaji wa huduma mbalimbali.

11. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili, 2023 Wizara imekusanya **Shilingi 400,139,396,734.49** sawa na asilimia **62** ya makadirio ambapo **Shilingi 8,116,780,685.14** zimekusanywa na idara na vitengo na **Shilingi 392,022,616,049.35** zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

### Matumizi ya Kawaida

12. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 533,456,916,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya

fedha hizo, Matumizi ya mishahara ni **Shilingi 500,196,732,000.00** (idara na vitengo **Shilingi 80,090,663,000.00** na Taasisi ni **Shilingi 420,106,069,000.00)** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 33,260,184,000.00** (idara na vitengo **Shilingi 25,558,821,658.00** na Taasisi **Shilingi 7,701,362,342.00**).

**13. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2023, Wizara imepokea Jumla ya **Shilingi 410,266,920,334.60** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46, ambazo ni sawa na **asilimia 76.91** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO – Fungu 18 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,979,133,163.28** sawa na asilimia **73** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**Miradi ya Maendeleo**

**14. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,022,370,550,796.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi 840,906,789,796.00** na fedha za nje ni **Shilingi 181,463,761,000.00.**

**15. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili 2023, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,063,782,313,215.36** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia **104.05** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 880,846,253,860.91** ni fedha za ndani na **Shilingi 182,936,059,354.45** ni fedha za nje.

**16. Mheshimiwa Spika**, ongezeko la kiasi cha fedha za ndani kilichopokelewa kinajumuisha: kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya ununuzi wa vishikwambi vya walimu, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, na wathibiti ubora wa shule; na Fedha kwa ajili ya Bodi ya Mkopo kilichoongezewa ili kukidhi mahitaji ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Aidha, ongezeko la kiasi cha fedha za nje kilichopokelewa kinajumuisha fedha zilizopatikana kutokana

na matokeo ya kutekeleza kwa ufanisi kwa viashiria vya miradi ya lipa kulingana na matokeo (Programme for Results).

**C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA**

**17. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mapitio ya sera na mapitio ya mitaala, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23, ulijielekeza katika kutekeleza maeneo ya kimkakati ikiwa ni pamoja na: (i) kuongeza fursa na kuimarisha elimu ya ufundi nchini; (ii) kuhimiza uandishi, uchapishaji na uchapaji wa vitabu hapa nchini; (iii) kuongeza wigo wa shule za ufundi; na (iv) kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo katika taasisi za Elimu ya Juu kwa kuanza kujenga kampasi za vyuo zenye kujielekeza katika mafunzo kwa vitendo katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

**18. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa maeneo hayo ya kimkakati ulieenda sambamba na utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo:

**a. Kuhuisha Sera, Mitaala, Sheria na Miongozo ya Utoaji wa Elimu na Mafunzo Nchini**

**20. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Mitaala katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Juu kwa lengo la kuleta mageuzi ya elimu nchini na kuwapatia wahitimu ujuzi na maarifa stahiki. Aidha, uhuishaji wa Sera unahusisha mabadiliko katika mfumo wa elimu ili kuwawezesha wahitimu kujiamini, kujiajiri na kuajirika katika mazingira ya utandawazi na kukidhi mahitaji ya soko. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ili kubaini utoshelevu wa sera hiyo na kuandaa taarifa ya mapitio ambayo imewezesha maandalizi ya Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 - Toleo

la mwaka 2023 ambalo limejielekeza katika utoaji wa elimu ya amali (elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) katika ngazi zote za elimu na mafunzo; na

(ii) imefanya mapitio ya mitaala ili kubaini utoshelevu wake na kuandaa taarifa ya mapendekezo ya mitaala kulingana na maelekezo ya sera.

**21. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Sera ya Elimu na Mafunzo Toleo la 2023 na Mitaala ya Elimu inapata maoni ya Wadau wengi kabla ya uidhinishwaji wake, Wizara imeendesha Kongamano la Kitaifa lililofanyika kuanzia **tarehe 12 hadi 14 Mwezi Mei 2023**, Mkoani Dodoma. Katika Kongamano hilo, zaidi wa Wadau wa Elimu 1,450 walishiriki (walioshiriki moja kwa moja ukumbini 1,200 na walioshiriki kwa njia ya mtandao 250) ikiwemo wanafunzi, walimu, wahadhiri, wakufunzi, wazazi, wadau wa maendeleo, na viongozi mbalimbali ikiwa ni pamoja na viongozi wa dini, siasa na kijamii. Vilevile, Wizara inaendelea kupokea maoni hadi tarehe 31 Mei, 2023. Aidha, Mwezi Juni, 2023 Wizara itaanza taratibu za kuomba idhini ili kuwezesha utekelezaji wake.

**22. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Elimu ya Awali, Msingi na Elimu ya Ualimu inatolewa kwa kuzingatia viwango na ubora stahiki, Serikali imeandaa miongozo kama ifuatavyo:

(i) Mwongozo wa Kitaifa wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali Tanzania Bara kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu ya awali kwa kuzingatia viwango vya ubora pamoja na kiongozi cha kutekeleza mwongozo husika;

(ii) Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo Shikizi vya Shule ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika vituo shikizi nchini;

(iii) Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji na Utekelezaji wa Shughuli za Ushirikiano wa Wazazi na Walimu katika Elimu ya

Awali na Msingi Tanzania Bara kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya wazazi na walimu katika kutoa huduma stahiki kwa wanafunzi;

(iv) Mwongozo wa Upimaji Shirikishi wa Matokeo ya Ujifunzaji kwa Wathibiti Ubora wa Shule kwa lengo la kuwawezesha wathibiti ubora kupima matokeo ya ujifunzaji wa wanafunzi wa elimu ya awali, darasa la kwanza na la pili; na

(v) imeandaa na kusambaza Mwongozo wa Chakula, Mwongozo wa Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo na Mwongozo wa Elimu ya Kujitegemea katika Vyuo Vya Ualimu. Vilevile, imehuisha Mwongozo wa Mashindano ya Michezo na Sanaa.

**b. Kuongeza Fursa za Elimu kwa Wote**

**22. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanaandikishwa wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum. Aidha, inaendelea kuhakikisha kuwa wanafunzi waliopata fursa za masomo wanashiriki kikamilifu katika masomo na kuhitimu. Azma hiyo, imefikiwa kwa kutekeleza afua mbalimbali zikiwemo:

(i) uandaaji wa Mfumo wa Usajili wa Shule kwa njia ya Kielektroniki (Online School Registration System) ili kurahisisha taratibu za usajili wa shule;

(ii) usajili wa jumla ya asasi 683 zilizokidhi vigezo kati ya 684 zilizoomba kwa mchanganuo ufuatao: shule za Awali pekee 26 zisizo za Serikali, shule za Awali na Msingi 309 (Serikali 150 na zisizo za Serikali 159) na Sekondari 346 (Serikali 209 na zisizo za Serikali 137) na Vyuo vya Ualimu viwili visivyo vya Serikali ili kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu nchini;

(iii) imesajili jumla ya wanafunzi 22,802 (Wanawake 11,641 na Wanaume 11,161) katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali ambapo Astashahada ya Elimu ya Msingi

15,177 (Wanawake 8,406 na Wanaume 6,771), Stashahada ya Ualimu 2,787 (Wanawake 1,076 na Wanaume 1,711) na Stashahada maalum ya ualimu wa sayansi sekondari wa miaka mitatu 4,838 (Wanawake 2,159 na Wanaume 2,679);

(iv) uandaaji wa Mpango wa Shule Salama unaolenga kupunguza vikwazo vya upatikanaji wa elimu hususan kwa wanafunzi walio katika mazingira magumu wakiwemo wenye mahitaji maalum; na

(v) imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu uandikishwaji na umuhimu wa Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kupitia vyombo ya habari, mitandao ya kijamii na maadhimisho ya Siku ya walemavu duniani, Wiki la Elimu Jumuishi, Siku ya Fimbo nyeupe kwa wasioona, Siku ya Braille duniani, na Siku ya watoto wenye Downsyndrome na Rare disease.

**23. Mheshimiwa Spika,** katika kutoa fursa kwa wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali, Serikali imewezesha kuwarejesha wanafunzi 1,967 (Wanawake 1,046 na Wanaume 86) katika Mfumo Rasmi wa Elimu. Vilevile, imedahili jumla ya wanafunzi 23,263 (Wanawake 15,006 na Wanaume 8,257) katika mikoa 26 ambao wanapata Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala (Alternative Education Pathway).

**24. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mamlaka ya Elimu Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha ujenzi wa shule mpya za msingi 40; madarasa 174 katika shule za msingi 70; mabweni manne katika shule za msingi tatu; nyumba za walimu 53 katika shule za msingi 53; mabweni manne katika shule za msingi nne;

matundu ya vyoo 6,634 katika shule za msingi 472 na ofisi moja. Aidha, imewezesha ukarabati wa shule kongwe 45 za msingi;

(ii) imewezesha ukamilishaji wa ujenzi wa shule mpya za sekondari 231 za Kidato cha 1 hadi cha 4 zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa kila shule, shule 10 za Kidato cha 5 na 6 kwa wanafunzi wa kike kati ya shule 26 zinazotarajiwa kujengwa kwa kila Mkoa zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kila shule. Aidha, imewezesha ujenzi wa madarasa 46 katika shule za sekondari 46; mabweni 72 katika shule za sekondari 54 nyumba za walimu 19 katika shule za sekondari 18; maabara 26 katika shule za sekondari 14, maktaba nne, mabwalo 22, ofisi sita. Vilevile, imewezesha upanuzi wa shule kongwe 18 na ukarabati wa shule kongwe 16 za sekondari;

(iii) imejenga shule ya mfano ya sekondari Dodoma katika eneo la Iyumbu yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 ambapo ujenzi umefikia asilimia 87; na

(iv) imejenga upya vituo vinne kwa ajili utoaji wa Elimu ya Sekondari Nje ya Mfumo Rasmi katika Mkoa wa Rukwa (Sumbawanga), Iringa (Iringa Mjini), Pwani (Kibaha Mji) na Manyara (Babati Mji). Aidha, imekarabati vituo vinne katika Mkoa wa Dar es Salaam (Makao makuu ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima), Morogoro (Morogoro Manispaa), Dodoma (Dodoma Jiji) na Ruvuma (Songea Manispaa).

**25. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia Walimu tarajali kwa kuboresha miundombinu katika Vyuo vya Ualimu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga, Mhonda na Dakawa ambapo ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji. Vilevile, imeendelea na ujenzi na

ukarabati wa miundombinu katika Vyuo vya Ualimu vitano ambavyo ni; Mamire, Vikindu, Songea, Singachini na Katoke. Ujenzi na ukarabati huo upo katika hatua za ukamilishaji. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutaimarisha mazingira ya utoaji wa elimu ya ualimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Ualimu;

(ii) imekamilisha ukarabati wa Chuo cha Ualimu Butimba na kuendelea na ukarabati wa maabara za Sayansi na TEHAMA katika vyuo sita vya ualimu ambavyo ni; Chuo cha Ualimu Morogoro, Mpwapwa, Tukuyu, Kasulu, Patandi na Dakawa. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia; na

(iii) imekamilisha kuunganisha Vyuo vya Ualimu 15 vya Serikali katika Mkongo wa Taifa kwa lengo la kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

**26. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetekeleza yafuatayo:

(i) imenunua na kusambaza vitimwendo 253 kwa wanafunzi wa shule za msingi 200 na sekondari 53 wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuwawezesha kumudu mazingira ya shule na nyumbani;

(ii) imenunua vifaa saidizi vya kuongeza usikivu (hearing aids) 100 kwa wanafunzi wa Elimu ya Msingi 30 na Vyuo Vikuu 70 kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, imewezesha upatikanaji wa huduma za kujikimu, ada na vifaa wezeshi kwa wanafunzi 130 (shule za msingi 122 na vyuo vya ufundi 8) wenye mahitaji maalum hususan wanaotoka katika mazingira magumu; na

(iii) imekamilisha ujenzi na kuzindua Shule ya Msingi Jumuishi ya mfano ya Lukuledi katika Halmashauri ya Masasi na Shule ya Sekondari Patandi katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 480 kila moja. Shule hizo zitaongeza fursa ya elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**c. Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu**

**27. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) imefanya tathmini ya jumla katika asasi 6,317 (Awali na Msingi 5,351, Sekondari 932 na Vyuo vya Ualimu 34) ambapo shule zilipewa ushauri wa kitaalam na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(ii) imefanya ufuatiliaji katika asasi 1,419 zikiwemo shule za awali na msingi 1,065 na sekondari 353 na Chuo cha Ualimu ambapo asilimia 50 ya asasi zilizotembelewa zilionesha mabadiliko chanya baada ya kufanyia kazi maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika tathmini ya jumla; na

(iii) imekamilisha ujenzi wa ofisi tano za Uthibiti Ubora wa Shule katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, Ubungo, Njombe, Bunda na Tarime kwa lengo la kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.

**28. Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya kikao cha wadau wa elimu maalum na jumuishi cha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi awamu ya III (National Strategy for Inclusive Education Phase III) 2021/22 - 2025/26 na kubaini kuongezeka kwa uelewa wa wadau kuhusu elimu jumuishi ikiwemo uzingatiaji wa viwango vinavyotakiwa katika ufundishaji na ujenzi wa majengo kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**29. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ujifunzaji wa mtoto kulingana na hatua za makuzi, Serikali imeandaa Kivunge cha Ubora katika Elimu ya Awali (Quality Early Learning Package) kwa lengo la kutengeneza maudhui ya ujifunzaji wa mtoto kulingana na hatua za makuzi. Kivunge hicho kinajumuisha Mwongozo wa ujifunzaji kwa michezo, Mwongozo wa Michezo na Vichezeo, Mwongozo wa Mwezeshaji, na Mwongozo wa
Mbinu za Ujifunzaji.

**30. Mheshimiwa Spika,** katika kujenga umahiri wa walimu na wakufunzi katika ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kuimarisha usimamizi wa shule na vyuo vya ualimu, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa moduli 12 za Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini (MEWAKA) wa Elimu ya Awali na Msingi na imetoa mafunzo kwa walimu 26,657 wanaofundisha elimu ya awali na msingi kupitia vituo vya walimu na shule teule;

(ii) imetoa mafunzo kuhusu Elimu ya Stadi za Maisha zinazolenga afya ya uzazi, VVU na UKIMWI na Jinsia kwa walimu 25,700 kati ya walimu 27,750 wa shule za msingi na sekondari waliolengwa ili kuwajengea uwezo wa kufundisha masuala mtambuka. Vilevile, imetoa mafunzo kuhusu darasa jumuishi kwa walimu 17,800 kati ya walimu 20,000 waliolengwa wanaofundisha Darasa la I – IV. Mafunzo yalilenga kuimarisha utekelezaji wa mitaala;

(iii) imetoa mafunzo kuhusu mbinu bora ya ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa vitendo kwa walimu wa sekondari 15,282 (Wanawake 3,985 na Wanaume 11,297) kati ya walimu 20,000 waliolengwa. Aidha, mafunzo kwa walimu 4,718 waliobaki yanaendelea kutolewa; na

(iv) imetoa mafunzo ya utunzaji wa mazingira na ujanishaji kwa watumishi 186 ambao ni Wakufunzi 140, Wakuu wa Vyuo

vya Ualimu 35, na Maafisa wa Wizara 11 kwa lengo la kuzingatia afua za mazingira katika utekelezaji wa shughuli za taasisi. Vilevile, imetoa mafunzo ya Elimu ya Usawa wa Kijinsia na Ujumuishi kwa Watumishi 125 ikiwa ni pamoja na Wakufunzi 46, Maafisa wa Wizara 31 na Wathibiti ubora wa Shule 48 ili kuimarisha uzingatiaji wa masuala hayo katika utendaji.

**31. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Watu Wazima, Serikali imewezesha ununuzi na usambazaji wa kompyuta za mezani 100, kompyuta mpakato 50, projekta 40, scanner 85, vishikwambi 85 na mashine tano za kurudufisha katika Vituo vya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Vilevile, imewezesha ununuzi wa vitabu 690 kwa ajili ya wasomaji, wakufunzi, wanafunzi na watumishi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika kampasi za Mwanza, Morogoro na Dar es Salaam.

**32. Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha ufundishaji wa masomo ya Amali (Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi stadi) kwa elimu ya msingi na sekondari ikiwa ni maandalizi ya utekelezaji Sera na Mtaala Mpya, Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(i) imeanza maandalizi ya Elimu ya Ualimu wa Ufundi ikiwa ni pamoja na kubainisha vifaa na mashine zinazohitajika katika mafunzo hayo; na

(ii) imeanza maandalizi ya utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Ualimu wa Ufundi na kubainisha Vyuo vya Ualimu 10 ambavyo vitatekeleza mtaala huo. Vyuo hivyo ni; Kitangali, Ndala, Nachingwea, Kleruu, Mtwara (U), Mpwapwa, Korogwe, Dakawa, Bunda na Kabanga.

**33. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuandaa Mkakati wa TEHAMA kwa Shule, Vyuo vya

Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Ualimu - ICT Strategy for Tanzania Schools, Folk Development Colleges and Teachers College.

**34. Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia na kuendeleza elimu ya ualimu nchini, Serikali imewezesha huduma ya chakula kwa wanafunzi 22,085 katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali 35. Vilevile, imewezesha mafunzo kwa vitendo (Block Teaching Practice - BTP) kwa wanafunzi 17,631 wa Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali.

**35. Mheshimiwa Spika,** ili kuibua na kuendeleza vipaji na vipawa kwa wanafunzi wa Vyuo vya Ualimu na kuhamasisha ushiriki katika michezo, kuimarisha afya, Serikali imeratibu Umoja wa Michezo na Sanaa Vyuo vya Ualimu Tanzania (UMISAVUTA) ngazi ya Kanda. Vilevile, imewezesha watumishi 89 (Wanawake 31 na Wanaume 58) ambapo kutoka Makao Makuu 36, Vyuo vya Ualimu 31, Uthibiti Ubora wa Shule 15, na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi saba kushiriki michezo kupitia Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) lililofanyika Kitaifa katika Mkoa wa Tanga.

**36. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa katika ngazi ya awali, msingi na sekondari inaendana na mahitaji ya sasa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha uandishi wa mihtasari 70 katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari Kidato cha 1 - 6. Vilevile, imekamilisha uandishi wa aina 64 za vitabu vya Sekondari Kidato cha 1 - 6 kwa masomo ya Sayansi, Sanaa, Biashara na Kilimo. Aidha, imekamilisha uandishi wa aina 35 za vitabu vya kiada kwa masomo ya ufundi ngazi ya sekondari Kidato cha 1 – 4; na

(ii) imekamilisha uandishi wa Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo 24 ya Elimu ya Awali na Msingi Darasa la III - VI kwa

shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia ili kuwawezesha walimu kufundisha kwa ufanisi na umahiri.

**37. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu katika shule zinazotumia Lugha ya Kiingereza kufundishia pamoja na kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wasioona na wenye uoni hafifu nchini, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imetafsiri vitabu 12 vya hadithi vya Elimu ya Awali vya Lugha ya Kiswahili kuwa katika Lugha ya Kiingereza. Vilevile, imebadilisha vitabu 12 vya kiada vya Elimu ya Awali (Lugha ya Kiswahili 6 na Lugha ya Kiingereza 6), na vitabu vitano vya kiada Kidato cha 1 - 4 kuwa katika maandishi ya Breli na maandishi yaliyokuzwa (large print);

(ii) imeandaa maudhui 58 ya kielektroniki ya Elimu ya Awali na maudhui 80 ya Darasa la I na II kwa Lugha ya Kiswahili. Vilevile, imeandaa maudhui 74 kwa Lugha ya Kiingereza katika mfumo wa katuni (animation-based lessons) kwa ajili ya kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu; na

(iii) imefanya tathmini ya miswada 285 ya vitabu vya ziada vya waandishi binafsi ikiwemo miswada 152 ya fasihi andishi na 133 ya maudhui ya kawaida ambapo miswada 80 imepata ithibati. Miswada hiyo itasaidia kuongeza upatikanaji wa vitabu kwa wanafunzi.

**38. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha upatikanaji wa vitabu kwa mwanafunzi katika elimu ya awali, msingi na sekondari ili kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na uchapaji wa vitabu 2,000,000 vya masomo ya Sayansi na Hisabati kwa ajili ya kusambaza katika Halmashauri zenye upungufu mkubwa;

(ii) imechapa na kusambaza nakala 12,307,578 za vitabu kwa mchanganuo ufuatao: nakala 2,535,564 za vitabu vya hadithi vya Elimu ya Awali; nakala 3,885,000 za Vitabu vya Hadithi vya Darasa la I - II; nakala 4,181,226 za vitabu vya Kiada Darasa I na II; nakala 1,687,140 za Vitabu vya Kiada vya Darasa la III, IV na V; nakala 17,104 za Vitabu vya Maandishi yaliyokuzwa Darasa la III, IV na V kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu; nakala 640 za Vitabu vya kiada vya maandishi ya breli kwa ajili ya watoto wa Elimu ya Awali wasioona; na nakala 904 za maandishi yaliyokuzwa kwa wenye uoni hafifu; na

(iii) imechapa na kusambaza nakala 525,000 za vitabu vya kiada vya masomo ya Mathematics, Agriculture, English Baseline Orientation course, Biology, Chemistry, Book keeping, Civics, English, Food and Human Nutrition, French, Geography, History, Information and Computer Studies, Kiswahili, Economics, Music, Physics, Textiles and Theatre Arts kwa kidato cha 1 – 6.

**39. Mheshimiwa Spika,** vitabu vyote vilivyochapwa na kusambazwa vinapatikana pia katika Maktaba Mtandao ambapo wanafunzi na walimu wanaweza kuvipata bila gharama yoyote ya kuunganishwa kwa mtandao (Zero - Rating) na hivyo kurahisisha upatikanaji wake.

**40. Mheshimiwa Spika,** katika kukuza ujuzi wa uandishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini pamoja na kutambua, kuibua, kukuza vipaji vya uandishi na kuongeza ari ya usomaji nchini, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu mashindano ya uandishi wa insha kwa wanafunzi 1,116 wa shule za sekondari ambapo washindi watano walipatikana kwa ajili ya kushiriki katika mashindano ngazi ya Kikanda; na

(ii) imesimamia utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi bunifu ambapo Mgeni Rasmi katika hafla hiyo alikuwa ni Rais Mstaafu wa Msumbiji, Mhe. Joaquim A. Chissano. Tuzo hiyo imehusisha mashindano ya uandishi wa riwaya na mashairi ambapo jumla ya miswada 283 (Riwaya 85, Ushairi 193 na nje ya nyanja za kushindaniwa 5) ilipokelewa. Katika Tuzo hiyo, mshindi wa kwanza kwa kila nyanja alizawadiwa fedha taslimu Shilingi 10,000,000.00, ngao, cheti pamoja na vitabu vyao kuchapwa na kusambazwa kwa gharama ya Serikali. Mshindi wa pili alizawadiwa Shilingi 7,000,000.00 na cheti na mshindi wa tatu Shilingi 5,000,000.00 na cheti kwa kila nyanja. Vilevile, tuzo hiyo itasaidia kuongeza idadi ya vitabu vilivyoandikwa na Watanzania badala ya kutegemea vitabu vinavyotoka nje ya nchi.

**41. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kutoa huduma ya maktaba nchini kwa ajili ya kupata maarifa na taarifa mbalimbali pamoja na kutoa fursa za mafunzo ya ukutubi, Serikali kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 596 sawa na asilimia 75 ya lengo la kudahili wanafunzi 800 katika chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka - SLADS;

(ii) imefanya uhamasishaji wa usomaji wa vitabu kwa jamii na shule kupitia programu mbalimbali zikiwemo: Programu ya Outreach kwenye vituo 43 vinavyotoa huduma za maktaba; Maonesho ya kimataifa ya vitabu yaliyofanyika katika Jiji la Dar es Salaam na Dodoma ambapo wadau takribani 858 kutoka katika shule na vyuo mbalimbali walishiriki; na Uendeshaji wa warsha kwa wachapishaji (Publishers Association of Tanzania – PATA). Vilevile, inaendelea kuandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Matumizi ya Maktaba Shuleni;

(iii) inaendelea na usimikaji wa Mfumo wa huduma za Maktaba Tanzania (Intergrated Library Manangement Information System – ILMIS) ambao utakuwa katika mtandao (Web based) na utawezesha watumiaji kupata huduma za maktaba popote kwa kutumia simu, kishikwambi au kompyuta;

(iv) imesambaza nakala za vitabu 21,200 katika maktaba za mikoa 20 ambayo ni Kagera, Mwanza, Mtwara, Kilimanjaro, Ruvuma, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Katavi, Kigoma, Lindi, Mara, Mbeya, Morogoro, Njombe, Rukwa, Singida, Tabora, Tanga, Shinyanga, na maktaba za Wilaya 19 ambazo ni: - Bagamoyo, Kibaha, Biharamuro, Chunya, Ilala, Kilosa, Kongwa, Kwimba, Lushoto, Masasi, Mbozi, Mbulu, Ngara, Pangani, Rombo, Ruangwa, Rulenge, Tunduru, Makete na maktaba ya Tarafa ya Mbweera – Wilaya ya Mbulu;

(v) imefanya kongamano la Kitaifa la Maktaba lililohusu uboreshaji wa huduma za maktaba Tanzania ambapo jumla ya wadau 4,720 walishiriki kongamano hilo lililofanyika katika mkoa wa Tanga; na

(vi) inaendelea na ukarabati wa jengo la Bodi ya Maktaba Makao Makuu Dar es Salaam ambapo ukarabati huu umefikia asilimia 90. Vilevile, imeanza ujenzi wa Maktaba ya Kumbukumbu ya Hayati Dkt. Joseph Pombe Magufuli Wilayani Chato ambapo ujenzi upo katika hatua ya msingi.

**42. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha uongozi na usimamizi wa elimu nchini, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu imeendelea kutoa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa elimu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imedahili na kutoa Mafunzo ya Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu na Uthibiti Ubora wa Shule kwa walimu 1,868 kati ya lengo la kudahili walimu 2,343;

(ii) imetoa mafunzo ya uongozi ya muda mfupi kwa Maafisa Elimu 1,233 kwa lengo la kuboresha usimamizi na uongozi wa elimu katika Ngazi ya Shule, Halmashauri na Mkoa; na

(iii) imeendelea kuimarisha mazingira ya kutolea Mafunzo ya Uongozi kwa kujenga jengo lenye ofisi 10, vyumba vya mihadhara vinne vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja katika Kampasi ya Mbeya ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 70.

**43. Mheshimiwa Spika,** katika eneo la upimaji na tathmini ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) kwa mwaka 2022 kwa wanafunzi **1,592,600** ambao ni sawa na asilimia **92.65** ya wanafunzi **1,718,896** waliosajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne. Katika mtihani huo wanafunzi **1,320,700** sawa na asilimia **82.95** walifaulu;

(ii) imeendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) wa mwaka 2022 kwa watahiniwa **1,350,881** ambao ni sawa na asilimia **97.59** ya watahiniwa **1,384,186** waliosajiliwa. Katika mtihani huo watahiniwa **1,073,402** sawa na asilimia **79.62** walifaulu;

(iii) imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili wa mwaka 2022 kwa wanafunzi **635,130** ambao ni sawa na asilimia **92.00** ya wanafunzi **690,341** waliosajiliwa. Katika mtihani huo wanafunzi **539,645** sawa na asilimia **85.18** walifaulu;

(iv) imeendesha Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) wa mwaka 2022 kwa watahiniwa **522,217** ambao ni sawa na asilimia **97.66** ya watahiniwa **534,753** waliosajiliwa. Katika mtihani huo watahiniwa **456,975** sawa na asilimia **87.79** walifaulu;

(v) imeendesha Mtihani wa Maarifa (QT) kwa watahiniwa **9,557** kati ya watahiniwa **12,110** waliosajiliwa kufanya mtihani ambapo watahiniwa **4,059** sawa na asilimia **42.47** walifaulu;

(vi) inaendelea na utahini wa Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE), 2023 kwa watahiniwa **106,946** waliosajiliwa na Mtihani wa Ualimu kwa watahiniwa **8,900** waliosajiliwa. Mitihani hiyo ilianza kufanyika tarehe 2 Mei, 2023; na

(vii) imekamilisha uchapaji wa vitabu vya taarifa za uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Elimu ya Msingi nakala 372,773 (Candidates‟ Item Response Analysis - CIRA - PSLE) mwaka 2021. Vitabu hivi husaidia wadau wa elimu kufanya tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji na kuweka mikakati ya kuboresha.

**d. Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Utoaji wa Elimu na Mafunzo katika Ngazi Zote za Elimu Nchini**

**44. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha mifumo ya usimamizi na utoaji wa elimu na mafunzo nchini kwa ngazi zote, Serikali imetoa mafunzo kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu (Education Sector Development Plan) na Mpango Mkakati wa Wizara (Strategic Plan) 2021/22 – 2025/26 kwa awamu mbili kama ifuatavyo:

a) awamu ya kwanza kwa wasimamizi na watekelezaji wa elimu 768 kwa mchanganuo ufuatao: Maafisa Elimu Mkoa 26; Maafisa Mipango Mkoa 26; Wakurugenzi wa Halmashauri 170; Maafisa Elimu Sekondari na Msingi 363; na Maafisa

mipango wa Halmashauri 183. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kujenga uelewa kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu Nchini na kujumuisha mpango huo katika mipango na bajeti za elimu kwa ngazi ya Halmashauri na Mkoa; na

b) awamu ya pili kwa watekelezaji wa masuala ya elimu 453 wakiwemo: Wakuu wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mkoa na Wilaya 43; Wathibiti Ubora wa Shule Wakuu kutoka katika Kanda 11 na Halmashauri 181; Wakuu wa Vyuo pamoja na Waratibu wa mafunzo wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 105; Wakuu wa Vyuo, Makamu na Wataaluma wa Vyuo vya Ualimu 113 ambapo wataalamu hao walipewa mafunzo kabilishi ya Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu na Mpango Mkakati wa Wizara (Strategic Plan) 2021/22 - 2025/26. Lengo la mafunzo lilikuwa ni kujenga uelewa kuhusu mipango ya Wizara na namna ya utekelezaji wa mipango hiyo katika ngazi husika.

**45. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kuimarisha usimamizi wa elimu nchini, Wizara imesambaza jumla ya vishikwambi 4,067 kama ifuatavyo: vishikwambi 1,352 kwa wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu; 305 kwa wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; 730 kwa wakufunzi wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi; na 1,680 kwa Wathibiti Ubora wa Shule Ngazi ya Kanda na Halmashauri. Aidha, imekabidhi vishikwambi 274,812 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na vishikwambi 6,600 kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar ili visambazwe kwa walimu wote wa shule za msingi na sekondari, maafisa elimu ngazi ya Mkoa, Halmashauri na Kata.

**e. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Mafunzo ya Amali)**

**46. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuongeza fursa za mafunzo na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 123,352 (Wanawake 65,894 na Wanaume 57,458) katika fani mbalimbali kwa Ngazi ya Astashahada ya Awali (Basic Technician Certificate), Astashahada na Stashahada. Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 20,025 (Wanawake 6,451 na Wanaume 13,574) walidahiliwa katika Bodi ya Masomo ya Sayansi na Teknolojia Shirikishi; Wanafunzi 41,187 (Wanawake 22,430 na Wanaume 18,757) walidahiliwa katika Bodi ya masomo ya Afya na Sayansi Shirikishi; na Wanafunzi 62,140 (Wanawake 37,013 na Wanaume 25,127) walidahiliwa katika Bodi ya masomo ya Biashara, Utalii na Mipango; na

(ii) imesajili vyuo 127 katika Bodi za Masomo zifuatazo: Afya na Sayansi Shirikishi vyuo vitatu; Biashara, Utalii na Mipango vyuo vinne; Sayansi na Teknolojia Shirikishi chuo kimoja na vyuo vya ufundi stadi (VET) 119; na kufanya jumla ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuwa 1,329 (Vyuo vya Elimu ya Ufundi TET 465, Vyuo vya Ufundi Stadi - VET 809 na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDC 55). Lengo kuu ni kudhibiti uanzishwaji na uendeshaji wa mafunzo kiholela.

**47. Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kusimamia Ubora wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya ufuatiliaji na tathmini katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi 864, kati ya hivyo 55 ni Vyuo vya Elimu ya Ufundi - TET na 809 ni vyuo vya Elimu na

Mafunzo ya Ufundi Stadi – VET na kubaini kuwa kuna mwamko mkubwa wa uwekezaji katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET) nchini; na

(ii) imeandaa na kuidhinisha Kitabu cha Mwongozo wa Uthibiti Ubora wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET Quality Assurance Handbook).

**48. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi katika taasisi za Elimu ya ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kuhusu upimaji na ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri kwa wakufunzi 1,206 wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji;

(ii) imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 1,980 wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa wadau; na

(iii) imeendelea kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi sita (Shahada ya Uzamivu 3, Uzamili 2 na Stashahada 1) wa Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika vyuo mbalimbali nchini.

**49. Mheshimiwa Spika,** katika kugharimia elimu ya amali (Elimu ya ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi), Serikali imewezesha huduma ya chakula kwa wanafunzi 18,723 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi – FDCs 54, Chuo cha Ufundi Arusha - ATC, Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam – DIT. Vilevile, imewezesha mafunzo kwa vitendo (Industrial Practical Training - IPT) kwa wanafunzi 2,091 wa Chuo cha

Ufundi Arusha - ATC, Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam – DIT.

**50. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuwezesha utoaji wa mafunzo ya ujuzi kupitia Mpango wa utoaji ruzuku (Bursary Scheme) kwa vijana 2,373 waliopo katika mazingira magumu ili waweze kujiajiri. Vilevile, imetoa mafunzo ya uanagenzi kwa wahitimu 2,000 na utarajali 3,030 wa fani ya uhandisi. Aidha, imewezesha mafunzo ya ubunifu na elimu mtandao kwa wanufaika 7,200 wa sekta na ngazi mbalimbali.

**51. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza fursa na ubora wa elimu ya ufundi, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha ujenzi wa Hospitali ya Taaluma na Tiba (Polyclinic) katika Chuo cha Ufundi Arusha. Kukamilika kwa hospitali hiyo kutawezesha utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwa wanachuo pamoja na huduma ya tiba kwa jamii. Vilevile, imenunua mashine tatu za kisasa kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa mafunzo kwa vitendo katika uzalishaji na ushauri wa kitaalam kuhusu ubora wa vifaa vya ujenzi, maabara, maji, upimaji udongo na mimea;

(ii) imekamilisha ujenzi wa jengo lenye madarasa nane yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 880 kwa wakati mmoja, maabara sita zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 270 kwa wakati mmoja, bweni la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 428 kwa wakati mmoja na ofisi 26 zenye uwezo wa kuchukua watumishi 104 katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(iii) imeanza ujenzi wa madarasa, ukumbi wa mihadhara, hosteli mbili, karakana tatu, maabara moja, jengo la nyumba za watumishi 10, jengo la utawala, maktaba, chumba cha

usanifu, ukumbi wa mikutano, kantini na sehemu za mapumziko ili kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Ufundi Arusha. Ujenzi upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji;

(iv) inaendelea na ujenzi wa Chuo cha Ufundi cha Dodoma kitakachokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,000 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi umefikia asilimia 86;

(v) inaendelea na ujenzi wa hosteli katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Karume Zanzibar ambapo ujenzi umefikia asilimia 45. Vilevile, inaendelea na ujenzi wa jengo la Maktaba itakayokuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 na ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja katika chuo hicho;

(vi) imekamilisha ukarabati wa kumbi nne za mihadhara zenye uwezo wa kuhudumia jumla ya wanafunzi 884 katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Kivukoni. Aidha, imekamilisha ukarabati wa jengo lenye ofisi 13 za walimu katika chuo hicho; na

(vii) inaendelea kukamilisha ujenzi wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Ufunzo ya Ufundi Stadi katika Wilaya 25 ambapo ujenzi umefikia asilimia 98. Aidha, Chuo cha Wilaya ya Mbarali na Chuo cha Wilaya ya Kishapu vimeanza kutoa mafunzo. Vilevile, imeanza maandalizi ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi 64 katika wilaya ambazo hazina vyuo hivyo pamoja na ujenzi wa Chuo Cha Mkoa wa Songwe.

**52. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Elimu ya Ufundi inatolewa kwa kuzingatia miongozo ya ubora, Serikali imeendelea kusogeza huduma za uendeshaji na usimamizi wa elimu hiyo kwa wadau nchini kwa kujenga ofisi tano za Kanda za Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi

Stadi katika mkoa wa Arusha, Tabora, Mtwara, Mwanza na Mbeya. Ujenzi umefikia asilimia 85 katika kanda zote.

**f. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu**

**53. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuongeza fursa za elimu na mafunzo ya Elimu ya Juu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi wa Elimu ya Juu 113,383 (Wanawake 49,188 na Wanaume 64,195) sawa na asilimia 88 ya waombaji kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza;

(ii) imetathmini na kutoa vibali 6,134 vya maombi yaliyokidhi vigezo kwa ajili ya kwenda kusoma katika Vyuo vya Elimu ya Juu nje ya nchi; na

(iii) imefanya ukaguzi wa kawaida katika Vyuo Vikuu 23 kati ya vyuo 30 ili kuhakiki ubora wa utoaji wa Elimu ya Juu katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu. Vilevile, imefanya tathmini ya mitaala 217 iliyowasilishwa na taasisi za Elimu ya Juu ambapo mitaala 49 imepata ithibati, mitaala 59 ipo katika hatua za uidhinishwaji, mitaala 60 imefanyiwa uchambuzi wa awali na mitaala 49 ilirudishwa kwa kutokidhi vigezo. Aidha, imetambua tuzo 2,425 zilizowasilishwa na wanafunzi waliosoma vyuo vikuu nje ya nchi.

**54. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na nchi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha wataalamu wetu wanapata uzoefu na ujuzi wenye kuendana na mahitaji ya kikanda na kimataifa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa Hati za Makubaliano (MoU) na nchi mbalimbali. Hati hizo ni za ushirikiano katika maeneo ya: Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili katika nchi ya Burundi, Rwanda, Malawi na Msumbiji; Elimu ya Juu katika nchi ya Algeria, India, Singapore, Comoro, Kenya, Israel na Cuba;

Sayansi na Teknolojia katika nchi ya Pakistan, Zambia na Kenya; na Elimumsingi katika nchi ya Afrika ya Kusini na Qatar. Aidha, imehuisha Hati za Makubaliano na nchi rafiki ya Msumbiji na Algeria kwa lengo la kuongeza wigo wa ushirikiano na fursa za ufadhili wa masomo ya Elimu ya Juu;

(ii) imetoa ufadhili kwa wanafunzi wanne kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kukuza Lugha ya Kiswahili na kuimarisha ushirikiano; na

(iii) imeratibu ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 76 wa Kitanzania katika nchi ya Uingereza (Jumuiya ya Madola) wanafunzi watatu, Hangaria 21 na China 52 katika ngazi ya Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamivu.

**55. Mheshimiwa Spika,** Serikali imewezesha mafunzo kwa vitendo katika kilimo kwa wanafunzi 250 nchini Israel kwa kipindi cha miezi 11 kwa lengo la kujifunza kwa vitendo masuala ya kilimo katika nchi hiyo.

**56. Mheshimiwa Spika,** katika kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na programu mbalimbali zinazotolewa katika taasisi za Elimu ya Juu nchini, Serikali imewezesha maonesho ya 17 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ambapo jumla ya taasisi 77 za ndani na nje ya nchi zilishiriki.

**57. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha huduma ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu pamoja na kushirikisha wadau kwa lengo la kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wenye sifa na uhitaji. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imehuisha Mwongozo wa Utoaji Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuboresha vigezo vya utoaji wa mikopo;

(ii) imeunganisha Mfumo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na wadau wa kimkakati ili kurahisisha utoaji wa taarifa na hivyo kuongeza ufanisi katika utoaji na urejeshaji wa mikopo;

(iii) imetoa jumla ya **Shilingi 652,763,079,647.00** kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambapo **Shilingi 652,176,491,647.00** zimetolewa kwa wanafunzi wanaosoma ndani ya nchi, **Shilingi 586,588,000.00** kwa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi. Jumla ya wanufaika wote ni 202,877 (mwaka wa kwanza 72,973 na wanaoendelea na masomo 129,904). Aidha, kupitia SAMIA Scholarship **Shilingi 2,754,370,430.00** zimetolewa kwa wanafunzi 593 wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi katika kidato cha 6 ambao wanaendelea kusoma masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati au Afya na Sayansi Shirikishi (Science, Technology, Engineering, Mathematics or Health and Allied Sciences) katika ngazi ya shahada;

(iv) imekusanya **Shilingi 141,311,839,428.89** kuanzia Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 kutokana na mikopo iliyoiva ikiwa ni sawa na **asilimia 61** ya lengo; na

(v) imetoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 65 wa kidato cha sita wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

**58. Mheshimiwa Spika,** Serikali imezindua huduma ya mikopo ya elimu inayotolewa na Benki ya NMB kwa ajili ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Mkopo huo una thamani ya **Shilingi bilioni 200** ambao unatolewa kupitia mzazi au mlezi ambaye ni mwajiriwa au mtumishi anayejiendeleza na mshahara wake unapitia Benki ya NMB. Aidha, mkopo huo unatolewa kuanzia kiasi cha **Shilingi 200,000.00** hadi **Shilingi 10,000,000.00** ambao utarejeshwa kwa riba nafuu ya **asilimia 9.**

**59. Mheshimiwa Spika,** natumie fursa hii kuushukuru uongozi wa Benki ya NMB kwa kuridhia kutoa fursa ya mikopo ya elimu yenye riba nafuu. Aidha, natoa rai kwa taasisi nyingine za kifedha pamoja na wadau mbalimbali wa elimu nchini kuiunga mkono Serikali katika jitihada za kutoa mikopo ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo ya elimu nchini.

**60. Mheshimiwa Spika,** katika kutoa na kueneza elimu ya ushirika ili kuchochea ari ya maendeleo ya ushirika na jamii, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa elimu kwa wadau kama ifuatavyo: watendaji 44 wa Chama Kikuu cha Ushirika Kilimanjaro (KNCU) na Cooperative Joint Enterprises (CJE); maafisa misitu 24 kutoka katika Wilaya zinazotekeleza mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki katika mkoa wa Tabora na wanachama 867 wa vikundi vya awali vya ushirika;

(ii) imetoa elimu kwa wadau mbalimbali na jamii kuhusu elimu ya ushirika kwa njia ya redio ambapo jumla ya vipindi 39 vya redio vilirushwa kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania - TBC na vipindi 16 kupitia redio za jamii; na

(iii) imetoa huduma za ushauri kuhusu masuala mbalimbali ya ushirika kwa washiriki 7,904 (Wanaume 5,475 na Wanawake 2,429) wakiwemo wanachama, viongozi na wafanyakazi wa vyama vya ushirika.

**61. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuwezesha mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi wa Taasisi za Elimu ya Juu kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na utendaji kazi. Katika kufikia azma hiyo Serikali, imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo ya kuandaa mitaala kwa wahadhiri 280 wa Vyuo Vikuu ili kuandaa mitaala kwa kuzingatia miongozo, viwango na mahitaji ya sasa. Aidha, imetoa

mafunzo kwa Wahadhiri 192 kuhusu namna bora ya ufundishaji; na

(ii) imewezesha mafunzo kwa watumishi 1,935 (mafunzo ya muda mrefu 845 na muda mfupi 1,090) wa Taasisi za Elimu ya Juu katika fani mbalimbali.

**62. Mheshimiwa Spika,** Serikali imewezesha upatikanaji wa wasaidizi 19 wa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Vilevile, imewapatia vifaa saidizi vikiwemo Luninga mbili, vishikwambi 10, kompyuta mpakato 10, vinasa sauti 10, fimbo nyeupe 10, magongo 10 na maboksi 40 ya karatasi za breli kwa lengo la kuimarisha ujifunzaji katika chuo hicho.

**63. Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya mapitio ya mwongozo wa utoaji wa ufadhili wa masomo kwa wanataaluma wa Vyuo Vikuu Binafsi katika programu za Afya na Sayansi Shirikishi. Lengo la maboresho hayo ni kuwezesha utoaji wa ufadhili ambapo jumla ya wanataaluma 24 walipata ufadhili (Shahada ya Uzamivu 17 na Shahada ya Umahiri 7) kati ya wanataaluma 42 walioomba.

**64. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kuongeza fursa za mafunzo katika Taasisi za Elimu ya Juu na Sayansi na Teknolojia, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeanza ujenzi wa Maabara Kuu ya Kemia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam itakayotumika kwa ajili ya utafiti na kutoa huduma ya kupima sampuli za viwandani ambapo ujenzi umefikia asilimia 25; na imeendelea na ujenzi wa jengo la Shule Kuu ya Uchumi kampasi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambapo ujenzi umefikia asilimia 60. Vilevile, imeendelea na upanuzi wa Hosteli ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambapo ujenzi umefikia asilimia 33;

(ii) imewezesha ujenzi wa majengo yaliyoungua na kununua vifaa vya maabara katika Taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar (Institute of Marine Sciences) kampasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iii) inaendelea na ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kwa kila bweni na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,500 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa. Ujenzi wa majengo hayo umefikia asilimia 10. Aidha, imekamilisha ujenzi wa maabara katika chuo hicho;

(iv) imekamilisha ujenzi wa jengo mtambuka lenye maabara nane, ofisi saba, madarasa nane, vyumba 11 vya maandalizi na stoo saba katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Aidha, imeanza taratibu za kupata hati miliki kwa ajili ya ujenzi wa kampasi ya chuo hicho katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Mkoa wa Ruvuma;

(v) inaendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wasomaji 2,500 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi umefikia asilimia 8.9 katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa jengo la ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia jumla ya wanafunzi 2,334 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi umefikia asilimia 46.6 na imekamilisha ukarabati wa jengo la utawala;

(vi) inaendelea na ujenzi wa kituo cha kudhibiti viumbe waharibifu (African Centre of Excellence Eastern and Southern Innovative Rodent Pest Management and Biosensor Technology Development) kilichopo Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ambapo ujenzi umefikia asilimia 50;

(vii) imekamilisha ukarabati wa vyumba vya madarasa 30, mabweni mawili, maabara, ofisi saba, nyumba 10 na miundombinu ya TEHAMA katika Chuo Kikuu Ardhi. Vilevile,

inaendelea na upanuzi wa jengo la Ardhi (Lands building) linalojumuisha studio nne zitakazokuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 160 kwa wakati mmoja, madarasa mawili yatakayokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 kila moja kwa wakati mmoja, ofisi tano za watumishi 10 ambapo ujenzi umefikia asilimia 15 katika chuo hicho;

(viii) imekarabati Maabara za Sayansi katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST) na kuwezesha ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) Kampasi ya Pemba;

(ix) imeendelea na ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 180 kwa wakati mmoja vikiwemo vyumba maalum viwili kwa ajili ya wanafunzi wa kike wenye watoto wanaonyonya katika Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia. Ujenzi huo umefikia asilimia 43;

(x) imeendelea na ujenzi wa madarasa matano na mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 160 kwa wakati mmoja katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam. Vilevile, imeanza ujenzi wa mabweni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kwa wakati mmoja katika Kampasi ya Mwanza kwa lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi; na

(xi) imeendelea na ujenzi wa hosteli mbili katika Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi umefikia asilimia 48.

**g. Kuimarisha Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa Maendeleo ya Taifa**

**65. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuchochea maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu nchini kwa lengo

la kuchangia maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa wabunifu wachanga 83 na rasilimali fedha kwa wabunifu 27 walioibuliwa katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) mwaka 2022 kwa lengo la kuendeleza bunifu na teknolojia ili zifikie hatua ya ubiasharishaji;

(ii) imefuatilia na kutathmini uendelezaji wa wabunifu waliotokana na MAKISATU mwaka 2019, 2020 na 2021 wanaoendelezwa na serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Bunifu 38 kati ya 283 zinazoendelezwa zimeshafikia hatua ya kuingia sokoni. Baadhi ya bunifu hizo ni pamoja na: Mita ya kulipia maji kabla ya matumizi (pre-paid water meter) kwa kutumia kadi Janja; trekta ndogo inayoendeshwa na injini ya pikipiki; mtambo wa umwagiliaji unaoendeshwa kwa kutumia simu ya kiganjani (smart irrigation system); ugunduzi wa kiatilifu kinachotumia vimeng'enya vya asilia (Biopesticide);

(iii) imetambua teknolojia mpya 27 zilizozalishwa nchini na hivyo kufanya jumla ya teknolojia zilizotambuliwa nchini hadi sasa kufikia 506. Lengo la utambuzi huo ni kuwa na kanzidata ya kitaifa kwa ajili ya rejea kuhusu taarifa za teknolojia na ubunifu zinazozalishwa nchini;

(iv) imeratibu mkutano wa wadau wa sayansi, teknolojia na ubunifu wakiwemo watanzania wanaoishi nje ya nchi (The First Multistakeholder and Diaspora Forum on Science Technology and Innovation). Mkutano huo ulifanyika kwa njia ya mtandao (zoom) na uliazimia mikakati ya pamoja ya kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi pamoja na watanzania wanaoishi nje ya nchi katika kubaini fursa za kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu;

(v) imeratibu maandalizi ya wiki ya ubunifu na maonesho ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa mwaka 2023 kwa lengo la kutambua na kuendeleza jitihada zinazofanywa na watafiti na wabunifu wa kitanzania na kuhamasisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, Wiki ya Ubunifu ya mwaka huu pamoja taasisi za Elimu, utafiti na maendeleo ilihusisha washiriki kutoka Jamhuri ya Afrika Kusini, Wizara za Kisekta, Kampuni za teknolojia, na maonesho ya bidhaa halisi za teknolojia na ubunifu badala ya sampuli kifani;

(vi) imeanza utekelezaji wa mradi wa ubunifu wa utengenezaji wa vifaa vya maabara itakavyotengenezwa hapa nchini kwa ajili ya shule. Mradi utachangia upatikanaji wa vifaa vya maabara kwa bei nafuu ambapo kwa sasa utekelezaji umefikia asilimia 60; na

(vii) imeratibu maadhimisho ya Siku Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi (Women and Girls in Science) yaliyofanyika tarehe 11 Februari, 2023 kwa lengo la kuhamasisha na kuongeza ushiriki wa wanawake na wasichana katika masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Katika maadhimisho hayo zaidi ya wanawake na wasichana 1,500 walishiriki.

**66. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kubidhaisha teknolojia na ubunifu kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali za kijamii na kuongeza ufanisi katika kuchangia maendeleo ya nchi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa mwongozo na programu ya simu ijulikanayo kama **"Kilimo cha Kisasa Mkononi Mwako**" na programu hiyo inapatikana katika Google play store kwa jina la "Mboga App" kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Mwongozo huo unamwezesha mwananchi kuanzisha kilimo cha mbogamboga kwa kutumia teknolojia za kisasa;

(ii) imeendeleza ubunifu wa Prepaid Water Meter kwa kutengeneza na kufunga mita 20 kwa majaribio katika Wilaya 10 za mikoa mitano ambapo kila Wilaya ilipata mita mbili kama ifuatavyo: Tanga (Handeni na Pangani), Morogoro (Morogoro Vijijini na Mvomero), Pwani (Bagamoyo na Mkuranga), Iringa (Iringa Vijijini na Mufindi), na Njombe (Makete na Wanging"ombe).
Ubunifu huo utawezesha udhibiti wa matumizi ya maji na ukusanyaji wa mapato;

(iii) imewezesha kampuni changa mbili za Teknolojia na Ubunifu ambao ni **'Smart Darasa** na **Dawa Mkononi'** kushiriki katika shindano la ubunifu ambalo lilifanyika nchini Afrika Kusini lenye lengo la kuendeleza ubunifu. Aidha, shindano hilo lilishirikisha waanzilishi 13 kutoka Namibia, Afrika Kusini, Botswana na Zambia ambapo ubunifu wa **„Dawa Mkononi'** kutoka Tanzania uliibuka mshindi wa pili; na

(iv) imepima jumla ya sampuli 743 kutoka kwa wakulima na watafiti kama ifuatavyo: sampuli za udongo 333, mbolea za viwandani mbili, maji 11, na mimea 397 ili kuongeza tija ya uzalishaji katika kilimo.

**67. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imeendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya mionzi ya nyuklia nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imepima sampuli 21,583 za vyakula, mbolea, tumbaku na bidhaa nyingine kati ya 28,000 zilizolengwa kupimwa kutoka mipakani, viwanja vya ndege na bandari ambapo kipimo kilionesha kuwa hakuna uchafuzi wa mionzi. Aidha, imefungua ofisi za udhibiti wa mionzi katika Kanda ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini, pamoja na mkoa wa Tabora, Katavi na Morogoro kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi;

(ii) imekagua vituo 184 vyenye vyanzo vya mionzi ambapo vituo 168 vilikuwa katika hifadhidata na vituo vipya 16 kwa lengo la kuhakikisha uwepo wa usalama kwa watumiaji;

(iii) imepima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,062 wanaofanya kazi katika vituo 426 vyenye vyanzo vya mionzi nchini kwa lengo la kuendelea kuimarisha usalama wa wafanyakazi katika maeneo yenye vyanzo vya mionzi. Vilevile, imepima viwango vya mionzi katika mazingira kwenye vituo 29 nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa teknolojia ya nyuklia inatumika bila kuhatarisha usalama wa mazingira; na imefanya ukaguzi wa vituo 42 vinavyotumia vyanzo vya mionzi isiyoayonisha (Non – Ionizing Radiation) kwa lengo la kuendelea kubaini na kuimarisha usalama wa wakazi wa maeneo husika;

(iv) imepima sampuli za hewa na kichungi safi cha Germanium kupitia kituo cha kupima uchafuzi wa hewa katika anga unaotokana na majaribio ya silaha za nyuklia chini ya mkataba wa kimataifa wa Comprehensive Nuclear Test - Ban Treaty (CTBT) for Non - Proliferation Test (NPT) of nuclear weapons ambapo takwimu za spectrometry zilionesha kuwa hapakuwa na majaribio ya nyuklia;

(v) imetoa jumla ya leseni 314 ambapo leseni 220 za kumiliki na kutumia vyanzo vya mionzi, 62 za uingizaji (import); saba za kupeleka nje ya nchi (export); na leseni 25 kwa ajili ya usafirishaji wa mionzi. Vilevile, imesajili vituo 43 vinavyotumia vyanzo vya mionzi kwa lengo la kuendelea kuongeza wigo wa matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia nchini; na

(vi) imeendelea na ujenzi wa ofisi na maabara ya mradi wa kuhifadhi mazao ya kilimo ikiwemo vyakula viharibikavyo kirahisi, vifaa tiba na vya viwandani Dar es Salaam kwa kutumia teknolojia ya mionzi ambapo ujenzi umefikia asilimia 63. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa ofisi na maabara za kupima mionzi katika kanda ya Arusha, Dodoma, Mwanza na

Zanzibar ambapo Arusha na Dodoma ujenzi umefikia asilimia 99, maabara Mwanza asilimia 86; ofisi Mwanza asilimia 84 na maabara Zanzibar asilimia 75.

**h. Kuimarisha na Kuendeleza Tafiti na Matumizi ya Matokeo yake katika Ajenda ya Maendeleo**

**68. Mheshimiwa Spika,** Serikali inatambua umuhimu wa utafiti na matumizi yake katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii na kuchangia maendeleo ya nchi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa ndani wa kufanya utafiti na kutumia matokeo ya utafiti kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imegharamia utafiti katika maeneo 21 ya sekta ya Mazingira, Usindikaji wa Mazao ya Kilimo na Mifugo, TEHAMA, Uvuvi, Maliasili na Afya kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia (MTUSATE);

(ii) imetoa mafunzo kwa viongozi 21 kuhusu uendelezaji na utekelezaji wa Kigoda cha Utafiti (Research Chair) kutoka katika Taasisi za Utafiti na Vyuo Vikuu, Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar, Tume ya Mipango - ZPC na Sekta Binafsi (Bakhresa group na TANOIL) ili kubaini na kuimarisha utafiti katika maeneo ya Uchumi wa Bluu, Uchumi wa Kidijiti, Kilimo, Chakula, Lishe na sekta ya Afya na mabadiliko ya miundo;

(iii) imeendeleza vigoda vya utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela. Vigoda hivyo vimelenga kutengeneza chanjo ya malaria na magonjwa ya mlipuko yanayoambukizwa na Wanyama;

(iv) imetoa machapisho 1,836 kupitia Taasisi za Elimu ya Juu katika majarida ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kuchangia katika kuvitangaza (Visibility) Vyuo hivyo; na

(v) imeandaa Mwongozo wa Uhawilishaji wa Teknolojia; Mwongozo wa Uendeshaji wa Kamati za Maadili ya Utafiti katika Taasisi; na Mwongozo wa Kitaifa wa Kujumuisha Masuala ya Jinsia (National Framework for Gender Mainstreaming) katika utafiti na ubunifu. Miongozo hiyo inalenga kuboresha uratibu, uendeshaji, usimamizi na ushirikishwaji katika masuala ya utafiti na ubunifu nchini.

**69. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuanzisha, kuratibu na kusimamia miradi mbalimbali ya utafiti na ubunifu katika taasisi za Elimu ya Juu na Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuongeza maarifa na kutatua changamoto katika jamii. Azma hiyo imefikiwa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imefanya miradi ya utafiti 418 kati ya 252 iliyolengwa kufanyika katika Vyuo Vikuu, Vyuo Vikuu Vishiriki na Taasisi za Utafiti na Maendeleo. Aidha, imetoa vibali 219 vya utafiti katika maeneo ya Sayansi, Afya, Kilimo, Mifugo, Sayansi ya Jamii, Uhandisi, TEHAMA, Uvuvi na Sanaa;

(ii) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 10 ya utafiti katika Sekta ya Maji, Afya, Kilimo na Mifugo inayofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) na kuratibiwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Lengo lilikuwa ni kubaini endapo utekelezaji wa miradi hiyo unafanyika kulingana na makubaliano; na

(iii) imeratibu na kusimamia utendaji wa mradi wa vituo vinne vya umahiri "African Centres of Excellence (ACE – II)" unaotekelezwa katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia. Lengo la kuanzishwa kwa vituo hivyo ni kujenga uwezo wa utoaji wa Elimu ya Juu na kufanya utafiti katika masuala ya Afya na Baiolojia ya Molekuli; Kilimo; Maji na Nishati Jadidifu.

**70. Mheshimiwa Spika,** ili kuhamasisha wataalamu kuandika na kuchapisha kazi za utafiti, Serikali imeandaa Mwongozo

wa Utoaji Tuzo kwa Watafiti watakao chapisha utafiti wao katika Majarida yenye hadhi ya Kimataifa „High Impact Factor Jounals‟ katika Fani za Sayansi Asilia na Tiba.

**D. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**71. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa washiriki 23 kutoka vyombo vya habari, wawakilishi wa Serikali kutoka Idara ya Habari Maelezo na wanachuo kutoka chuo Kikuu cha SUZA kuhusu nafasi ya vyombo vya habari katika kukuza utawala wa haki na sheria;

(ii) imeratibu mkutano wa uhamasishaji wa kupinga mila potofu hususan ukeketaji kwa wanawake kwa Washiriki 33 katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang‟ mkoani Manyara;

(iii) imeendesha warsha ya kuwajengea uwezo Viongozi wa Kata katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuhusu usawa wa kijinsia katika muktadha wa elimu ya uraia wa kidunia (Global Citizenship Education);

(iv) imeratibu mafunzo dhidi ya mapambano ya matumizi ya dawa za kuongeza nguvu na mbinu haramu michezoni kwa kushirikiana na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo washiriki 230 wakiwemo wakufunzi, viongozi wa michezo, wanamichezo na watunga sera walishiriki;

(v) imenunua samani za ofisi za watumishi 20 wapya; na inaendelea na hatua za mwisho za kusimika Mfumo wa Serikali Mtandao (e-GA);

(vi) imetathmini utekelezaji wa mkataba unaohusu urithi wa utamaduni usioshikika (Mkataba wa UNESCO wa 2003) ambapo matokeo ya tathmini hiyo yalipendekeza Mwenge

wa Uhuru, sherehe za kimila za mwaka – Kogwa (Tambiko la kimila linalofanyika kila mwaka Makunduchi, Zanzibar) kuwa sehemu ya urithi usioshikika;

(vii) inaendelea na tathmini ya mpango wa kujumuisha eneo la "Speak Gulf" kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuwa chanzo kikuu cha maji wakati wa kiangazi ukiacha Mto Mara;

(viii) imeshirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Ufaransa na Mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika UNESCO kuratibu maadhimisho ya siku ya Kiswahili Duniani yaliyofanyika kwa mara ya kwanza katika Makao Makuu ya UNESCO nchini Ufaransa tarehe 7 Julai, 2022; na

(ix) imeendelea kufanya utambuzi wa Taasisi zinazokidhi vigezo vya kujiunga na Mitandao ya Elimu ya UNESCO. Vilevile, imehuisha mikataba minne inayohusiana na Elimu ya Juu.

## E. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**72. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vitano vyenye lengo la kuongeza ubora wa elimu, kuwezesha vijana wa Kitanzania kupata maarifa, ujuzi, kujiamini, kujiajiri na kuajirika.

**73. Mheshimiwa Spika**, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/24 ni kama vifuatavyo:

(i) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu na kuanza utekelezaji;

(ii) Kuongeza fursa na ubora wa mafunzo ya amali (Ufundi) katika elimu ya sekondari na vyuo vya Kati vya Amali;

(iii) Kuongeza fursa na ubora wa Elimu ya Msingi na Sekondari;

(iv) Kuongeza fursa na ubora wa Elimu ya Juu; na

(v) Kuimarisha uwezo wa nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

**a. Kukamilisha Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu**

**74. Mheshimiwa Spika,** Serikali itakamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu na kuanza utekelezaji wake kwa lengo la kuimarisha maarifa na ujuzi kwa wahitimu wa ngazi zote za elimu. Sambamba na kukamilisha mapitio ya sera na mitaala ya elimu, Serikali itatekeleza yafuatavyo:

(i) itafanya mapitio na marekebisho ya sheria ya elimu kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 na sheria mbalimbali za Taasisi za Elimu ili iendane na mahitaji ya toleo jipya la sera pamoja na mitaala; na

(ii) itaandaa Mwongozo wa Chakula na Lishe pamoja na Mwongozo wa Utunzaji wa Mazingira katika Taasisi za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa lengo la kuhakikisha kuwa viwango vya utolewaji wa chakula katika vyuo vinatekelezwa ipasavyo na watoa huduma.

**b. Kuongeza Fursa na Ubora wa Mafunzo ya Amali (Ufundi na Ufundi Stadi) kwa Sekondari na Vyuo vya Kati vya Amali**

**75. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuboresha mafunzo ya Amali (Ufundi na Ufundi Stadi) kwa shule za sekondari na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ukarabati shule za sekondari za ufundi na kuzipatia vifaa vya kujifunzia na kufundishia; Aidha, itaendelea kukiwezesha Chuo cha Ualimu Kleruu na Mtwara Ufundi kuendelea kutoa mafunzo ya ualimu wa ufundi kwa lengo la kuongeza walimu wa ufundi nchini;

(ii) itaboresha vyuo vya ualimu 10 ikiwa ni pamoja na chuo cha ualimu Mtwara Kawaida na Mtwara ufundi na kuwawezesha walimu tarajali kupata mafunzo ya Shahada ya Amali kwa kutumia wahitimu wa Vyuo vya Ufundi (TET) na Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
Stadi (VET); na

(iii) itajenga karakana 10 na kuweka mitambo na vifaa katika vyuo vya ualimu ambavyo ni: Kitangali, Ndala, Nachingwea, Kleruu, Mtwara (U), Mpwapwa, Korogwe, Dakawa, Bunda na Kabanga kwa lengo la kuimarisha utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi kwa vitendo.

**76. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuongeza fursa za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini kwa kuendelea kusajili na kudahili wanafunzi katika vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Katika kufikia azma hiyo, yafuatayo yatatekelezwa:

(i) itasajili vyuo 130 vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na hivyo kuwa na jumla ya vyuo 485 vya elimu ya ufundi na vyuo 973 vya mafunzo ya ufundi stadi ambavyo vitaongeza idadi ya wanachuo kutoka 380,748 hadi kufikia 680,000. Aidha, usajili wa vyuo hivyo utaongeza fursa ya mafunzo kutoka kwa wahitimu katika ngazi mbalimbali za elimu pamoja na mwananchi yeyote anayejua kusoma na kuandika kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajirika;

(ii) itaongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 51,382 hadi 66,459

wakiwemo 5,000 kutoka kwenye mazingira magumu; 1,500 wenye mahitaji maalum; na wajasiriamali 2,000 watakaopatiwa mafunzo kupitia programu ya INTEP; na

(iii) itadahili wanafunzi 660 katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro – MVTTC kwa lengo la kuongeza idadi ya walimu wanaofundisha katika Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi.

**77. Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia ubora wa Mafunzo ya Amali (Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi), Serikali itaendelea kusimamia kikamilifu shughuli za ithibati, uhakiki wa mitaala na tathmini kwa taasisi na vyuo vya elimu ya ufundi ili ziwe na ubora unaokubalika kitaifa na kimataifa. Katika kufikia azma hiyo Serikali kupitia Baraza la Taifa ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi itatekeleza yafuatayo:

(i) itatoa ithibati kwa vyuo 70 vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa lengo la kuwezesha vyuo kukidhi viwango vya utoaji wa elimu bora;

(ii) itafanya ufuatiliaji, uthibiti na tathmini kwa vyuo 400 vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na kuhakiki mitaala 230 ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuthibiti ubora wa elimu na mafunzo;

(iii) itahakiki udahili wa wanafunzi 250,000 wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Aidha, udahili huu utaongeza kiasi kikubwa cha rasilimaliwatu yenye weledi wa kutumika katika uzalishaji viwandani; na

(iv) itaongeza idadi ya walimu wa amali (mafunzo ya ufundi stadi) katika taasisi za umma kutoka 788 hadi 900 ili kukidhi mahitaji ya walimu wa masomo ya ufundi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuwajengea umahiri walimu wa vyuo vya Elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuinua ubora wa mafunzo yatolewayo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itatoa mafunzo kwa walimu takribani 1,300 wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kuhusu ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri (CBET) kwa lengo la kuwa na walimu mahiri watakaotoa mafunzo kwa wanachuo ili waweze kujiajiri na kuajirika; na

(ii) itatoa mafunzo kwa wakufunzi 150 wa Taasisi za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa lengo la kuwaongezea uwezo wa ufundishaji wa mitaala inayoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko la ajira.

**78. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ujuzi kwa watumishi wanaofanya kazi viwandani, Serikali itaendelea kutekeleza programu ya uimarishaji wa ujuzi (Skills Enhancement Programme - SEP) katika makampuni 12. Vilevile, itatoa mafunzo kwa wanagenzi 18,000 kutoka sekta isiyo rasmi na kuwezesha mafunzo ya uanagenzi katika vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi vya mikoa minne.

**79. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu ya Ufundi Stadi kwa washiriki 17,000 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuwawezesha kupata ujuzi na maarifa ya kujiajiri au kuajiriwa.

**80. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia katika utoaji wa mafunzo ya amali kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itandaa Miongozo miwili ambayo ni Technology Transfer Manual na Technology commercialization Framework

itakayosaidia katika uingizaji teknolojia sokoni na uhawilishaji katika matumizi;

(ii) itakamilisha uanzishaji wa programu nne mpya za Ngozi kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ambazo ni:Textile Technology, Fashion and Design Technology, Bio Processing Technology and Post Harvesting Technology kwa lengo la kuzalisha wataalam; na

(iii) itawezesha upatikanaji wa ekari 200 za ardhi kwa ajili ya upanuzi wa kampasi ya Myunga – Songwe ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) pamoja na ununuzi wa basi kwa ajili ya kuwezesha mafunzo viwandani katika kampasi hiyo.

**81. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini inatolewa kwa vitendo kwa lengo la kukuza na kuendeleza ujuzi na umahiri. Katika kufikia azma hiyo itatekeleza yafuatayo:

(i) itarasimisha ushirikiano na taasisi/mashirikia 60 kutoka sekta rasmi kwa lengo la kuongeza fursa kwa wanafunzi na walimu wa elimu ya mafunzo ya ufundi stadi ili kuwezesha wanafunzi kupata mafunzo kwa vitendo katika maeneo ya kazi;

(ii) itanunua vifaa vya kisasa vitakavyotumika katika maabara ya udongo, maji na mimea katika Chuo cha Ufundi Arusha ili kuongeza uzalishaji na utoaji wa ushauri wa kitaalamu; na

(iii) itaongeza ushirikiano na wadau mbalimbali wa kitaifa na kimataifa kama ifuatavyo: ndani ya nchi kutoka 23 hadi 26; kanda ya Afrika Mashariki kutoka 42 hadi 44 na kimataifa kutoka 39 hadi 43 kupitia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela.

**82. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa inawezesha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itanunua vifaa vya msingi vya mafunzo ya Ufundi Stadi katika vyuo vitano ambavyo ni; Mwanza, Newala, Ndolage, Songea na Makete kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo na kukuza ujuzi;

(ii) itanunua na kusambaza kompyuta 700 katika vyuo vya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa ajili ya kuimarisha mafunzo ya TEHAMA, pamoja na kukamilisha uunganishaji wa mfumo wa mawasiliano ndani na nje; na

(iii) itanunua vifaa vya kisasa vya maabara ili kuboresha utoaji wa mafunzo katika fani za Sayansi na Teknolojia ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya.

**83. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuwakutanisha wadau wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi ili kubadilishana uzoefu na kupendekeza namna bora ya kuendeleza ubunifu unaopatikana nchini.

**84. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi 64 katika wilaya ambazo hazina vyuo hivyo pamoja na ujenzi wa Chuo cha Mkoa wa Songwe na itaanza kutoa mafunzo ya amali katika vyuo 29 vilivyokamilika. Vilevile, itakamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya Chuo cha Ufundi Dodoma ambapo kukamilika kwa awamu hiyo kutawezesha kudahili wanafunzi 1,500.

**85. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi na kuboresha miundombinu ya vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaanza ujenzi wa jengo la ofisi ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi - NACTVET na jengo la ofisi ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi – VET jijini Dodoma ili kuondoa gharama za pango;

(ii) itaendelea na ujenzi wa vyuo vipya vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika Wilaya ya Kigamboni na Karagwe. Aidha, itaongeza miundombinu mbalimbali katika vyuo sita vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kama ifuatavyo: Mabweni mawili, bwalo la chakula na nyumba ya mtumishi katika Chuo cha Namtumbo; Mabweni, nyumba ya mkuu wa chuo, bwalo na jiko katika Chuo cha Ileje; Karakana nne kwa ajili ya fani ya umeme, ufundi bomba, ufundi magari na ujenzi katika Chuo cha Kihonda; Madarasa, jengo la utawala, nyumba mbili za watumishi, karakana ya kompyuta, uchomeleaji na uungaji vyuma, kibanda cha mlinzi na bweni katika Chuo cha Oljoro – Arusha; Mabweni mawili, bwalo na jiko katika Chuo cha Kanadi; Bweni na nyumba mbili katika Chuo cha Nyamidaho;

(iii) itakamilisha ujenzi wa kafeteria na uwekaji wa mfumo wa usambazaji wa maji safi kwenye nyumba za watumishi katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro na maabara ya sayansi katika chuo cha VETA mkoa wa Lindi;

(iv) itaanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa maktaba ya kisasa katika Chuo cha Ufundi Arusha itakayokuwa na uwezo wa kuhudumia watumiaji 1,500 kwa wakati mmoja;

(v) itaanza ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia nguvu za maji (turbine) katika Kituo cha Mafunzo Kikuletwa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vitendo katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(vi) itakamilisha ujenzi wa miundombinu katika chuo cha ufundi Arusha kama ifuatavyo: madarasa matano; mabweni mawili; ukumbi wa mihadhara; karakana tatu; maabara; jengo la makazi linaloweza kutumiwa na watumishi 10; jengo la utawala; maktaba; chumba cha usanifu; na ukumbi wa mikutano. Vilevile, itaongeza miundombinu katika kituo cha mafunzo Kikuletwa na kuweka vifaa tiba vya kutolea huduma za afya katika Hospitali ambayo itatumika na wanafunzi wa programu ya vifaa tiba (Biomedical) kwa mazoezi ya vitendo sambamba na kutoa huduma za afya kwa wanafunzi, wafanyakazi na wananchi wa maeneo ya jirani;

(vii) itaendelea na ujenzi katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kama ifuatavyo: mabweni mawili ya wanafunzi katika Kampasi ya Karume Zanzibar yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,536 (wanaume 768 na wanawake 768); maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 na ukumbi wa mihadhara utakaohudumia wanafunzi 1,000 kwa mara moja katika Kampasi ya Kivukoni; jengo la utawala na madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,800 katika kampasi ya Pemba. Vilevile, itagharamia mradi wa hosteli ya wanafunzi katika majengo yaliyokuwa ya NSSF Kijichi pamoja na kuanza ujenzi wa kumbi za mihadhara na ofisi za wahadhiri katika Kampasi ya Kivukoni na ukarabati wa miundombinu chakavu ya majitaka, umeme, barabara na majengo;

(viii) itakamilisha ujenzi katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kama ifuatavyo: Hosteli mbili za wanafunzi zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 800 kwa wakati mmoja na uwekaji wa samani; jengo la kitaaluma, karakana mbili, jengo la utawala na kituo cha ubunifu na uhaulishaji wa Teknolojia katika kampasi kuu ya Mbeya; jengo la kitaaluma na karakana katika kampasi ya Rukwa;

(ix) itajenga miundombinu katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kama ifuatavyo: maabara tisa zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 360 kwa wakati mmoja; vyumba vya mihadhara vine vyenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 400 kwa wakati mmoja; Madarasa matano yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 200 kwa wakati mmoja; chumba cha mikutano chenye uwezo wa kuhudumia watu 55, ofisi 52 zenye uwezo wa kuhudumia watumishi 98; chumba cha ubunifu chenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 63; ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuhudumia watu 400; mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 (wanawake 150 na wanaume 150). Vilevile, itakarabati mabweni sita, bwalo pamoja na miundombinu ya maji taka;

(x) itajenga miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika kampasi ya DIT-Mwanza kama ifuatavyo: ukumbi wa mhadhara wenye uwezo wa kuchukuwa wanafunzi 1,500 kwa wakati mmoja; kiwanda cha kuchakata ngozi chenye uwezo wa kuchakata ngozi 50 kwa siku, kutengeneza jozi 100 za viatu kwa siku pamoja na bidhaa nyingine kama pochi, mikanda na mipira ya miguu; jengo kwa ajili ya ujasiriamali, ubunifu na uhaulishaji wa teknolojia; na jengo la kufundishia (Teaching Complex); na

(xi) itakarabati na kuboresha karakana nne katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro; miundombinu ya jiko ili kuwezesha matumizi ya nishati ya gesi katika chuo cha VETA Moshi, Mara, na Pwani. Vilevile, itakamilisha ukarabati wa chuo cha Elimu ya Ufundi na Mafunzo Stadi Dodoma, Dar es Salaam, Dakawa, Mikumi, Mwanza, Kigoma, Mtwara, Wanging"ombe, Kitangiri na Chuo cha Ufundi cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii – Njiro.

**86. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendeleza dhana ya mafunzo viwandani (Teaching factory) itakayowezesha wahitimu katika kila ngazi kupata ujuzi wa kujiajiri kupitia mafunzo katika viwanda vya kufundishia. Katika kutekeleza

azma hii, Serikali itakamilisha ujenzi wa kiwanda cha vipuri vya Bajaji, Fuso na Pikipiki katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam.

**b. Kuwezesha Ongezeko la Fursa na Ubora wa Elimu ya Msingi na Sekondari**

**88. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuongeza fursa za Elimu kwa kutoa ithibati kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itasajili shule za msingi na sekondari takribani 560 ambapo awali pekee 20, awali na msingi 380 (Serikali 250 na zisizo za Serikali 130), sekondari 165 (Serikali 135 na zisizo za Serikali 30), chuo cha ualimu kimoja cha binafsi na nyingine kwa kuzingatia maombi yatakayowasilishwa na kukidhi vigezo; na

(ii) itaanza kusajili shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuwafikia wadau wengi zaidi.

**89. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutoa fursa za elimu na mafunzo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, kutoa ushauri pamoja na utoaji wa mafunzo kazini. Katika kufikia azma hiyo Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itanunua na kusambaza zana na vifaa saidizi kwa wakufunzi, walimu na walimu tarajali wenye mahitaji maalum ili kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa elimu maalumu; na

(ii) itafanya ufuatiliaji na tathmini katika shule zinazopokea wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalamu. Aidha, itatoa mafunzo kwa waangalizi wa wanafunzi ili kuongeza ubora wa huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**90. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mifumo ya ukusanyaji takwimu za walimu, matumizi ya teknolojia na tathmini ya hali ya ufundishaji na ujifunzaji Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya tathmini ya mifumo ya ukusanyaji wa takwimu za walimu ili kuwa na mfumo thabiti utakaosaidia uimarishaji wa mipango na ufuatiliaji wa masuala anuai ya walimu nchini;

(ii) itafanya tathmini ya kubaini teknolojia za elimu zilizopo na matumizi yake katika kufundishia na kujifunzia na kuchagua teknolojia ambazo zitaboreshwa ili ziweze kuendana na mazingira ya kitanzania. Aidha, itaandaa Mwongozo Jumuishi wa Teknolojia husika kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji nchini; na

(iii) itaandaa mwongozo na zana za upimaji wa ujifunzaji wa wanafunzi wa madarasa ya awali (early grade) kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji.

**91. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kubaini na kukuza vipaji vya uandishi unaozingatia ubunifu kwa lengo la kujenga tabia ya kujisomea, kuhifadhi historia, amali za jamii pamoja na kuimarisha vipaji vya sanaa na michezo. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itasimamia utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi unaozingatia ubunifu wenye lengo la kuwatambua na kuwazawadia waandishi mahiri katika nyanja za riwaya, hadithi fupi na ushairi kwa lengo la kukuza sekta ya uchapishaji na kuongeza hifadhi ya vitabu katika maktaba zetu nchini,

(ii) itaratibu mashindano ya uandishi wa insha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini

mwa Afrika ili kukuza ujuzi wa uandishi (writing skills) kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini; na

(iii) itaendelea kuratibu mashindano ya Michezo na Sanaa kwa Vyuo vya Ualimu Tanzania (UMISAVUTA) kwa lengo la kuibua, kuendeleza na kuimarisha vipaji vya sanaa na michezo kwa wanachuo.

**92. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uthibiti ubora wa elimu katika ngazi ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaimarisha mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule kwa kufanya ugatuaji kutoka ngazi ya kanda kwenda ngazi ya mikoa kwa ajili ya kusogeza huduma karibu na wadau na kuzifikia asasi nyingi;

(ii) itafanya tathmini ya jumla katika nyanja zifuatazo: mafanikio ya wanafunzi; ubora wa ufundishaji kwa ujifunzaji na upimaji; ubora wa uongozi na utawala; ubora na mazingira ya shule na matokeo yake katika ustawi, afya na usalama wa wanafunzi na ushiriki wa jamii katika asasi takribani 6,700 (shule za Awali na Msingi 5,220, Sekondari 1,422; na Vyuo vya Ualimu 58) kwa lengo la kutoa ushauri na mapendekezo kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;

(iii) itafanya tathmini ya ufuatiliaji katika asasi 1,280 (Awali na Msingi 1,021; Sekondari 253; na Vyuo vya Ualimu 6) zilizopata matokeo yasioridhisha wakati wa tathmini ya jumla ili kubaini hali ya utekelezaji wa ushauri na mapendekezo yaliyotolewa katika tathmini ya jumla;

(iv) itanunua magari 12 na kuweka samani katika ofisi 195 za uthibiti ubora wa shule kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji wa kazi;

(v) itaendelea kuimarisha mfumo wa uthibiti ubora wa ndani ya shule kwa kuandaa moduli ya Uthibiti Ubora wa Shule kwa lengo la kuimarisha mfumo wa taarifa za Uthibiti Ubora wa Shule kuanzia ngazi ya shule na kuwezesha upatikanaji wa taarifa; na

(vi) itafanya mapitio ya kiunzi cha uthibiti ubora wa shule na zana zake pamoja na kutoa mafunzo kwa Wathibiti Ubora wa Shule kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wao.

**93. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha matokeo ya ujifunzaji na ufaulu wa wanafunzi, Serikali itaendelea kuwajengea uwezo walimu wanaofundisha katika shule za msingi, sekondari pamoja na wathibiti ubora wa shule kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itatoa mafunzo kwa walimu 10,000 wa masomo ya Sayansi na Hisabati wa shule za sekondari Kidato cha 1 – 4; mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 4,500 wa shule za sekondari 1,300; mafunzo kuhusu programu ya shule salama kwa wakuu wa shule za Sekondari na Wathibiti Ubora wa Shule 1,378; mafunzo kuhusu unasihi na ulinzi wa mtoto kwa walimu 3,370 wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu; mafunzo kuhusu ufundishaji wa moduli za masomo 18 hatua ya I na II kwa walimu 600 kutoka katika vituo 151 vya Elimu kwa Njia Mbadala kwa lengo la kuongeza umahiri na kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji; na

(ii) itaendelea kuwajengea uwezo walimu 12,000 wa shule za msingi katika upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika mikoa 10 iliyokuwa na wastani wa chini wa stadi hizo kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

**94. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha Elimu ya Ualimu, Serikali itaendelea kuimarisha maandalizi ya walimu tarajali katika vyuo vya Ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itatoa mafunzo kwa vitendo kwa wanachuo wa Vyuo vya Ualimu zaidi ya 17,000 kwa lengo la kuhakikisha walimu tarajali wanapata stadi stahiki za ufundishaji na ujifunzaji;

(ii) itatoa mafunzo kazini kwa wakufunzi 250 katika Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali kuhusu TEHAMA, mbinu shirikishi, usawa wa kijinsia kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu ya ualimu; na

(iii) itanunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na vifaa vya maabara na kemikali katika Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali.

**95. Mheshimiwa Spika,** Serikali itakamilisha uandaaji wa mitaala ili kuendana na mahitaji ya sasa na kuwezesha wahitimu kuwa na ujuzi na maarifa stahiki kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaidhinisha mitaala minne na mihtasari 70 ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari Kidato cha 1-6. Aidha, itaidhinisha mitaala mitatu na mihtasari 15 ya elimu ya ualimu ili kukidhi mahitaji ya sasa katika elimu; Vilevile itaboresha na kuidhinisha mitaala na mihtasari rekebifu kwa ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari Kidato cha 1 - 4 kwa lengo la kuwezesha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kujifunza kwa umahiri;

(ii) itaandaa miongozo ya wawezeshaji kuhusu utekelezaji wa mitaala mipya kwa walimu wa ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na wakufunzi wa vyuo vya ualimu ili kuwawezesha kutekeleza mitaala kwa ufanisi;

(iii) itaandaa miongozo ya kufanya tathmini endelevu ili kuwawezesha walimu wa ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari kukuza umahiri wa wanafunzi wa ngazi husika katika kujifunza; na

(iv) itaandaa moduli za mafunzo kazini kwa walimu ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na wakufunzi wa elimu ya ualimu ili kukuza umahiri wa uchambuaji wa vipengele vya mitaala na utekelezaji wake.

**96. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari kwa lengo la kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi na hivyo kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na kujenga tabia ya kujisomea. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itachapa na kusambaza vitabu vya kiada na kiongozi cha Mwalimu kwa Elimu ya Awali nakala 6 kwa shule zinazotumia Kiswahili na nakala 6 kwa shule zinazotumia Kiingereza; Darasa la kwanza nakala 6 kwa shule zinazotumia Kiswahili na nakala 6 kwa shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia; Darasa la III nakala 12 kwa shule zinazotumia Kiswahili na nakala 12 kwa shule zinazotumia Kiingereza; vitabu vya kiada nakala 31 na Kiongozi cha Mwalimu nakala 31 kwa Kidato cha 1; vitabu vya kiada nakala 29 na Kiongozi cha Mwalimu nakala 29 kwa kidato cha 5;

(ii) itachapa na kusambaza vitabu vya kiada kama ifuatavyo: Elimu ya Awali masomo 12, Darasa la I na II masomo 24, Darasa la III masomo 24, Sekondari Kidato cha 1- 4 masomo 31; na Kiongozi cha Mwalimu nakala 108 na miongozo 42 ya kufundishia Elimu ya Awali, Darasa la I na II, Darasa la III hadi la VI na Sekondari Kidato cha 1 - 4;

(iii) itachapa na kusambaza vitabu vya kiada katika maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya Elimu ya Awali, Darasa la I na III, Sekondari Kidato cha 1 na Elimu ya Ualimu kwa masomo 67 kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na vitabu vya nukta nundu masomo 67 kwa ajili ya wanafunzi

wasioona kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa watoto wenye mahitaji maalum; na

(iv) itabadilisha vitabu sita vya Elimu ya Awali na vitabu sita vya kiada vya Darasa la I kuwa katika maandishi yaliyokuzwa na nukta nundu kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona.

**97. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza idadi ya vitabu vya ziada na rejea vitakavyosaidia walimu na wanafunzi kukuza uelewa wa mada mbalimbali, Serikali itatathmini vitabu vya ziada na rejea kutoka kwa waandishi binafsi. Aidha, itawezesha uchapaji wa vitabu vya Viongozi mbalimbali wa Kitaifa kwa lengo la kukuza uzalendo na maarifa kwa wanafunzi. Vitabu hivyo ni pamoja na: Maisha ya Benjamin William Mkapa; Kitabu cha Maisha ya Alli Hassan Mwinyi; Kitabu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere – Shivji, Shida na Makalla; na 38 Reflections on Mwalimu Nyerere by Mark Mwandosya and Balozi Mwapachu.

**98. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya TEHAMA kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaboresha mfumo wa kufundishia na kujifunzia kwa Elimu ya Sekondari na kuandaa maudhui ya kidijiti yatakayoimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA; na itaendelea kuimarisha utoaji wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) kwa kutumia TEHAMA kupitia mfumo wa kujifunzia na kufundishia (Learning Management System) unaopatikana kwa anuani ya https://tcpd.tie.go.tz. Utaratibu huu utasaidia kuwafikia walimu wengi na kupunguza gharama za mafunzo ya ana kwa ana.

**99. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kufanya tafiti katika ngazi ya elimu msingi, Sekondari na vyuo vya ualimu

kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itafanya utafiti katika maeneo matatu na itatoa ushauri elekezi katika maeneo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa lengo la kutatua changamoto zinazojitokeza katika eneo la uongozi na usimamizi wa elimu;

(ii) itafanya utafiti katika maeneo mawili ya tathmini ya upimaji wa Elimu ya Sekondari Kidato cha Pili ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji; na

(iii) itafanya utafiti tatuzi katika maeneo matatu ya kielimu katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu kwa ajili ya kubaini mafanikio na changamoto za utoaji wa elimu nchini na kutoa mapendekezo stahiki.

**100. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu na kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.
Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake itatekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ujenzi wa vyumba 90 vya madarasa katika shule 20 za msingi na shule 10 za sekondari, matundu ya vyoo 360 katika shule 15 za Sekondari, mabweni 10 ya wasichana yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 120 kila moja katika shule 10 za sekondari, nyumba 38 za walimu katika shule 10 za msingi na sekondari, na maabara 20 za sayansi katika shule 10 za sekondari. Vilevile, itawezesha ujenzi wa miundombinu katika shule 10 za wanafunzi wenye mahitaji maalum (Mabweni 3, madarasa 14 na matundu ya vyoo 70) kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania;

(ii) itawezesha ujenzi wa vyoo, miundombinu ya maji na usafi wa mazingira katika shule za msingi 450; na

(iii) itakarabati miundombinu ya maabara za kilimo, sayansi, lugha na sayansi kimu katika vyuo saba vya Ualimu vya Serikali ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo hayo kwa vitendo. Aidha, itaendelea kuunganisha vyuo vya ualimu 11 vya Serikali katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**101. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha huduma za maktaba nchini kwa lengo la kuamsha ari ya Watanzania kupenda kujisomea na kuelimika. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania itatekeleza yafuatayo:

(i) itaandaa Sera ya Taifa ya Huduma za Maktaba na Uendeshaji nchini kwa lengo la kuongeza uelewa wa kanuni, taratibu na miongozo ya huduma za maktaba na uendeshaji; na

(ii) itanunua na kuweka samani katika maktaba 43 nchini kwa lengo la kuboresha mazingira ya usomaji na ujifunzaji pamoja na kuongeza idadi ya watumiaji.

**102. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya maktaba kwa lengo la kuboresha mazingira ya kujisomea na kujifunza kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea na ujenzi wa jengo la maktaba ya Taifa Makao Makuu Dodoma litakalohifadhi nyaraka na machapisho kwa lengo la kutunza historia, maarifa, maadili, mila na desturi za Mtanzania;

(ii) itajenga maktaba ya Mkoa wa Singida ambayo itawezesha upatikanaji wa huduma za maktaba kwa wananchi zikiwemo huduma za rejea (reference sections), usomaji, kujifunza, utafiti na sehemu za huduma za jamii ikiwemo michezo ya watoto;

(iii) itakamilisha ujenzi wa maktaba ya kumbukumbu ya John Pombe Magufuli – Chato na kuweka miundombinu ya TEHAMA, samani, mfumo wa maji taka, umeme wa nishati ya jua pamoja na kuchimba kisima;

(iv) itaendelea na ukarabati wa Maktaba Kuu ya Taifa (National Central Library) Dar es Salaam na kuanza ukarabati wa Maktaba ya Mkoa wa Tanga, Mtwara, Musoma na Mbeya; na

(v) itakarabati miundombinu ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS) – Bagamoyo kwa lengo la kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

**103. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali wanapata fursa ya elimu, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo wa Kuwarejesha Shuleni Wanafunzi Waliokatisha Masomo katika Elimu ya Msingi na Sekondari kwa sababu mbalimbali kwa lengo la kubaini changamoto za utekelezaji wake; na

(ii) itachapa moduli 18 za masomo kwa Hatua ya I na II kwa ajili ya vituo 151 vya elimu ya sekondari kwa Njia Mbadala ili kuongeza fursa za upatikanaji na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

**104. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kukuza na kuendeleza kisomo na elimu kwa umma kwa kuanzisha madarasa 1,000 ya kisomo yanayolenga kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Watu Wazima. Aidha, itaendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea ujuzi vijana 12,000 kupitia Mpango wa elimu changamani kwa walio nje ya shule awamu ya pili (IPOSA).

**105. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha uongozi na usimamizi wa elimu nchini, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu itatekeleza yafuatayo:

(i) itatoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na usimamizi wa elimu kwa walimu wakuu 6,500 wa shule za msingi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kusimamia ufundishaji na ujifunzaji; na

(ii) itadahili walimu 2,047 katika ngazi ya Astashahada; na Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu na Uthibiti Ubora wa Shule katika kampasi ya Bagamoyo, Mbeya na Mwanza. Aidha, itadahili walimu 120 katika Shahada ya Usimamizi wa Elimu.

**106. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira ya utoaji mafunzo ya usimamizi wa elimu, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu, itajenga kumbi za mihadhara katika kampasi ya Bagamoyo na Mwanza zenye uwezo wa kuchukua wanachuo 1,000 kila moja. Aidha, itakarabati majengo matatu katika kampasi ya Bagamoyo kwa lengo la kuongeza udahili kwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

**107. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania itaendelea kufanya upimaji na tathmini ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendesha Mtihani wa Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa wanafunzi 1,815,792 wanaotarajiwa kufanya mtihani wa upimaji mwezi **Oktoba, 2023**;

(ii) itaendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 1,537,171 wanaotarajiwa kufanya mtihani mwezi **Septemba, 2023**;

(iii) itaendesha Mtihani wa Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa wanafunzi 691,078, Kidato cha Nne kwa watahiniwa 610,330 na mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 8,500 wanaotarajiwa kufanya mtihani mwezi Novemba, 2023;

(iv) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 94,920 na watahiniwa 8,505 kwa ngazi ya Cheti na Stashada ya Ualimu wanaotarajiwa kufanya mtihani mwezi **Mei, 2024**;

(v) itaendesha Upimaji wa Sampuli wa Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa sampuli ya wanafunzi wa Darasa la Pili mwezi **Januari 2024**; na

(vi) itachapa na kusambaza vitabu vya tathmini ya upimaji na mitihani ya Kitaifa katika ngazi ya Elimu ya msingi na sekondari.

**d. Kuongeza Fursa na Ubora wa Elimu ya Juu**

**108. Mheshimiwa Spika,** Serikali itahuisha mitaala ya Elimu ya Juu kwa lengo la kuwezesha wahitimu kupata ujuzi wenye kuendana na mipango ya nchi, kikanda na kimataifa. Aidha, itaendelea kuziwezesha Taasisi za Elimu ya Juu kushiriki katika agenda ya maendeleo kupitia utafiti wenye kutatua changamoto katika jamii na kuvutia wanafunzi na Wahadhiri kutoka nje ya nchi.

**109. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaratibu na kuongeza fursa za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Elimu ya juu kama ifuatavyo:

(i) itatoa nafasi 100 za ufadhili wa masomo kutoka nchi rafiki na mashirika mbalimbali nje ya bara la Afrika kwa wanafunzi wa elimu ya juu; na

(ii) itahuisha kanzidata ya mfumo wa ufadhili (scholarship portal) kwa wanafunzi wanaopata ufadhili wa masomo

ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuunganisha mifumo ya taarifa za wanafunzi wote wanaosoma nje ya nchi.

**110. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na uthibiti ubora wa elimu katika ngazi ya Elimu ya Juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaratibu udahili na kuhakiki maombi ya wanafunzi 135,000 wa mwaka wa kwanza wanaotarajiwa kuomba udahili katika vyuo vya Elimu ya Juu kwa lengo la kujiunga na programu mbalimbali za masomo kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada ya Awali na Umahiri;

(ii) itasajili na kukagua Asasi 15 zinazoratibu wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzitambua na kuzisajili zitakazokidhi vigezo kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania;

(iii) itakagua na kufanya tathmini na ufuatiliaji wa Vyuo Vikuu 36 kwa lengo la kuhakiki ubora; na

(iv) itafanya tathmini ya tuzo 3,000 zilizotolewa katika vyuo vikuu vya nje na kuzitambua zitakazokidhi vigezo pamoja na kufanya tathmini ya programu 200 za masomo mbalimbali katika Vyuo Vikuu nchini na kuzipa ithibati kwa zitakazokidhi vigezo.

**111. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaboresha ukusanyaji na utoaji taarifa za elimu ya juu kwa kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya Tume ya Vyuo Vikuu kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati na matumizi yake katika kupanga mipango na kufanya maamuzi.

**112. Mheshimiwa Spika,** katika kuwezesha wanafunzi wa Tanzania wenye uhitaji na stahiki ya kupata mkopo kwa ajili ya elimu ya juu, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka 202,877 hadi 210,169;

(ii) itaendelea kusajili wanafunzi 72,361 wa mwaka wa kwanza katika mfumo wa malipo wa kidijitali (DIDiS);

(iii) itaboresha mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Mikopo na utunzaji wa nyaraka (iLMS, MUSE, DIDis) Gateway, OLAMS, MEL na eDMS kuwa wenye ufanisi na tija;

(iv) itaendelea kutoa fursa za Elimu ya Juu kwa wanafunzi wenye ufaulu uliojipambanua kutoka wanafunzi 593 hadi 1200 kupitia Samia Skolashipu;

(v) itatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 50 kupitia Chuo kikuu cha Dar es Salaam, wanafunzi 20 kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma wenye ufaulu wa juu kwenye masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati hususani wanafunzi wa kike waliohitimu mtihani wa Taifa Kidato cha Sita; na

(vi) itaendelea kukusanya madeni ya mikopo ya kiasi cha **Shilingi Bilioni 230** kutoka kwa wanufaika na kutambua wanufaika wapya **40,000** ambapo **asilimia 30** watatoka katika sekta isiyo rasmi. Aidha, itakagua waajiri **8,000** kwa lengo la kutambua na kukusanya marejesho kutoka kwa wanufaika.

**113. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaboresha mafunzo ya udaktari na kuongeza utoaji huduma katika vitengo mbalimbali vya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili ikiwemo shule ya meno na kuendelea na mradi wa ujenzi wa Kliniki ya Uporoto (Uporoto Polyclinic) kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kufundishia, utafiti na kutoa huduma za tiba kwa jamii. Vilevile, itaimarisha miundombinu ya kufundishia katika kituo cha umahiri cha magonjwa ya moyo na mishipa ya damu kampasi ya Mloganzila. Aidha,

itakarabati Kituo cha Kufundishia na Utafiti cha Bagamoyo (Bagamoyo Training Unit) katika chuo hicho.

**114. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na mataifa mengine katika uendelezaji wa Elimu ya Juu nchini kwa kutoa ufadhili wa wanafunzi watano raia wa China kusoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na kufadhili wanafunzi watano raia wa Oman na 10 raia wa Poland kusoma katika Vyuo Vikuu vya hapa nchini kulingana na mikataba. Aidha, itaratibu nafasi takribani 100 za ufadhili wa masomo kutoka nchi rafiki na mashirika mbalimbali Afrika na nje ya Bara la Afrika kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

**115. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaboresha utoaji wa elimu kwa umma na huduma kwa wateja kupitia programu za uhamasishaji, vyombo vya habari, uanzishaji wa kituo cha kisasa cha kupokea simu za wateja, pamoja na uratibu wa maonesho ya 18 ya Elimu ya Juu nchini ili kutoa elimu kwa umma kuhusu programu mbalimbali zitolewazo na taasisi za elimu ya juu.

**116. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Chuo cha Ushirika Moshi itatoa elimu ya ushirika ili kuchochea maendeleo ya jamii kwa kushirikiana na wadau, hususan Wizara ya Kilimo; Tume ya Maendeleo ya Ushirika; Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika; Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania; na Vyama vya Ushirika nchini na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**117. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa watumishi katika taasisi za Elimu ya Juu nchini, Serikali itaendelea kutoa ufadhili kwa Wanataaluma na Wataalam 1,197 wa elimu ya juu kati yao 1,147 watahudhuria mafunzo ya muda mrefu na 50 watahudhuria mafunzo ya muda mfupi.

**118. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi za vyuo vikuu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kampasi ya Mizengo Pinda – Katavi na kuboresha mtandao wa mawasiliano katika chuo Kikuu cha Dodoma kwa kuongeza kipimo data (bandwitdth) cha mtandao kutoka 622.08 Mbps hadi 933.12 Mpbs; na

(ii) itanunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi 55 wenye mahitaji maalum katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kwa lengo la kuboresha mafunzo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**119. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha mindombinu ya Taasisi za Vyuo Vikuu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itajenga kampasi 14 za vyuo vikuu katika mikoa ambayo haina kwa lengo la kuleta mageuzi ya kiuchumi;

(ii) itaanza ujenzi wa jengo la ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu pamoja na kuanza ujenzi wa ofisi za Tume ya Vyuo Vikuu katika jiji la Dodoma;

(iii) itaendelea na ujenzi wa Maabara Kuu ya Kemia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo itatumika kwa ajili ya utafiti na kutoa huduma za kupima sampuli za viwandani, na kuendelea na ujenzi wa jengo la Shule Kuu ya Uchumi katika chuo hicho;

(iv) itajenga ukumbi wa mitihani na ukumbi wa mkutano katika kituo cha chuo Kikuu Huria cha Morogoro. Vilevile, itakarabati majengo ya ofisi Makao Makuu Kinondoni pamoja na kituo cha Shinyanga, Kinondoni, Mtwara,

Dodoma, Singida, Kilimanjaro, Rukwa na kituo cha uratibu cha Mafia katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania;

(v) itajenga majengo matano mapya katika kampasi ya Chuo cha Ardhi kampasi ya Mwanza ambayo ni: madarasa nane; vyumba vya studio vinne; ofisi za watumishi 90; bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400; bwalo la chakula na nyumba ya watumishi yenye uwezo wa kuchukua familia 24;

(vi) itajenga majengo manne mapya katika kampasi kuu ambayo ni: Maabara ya matumizi anuwai (Multipurpose Laboratory) inayojumuisha maabara saba; Jengo la Studio lenye vyumba 15; Jengo la Karakana (Multipurpose workshops building) lenye jumla ya karakana 10; na Jengo la Madarasa (Multipurpose classrooms) lenye vyumba vya madarasa 28 katika Chuo Kikuu Ardhi;

(vii) itajenga jengo la upasuaji katika zahanati ya Kampasi Kuu Mzumbe kwa lengo la kusogeza huduma kwa wanachuo na jamii inayozunguka;

(viii) itaanza ujenzi wa miundombinu katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kama ifuatavyo: Ujenzi wa ofisi na majengo ya taaluma katika Hosteli ya kihonda kwa ajili ya Ndaki ya Sayansi ya Jamii na Insia; Ujenzi wa majengo mawili ya taaluma (Academic Blocks) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 3,500 katika kampasi ya Edward Moringe na Solomoni Mahlangu; Ujenzi wa maabara ya mafunzo ya anatomi ya mifugo; na Ujenzi wa vitalu nyumba 10 vya kupangisha kwa wahitimu. Aidha, itakamilisha hosteli mbili za wanafunzi katika kampasi ya Solomoni Mahlangu na Mizengo Pinda na kuendelea na ujenzi wa majengo ya Ndaki ya Uchumi na Mafunzo ya Biashara;

(ix) itaanza ujenzi wa jengo la Midia anuai na Mahitaji Maalum (Multimedia and Special Needs Education Building) katika Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Mkwawa;

(x) itaendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 180 kwa lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela;

(xi) itaendelea na upanuzi wa bweni la Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kujenga ghorofa mbili zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,280 hivyo kuongeza idadi ya wanafunzi kufikia 5,120;

(xii) itakarabati miundombinu katika Chuo Kikuu Ardhi kama ifuatavyo, madarasa 50, maabara mbili, mabweni wawili ya wanafunzi, ofisi 25 za watumishi, nyumba 16 za watumishi na miundombinu ya TEHAMA;

(xiii) itajenga Maabara ya Anatomia ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa kozi za tiba na uuguzi katika Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na kujenga mabweni yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 260 kwa wakati mmoja katika Kituo cha Mafunzo cha Iringa. Vilevile, itakarabati ukumbi wa Chimwaga. Aidha, itachimba visima vya maji ili kuwezesha upatikanaji wa maji safi na salama wa uhakika katika mazingira ya chuo; na

(xiv) itaendelea na ujenzi wa jengo la maktaba, jengo la kumbi za mihadhara na hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,500 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

**e. Kuimarisha Uwezo wa Nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili Kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda**

**120. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kusimamia maendeleo ya utafiti na kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kupitia Taasisi zilizo chini ya wizara kwa lengo la kuleta maendeleo na kuboresha ustawi wa jamii. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya utafiti katika maeneo 177 ya elimu, sayansi na teknolojia, lugha, kilimo, biashara, uvuvi, mifugo, tiba, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano, maliasili, watu wenye mahitaji maalum, kilimo na chakula, uongozi na biashara kwa lengo la kuongeza maarifa na kutatua changamoto mbalimbali katika jamii. Aidha, itaandaa machapisho 1,806 kwa lengo la kueneza matokeo ya utafiti kwa jamii;

(ii) itafanya utafiti wa taarifa za ajira kupitia Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi – NACTVET ili kubaini mahitaji halisi ya soko la ajira na kupata taarifa zitakazowezesha kuboresha mitaala na kushauri wadau wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kuhusu soko la ajira;

(iii) itaendelea kugharimia wanafunzi na wanataaluma kwa ajili ya utafiti na ubunifu wa miradi 42 ili kuendeleza na kuzalisha ubunifu katika maeneo mbalimbali kwenda katika hatua ya atamizi;

(iv) itafanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kusimika kinu cha utafiti cha kinyuklia (Research Reactor) kwa lengo la kuboresha sekta mbalimbali ikiwemo afya, kilimo, viwanda na elimu; na

(v) itanunua vifaa na kuboresha maabara 10 za utafiti katika taasisi za Utafiti na Maendeleo kwa lengo la kuimarisha mazingira ya utafiti na ubunifu nchini.

**121. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuwatambua wabunifu, kuwaendeleza na kubiasharisha ubunifu wao pamoja na kuendeleza miradi mbalimbali ya ubunifu kwa lengo la kukuza utaalamu asilia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaanzisha mikataba mipya mitano ya ushirikiano na taasisi na mashirika ya maendeleo ya ndani na nje ya nchi itakayoleta tija kwenye nyanja za ubunifu, utafiti na taaluma katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam;

(ii) itaendeleza teknolojia zinazozalishwa na wabunifu nchini kupitia majukwaa mbalimbali yaliyopo kama vile kumbi za ubunifu na mashindano ya kitaifa ya ubunifu; na

(iii) itaweka mazingira wezeshi kwa kuboresha mifumo ya TEHAMA inayoziunganisha taasisi za utafiti pamoja na mifumo ya uratibu wa utafiti na ubunifu ili kubiasharisha bidhaa zinazozalishwa na wabunifu na kuziendeleza.

**122. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kuchangia utunzaji wa mazingira na kuongeza matumizi ya nishati mbadala nchini, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itaanzisha kituo cha umahiri kitakacho tekeleza kazi za ujasiriamali, ubunifu, na uhawilishaji wa Teknolojia kwa kubiasharisha ubunifu ikiwemo kubadilisha magari yanayotumia mafuta ya petroli kutumia gesi asilia na bajaji zinazotumia mafuta ya petroli kutumia umeme. Vilevile, itaanzisha programu ya Teknolojia ya Anga ya Juu kwa ajili ya kuandaa wataalamu wa teknolojia ya Satellite.

**123. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha huduma za jamii na kutatua changamoto mbalimbali, Serikali kupitia vyuo vikuu pamoja na taasisi za sayansi na teknolojia itaendelea

kutoa huduma ya ushauri wa kitaalamu katika nyanja ya elimu, sayansi, sayansi jamii, mazingira, kilimo na chakula, nishati, TEHAMA, uongozi na biashara, utalii, maliasili, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano; huduma nyingine ni katika maeneo ya uimara wa udongo, kokoto na lami, ubora wa maji, usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi kwa walengwa mbalimbali.

**124. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Taasisi za Teknolojia itaendelea kuzalisha wataalamu wenye ujuzi unaohitajika kwa ajili ya uendelezaji wa miradi (Project Sustainability) ya kimkakati ya Taifa ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), Uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere (Hydro - Electric Power Project) na usafirishaji wa mafuta katika bomba (EA Crude Oil pipeline project).

**125. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha matumizi salama ya mionzi ya nyuklia nchini, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki itatekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kudhibiti matumizi ya mionzi nchini kwa kukagua vituo 900 vyenye vyanzo vya mionzi ili kuhakikisha usalama wa wagonjwa, wafanyakazi na jamii. Aidha, itapima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,110 wanaofanya kazi kwenye mazingira yenye vyanzo vya mionzi. Vilevile, itafuatilia hali ya usalama wa hewa katika anga kupitia vituo 1,045. Aidha, itasimamia kituo maalumu cha kupima hewa katika anga kwa lengo la kudhibiti uchafuzi unaotokana na mionzi;

(ii) itaendelea na utekelezaji wa mradi wa Multipurpose Irradiator ili kuleta ufanisi katika uhifadhi wa mazao ya kilimo ikiwemo vyakula vinavyoharibika kirahisi, vifaa tiba na vya viwandani. Aidha, itaanzisha mradi wa kituo cha uboreshaji wa mbegu za mazao ya kilimo (Plant Breeding Facility) kwa kutumia teknolojia ya nyuklia ili mbegu ziwe na uwezo wa

kustahimili ukame, magonjwa na kutoshambuliwa na wadudu;

(iii) itaendelea kukusanya na kusafirisha mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika na kuyahifadhi katika kituo maalumu cha mabaki ya mionzi (Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF); pamoja na kuendelea na ujenzi wa maabara za kanda katika mkoa wa Dar es Salaam, Mbeya na Zanzibar kwa lengo la kusogeza huduma za udhibiti wa mionzi na teknolojia ya nyuklia kwa wananchi;

(iv) itakamilisha mchakato wa uanzishaji wa chuo cha mafunzo ya ulinzi na usalama wa kinyuklia (Tanzania Atomic Energy College) ili kuongeza wataalamu wa kinga na usalama wa mionzi pamoja na wataalamu wa kutengeneza vifaa vinavyotumia teknolojia ya mionzi hospitalini, viwandani, barabarani pamoja na sekta mbalimbali ikiwemo ujenzi na madini; na

(v) itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kituo cha utafiti cha tiba za saratani (Oncology Research Centre) ili kuleta tija na ufanisi katika kukabiliana na tatizo la saratani nchini kwa kuongeza uwezo wa utafiti na uchunguzi kwa kutumia teknolojia ya nyuklia.

## F. TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

**126. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO, itaendelea kuratibu, kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mikataba 10 ya Kimataifa ya UNESCO ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa mikataba hiyo;

(ii) kutoa elimu kwa Taasisi na Mamlaka za Serikali kuhusu Mkataba wa 2001 wa Urithi wa Chini ya Bahari (Underwater Heritage) ambao Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipo mbioni kuuridhia; na

(iii) kufuatilia na kutathmini maeneo mapya ya urithi yaliyopendekezwa na wadau ili kuongeza maeneo zaidi ya urithi wa dunia nchini yanayotambuliwa na UNESCO kwa lengo la kuongeza vivutio vya utalii.

## G. SHUKRANI

**127. Mheshimiwa Spika,** natumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa QS Omary Juma Kipanga (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu na kufikia malengo ya wizara. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Profesa Carolyne Ignatius Nombo, Naibu Makatibu Wakuu, Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Franklin Jasson Rwezimula kwa kunipa ushirikiano. Vilevile, bila kuwasahau Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kuwezesha kuandaliwa kwa hotuba hii.

**128. Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru pia Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Walimu, Wanafunzi, na Wadau wote wa Elimu kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wamiliki na Mameneja wa Shule, Vyuo na Taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu nchini.

**129. Mheshimiwa Spika,** nawashukuru vilevile Washirika wa Maendeleo na Wadau wote wa Elimu ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa Mipango na Miradi ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za: Misri, Msumbiji,

Morocco, Namibia, Tunisia, Mauritius, Comoro, Ethiopia, Zimbabwe, Algeria, Afrika Kusini, Malawi, Umoja wa Falme za Kiarabu, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Finland, Hungary, India, Indonesia, Italia, Israel, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Malaysia, Netherland, New Zealand, Norway, Palestina, Romania, Saudi Arabia, Sweden, Thailand, Ufaransa, Urusi, Uswisi, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani na Venezuela. Aidha, natambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

**130. Mheshimiwa Spika,** napenda pia kushukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na: Swedish International Development Agency (SIDA), Umoja wa Nchi za Ulaya, Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO), Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, Global Partnership in Education (GPE), United Nations International Children‟s Emergency Fund (UNICEF), United Nations Development Programme (UNDP), United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO), United States Agency for International Development (USAID), Benki ya Dunia, Inter University Council for East Africa (IUCEA), Human Development Innovation Fund (HDIF), Deutscher Akademischer Austauschdienst (DAAD), British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Commonwealth Secretariat, Aga Khan Education Services, Japan InternationalCooperation Agency (JICA), Karibu Tanzania Organization (KTO), Korea International Cooperation Agency (KOICA), Water Aid, Plan International, Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Mo Foundation, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) na Christian Social Services Commission (CSSC).

## H. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24

**131. Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Elimu,

Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,675,753,327,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:

(i) **Shilingi 537,880,762,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 500,957,569,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 36,923,193,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(ii) **Shilingi 1,137,872,565,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 979,083,678,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 158,788,887,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**132. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,733,888,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara ni **Shilingi 1,124,980,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 1,608,908,000.00).**

**133. Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Fungu 46 na Fungu 18 yenye jumla ya **Shilingi 1,678,487,215,000.00.**

**134. Mheshimiwa Spika,** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**135. Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara http://www.moe.go.tz.

**136. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waziri Profesa.

Waheshimiwa tuna wageni ambao wameingia muda huu; wageni wa 30 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Kwaya ya Nyota njema kutoka Mt. Andrea Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Anna Lupembe wana maombi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 116 wa Mheshimiwa David Kihenzile, wanachama wa *Tanzania Red Cross Society* kutoka matawi ya vyuo vikuu na kati Dodoma Mjini wakiongozwa na Ndugu Geofrey Mtasiwa, karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia wabunge wote kwamba Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, itaendesha semina kuhusu utendaji kazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*. Semina hiyo itafanyika siku ya Jumatano tarehe 17 Mei, 2023 mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge saa 07.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa wote mnaombwa kuhudhuria.

Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii imetokana na uchambuzi wa kamati katika maeneo makuu manne yafuatayo: -

(i) Kuzingatiwa kwa ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(ii) Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(iii) Mpango na vipaumbele vya kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2023/2024; na

(iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuzingatiwa kwa Maoni, Ushauri na Maelekezo ya Kamati. Kamati ilitoa maoni, ushauri na maelekezo katika maeneo mahsusi saba, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati katika maeneo yaliyo mengi, hususan, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza kikamilifu maeneo mahsusi yafuatayo:-

(i) Kuongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kulikowezesha wanafunzi takriban wote stahiki kupata mikopo na hivyo kudahiliwa katika vyuo mbalimbali vya elimu ya juu nchini.

(ii) Kukamilisha mchakato wa kupitia sera ya elimu na mafunzo na mitaala ya elimu nchini, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais pamoja na kukidhi kilio cha siku nyingi cha wadau wa elimu nchini. Kamati inayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mchakato huu sasa upo hatua za mwisho ambapo wadau mbalimbali wa elimu wanatoa maoni yao katika rasimu mbili, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Aidha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ilitoa maoni na ushauri

mahsusi kuhusu rasimu husika na kuwasilisha maoni hayo Wizarani kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

(iii) Kukamilisha ujenzi wa vyuo 29 vya elimu ya ufundi stadi *(VETA)* vikiwemo vyuo 25 katika wilaya na vyuo vinne katika mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutekeleza kikamilifu ushauri na mapendekezo ya Kamati katika maeneo mengine yafuatayo:-

(i) Kuendelea kushughulikia upungufu wa watumishi katika sekta ya elimu;

(ii) Kudumisha uhuru wa kitaaluma katika vyuo vikuu;

(iii) Serikali iandae na kutekeleza mkakati wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya kati na mafunzo ya amali. Suala hili ni muhimu sana kwa kuzingatia mwelekeo mpya wa sera ya elimu na mafunzo ambapo mkazo wa sasa unawekwa kwa elimu na mafunzo ya amali. Serikali iliahidi kuandaa mkakati wa kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi katika vyuo ya mafunzo ya amali kwa kuanzia na maeneo ya kilimo, ufugaji, uvuvi, afya, uhandisi na TEHAMA. Hata hivyo, Kamati haijaona mkakati huu bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; Kamati ilikagua jumla ya miradi minne iliyopangiwa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kwa ujumla wake Kamati iliridhishwa na maendeleo ya utekelezaji wa miradi hiyo. Hata hivyo, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo mahususi kwa kila mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu; Taarifa za Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na

Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kwa kuzingatia vipaumbele vya Wizara kwa mwaka husika. Kwa ujumla wake shughuli nyingi zilizopangwa katika mpango wa mwaka 2022 zinaendelea kutekelezwa vizuri na ufanisi unaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya, Kamati ilibaini, pamoja na changamoto zingine, upungufu mkubwa wa Wakufunzi na Wahadhiri, hususani katika masomo ya sayansi na mafunzo ya ufundi stadi. Kwa mfano, kwa mujibu wa taarifa za Wizara kwa Kamati, hadi kufikia mwaka 2022 kulikuwa na upungufu wa asilimia 69 ya wakufunzi katika vyuo vya ufundi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 642.7 ikihusisha makusanyo kutoka Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi, wakati taarifa inakabidhiwa kwenye Kamati, Wizara ilishakusanya jumla ya shilingi bilioni 338.199 sawa na asilimia 54.14 ya lengo. Kamati inaihimiza Wizara kuhakikisha kuwa Idara na Taasisi husika zinakusanya maduhuli yote yaliyopangwa, kabla au ifikapo Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Fungu la 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 1.55 na hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya shilingi bilioni 104 zilishatolewa na kutumika, sawa na asilimia 66.87.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Fungu la 18 – Tume ya *UNESCO,* Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 2.79 na hadi kufikia Machi, 2023, kiasi cha shilingi bilioni 1.557 sawa na asilimia 57.45 ya bajeti iliyoidhinishwa kilikuwa kimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne; Taarifa ya Mapitio ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa mwaka wa fedha

2023/2024, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbekle vikubwa vitano, ikiwa ni pamoja na kukamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na mitaala ya elimu na kuanza utekelezaji wake. Kamati itaendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa jambo hili muhimu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 1.638 ikiwemo shilingi bilioni 535.880 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya idara na taasisi zake na shilingi trilioni 1.12 kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Kwa ujumla wake bajeti ya mwaka huu imeongezeka kwa asilimia 5.30 ukilinganisha na bajeti ya mwaka uliuopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tume ya *UNESCO* - Fungu 18. Waziri anaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 2.733. Bajeti kwa Fungu hili imeongezeka kwa takribani asilimia moja ikilinganishwa na bajeti ya m aka unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne; Maoni na Ushauri wa Kamati.

(a) Mafanikio na changamoto; Kamati inaipongeza Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa ufanisi mkubwa wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022. Hususan, kamati inaipongeza Wizara kwa kusimamia vyema mchakato wa mapitio ya Sera na Mitaala ya Elimu na Mafunzo na kukamilisha kazi hii muhimu kwa maendeleo ya Sekta ya Elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya kipekee kabisa, Kamati inampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utashi wake wa kisiasa, ujasiri na uthubutu wa kuruhusu mchakato wa kufanya mageuzi makubwa sana katika Sekta

ya Elimu. Mageuzi ambayo yataacha alama katika sekta ya elimu kwa muda mrefu ujao. Katika hili Mheshimiwa Rais ametekeleza kikamilifu nia yake ya kufanya mabadiliko au mageuzi au *reforms* katika Sekta ya Elimu ambayo ni moja ya *R* katika falsafa yake ya *4Rs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaipongeza serikali kwa kuendelea kuifanya sekta ya elimu kuwa moja ya vipaumbele vikubwa katika mipango yake ya maendeleo. Hali hii inadhihirishwa zaidi na ongezeko la bajeti ya kila mwaka kwa Sekta ya Elimu. Katika kipindi cha miaka mitano mfufululizo Sekta ya Elimu imekuwa ikitengewewa zaidi ya asilimia 17 ya Bajeti Kuu ya Serikali na hivyo kukidhi vigezo vya kimataifa vinavyotaka kuwa bajeti ya Sekta ya Elimu isipungue asilimia 16 ya Bajeti yote ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, katika uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2022/2023, pamoja na uchambuzi wa mpango wa bajeti ya Mwaka 2023/2024, Kamati imebaini changamoto za jumla zifuatazo katika uendeshaji wa sekta ya elimu nchini:-

(i) Uwepo wa mgongano na mwingiliano wa majukumu katika uendeshaji wa elimu na uendeshaji wa shule kwa upande wa elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu ya sekondari baina ya Ofisi ya Rais, Tawala la Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mgongano na mwingiliano huu unajidhihirisha zaidi katika maeneo ya utawala wa elimu, ujenzi wa miundombinu na utoaji wa miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa elimu.

(ii) Upungufu mkubwa wa Walimu katika sekta ya elimu ya msingi, awali na sekondari na Wakufunzi na Wahadhiri katika ngazi za elimu ya mafunzo ya ufundi na amali na elimu ya juu.

(iii) Kutozingatiwa kikamilifu kwa uhuru wa kitaaluma, ambao ndio msingi mama wa uendeshaji wa vyuo vikuu duniani. Hali hii inadhihirishwa na kutokuzingatiwa kikamilifu kwa Sheria ya Vyuo Vikuu ya Mwaka 2005, hususani Kifungu cha 45E, na *Charters* za vyuo vikuu husika, katika ajira za watumishi wa vyuo hivyo.

(iv) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya elimu ya juu nje ya mafunzo. Kwa mfano, pamoja na kuongezeka kwa bajeti ya maendeleo kwa asilimia nane sehemu kubwa ya bajeti ya elimu ya juu, yaani asilimia 67% imeelekezwa kwenye kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Hali hii imefanya kuwa na bajeti finyu sana kwa ajili ya utekelezaji wa sekta za utafiti, sayansi na teknolojia, ambazo ni sehemu muhimu ya majukumu ya Wizara hii. Uchambuzi wa taarifa za wizara unaonesha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya fedha za utafiti katika vyuo vikuu nchini hutoka nje ya nchi.

(v) Pamoja na kwamba Serikali imeonesha nia njema ya kuanza kutoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi katika vyuo ya elimu na mafunzo ya amali, vyuo vya kati, hakuna mkakati ulioandaliwa wala bajeti bayana iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wake.

(vi) Kuna udhaifu katika udhibiti ubora mashuleni kwa kuwa shule nyingi hazikaguliwi. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, ni asilimia 26.4 pekee ya shule za msingi zilizopangwa kukaguliwa ndizo zilizokaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushauri na Mapendekezo; katika kukabiliana na changamoto zilizoelezwa hapo juu, Kamati inashauri hatua zifuatazo:-

(i) Serikali ifanye tathimini ya kina kuhusu utekelezwaji wa Sera ya Ugatuaji katika Sekta ya Elimu Nchini ili kubaini changamoto na mafanikio yake. Aidha, kwa kibali cha Spika, Kamati za Kudumu za Bunge za Elimu, Utamaduni na Michezo

na TAMISEMI zimepanga kufanya kikao cha pamoja kwa ajili ya kutafakari suala hili kwa kina na kutoa ushauri wa pamoja.

(ii) Serikali iandae na kutekeleza mkakati wa kati na muda mrefu wa ajira za Walimu, Wakufunzi na Wahadhiri katika shule, vyuo vya elimu na mafunzo ya amali na vyuo vikuu.

(iii) Serikali isimamie kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Vyuo Vikuu katika kulinda na kudumisha uhuru wa kitaaluma, ikiwemo kuhakikisha kuwa ajira za watumishi katika vyuo vikuu vinazingatia kikamilifu sheria hii na misingi ya ajira za Wahadhiri katika vyuo vikuu duniani.

(iv) Serikali na wadau wengine kuandaa mkakati mpya wa ugharamiaji wa elimu ya juu, hususan katika kugharamia ada na gharama za chakula na malazi kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ili kutoa nafasi kwa bajeti ya shughuli zingine muhimu katika taasisi za elimu ya juu, ikiwemo utafiti na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

(v) Wizara iandae mkakati kwa ajili ya ugharamiaji wa elimu na mafunzo ya amali, yaani vyuo vya kati, ikiwemo kuainisha vipaumbele kwa ajili ya wanafunzi watakaopatiwa mikopo hiyo.

(vi) Serikali iimarishe udhibiti ubora kwa kuongeza bajeti ili shule nyingi zaidi ziweze kukagaliwa kwa mujibu wa vigezo vilivyopo. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuunda chombo huru kitakachohusika na udhibiti ubora na usimamizi wa elimu kwa ujumla kwa ngazi ya awali, msingi na sekondari kama ambavyo kuna chombo kama hicho kwa ngazi ya elimu ya ufundi na elimu ya juu.

(vii) Kutokana na ukubwa na wingi wa majukumu ya Wizara hii, ni maoni ya Kamati kuwa Tume ya Taifa ya *UNESCO* imekuwa haipewi uzito stahiki katika mipango ya

maendeleo. Kamati inashauri usimamizi wa Tume hii uhamishiwe Wizara nyingine inayoshughulikia masuala mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho; kwa niaba ya Kamati napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, wewe Mheshimiwa Naibu Spika na wasaidizi wenu kwa maana ya Wenyeviti wa Bunge kwa namna ambavyo mnatekeleza majukumu yenu kwa umakini na weledi wa hali ya juu katika kuliwezesha Bunge letu tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali na kuishauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia na wasaidizi wake, Mheshimiwa Omari Shaban Kipanga, Naibu Waziri na Profesa Carolyne Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa kipekee kabisa, naomba uniruhusu kuwapongeza Walimu wote nchini, pamoja na Wakufunzi na Wahadhiri katika taasisi mbalimbali za elimu nchini kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuelimisha na kulea kizazi cha leo na cha kesho kwa ajili ya Taifa hili. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu ya Elimu, Utamaduni na Michezo kwa kazi kubwa waliyoifanya tangu tulipoteuliwa mwezi Februari 2023 na kwa ushirikiano na upendo tulionao katika kutekeleza majukumu yetu. Majina ya Wajumbe hawa ni pamoja na Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, ambaye ni mimi, Mwenyekiti. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Makamu Mwenyekiti. Mheshimiwa Aloyce John Kamamba…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya majina yameshaingia kwenye *Hansard*, ahsante. Malizia tu.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, si muda bado upo?

**NAIBU SPIKS:** Hapana, tunataka wachangiaji wengi.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, basi naomba majina yote ya Wajumbe yaingie kwenye *Hansard*.

**NAIBU SPIKA:** Mtapongezana kwenye Kamati huko.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba nimalizie hotuba yangu kwa kumshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja naye, napenda kumshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Michael Chikokoto na Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Magili pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Eunike Donati Shirima na Ndugu Happiness Ndalu, wakisaidiana na Ndugu Waziri Kizingiti kwa kuihudumia Kamati na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**16 MEI, 2023**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

***[Imetolewa chini ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]***

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1. Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne ambazo ni:-

(i) Maelezo ya jumla, yanayobainisha msingi na muundo wa
Taarifa;

(ii) Ufafanuzi na uchambuzi wa matokeo ya Ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(iii) Maoni na ushauri wa Kamati, ambapo inakamilisha uchambuzi kwa kutoa maoni kutokana na uchambuzi unaojenga msingi wa ushauri wa Kamati; na

(iv) Ushauri kwa Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia aliyoitoa mapema leo.

## 1.2. Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Kamati katika kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, hususan Kifungu cha 6 (7) (a), kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023. Aidha, Kanuni ya 117(2) imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 yachambuliwe na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 21 Machi,2023, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na matokeo yake ni Taarifa hii inayowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu. Kwa msingi huo, ninaliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuijadili sambamba na Hoja ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia iliyotolewa mapema leo .

## 1.3. Mawanda ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na

Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 iliyochambuliwa na Kamati inazingatia maeneo makuu yafuatayo:-

(i) Kuzingatiwa kwa ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(ii) Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(iii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi kufikia mwezi Machi 2023;

(iv) Mpango na vipaumbele vya kazi zinazopangwa kufanyika kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

(v) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UFAFANUZI WA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inaitaka Kamati kutumia siku zisizozidi saba kwa ajili ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Aidha, Kanuni ya 117(2), inatoa siku zisizozidi tisa kwa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa bajeti. Kanuni hiyo inatambua umuhimu wa kufanya ulinganisho kati ya utekelezaji wa bajeti unaoripotiwa na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa msingi huo, taarifa hii inaripoti matokeo ya shughuli kuu tatu ambazo ni:-

a) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

b) Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;na

c) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Mambo hayo kwa pamoja yameweka msingi wa Maoni na Ushauri wa Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kwa sababu hiyo, ninaliomba Bunge lako Tukufu lizingatie kwa pamoja matokeo ya Uchambuzi kama inavyofafanuliwa katika taarifa hii.

**2.1 Kuzingatiwa kwa Maoni, Ushauri na Maelekezo ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitoa maoni, ushauri na maelekezo katika maeneo mahsusi saba (7). Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kutoka kwa Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati katika maeneo yaliyo mengi. Hususan, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza kikamilifu maeneo mahsusi yafuatayo:

i) Kuongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kulikowezesha wanafunzi karibu wote stahiki kupata mikopo na hivyo kudahiliwa katika vyuo mbalimbali vya elimu ya juu nchini

ii) Kukamilisha mchakato wa kupitia sera ya elimu na mafunzo na mitaala ya elimu nchini, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais pamoja na kukidhi kilio cha siku nyingi cha wadau wa elimu nchini. Kamati inayo furaha kulitaarifu Bunge tukufu kuwa mchakato huu sasa upo hatua za mwisho ambapo wadau mbalimbali wa elimu wanatoa maoni yao katika rasimu mbili. Wadau hawa ni pamoja na waheshimiwa wabunge. Aidha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ilitoa maoni na ushauri mahsusi kuhusu rasimu husika na kuwasilisha wizarani kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

iii) Kukamilishaa ujenzi wa vyuo vya elimu ya ufundi stadi (VETA) 29, vikiwemo vyuo 25 katika wilaya na vyuo vinne (4) katika mikoa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kutekeleza kikamilifu ushauri na mapendekezo ya Kamati katika maeneo yafuatayo:

(i) Kuendelea kushughulikia upungufu wa watumishi katika sekta ya elimu, ikiwemo kupitia upya na kurudisha utaratibu wa ajira za mikataba kwa maprofesa wa vyuo vikuu waliostaafu ili waendelee kutumikia ili taifa liendelee kunufaika na uwekezaji mkubwa lililofanya kwa maprofesa hawa.

(ii) Kudumisha uhuru wa kitaaluma katika vyuo vikuu, ikiwemo kuhakikisha kuwa ajira za wanataaluma zinafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Vyuo Vikuu na Charters za vyuo vikuu husika, badala ya utaratibu wa sasa ambapo ajira za wanataaluma zinafanywa na Sekretariati ya ajira.

(iii) Serikali iandae na kutekeleza mkakati wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya kati na mafunzi ya amali. Suala hili ni muhimu sana kwa kuzingatia mwelekeo mpya wa sera ya elimu na mafunzo ambapo mkazo sasa

unawekwa kwa elimu na mafunzo ya amali. Serikali iliahidi kuandaa mkakati wa kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi katika vyuo ya mafunzo ya amali kwa kuanzia na maeneo ya kilimo, ufugaji, uvuvi, afya, uhandisi na tehama. Hata hivyo, Kamati haijaona mkakati huu bayana.

### 2.2 Taarifa ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitekeleza miradi ya Maendeleo iliyokuwa imetengewa jumla ya Sh. **1,022,370,550,796/-**. Kamati ilikagua miradi minne ifuatayo:

a) ***Mradi Namba 4315: Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA)***

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa elimu ya juu kwa mabadiliko ya kiuchumi **(HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION (HEET) PROJECT**), unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, 2021/2022 - 2025/2026. Mradi huu una maeneo saba (7) yafuatayo:-

i. Ujenzi wa majengo mapya, ukarabati na ununuzi wa vifaa;

ii. Kuanzisha na kuboresha mitaala;

iii. Kuanzisha na kuimarisha uwezo wa kiuvumbuzi na tafiti zenye tija;

iv. Kujenga uhusiano wa kiutendaji na sekta binafsi;

v. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA;

vi. Kujenga uwezo wa kuzalisha mapato ya ndani; na

vii. Kuwajengea uwezo wanataaluma na viongozi.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia mradi wa HEET, Chuo kikuu cha Kilimo cha Sokoine kimetengewa kiasi cha Shilingi **Bilioni 73.6** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizoorodheshwa kwenye mradi huo. Hadi kufikia Machi, 2023, Chuo kilikuwa kimepokea Shilingi **Bilioni 9.5** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na kilishatumia jumla ya **Shilingi Bilioni 1.07** kwa ajili ya matumizi ya kugharamia mafunzo kwa ajili ya wanataaluma waliopo masomoni (Long – term training).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaihimiza wizara kusimamia mradi huu kwa karibu ili ukamilike kwa muda uliopangwa na kuhakikisha kuwa tija tarajiwa inapatikana.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na kukagua mradi lengwa, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kukagua programu zingine za kitaaluma zinazoendelea kutekelezwa chuoni hapo, zikiwemo programu ya shamba darasa, ufugaji wa samaki na maabara ya upasuaji wa wanyama. Kamati iliridhishwa na kuupongeza uongozi wa chuo na wizara kwa hatua kubwa ambayo SUA imefikia katika kuwapatia wanafunzi mafunzo ya vitendo na kuwaandaa kujitegemea mara watakapohitimu masomo yao.

b) ***Mradi wa Kujenga Ujuzi kwa Maendeleo na Uingiliano wa Kikanda Katika Africa Mashariki Unaotekelezwa na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) Kampasi Kuu ya Dar Es Salaam***

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unajulikana kama *East Africa Skills for Transformation and Regional Intergration Project (EASTRIP)*, unaotekelezwa katika Taasisi ya Teknolojia Dar Es Salaam. Mradi huu una thamani ya **Dola za Marekani 32,500,000/-** ikiwa ni sawa na **Shilingi Bilioni 74.80,** ambao ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Mradi una lengo la kuanzisha

vituo viwili vya Umahiri kwa Kampasi za Dar Es Salaam na Mwanza.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kukagua mradi katika Kampasi ya Dar es Salaam ambao una jumla ya **Shilingi Bilioni 37.40** ambapo unahusisha kuanzishwa kwa kituo cha Umahiri cha TEHAMA (Regional Flagship TVET Centre in ICT: RAFIC)

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la mradi ni kutoa elimu ya ufundi kupitia mafunzo ya vitendo, utafiti, ubunifu na maendeleo ya teknolojia inayofaa. Vile vile, mradi huu unatekelezwa kwa lengo la kuendeleza walimu na wafanyakazi waendeshaji katika maeneo yafuatayo: -

i. Kuongeza tija katika utendaji;

ii. Kuhuisha na kuanzisha mitaala mipya kwa kuzingatia dhana ya mafunzo viwandani;

iii. Kuimarisha uhusiano na viwanda ili kuwezesha dhana ya ufundishaji ya mafunzo viwandani;

iv. Ununuzi wa vifaa bora na vya kisasa vya kufundishia; na

v. Kujenga miundombinu.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mambo mengine, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa mradi huu unakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwemo upungufu wa wafanyakazi wenye mafunzo viwandani na idadi ndogo ya wafanyakazi wa kike. Aidha, Kamati ilibainisha kuchelewa kwa mradi huu. Pamoja na kwamba fedha zote zinazohitajika kwa ujenzi wa mradi huu zipo, kasi ya ujenzi wa majengo mawili ya mradi huu ni ndogo sana. Kamati inaihimiza Wizara kuongeza kasi ya usimamizi wa mradi huu ili tija tarajiwa ipatikane.

c) ***Mradi wa Ujenzi wa Maktaba na Ukumbi wa Mihadhara Katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Kivukoni***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipanga kutembelea na kukagua **Mradi Na. 4381** ambao ni Upanuzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Dar Es Salaam. Hata hivyo, mradi huo haujaanza kwa Kampasi ya Dar Es Salaam. Badala yake, Kamati ilitembelea na kukagua mradi ujenzi wa ukumbi wa mihadhara unaotekelezwa chuoni hapo.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusisha ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja na ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1000 kwa wakati mmoja. Majengo yote kwa pamoja yatagharimu kiasi cha ***Shilingi Bill 15.5***.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2023, ujenzi wa mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 25.

**d) Mradi Na. 6364: Uanzishwaji wa Kituo cha Umahiri wa Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu eneo la Mloganzila (MUHAS)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa na kukagua maendeleo ya mradi tajwa hapo juu. Mradi huu unagharimu jumla ya Shilingi Bilioni 21.80, na unahusisha shughuli zifuatazo:-

i. Ujenzi wa jengo la Kituo lililokamilika na kuzinduliwa tarehe 4 Desemba 2021;

ii. Kutoa ufadhili wa mafunzo kwa wataalamu mbalimbali wa mambo ya moyo na mishipa ya fahamu wapatao 38;

iii. Kuandaa mitaala kwa ajili ya kufundishia wanafunzi wa Moyo na Mishipa ya Damu;

iv. Kununua na kuweka vifaa vya TEHAMA, samani za ndani, alama za milangoni, mapazia, vifaa vya maabara na kuweka samani katika kumbi za mikutano;

v. Kufanya Tafiti za magonjwa ya moyo na mishipa ya damu; na

vi. Kuchapisha na kufanya makongamano kwa ajili ya kusambaza matokeo ya tafiti.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa lengp la kuanzishwa kwa kituo cha umahiri cha Afrika Mashariki cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu ni kutoa mafunzo na kutengeneza wataalamu wabobezi katika kuzuia, kutibu na kupunguza athari zinazotokana na magonjwa ya moyo na mishipa ya damu katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa pamoja na mradi huu kukamilika kwa asilimia100, utekelezaji wake ulikabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo kukosekana kwa misamaha ya kodi kwa wakati. Kamati inahimiza mamlaka husika kutoa ushirikiano wa kutosha katika kupatikana kwa misamaha ya kodi kwa miradi muhimu kama hii kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

### 2.2.1 Yatokanayo na Ukaguzi wa miradi

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Uchambuzi wa taarifa hizo ulilinganishwa na hali halisi ya hatua zilizofikiwa pamoja na madhumuni ya kutekelezwa kwa

miradi inayohusika. Matokeo ya shughuli hiyo yanaonesha kama ifuatavyo: -

i) Hadi kufikia mwezi Februari,2023, fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi hiyo zilikuwa zimepatikana kwa kiasi cha **asilimia 70.2** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa fedha za ndani kwa miradi ya maendeleo zilishatolewa kwa **asilimia 68.8** na **asilimia 99.9** ya fedha za nje.

ii) Kwa ujumla hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa mujibu wa Mpango kazi inatoa matumaini makubwa ya kukamilika kwa miradi husika ndani ya muda uliowekwa kwa mujibu wa mikataba

iii) Kuna ushirikiano mzuri katika utekelezaji wa miradi baina ya wadau mbalimbali wa elimu na taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia yatokanayo na ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyoanishwa hapo juu, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:

i) Bado kuna uwiano usioridhisha baina ya wanafunzi wa kike na wa kiume katika masomo ya sayansi. Kamati inaihimiza serikali kuendelea kuhamasisha na kuwawezesha vijana wa kike kujiunga na masomo ya sayansi katika taasisi za elimu nchini.

ii) Kuna haja ya vyuo vikuu nchini kujiimarisha katika mawasiliano ya umma ili matokeo ya tafiti yawafikie wadau walio wengi nje ya tasnia ya taaluma;

iii) Kamati imebaini kuwa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS) hakina Hospitali ya kujifunzia. Hali hii inapelekea Chuo cha MUHAS kuwa na mgongano na Hospitali ya Taifa Muhimbili katika utendaji hasa wakati wanafunzi wanapokuwa wakifanya mafunzo kwa vitendo.

Kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatenga fedha kwa ajili ya kuanza Ujenzi wa Hospitali kubwa eneo la Mloganzila mahsusi kama Hospitali ya kujifunzia kwa Wanafunzi wa MUHAS (Teaching Hospital).

### 2.3 Taarifa za Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Katika kupitia utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilifanya uchambuzi wa mambo makuu matatu yafuatayo:

i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama ilivyoainishwa katika Sehemu 2.1 ya Taarifa hii hapo juu;

ii) Ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na

iii) Utekelezaji wa bajeti iliyopangwa na kuidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulijulisha Bunge lako tukufu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kutokana na Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Lengo ni kuliwezesha Bunge kupata uwiano utakaosaidia katika mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kama yaliyowasilishwa na mtoa hoja.

#### 2.3.1 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulikumbusha Bunge lako tukufu kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 642,667,620,483.06** kwa mwaka

wa fedha 2022/2023, ikiwa imehusisha makusanyo kutoka Idara, vitengo na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kama inavyooneshwa katika Jedwali la 1 hapa chini.

**Jedwali 1: Uchanganuzi wa Maduhuli hadi kufikia Machi, 2023**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MADUHULI | MAKUSANYO HALISI HADI MWEZI MACHI,2023 | ASILIMIA YA LENGO |
|---|---|---|---|
| Idara na Vitengo | 8,680,995,000.00 | 6,546,086,027.00 | 75.41 |
| Taasisi | 633,986,625,483.06 | 331,653,392,514.42 | 52.31 |
| **JUMLA** | **624,667,620,483.06** | **338,199,478,541.42** | **54.14** |

**Chanzo: Takwimu zilizotolewa katika Uk. wa 5 wa Randama iliyowasilishwa kwenye Kamati**

**Mheshimwa Spika,** uchambuzi umeonesha kuwa hadi mwezi Februari,2023, lengo la jumla la makusanyo ya maduhuli kwa Wizara hii lilifikiwa kwa **asilimia 54.14** ikiwa ni robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji wa bajeti. Aidha, lengo la ukusanyaji wa maduhuli kutoka katika Idara na Vitengo lilifikiwa kwa **asilimia 75.41** na **asilimia 52.31** kutoka kwenye Taasisi na Asasi za Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi unaonesha kuwa maduhuli yaliyokusanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa takribani **asilimia 91.18** yanatokana na ada ya mafunzo na mitihani. Aidha chanzo kingine kikuu ni Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima inayochangia kwenye maduhuli ya wizara kwa karibu asilimia **71.35.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwenendo huo wa makusanyo ya maduhuli, ni dhahiri kwamba upo uwezekano wa lengo la Wizara kutofikiwa kikamilifu ifikapo tarehe 30 Juni, 2023. Kamati inahimiza Wizara kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa maduhuli na kujipanga vizuri zaidi katika kupanga malengo

na kuweka mikakati ya usimamizi itakayowezesha kufikiwa kwa malengo ya makusanyo ya maduhuli kikamilifu.

### 2.3.2 Utekelezaji wa Majukumu na Mipango ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kwa kuzingatia vipaumbele vya wizara kwa mwaka husika, ambavyo ni:

i) Kuhuishwa Sera,Sheria na Miongozo ya utoaji wa Elimu na mafunzo Nchini;

ii) Upatikanaji wa fursa za Elimu kwa watoto wenye umri wa kwenda shule;

iii) Kuimarisha ubora na mifumo ya usimamizi katika kutoa Elimu ya Awali, Msingi,Sekondari,Elimu ya Ufundi,Elimu ya juu na Elimu ya Ualimu;

iv) Kuongeza fursa katika kudahili wanafunzi na kuimarisha ubora wa Elimu;

v) Kuimarisha matumizi ya Sayani ,Teknolojia na Ubunifu kwa maendeleo ya Taifa;

vi) Kuimarisha na kuendeleza Tafiti na matokeo yake katika Ajenda ya Maendeleo.

**Mheshimwa Spika**, Kwa ujumla wake, shughuli nyingi zilizopangwa katika Mpango wa Mwaka 2022/2023 zinaendelea kutekelezwa vizuri na ufanisi unaonekana. Baadhi ya shughuli hizi na matokeo yake ni:

- **Kuongeza** udahili wa Wanafunzi katika Elimu ya Juu hadi kufikia wanafunzi **113,383,** kati yao wanawake **49,188** na

wanaume **64,195** ikiwa sawa na **asilimia 88** ya waombaji wa ngazi ya shahada ya kwanza

- **Kudahili** wanafunzi **15,851** sawa na **asilimia 89** ya waombaji katika ngazi ya National Technical Award **(NTA);**

- **Kutoa** mikopo kwa wanafunzi **72,973** kwa mwaka wa kwanza na **129,904** kwa wanafunzi wanaoendelea, ikiwa imetumia Jumla ya **Shilingi 650,256,913,598.00** kuwalipia wanafunzi hawa kupitia Bodi ya Mikopo, sawa na **asilimia 63.6** ya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo ya Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilibaini, pamoja na changamoto zingine, upungufu mkubwa wa wakufunzi na wahadhiri, hususani katika masomo ya sayansi na mafunzo ya ufundi stadi. Kwa mfano, kwa mujibu wa taarifa za Wizara kwa Kamati, vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini vina mahitaji ya wakufunzi 899. Hata wakufunzi waliopo ni ni 279 pekee (sawa na 31.1% ya mahitaji), ikiwa na upungufu wa asilimia 69. Kamati inahimiza serikali kuwekeza katika kuajiri wakufunzi na wahadhiri sambamba na ujenzi wa miundo mbinu katika taasisi za elimu nchini.

### 2.3.3 Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwenye bajeti ni muhimu katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Kamati ilipitia randama ya Wizara na kuchambua namna fedha zilivyokuwa zinapelekwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.2.**

**Jedwali Na.2: Mchanganuo wa upatikanaji wa Fedha kwa Fungu Na. 46**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 500,196,732,000.00 | 306,509,665,232.19 | 61.28 |
| Matumizi Mengineyo | 33,260,184,000.00 | 16,655,065,652.87 | 50.08 |
| Miradi ya Maendeleo | 1,022,370,550,796.00 | 717,267,718,200.36 | 70.2 |
| JUMLA | 1,555,827,466,796.00 | 1,040,432,449,085.42 | 66.87 |

**Chanzo: Takwimu za Upatikanaji wa fedha kwenye Randama iliyowasilishwa kwa kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ***Fungu 46*** (Jedwali Na. 02), uchambuzi umeonesha mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa. Hadi kufikia mwezi Machi 2023, Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 66.87** ya fedha iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ***Fungu 18***, Tume ya UNESCO (Jedwali Na. 03), katika Mwaka wa fedha 2022/2023, iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 2,709,163,000.00**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 1,176,870,000** ni mishahara **na Shilingi 1,532,293,000.00** kwa ajili ya matumizi mengine.

**Kielelezo Na. 3: UPATIKANAJI WA FEDHA (FUNGU 18) kwa Mwaka 2022/2023**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHO-POKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 1,176,870,000 | 695,247,920 | 59.08 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi mengineyo** | **1,532,293,000** | **862,248,117** | **56.27** |
| **JUMLA** | **2,709,163,000** | **1,557,496,037** | **57.49** |

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Februari, 2023 kiasi cha Shilingi **1,557,496,037.28** sawa na **asilimia 57.49** ya Bajeti iliyoidhinishwa kilikuwa kimepokelewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 695,247,920.00** sawa na **asilimia 59.08** ya bajeti ya mishahara ilikuwa imepokelewa na **Shilingi 862,248,117.28** sawa na asilimia 56.27 kwa ajili ya matumizi Mengineyo nayo ilikuwa imepokelewa kama inavyonekana kwenye **Kielelezo Na. 3** hapo juu.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/20224

### 3.1 Mpango na Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuliwezesha Bunge kujadili Hoja ya Waziri wa Elimu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi, utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Wizara kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia Ukomo wa Bajeti wa Wizara (***Fungu 46***) ambao ni **Shilingi Trilioni 1, 638, 253, 357,**
**000.00.**

**Mheshimiwa Spika**, Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

i) Kukamilisha mapitio ya sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu na kuanza utekelezaji wake kwa lengo la kuimarisha ujuzi kwa wahitimu wa kila ngazi ya elimu;

ii) Kuongeza fursa na ubora wa mafunzo ya amali (ufundi) kwa sekondari na vyuo vya kati vya Amali; na

iii) Kuwezesha ongezeko la fursa na ubora wa elimu ya msingi na sekondari

iv) Kuongeza fursa na ubora wa Elimu ya Juu

v) Kuimarisha uwezo wan chi katika tafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

### 3.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

#### 3.2.1 Makadirio ya Maduhuli ya Serikali Yatakayokusanywa

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara hii imepanga kukusanya jumla ya Shilingi **677,281,812,265.64** kutoka katika vyanzo mbalimbali kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 3**. Makusanyo hayo ni ongezeko la **asilimia 6.82** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Jedwali Na.3 Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli kutokana na Vyanzo vikuu vya Mapato**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MADUHULI 2022/2023 | MAKUSANYO HALISI HADI MWEZI MACHI,2023 | % LENGO | MAKADIRIO YA MADUHULI 2023/2024 | %ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|---|
| IDARA NA VITENGO | 8,680,995,000.00 | 6,546,086,027.00 | 75.41 | 11,660,695,000.00 | 34.32 |
| TAASISI | 633,986,625,483.06 | 331,653,392,514.42 | 52.31 | 665,621,117,265.64 | 05.00 |
| JUMLA | 642,667,620,483.06 | 338,199,478,541.42 | 54.14 | 677,281,812,265.64 | 06.82 |

**Chanzo: Takwimu za Upatikanaji wa fedha na Makadirio ya Ukusanyaji wa maduhuli kwenye Randama iliyowasilishwa kwa kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na nia njema ya Wizara ya kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka ujao wa fedha ukilinganisha na mwaka uliopita, Kamati ina mashaka kama lengo la ukusanyaji wa mapato litatekelezeka, kwani hadi kufikia Machi, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya **asilimia 52.62** tu ya lengo lake kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni, 2023. Kamati ina maoni kwamba, lengo la ukusanyaji wa maduhuli lizingatie hali halisi ya uwezo wa wizara na taasisi zake.

### 3.2.2 Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Wizara (***Fungu 46***) inaomba jumla ya **Shilingi 1,638,253,327,000.00**, ikiwemo ***shilingi 535,880,762,000.00*** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Idara na Taasisi na ***Shilingi 1,102,372,565,000.00*** kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Mchanganuo zaidi ya maombi ya fedha hizi umeoneshwa katika Jedwali Na. 4 hapa chini.

**Jedwali Na 04 Mchanganuo wa Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa 2022/2023 na mwaka 2023/20224**

| **AINA YA MATUMIZI** | **BAJETI ILIYOIDHINISHWA MWAKA 2022/2023** | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024** | **% ONGEZEKO** |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 500,196,732,000.00 | 500,957,569,000.00 | 0.15 |
| Matumizi Mengineyo | 33,260,184,000.00 | 34,923,193,000.00 | 5.00 |
| *JUMLA* | *533,456,916,000.00* | *535,880,762,000.00* | *0.45* |
| | | | |
| Miradi ya Maendeleo | 1,022,370,550,796.00 | 1,102,372,565,000.00 | 7.82 |
| **JUMLA KUU** | **1,555,827,466,796** | **1,638,253,327,000** | **5.30** |

**Chanzo: Takwimu za Makadirio ya matumizi ya Kawaida kwenye Randama iliyowasilishwa kwa Kamati.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya Bajeti yote ya Matumizi ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yameongezeka kwa **asilimia *5.30*** ambapo inahusisha Matumizi ya Kawaida na yale ya Miradi ya Maendeleo (**DEV**) ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa fedha 2022/2023;

(ii) Makadirio ya Matumizi ya Shughuli za kawaida yameongezeka kwa **asilimia 0.45** ambapo inahusisha matumizi ya mishahara (**PE**) na matumizi mengineyo (**OC**);

(iii) Mishahara (**PE**) katika Bajeti ya mwaka 2023/2024 inakadiriwa kuongezeka kwa **asilimia 0.15** pekee ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2022/2023;

(iv) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya shughuli za uendeshaji yaani matumizi mengineyo (**OC**) yameongezeka kwa **asilimia *5.0*** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(v) Bajeti ya matumizi ya Maendeleo (**DEV**) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **asilimia 7.82** ukilinganisha na ile ya mwaka wa fedha 2023/2024. Hata hivyo, ongezeko kubwa la bajeti ya maendeleo limeelekeezwa katika Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kiasi cha **Shilingi Bilioni 738.73 (sawa na 67%)**, huku kiasi cha **shilingi Bilioni 363.61 pekee (33%)** zikiwa zimeelekezwa katika maeneo mengine ya maendeleo, ikiwemo mafunzo ya walimu, utafiti, sayansi na teknolojia, uthibiti ubora na kuimarisha miundombinu na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia.

(vi) **Mheshimiwa Spika,** Ni vigumu kupata picha kamili ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya sekta yote ya elimu kwa kuwa sehemu kubwa ya fedha kwa ajili ya sekta ndogo za elimu ya awali, msingi na sekondari zinatengwa kupitia Ofisi

ya Rais-TAMISEMI. Hata hivyo, katika kuchambua bajeti ya wizara hii Kamati ilibaini kiasi cha **Shilingi Bilioni 138.50** kilichotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu ya awali, msingi na sekondari. Hii inaashiria kuwa bado kuna mgongano na muingiliano wa majukumu baina ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika uendeshaji wa sekta ya elimu nchini. Hii inathibitishwa pia na ukweli kwamba katika siku za hivi karibuni Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali katika uendeshaji wa elimu nchini, wakati hili ni jukumu la msingi la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**Mheshimwa Spika**, kwa upande wa Tume ya UNESCO **(*Fungu 18*)** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imekadiriwa kutumia **Shilingi 2,733,888,000/=.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,124,980,000/=** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 1,608,908,000/=** kwa ajili ya Matumizi mengineyo ya Tume.

**Jedwali Na.07 Mchanganuo wa Ulinganisho wa makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2022/2023 na mwaka 2023/2024 (fungu 18)**

| AINA YA MATUMIZI | FEDHA ILIYOIDHINISHWA 2022/2023 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024 | % ONGEZEKO |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 1,176,163,000 | 1,124,980,000 | - 4.35 |
| MATUMIZI MENGINEYO | 1,532,293,000 | 1,608,908,000 | 5.00 |
| **JUMLA** | **2,709,163,000** | **2,733,888,000** | **1.00** |

**Mheshimwa Spika,** uchambuzi wa Bajeti ya Fungu 18, Tume ya UNESCO unaonesha kuwa:

(i) Bajeti ya **Fungu 18** imeongezeka kwa asilimia 1.00 ikilinganishwa na Mwaka wa fdha 2022/2023;

(ii) Fedha za Mishahara imepungua kwa **asilimia 4.35** na hii ni kwa sababu ya kustaafu kwa baadhi ya Watumishi; na

(iii) Fedha za Matumizi mengineyo (**OC**) zimeongezeka kwa **asilimia 5.00** hali itakayo ongeza Ufanisi na tija katika utendaji wa Tume.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Mafanikio na Changamoto

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza serikali, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa ufanisi mkubwa wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/2023. Kwa kipekee kabisa, Kamati inaipongeza Wizara kwa kusimamia vyema mchakato wa mapitio ya Sera na Mitaala ya Elimu na Mafunzo na kukamilisha kazi hii muhimu kwa maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kamati inaipongeza serikali kwa kuendelea kuifanya sekta ya elimu kuwa moja ya vipaumbele vikubwa katika mipango yake ya maendeleo. Hali hii inadhihirishwa zaidi na ongezeko la bajeti ya kila mwaka kwa sekta ya elimu. Katika kipindi cha miaka mitano mfufululizo sekta ya elimu imekuwa ikitengewewa zaidi ya asilimia 17 ya bajeti kuu ya serikali, na hivyo kukidhi vigezo vya kimataifa vinavyotaka kuwa bajeti ya sekta ya elimu isipungue asilimia 16 ya bajeti yote ya serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, katika uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2022/2023, pamoja na mpango na bajeti ya mwaka 2023/2024, Kamati imebaini changamoto za jumla zifuatazo katika uendeshaji wa sekta ya elimu nchini.

(i) Mgongano na muingiliano wa majukumu katika uendeshaji wa elimu na uendeshaji wa shule kwa upande wa elimu ya awali, elimu ya msingi, na elimu ya sekondari baina ya Ofisi ya Rais – Tawala la Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mgongano na muingiliano unajidhihirisha katika maeneo ya utawala wa elimu, ujenzi wa miundombinu, na utoaji wa miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa elimu

(ii) Upungufu mkubwa wa wakufunzi na wahadhiri katika ngazi za elimu na mafunzo ya ufundi na amali na elimu ya juu

(iii) Kutozingatiwa kikamilifu kwa uhuru wa kitaaluma, ambao ndio msingi mama wa uendeshaji wa vyuo vikuu duniani. Hali hii inadhihirishwa na kutokuzingatiwa kikamilifu kwa Sheria ya Vyuo Vikuu ya Mwaka 2005 (hususani Kifungu cha 45e) na Charters za vyuo husika, katika uendeshaji wa vyuo vikuu na hususani ajira za watumishi wa vyuo hivyo

(iv) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya elimu ya juu nje ya mafunzo. Kwa mfano, sehemu kubwa ya bajeti ya elimu ya juu (67%) imeelekezwa kwenye kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Hali hii imefanya kuwa na bajeti finyu sana kwa ajili ya utekelezaji wa sekta za utafiti, sayansi na teknolojia, ambazo ni sehemu muhimu ya majukumu ya wizara hii. Uchambuzi wa taarifa za wizara unaonesha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya fedha za utafiti katika vyuo vikuu nchini hutoka nje ya nchi.

(v) Pamoja na kwamba Serikali imeonesha nia njema ya kuanza kutoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi katika vyuo ya elimu na mafunzo ya amali (vyuo vya kati), hakuna mkakati ulioandaliwa wala bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wake.

(vi) Kuna udhaifu katika uthibiti bora mashuleni kwa kuwa shule nyingi hazikaguliwi. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni shule za msingi 4,663 pekee zilikaguliwa ikiwa ni asilimia 26.4 ya lengo.

**Ushauri na Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na changamoto zilizoelezwa hapo juu, Kamati inashauri hatua zifuatazo:

i) Serikali ifanye tathimini ya kina kuhusu utekelezwaji wa sera ya ugatuaji katika sekta ya elimu ili kubaini changamoto na mafanikio yake. Aidha, kwa kibali chako, Kamati za Kudumu za Bunge za: Elimu, Utamaduni na Michezo na TAMISEMI zimpanga kufanya kikao cha pamoja kwa ajili ya kutafakari suala hili na kutoa ushauri wa pamoja

ii) Serikali iandae na kutekeleza mkakati wa muda wa kati na mrefu wa ajira za walimu wakufunzi na wahadhiri katika shule, vyuo vya elimu na mafunzo ya amali na vyuo vikuu

iii) Serikali isimamie kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Vyuo Vikuu katika kulinda na kudumisha uhuru wa kitaaluma, ikiwemo kuhakikisha kuwa ajira ya watumishi katika vyuo vikuu vinazingatia kikamilifu sheria hii na misingi ya ajira za wahadhiri katika vyuo vikuu duniani

iv) Serikali na wadau wengine kuandaa mkakati mpya wa ugharamiaji wa elimu ya juu, hususan katika kugharamia ada na gharama za chakula na malazi kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ili kutoa nafasi kwa bajeti ya shughuli zingine muhimu katika taasisi za elimu ya juu, ikiwemo utafiti na maendeleo ya sayansi na teknolojia

v) Wizara iandae mkakati kwa ajili ya ugharamiaji wa elimu na mafunzo ya awali, ikiwemo kuainisha vipaumbele kwa ajili ya wanafunzi watakaopatiwa mikopo katika vyuo hivi

vi) Kama hatua za muda mfupi, Serikali iimarishe uthibiti bora kwa kuongeza bajeti ili shule nyingi zaidi ziweze kukagaliwa kwa mujibu wa vigezo vilivyopo. Katika hatua ya muda mrefu, kuna haja ya Serikali kuunda chombo huru kitakachohusika na uthibiti ubora na usimamizi wa elimu kwa ujumla kwa ngazi ya awali, msingi na sekondari.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ninapenda kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa namna mnavyotekeleza majukumu yenu kwa umakini na weledi wa hali ya juu katika kuliwezesha Bunge letu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** ninapenda pia kumpongeza na kumshukuru sana ***Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb),*** Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, na wasaidizi wake, Mhe. Omary Shaban Kipanga (Mb), Naibu Waziri; na Prof. Carolyne Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake, na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wa kipekee kabisa, ninaomba uniruhusu kuwapongeza walimu wote nchini, pamoja na wakufunzi na wahadhiri katika taasisi mbalimbali za elimu nchini, taasisi za umma na taasisi za binafsi, kwa kazi

kubwa wanayoifanya ya kuelimisha na kulea kizazi cha leo na cha kesho kwa ajili ya Taifa hili. Tunawashukuru sana!

**Mheshimiwa Spika,** ninawapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati yetu ya Elimu, Utamduni na Michezo kwa kazi kubwa waliofanya tangu tulipoteuliwa mwezi Februari 2023, na kwa ushirikiano na upendo tulio nao katika kutekeleza majukumu yetu.
Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Prof Kitila Alexander Mkumbo, Mb M/kiti
2. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe.Aloyce John Kamamba, Mb
4. Mhe. Esther Edwin Maleko, Mb
5. Mhe.Hamisi Shabani Taletale, Mb
6. Mhe.Hassan Zidadu Kungu, Mb
7. Mhe.Kassim Ali Khamis, Mb
8. Mhe.Musa Ramadhani Sima, Mb
9. Mhe. Mwanakhamis Kassim Said, Mb
10. Mhe Nusrat Shaaban Hanje, Mb
11. Mhe.Rose Syprian Tweve, Mb
12. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
13. Mhe.Ahmed Yahya Abdulwakil, Mb
14. Mhe. Anastazia James Wambura, Mb
15. Mhe.Jumanne Kibera Kishimba, Mb
16. Mhe.Jenejely James Ntate, Mb
17. Mhe Dkt. T hea Medard Ntara,Mb
18. Mhe.Tunza Issa Malapo, Mb
19. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb
20. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb

**Mheshimiwa Spika**, Ninaomba nimalizie hotuba yangu kwa kumshukuru sana Katibu wa Bunge ***Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi***, *ndc* kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika kutekeleza majukumu ya Kamati Kiufanisi. Pamoja naye, napenda kumshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, *ndc* na

Mkurugenzi Msaidizi Ndg Gerald Magili pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg Eunike Donati Shirima na Ndg Happiness Ndalu wakisaidiana na Ndg. Waziri Kizingiti kwa kuihudumia Kamati na kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimwa Spika**, Ninaomba Kuwasilisha, na Ninaunga Mkono Hoja.

Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**

16 MEI,2023

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Profesa kwa kusoma vizuri.

Waheshimiwa sasa tunaanza michango na tunaanza mchango wetu wa kwanza na Mheshimiwa Rashid Shangazi, akifuatiwa na Mheshimiwa Esther Malleko, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Nianze kwa pongezi, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na kubwa ambayo anaifanya hasa katika eneo la kuboresha miundombinu ya elimu; elimu

msingi, elimu *secondary*, lakini pia na katika ngazi ya vyuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameelekeza pesa zile za UVIKO takribani shilingi bilioni 300 kwa mkupuo mmoja kwenda katika Sekta ya Elimu ambazo zimekwenda kujenga madarasa takribani 13,000 nchi nzima na sasa tumeweza kuona tija kubwa ya elimu, hasa katika eneo la miundombinu. Hii ni historia, ni lazima tuiseme bila kificho, kwa sababu, katika uhai wa Taifa letu hakuna uwekezaji mkubwa kwa wakati mmoja katika Sekta ya Elimu ambao umefanyika kuliko kipindi hiki cha miaka miwili ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nimpongeze pia, Waziri mwenye dhamana hii ya Sekta ya Elimu, kaka yangu, mtani wangu, Mheshimiwa Profesa Mkenda pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Kipanga, lakini na watumishi wote wa Wizara hii ya Elimu kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya. Kipekee niwapongeze kwa rasimu ile ya Sera ya Elimu, ni rasimu ambayo imekuja wakati muafaka na wakati sahihi. Niwaombe sana sasa waendelee kuchukua na kupata maboresho kutoka kwa wadau mbalimbali ili tuboreshe jambo letu hili liweze kuwa na tija ambayo tunaikusudia, lakini ambayo itakuwa ya muda mrefu zaidi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwapongeze Kamati, wamefanya kazi nzuri, wasilisho zuri. Kwa hiyo, kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia katika eneo ambalo Kamati imelitaja kama changamoto. Eneo ambalo kuna mgongano wa wazi kati ya taasisi mbili za Serikali, Wizara mbili; Wizara ya Elimu ambayo kimsingi inasimamia sera, lakini kuna Wizara ya Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa ambayo yenyewe inasimamia utekelezaji wa elimu katika Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa wawili kuna wakati wanatoa maelekezo ambayo yanawachanganya, hasa sekta binafsi. Kwa bahati mbaya sana sekta binafsi haina chombo ambacho inakisimamia, hakuna Wizara mahususi ambayo inaisimamia sekta binafsi ya utoaji wa elimu. Hawa kama Wizara wanasimamia eneo la sera peke yake, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanasimamia shule, lakini wanasimamia shule zinazomilikiwa na umma, maana yake ni kwamba, shule za sekta binafsi hazina msimamizi. Ndio maana kuna nyakati yanatoka matamko ambayo moja kwa moja yanaenda kuathiri utendaji kazi wa shule hizi za binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe kwamba, kama ambavyo pia Kamati imeshauri, ni vizuri Serikali ikatengeneza chombo ambacho kitakuwa kinasimamia Sekta ya Elimu msingi na sekondari, kwa maana kama *Tanzania Education Sector Authority,* ili iweze kuchukua wajibu kama wa *TCU* katika ngazi ya vyuo vikuu kwa sababu *TCU* wanasimamia vyuo vikuu vyote vya binafsi na vile vya umma, lakini ukija katika vyuo vya kati kwa maana ya vinavyotoa *certificate* na *diploma* ambapo kuna *NECTA VETA* pale, nayo inasimamia eneo la vyuo binafsi, lakini na vyuo vya umma. Kwa hiyo, hii itasaidia sana katika kuondoa huu mgongamo ambao upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo linafanyika, si jema sana kwenye sekta ya binafsi. Kuna tozo karibu 17 ambazo zinatozwa katika sekta binafsi. Kwa kweli, tunawanyanyasa kwa sababu, hawa ni watoa huduma, lakini sisi tunawachukulia zaidi kama wafanyabiashara. Kwa nini nasema ni watoa huduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukiangalia wanafunzi walioko katika shule za binafsi kuanzia awali mpaka sekondari

ni takribani wanafunzi 860,000. Maana yake ni kwamba, shule hizi zisingekuwepo Serikali ilikuwa ina wajibu wa kuhakikisha kwamba, watoto hawa wanakuwa na miundombinu, wanakuwa na Walimu, wanakuwa na *capitation,* wanakuwa na kila kitu ili waweze kupata elimu, lakini watoto hawa wakimaliza elimu huko wanakosoma, wanakuja kuajiriwa katika Taifa hili ambalo pia, watatoa mchango wao. Sasa ni kwa nini sisi bado tunaichukulia sekta ya binafsi ya elimu kama biashara, badala ya kuichukulia kama wasaidizi na watoa huduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo napenda kushauri kwamba tozo hizi 17 kama ambavyo tumeweza kupunguza tozo kwenye kilimo, tumepunguza tozo kwenye mazao mbalimbali na sasa tutazame tozo hizi katika sekta ya elimu, tukianza na *service levy* ambayo kwanza inakinzana hata na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa. Hili ni jambo la muhimu sana la kulitazama.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ukilitazama hapa utaona kwamba sekta binafsi ina mchango mkubwa katika eneo hili ni idadi ya walimu ambao wameajiriwa na sekta binafsi. Takribani walimu 55,000 hii ni idadi kubwa sana. Na hawa huko walipo wanalipa kodi za Serikali na wanasaidia sasa eneo zima hili la kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba zisingekuwepo hizi hawa nao ilikuwa ni tatizo ambalo Serikali ilibidi iwatafutie ajira. Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu sana, kuwatazama sekta binafsi kama watoa huduma na tusiwatazame kama wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninataka kulisema ni hili la udhibiti ubora ambalo limezungumzwa, ni jambo ambalo kwa kweli inabidi tutafute chombo ambacho ni huru zaidi kama *CAG* fulani hivi wa upande wa elimu, ili atoke katika ofisi ambayo haina hata mgongano wa

kimaslahi na hawa anaokwenda kuwasimamia. Hii itaongeza tija kubwa sana katika elimu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ni kikwazo, naliona sasa limekuwa kama ni *fashion,* kuna wakati tunazungumza suala la elimu bila malipo ama elimu bure ambapo Serikali inaweka ruzuku pale. Lakini sasa kuna utitiri wa mitihani ambayo inafanyika, kuna mtihani wa Kijiji, mtihani wa Kata, mtihani wa ujirani mwema, wa Jimbo, yote hii inakwenda kwa mzazi. Kwa hiyo, mzazi huyuhuyu aliyeondolewa mzigo wa michango huku anajikuta sasa anachangia mitihani ambayo imekuwa mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukatai, mitihani ni kipimo, lakini hawa walimu nao ambao kila siku wako katika hatua mbalimbali za kuandaa mitihani, mitihani yenyewe inatakiwa ichapwe, inatakiwa isimamiwe, inatakiwa isahihishwe, wanapoteza muda mrefu wa kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote tumesoma katika hizi shule. Huko zamani hakukuwa na utitiri huu wa kupima mitihani ambayo ni mingi kiasi hiki. Kwa hiyo, ninadhani kwamba ni busara sana tuangalie eneo hili vizuri kuona kama kuna tija ya huu utitiri wa mitihani. Kwa sababu pia unachukua muda mrefu sana kuanzia kuandaa, kusimamia, kusahihisha na mambo mengine. Kwa hiyo kwa maoni yangu, nadhani inapunguza muda wa kufundisha na ndiyo maana sasa watoto wetu wakati mwingine labda wanakuwa ni wa matokeo zaidi kuliko wa hali halisi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ninalotaka kulichangia ni suala la sekta binafsi kama ambavyo nimetangulia kusema na usimamizi mzima wa sekta hiyo, na hasa yale maeneo ambayo bado tunayaona kwamba hayana chombo kinachosimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni ilitokea sintofahamu ya mabasi yanayosafirisha watoto, hasa katika shule binafsi kwa sababu ndiyo zenye utaratibu huo, lakini yakatoka matamko kutoka kwa Kamishna wa Elimu na kwingineko, kitu ambacho kwa kweli siyo sawa, ni lazima hawa wadau wakae kwa pamoja waweze kutafuta suluhisho la pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yangu ni nini, maana yangu ni kwamba sasa hivi tukitazama, kwa mfano watoto wanaokuwa bweni wameambiwa waanzie angalau darasa la tano ni jambo jema, lakini lazima watu wakae kwa pamoja tutazame hizi changamoto vizuri ili tupate suluhisho la pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mabasi tusitake kuaminishwa kwamba wanaume ndiyo watu ambao hawafai katika jamii, kwamba akifanya kosa mwanaume mmoja basi wanaadhibiwa wanaume wote, kwamba sasa kwenye basi awepo mhudumu wa kike na wa kiume, lakini tunajua kabisa mmomonyoko wa maadili umeigusa jamii yote, wake kwa waume.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Malleko, wajiandae Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Dkt. Ntara.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika sekta hii muhimu kabisa ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu mpendwa, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya. Tumeona bajeti ya sekta ya elimu imeongezwa kwa wastani wa asilimia 18,

imetoka bilioni 4.7 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia bilioni 5.7 kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiache pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Kaka yangu, Mheshimiwa Profesa Mkenda, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Kipanga, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nitakuwa ni mchoyo wa fadhila pia nisipowapongeza Watendaji wote wa Wizara hii kwa sabbau tunaona kazi nzuri sana inayofanyika ya kuendeleza elimu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Wizara ya Elimu kwa kazi kubwa wanayoifanya. Tumeona wigo wa elimu bila ada umeongezwa kwa Kidato cha Nne, Kidato cha Tano na Kidato cha Sita. Serikali inatenga takribani shilingi bilioni 10.3 kila mwaka kwa ajili ya fidia za kulipia ada wanafunzi hawa, tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu imeongezwa sana na sasa imefika asilimia 14.7. Ilitoka bilioni 570 na sasa imefika bilioni 654. Jamani hilo ni jambo kubwa sana la kuipongeza Serikali yetu. Fedha za kujikimu wanafunzi wa elimu ya juu zimetoka kuanzia shilingi 8,500 hadi kufikia 10,000 hii ni hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Serikali, lakini bado sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto na mahitaji mengi. Niende kwenye changamoto chache. Leo kutokana na ongezeko kubwa la udahili wa wanafunzi wanaoendelea katika ngazi zote, mfano kidato cha kwanza, udahili umeongezeka kutoka wanafunzi 780,376 kwa mwaka 2021 hadi kufikia wanafunzi 173,941 kwa mwaka 2023. Hili ni ongezeko la asilimia 38. Kwa ongezeko hili tunakuwa tunahitaji miundombinu ya madarasa na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hii ya miundombinu na walimu, nianze na changamoto ya miundombinu. Miongozo inaelekeza kwamba darasa moja liwe na wanafunzi 45, lakini kwa sasa darasa moja lina wanafunzi 74 kwa shule za msingi. Kwa shule za awali mwongozo unasema darasa moja liwe na wanafunzi 40, lakini kwa sasa darasa moja lina wanafunzi 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na takwimu za *BEST,* kitabu hiki cha takwimu za elimu ambacho kinatolewa na Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI. Tunaona kwa uwiano huu tukisema mwalimu amfikie kila mwanafunzi mmoja mmoja, anawezaje kumfikia mwanafunzi mmoja mmoja katika msongamano mkubwa kama huu? Kwa hiyo tunaona ni namna gani elimu yetu haitafikia kile kiwango tunachohitaji kwa sababu huku kwenye msingi ndiko tunakoenda kukuza elimu ya wanafunzi ili waweze kufanya vizuri katika ngazi za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo inafanya shule za msingi kuwa na uhaba mkubwa sana wa madarasa. Na kwa sasa tuna uhaba wa madarasa takribani vyumba 102,485, ni uhaba mkubwa sana. Changamoto hii inasumbua sana katika ufundishaji na kwa utafiti uliofanyika inaonekana kuna vyumba ambavyo wanafunzi wanakaa hata zaidi ya 100 kwenye chumba kimoja. Kwa hiyo tuangalie namna ya kuweza kurekebisha changamoto hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye changamoto ya pili ambayo ni walimu; kwa mujibu wa Hotuba ya Bajeti ya TAMISEMI ya mwaka huu, shule za msingi zina uhaba wa walimu 100,958 na shule za sekondari zina uhaba wa walimu 74,743. Pamoja na TAMISEMI kupata kibali cha kuajiri walimu 13,130, bado uhaba wa walimu utaendelea kubaki kwa sasa tutakuwa na uhaba wa walimu wa takribani 162,551.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea kuajiri kwa utaratibu huu itatuchukua miaka 10 mpaka 15 kuweza kutatua changamoto hii ya walimu. Nasema hivyo kwa sababu wakati Serikali inaajiri kuna walimu wanastaafu na kuna walimu wanaofariki, lakini pamoja na hao wanafunzi bado wanaendelea kudahiliwa kwa hiyo ongezeko la wanafunzi linaendelea kuwa kubwa na wakati changamoto ya walimu ikiendelea kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sensa yetu ya 2012, Watanzania walikuwa milioni 44 na sasa ni milioni 61. Inaonekana hapo katika hiyo miaka kumi hao watu waliozaliwa ni watoto na wanahitaji elimu, sasa tusipotengeneza miundombinu mapema ukifika wakati huo tutapata changamoto, wanasema ukitaka kuliua Taifa uue elimu, kwa hiyo sisi tunataka kuboresha kwenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwenye jambo hili, ninaishauri Serikali iweze kuongeza bajeti ya elimu kwa asilimia 20. Kuna Azimio la Incheon la Mwaka 2015 ambalo lilizitaka nchi zote zilizo Ukanda wa Kusini mwa Jangawa na Sahara ziweze kutenga asilimia 20 ya bajeti yote ya Taifa kwenda kwenye sekta ya elimu ili kuweza kukabiliana na changamoto kama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itaweza kutoka hapa kwenye asilimia 18 tunayotenga sasa tukaenda kwenye asilimia 20, tunaweza kutatua changamoto hizi ambazo ni za miundombinu na walimu tukaweza kuajiri walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaishauri Serikali iangalie itakuja na mpango gani mahsusi wa kuweza kuajiri walimu kuendana na ongezeko. Tumeona ongezeko la watoto na upungufu wa walimu. Kwa hiyo, ninashauri Serikali ije na mpango wa miaka mitano, mitano wa kuona katika kipindi cha miaka tunaangalia uhaba wa walimu tulionao

tunaugawanya kwa hiyo miaka mitano, tunaona ni namna gani tunaweza kuajiri walimu, hata tukiajiri kila mwaka walimu 25,000 tutakuwa tumepunguza sana tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongeze pale alipokuwa amechangia Mheshimiwa Shangazi. Leo sekta ya elimu inasaidiana sana na wadau hawa wenye shule binafsi, kwa sababu nia yetu ni moja kuweza kuendeleza wanafunzi au Watanzania kupata elimu bora. Sasa inapoonekana upande huu wa wadau wa elimu na Serikali wanakinzana inaonekana kama kuna namna fulani ambayo hawaendi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo yanafanyika ambayo siyo mazuri, wawekwe pamoja wazungumze, watatue hizo changamoto.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Malleko kwa mchango mzuri.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja tu nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde mbili.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kuna mbunifu anaitwa Mataka, ameweza kubuni namna gani ya kufanya ufundishaji wa Hisabati, Kiswahili pamoja na Kiingereza…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, mengine andika, unawakosesha wenzako. Mheshimiwa Nyongo, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Ntara na Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami awali ya yote nitoe pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa fedha nyingi anazozitoa kwa ajili ya ujenzi wa sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Mama ametoa fedha nyingi sana kwa maana ya kupeleka fedha kwenye sekta ya elimu pamoja na sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, kwa kazi kubwa anayofanya, pamoja na Naibu Waziri wake ambaye ni Mheshimiwa *QS* Kipanga. Vilevile nimpongeze sana Katibu Mkuu wa Wizara hii, Dada yangu Profesa Carolyne Nombo, anafanya kazi vizuri sana na Naibu Makatibu wakuu wake wwili ambao ni Profesa James Mdoe na Dkt. Rwezimula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi kwa Kamishna wa Elimu ambaye ndiyo Mwalimu Mkuu wa Tanzania pamoja na Wakuu wa Taasisi zote ambazo ziko chini ya Wizara hii ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nikueleze, katika Wizara ambazo wanasikiliza ushuri, Wizara ya Elimu wanasikiliza sana ushauri na hasa wa Kamati. Mnafahamu mimi nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, nimefanya nao kazi, kwa kweli Wizara ina viongozi wanaosikiliza sana ushauri wa Wabunge. Mwenyezi Mungu awabariki kwenye jambo hili, endeleeni kusikiliza ushauri na kuishinikiza Serikali kutimiza yale ambayo Wabunge wanayashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kupongeza Wizara na hasa katika Jimbo langu la Maswa Mashariki. Wamenipa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi ya Mwabalatulu katika Kata ya Mpindo, lakini vilevile wamenipa fedha kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wasichana katika Shule ya Mwangala Sekondari, wamenipa fedha kwa ajili ya ujenzi au ukarabati wa shule kongwe ambayo fedha tulipeleka katika Shule ya Msingi Shanwa. Kwa kweli ukarabati umefanyika na kwa kweli wamefanya kazi kubwa na nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado niendelee kushukuru kwa fedha walizozitoa katika programu ya ujenzi wa shule 63 za *VETA,* Maswa nayo imekuwa mnufaika, tumepata fedha ambayo inakwenda kujenga shule ya *VETA* na kwa kweli ujenzi huu unaendelea. Niwaombe Wanamaswa wenzangu kwamba tuusimamie vizuri ujenzi huu ili tuweze kupata shule kwa haraka na watoto wetu waweze kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kupongeza Wizara hii, kama nilivyosema wanasikiliza ushauri. Niwapongeze sana kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuandaa mitaala na sera ya elimu. Tumeona hapa juzi Tarehe 12 – 14 kongamano kubwa hapa Dodoma. Haijawahi kutokea, watu 1,500, wataalam mbalimbali wadau wa elimu wamekuja katika Mji wa Dodoma kutoa mawazo yao kuhusu namna ya kuboresha sera na mitaala ya elimu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado taarifa kupitia kwa Mheshimiwa Waziri inasema kuna Watanzania 250 nao ni wataalam, wametoa maoni yao na ushauri wao kupitia njia ya mtandao katika kuhakikisha kwamba wanatoa michango yao ili kuboresha suala la elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutoa ushauri katika sekta ya elimu ya ufundi. Tumeona ujenzi wa *VETA,* kila Wilaya *VETA* zinakwenda kujengwa. Tumeona mikakati ya Wizara ya Elimu katika kutoa elimu ya ufundi, sawa kabisa. Ushauri

wangu tuendelee kuwafundisha walimu ambao watakwenda kufundisha elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru mkakati wa Wizara ya Elimu mmetenga vyuo kumi vya mwanzo kwa ajili ya kutoa elimu ya walimu wanaokwenda kufundisha ufundi. Mahitaji ya walimu wa ufundi yanakwenda kuongezeka, tunaomba sana vyuo hivi ambavyo mnakwenda kuviandaa basi mviandae vizuri na kuhakikisha kwamba mnafanya udahili wa kutosha kuhakikisha kwamba vijana wengi wanakwenda kupata elimu ya ufundi na ufundi wenyewe ni ule wa kisasa kwa teknolojia za kisasa ili hawa waende kuwafundisha wanafunzi katika hivi vyuo ambavyo tunakwenda kuvianzisha katika kila Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa sababu tunakwenda kujenga vyuo vya *VETA* lakini tusipokuwa makini tutaanza tena mgogoro uleule wa kutafuta walimu wa ufundi. Kwa hiyo, ni lazima tujiandae kwa hili. Tunajenga vyuo, basi tuandae na *human resources* kwa maana ya walimu wanaokwenda kufundisha elimu hii ya ufundi katika vyuo hivyo, hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vyuo hivi vinavyokwenda kujengwa, baada ya muda kidogo, miaka miwili, mitatu kutakuwa na uzalishaji wa wanafunzi ambao wamepewa elimu katika vyuo hivi. Baada ya kuzalishwa katika vyuo hivi, hao wanafunzi wanakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri. Kwanza Wizara hii pamoja na Serikali kupitia Hazina, Waziri wa Fedha kama yupo ananisikia, tuanze kutenga fedha kwa ajili ya *training factories* katika Wilaya zote hapa nchini. Hizi *training factories* zitaendelea kupokea wanafunzi, watajifunza wanafunzi mbalimbali, lakini hizi *factory* zitumike kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali ambazo zinatokana na mazingira husika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ambao ninaweza nikautoa katika hili, kuna maeneo ya uchimbaji wa madini, kwa mfano uchimbaji wa dhahabu, kuna mitambo mingi inatumika maeneo yale na kuna vipuli vinaagizwa kutoka maeneo mbalimbali, lakini tukiwa na *factory industries,* yaani kwa maana ya kwamba viwanda vidogo ambavyo vinaweza vikazalisha vipuli katika maeneo hayo, na wanafunzi wa maeneo yale wakaingia kwa ajili ya uzalishaji wa vipuli katika maeneo hayo hayo, hili litakuwa na tija kwa maana ya kwamba wataendelea kupata mafunzo na pia wataendelea kupata kipato kwa sababu watakuwa wanazalisha. Kwa hiyo, hizi *factories* ni *very very important.* Serikali sasa ianze kuangalia kwa sababu tayari tunakwenda kupata *output* kubwa ya wanafunzi waliojifunza katika vyuo hivi vya *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kushauri tena, tumeambiwa, hata msemaji aliyepita amezungumza kwamba tukitaka kujenga Taifa, tujikite katika kuwekeza kwenye elimu, lakini vile vile tuelewe kabisa kuwekeza kwenye elimu ni njia ya kumkomboa kijana wa Kitanzania. Pia kuna jambo lingine la michezo ambalo Mheshimiwa Waziri amezungumza, kwenda kuanzisha vyuo vya michezo kwa maeneo mbalimbali. Kwa kweli lazima tufundishe vijana wengine ambao wanakwenda kufundisha elimu ya michezo katika vyuo mbalimbali. Tuna vijana wa kitanzania wana uwezo mkubwa, wana vipaji vya mpira, michezo mbalimblia ikiwa ni pamoja na vipaji vya usanii kwa maana ya kuimba na kucheza ngoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tupate walimu wa kufundisha na kuweza kufanya *talent identification.* Siyo hivyo tu, ni lazima tuweke na mkakati wa kufanya *talent development,* kwa maana ya kwamba lazima vipaji hivi viendelezwe ikiwa ni pamoja na yale masuala ya uvumbuzi mbalimbali ambao tayari Wizara ya Elimu imeanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwenye suala la *UNESCO*. Niungane na Kamati, imetoa ushauri mzuri, na tumekuwa tukitoa ushauri mara kwa mara. Tume ya *UNESCO* iko chini ya Wizara ya Elimu. Tume ya *UNESCO* haifai kukaa chini ya Wizara ya Elimu. Serikali naomba msikie, Tume ya *UNESCO* inasimamia mambo mbalimbali na mambo mtambuka ikiwemo masuala ya urithi wa dunia. Kwa mfano, yule mjusi mkubwa aliyeko Ujerumani, mtu wa kwanza kwenda kumdai yule mjusi ni Tume ya *UNESCO*. Sasa lini Wizara ya Maliasili itaongea na Wizara ya Elimu kuhusu *UNESCO* aibuke aende kule kumdai yule mjusi?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *UNESCO* ni suala mtambuka. Kamati imesema kwamba iende kwenye Wizara mtambuka. Ingesema tu moja kwa moja *straight* kwamba *UNESCO* iende chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ikafanye kazi yake vizuri. Hilo naomba nitoe ushauri, na kwa kweli bila kufanya hivyo *UNESCO* itaonekana kama vile ni mtoto ambaye hajaliwi na Wizara ya Elimu, na kwa kweli hana kazi na Wizara ya Elimu. Ana *component* moja tu. Tunaomba sana, ushauri wa kamati unaposema kwamba *UNESCO* iondolewe chini ya Wizara ya Elimu, ushauri huo uzingatiwe, iende chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ikafanye kazi yake inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ntara, jiandae Mheshimiwa Neema Lugangira na Mheshimiwa Aloyce Kamamba.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa, nami nipongeze sana kwa kazi

nzuri inayofanywa katika Wizara ya Elimu. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuyatenda hayo, nampongeza Waziri na watendaji wote na hasa Wakurugenzi wa taasisi mbalimbali katika Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zangu zinakwenda kwa sababu sasa hivi tunaona vyuo vya ufundi vinajengwa vya kutosha halafu kuna hii *project* ya *HEET* imesaidia sana katika kuboresha mitaala na pia ujenzi wa mashule. Pia hii bodi ya mikopo tulianza na shilingi bilioni 450, leo hii shilingi bilioni 654 ndiyo zimepelekwa kwa wanafunzi. Hili jambo Waheshimiwa Wabunge wenzangu limeleta utulivu mkubwa sana katika vyuo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba tu hapo kwenye *HEET,* Mheshimiwa Waziri ananisikia, mmetoa mgawanyo mzuri sana wa *Universities* hizi za Serikali, sasa tupate hata mgawanyo wa fedha za *HEET* katika *universities* zile za binafsi, tunaziita *private universities;* ule mgawanyo mnasema kwamba wao wamepewa fedha kwa ajili ya kuwasomesha, lakini tupate mgawanyo unaoonesha kwamba, je, *universities* zitapata mgawanyo wa walimu wangapi kwenda kusoma, ili na wao watulie? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwa hawa watendaji wa kati. Watendaji wa kati ndio msingi mkubwa sana wa kuchochea maendeleo hasa kwenye uchumi. Vyuo vyetu vitano kama unakumbuka; *DIT, MUST, ATC, NIT* na kile Chuo cha Maji viliondoa kabisa malengo yake ya zamani. Yale malengo yaliondoka kabisa, kwa sababu vyuo hivi vyote sasa vilijikita katika kutoa shahada. Siyo vibaya, lakini naomba sasa vyuo hivi virudi kwenye malengo yake ya zamani, ndiyo tutapata hao mafundi tunaowaita mafundi mchundo na wahandisi. Wajikite pia katika yale malengo ya zamani kama nilivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kozi za kati kwa sasa hivi kwa wasichana ni asilimia 25 tu kwa taarifa, sasa tuangalie, tuongeze juhudi za kuona wasichana pia wanajiunga katika hizo kozi za kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Tanzania uwiano wa watendakazi kwa sasa, nina maana ya mhandisi, fundi mchundo na mafundi stadi ni kumi kwa tisa kwa saba (10:9:7). Sasa hii haikubaliki, tumegeuza. Sasa muundo au uwiano unaotakiwa kidunia au kiulimwengu ni moja kwa tano kwa ishirini na tano (1:5:25). Yaani unapokuwa na mhandisi mmoja, basi uwe na hao mafundi mchundo watano, uwe na mafundi stadi Shirini na tano, lakini sisi tunafanya *vice versa* na ndiyo maana tunapata shida sana katika watendaji hawa mafundi mchundo na hawa mafundi stadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumegeuza ndiyo, tunazalisha shahada, siyo mbaya, lakini sasa tuone, kama nilivyosema, ukuaji wetu wa uchumi sasa hivi tujipange kuona kwamba hawa mafundi watendaji kazi wanakuwa wakubwa zaidi na namba yao inaongezeka zaidi. Sisemi kwamba shahada tuziondoe, Hapana, la hasha, lakini nasema tujipange kuona kwamba uwiano huu twende kidunia zaidi, ndiyo tunaweza kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali sasa kuongeza hiyo bajeti ya mikopo, wastani wa asilimia 70 mpaka 80 zinakwenda kwa wanafunzi wale wanaochukua masomo ya *arts,* hiyo ndiyo taarifa. Yaani wa masomo ya *arts* asilimia 70 mpaka 80 ndiyo zinakwenda kwao, ukiangalia hii bajeti ya mikopo. Sasa ukiangalia wanafunzi wanapomaliza masomo, wengi wao wanakaa muda mrefu sana bila kupata ajira, lakini ndio wamechukua hiyo asilimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa tuanze kujitafakari, yaani hiyo iwe katika mpango, akilini mwetu, tuanze kujipanga sasa. Je, watoto hawa wanaomaliza Kidato

cha Nne na cha Sita, siyo vema wakaanza kupata mikopo ili waweze kujiunga na kusomea ujuzi uwasaidie kujiajiri? Hilo mliweke yaani kama mpango wa baadaye, muanze kulifikiria sasa hivi. Maana yake tunapompa mkopo huyu mtoto anayemaliza Chuo Kikuu halafu unakuta hata ajira hana, amesoma tu shahada, ajira hana. Inaleta shida na wakati mwingine kumwongezea mzigo wa umasikini. Kwa hiyo, tujipange kwenye eneo hilo tuione kama sasa tunaweza kufanya, akimaliza *form four* au *form six,* anapata mkopo, anakwenda kwenye fani za ujuzi na kuweza kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye ujenzi wa vyuo vikuu. Hili nalisema kwa masikitiko makubwa sana. Mkoa wa Mtwara na Ruvuma, yaani hata ukiangali vile vyuo vikuu vya *private* vingi vimekufa. Nilikuwa nafikiria, hivi Serikali, haiwezi kusaidia? Kwa mfano, tulikuwa na chuo cha udaktari pale Peramiho, kikafungwa, wale wanafunzi wakapelekwa Mbeya. Yale majengo yako pale, wananchi wa kuzunguka yale maeneo ya Peramiho waliwekeza sana katika majumba na mashamba, lakini sasa hivi wamebaki pale hakuna kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukafikiria wakati mwingine tukasikia kuna chuo Tunduru, *Branch* ya *SUA*. Ghafla tukaona ile *SUA* imekwenda Katavi. Siwaonei wivu, wala sikatai, lakini pale ambapo wazo la Tunduru lilianza, kwa nini halikuendelezwa, badala yake sasa nguvu ziko Katavi? Sasa wanasema huenda kikaendelezwa. Naomba Mheshimiwa Waziri Chuo cha Tunduru pale *branch* ya *SUA,* nguvu mnazozipeleka kule Katavi zianze pale kwanza, kwa sababu Katavi ilikuwa ni ya pili. Kule hatuna mradi mkubwa, nikwambie ukweli. Hatuna mradi mkubwa wowote Ruvuma wala huko Mtwara. Miradi mikubwa na sisi tunaipenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mnafikiria kujenga Chuo Kikuu sijui cha *IT* Dodoma, niliwaza sana. Kwa nini hamkukipeleka Ruvuma? Dodoma kuna hii *UDOM* ambayo

sasa hivi imekuwa kubwa na ina changamoto za kutosha. Kwa nini hiyo *IT* mnayosema chuo kikubwa kinajengwa hapa Dodoma kisijengwe hata kule kusini tukawa na sisi na mradi mkubwa? Miradi mikubwa nasema hata ya maji, hatuna, Ruvuma na Mtwara ni shida. Kwa hiyo hii ya vyuo, niwaombe sana msaidie kama ambavyo Mheshimiwa Mkapa alivyosaidia ile *Muslim University* ya pale Morogoro, walikuwa na changamoto ya majengo, akawasaidia akawapa majengo. Serikali ulizeni hivi vyuo, kwa nini hiki chuo cha udaktari pale Peramiho kimekufa? Kwa nini kile chuo kingine cha St. Joseph, Ruhuiko kinakufa na ninyi mpo? Hebu wasaidieni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo vyuo vikuu, nirudi tena. Kila siku tunaongea hapa, Chuo cha *UDOM* ni Chuo Kikubwa Afrika Mashariki. Nenda pale, utashangaa. Yale majengo yanaporomoka, *roof* inaanza kudondoka, vigae chini vimepasuka, na mabomba ya maji yamepasuka. Nimekwenda pale nikaingia kwenye vyoo vya kule *UDOM,* yaani mpaka unaona aibu. Kuna mlipuko utatokea. Maji yanapotea pale kwa sababu mabomba yote yamepasuka. Wana upungufu wa maji karibu lita milioni 1.1, Serikali mpo. Sitaki Mheshimiwa Waziri tuongozane, nenda ukaone *UDOM,* hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu pale pale *UDOM* kuna jengo la Chimwaga. Ule ni ukumbusho mkubwa sana. Sasa tuangalie, Chimwaga tunaiacha hivi hivi? Tuliingia mle ndani wakati tunafanya lile kongamano, yaani unaingia mle ndani unafurahi. Ni ukumbi mkubwa mno, lakini angalia nje. Ynatakiwa ukarabati ufanyike, tena kwa kumuenzi Mwalimu Nyerere na kwa kuenzi Makao Makuu ya hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia shule kongwe. Kuna shule kongwe zimesahaulika kabisa. Kuna shule kongwe ambayo Mheshimiwa Mkapa amesoma huko, Marehemu Mheshimiwa Profesa Mbilinyi alisoma huko,

inaitwa Shule ya Kigonsera, hakuna maktaba, *you can't imagine*. Kuna *form five,* pale wapewe maktaba, na watoto wajifunze kujisomea, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nimeambiwa Mheshimiwa Neema atachangia jioni, kwa hiyo sasa atachangia Mheshimiwa Mafuwe, ajiandae Mheshimiwa Kamamba na Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli kwenye sekta ya elimu kule kwetu Hai amefanya mambo makubwa sana. Pamoja na kwamba ni TAMISEMI, lakini kwa kweli tunashukuru shule zetu zile kongwe, kwa maana ya *Machame Girls* na Lyamungo, sasa hivi zinang'aa, zimefanyiwa marekebisho; pale *Hai Day* na kila mahali kwa kweli kwenye sekta ya elimu ametufanyia mambo makubwa sana. Nampongeza na apokee salamu nyingi za shukurani kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayofanya kwenye sekta hii. Hongera sana. Naibu Waziri pamoja na wasaidizi wako wote tunatambua mchango mkubwa sana. Pia nawashukuru sana walimu wetu na watendaji wote kwenye sekta ya elimu kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa Taifa letu. Ikumbukwe haya yote tunayojadili kwenye bajeti hapa, mtekelezaji wake kwenye ubora na kwenye kila kitu ni wale watumishi. Kwa hiyo, naomba nitambue mchango wao mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwenye sekta ya elimu na afya kuna wadau wetu wa maendeleo, na hawa sio wengine ni taasisi za dini. Naomba kwa nafasi hii nimshukuru sana Shehe Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, kuna taasisi nyingi zinatoa elimu kule kwetu Hai kama Mudio na nyingine. Pia

namshukuru Baba Askofu Dkt. Fredrick Shoo, ametuletea pale kwetu chuo kikuu, kinaendelea pale. Vile vile pale *KCMC* kuna chuo kizuri ambacho kinatoa elimu kwa wauguzi wetu na madaktari wetu, nawapongeza sana. Kipekee, nampongeza sana Dkt. Masenga kwa kazi nzuri anayoifanya pale *KCMC* na kule Mkwarungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kuzungumza eneo moja linalohusu stahiki za Wahadhiri wa Chuo Kikuu. Tumekuwa tukizungumza hapa habari ya walimu, tumetoka kwenye walimu, na leo naomba nizungumzie Wahadhiri wa Vyuo Vikuu. Bahati nzuri na Waziri naye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu, anaelewa adha ambayo wanapata Wahadhiri wenzake. Tusipotazama eneo hili tukawapa heshima stahiki, hata hii mitaala tunayoenda kuiandaa bado haitatusaidia, kwa sababu watekelezaji na wasimamizi ni hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mwalimu anayesimamia *research* ana wanafunzi zaidi ya 20. Hebu niambie, tunaenda kutengeneza watu wa *Ph.D* wa aina gani? Nami kwa ku- *declare* tu, ni mwanafunzi wa *Ph.D* pale *UDOM*. Kwa hiyo, naona ugumu ulivyo. Unamtafuta mwalimu wiki tatu, na siyo kwa makusudi anafanya hivyo, lakini ana wanafunzi wengi. Akitoka hapo, unakuta anamiliki saluni Dodoma. Hata walioko kule *SUA* ambao tulitegemea wamiliki mashamba, wamiliki mifugo, tunakutana nao wanamiliki *bar* huku. Kwa nini wanafanya hivi? Stahiki zao hazitoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, leo nitasimama hapa kuomba sana Mheshimiwa Waziri, ninafahamu linahusisha Wizara nyingi, lakini kwenye eneo hili kaa na Wizara wenzako wanaohusika kwenye jambo hili, tuwape heshima hawa wahadhiri, ndiyo kiwanda kinachofyatua watu wa kuja kutusaidia kwenye sekta zote. Tukiendelea kuwaacha, waache ku-*concentrate* kwenye eneo la elimu, wakawa na shughuli nyingi wanazofanya za kujitafutia kipato,

hatutawatendea haki. Nami nashauri, hawa watu, wakifika *level* fulani ya uprofesa, ili aweze kutulia kule alipo afanye kazi yake kwa umakini, ni lazima tuangalie stahiki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimeanza viashiria vya utafiti wangu, kuona ni kwa namna gani watu wanaotoka kwenye taasisi za elimu kukimbilia maeneo mengine, hata humu ndani, *gap* linalobaki kule, nani anayelitunza? Naomba sana, majibu ya haraka ni kwamba hawa watu wapate stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumze kuhusiana na nidhamu ya wanafunzi walioko chuo kikuu. Mheshimiwa Waziri tusipotazama jambo hili litatuletea shida. Hao walioko chuo kikuu wengi wanasoma *degree*. Kwa hiyo, tunawaandaa kuwa viongozi. Sijui ukipita hapo Dodoma unajifunza jambo gani, au pale *UDOM*? Ukimwona kijana aliyeko sasa hivi mwaka wa tatu, anafanana kuandaliwa kuja kuwa kiongozi na msimamizi wa taasisi wa Serikali? Wakati mwingine wahadhiri kule wanalalamika kwamba eti sisi wanasiasa, wakiguswa kidogo, sisi ndio tunawatetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisimame hapa niseme kwamba hawa ndio viongozi tunaowaandaa. Ukimwona mtoto mwenye *degree* leo, unapishana naye Mheshimiwa Waziri, kwa kweli inasikitisha. Huwezi kumtofautisha na aliyeko *Form Two* na anayesomea *degree*.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakutana na mtoto kala ndala anapita kwenye mitaa ile *physical appearance* ya kuandaliwa kama kiongozi haifanani. Niombe mambo haya, wenzetu wa *SAUT* wamejitahidi sana kufanya hivyo. Mambo ya nidhamu yanaenda sambamba na utoaji wa taaluma, hatuwezi kuviacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwenye eneo hilo pia…

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana kabisa na anachokizungumza Mheshimiwa Saashisha. Wanafunzi wengi wanakulia *boarding schools,* wanapofika kwenye *level* ya chuo kikuu wanakuwa wamepata uhuru mkubwa sana. Mwanafunzi mazingira haya anakuwa hana *control* yoyote na hawa ndio wanategemewa kuja kuwa watumishi wetu. Mheshimiwa Waziri pia wanafunzi wanao *disco* idadi imekuwa ni kubwa sana kwenye vyuo kutokana na jambo hilo ni vema Serikali ikaangalia jinsi gani ya kuli–*control.*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha, taarifa hiyo.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa mikono miwili na niendelee kusisitiza kwa kweli Mheshimiwa Waziri tazama eneo hili ili tuweze kupima elimu yetu kabla hatujaenda kwenye utekelezaji wa mtaala mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie kwenye kuchangia mtaala mpya ambao tunaendelea na majadiliano nao. Nilikuwa natamani Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa utuambie hivi mmefanya tathimini ya utekelezaji wa mtaala wetu tangu tumepata uhuru mpaka hapa tulipo umetupa matokeo gani? Nitaomba kupata hilo na kama hatujafanya wakati tunaendelea basi tuweke fikra zetu kutazama huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikisema hapa Mheshimiwa Waziri na mwaka jana nilichangia, kwamba mawazo yangu ninafikiri ili tuwe na mtaala mzuri tutanguliwe na malengo ya Serikali na sijui kwa nini linakuwa gumu hili? Nichukue wito huu kukuomba wewe una wataalam wengi

Maprofesa wako huko hebu wafanye utafiti ni namna gani nchi yetu inaweza ikawa na malengo na maono ya muda mrefu. Tuwe na *Tanzanian interests* za kwetu ambazo tulitekeleza kwa kipindi cha miaka 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungekuwa na malengo hayo na maono hayo ya miaka 100 tunapokuja kutengeneza mtaala huu unatakiwa u–*reflect National objectives*. Yale malengo ya Serikali ya miaka mitano, malengo ya Serikali ya miaka 100 basi mtaala huu unamwandaa mtanzania aweze ku-*fit* kwenye malengo tunayotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tumeshaanza mchakato kwa kutazama malengo ya miaka mitano *fine*. Lakini tunajua mtaala huu muda wake wa utekelezaji unaendelea hauna kikomo. Utaendelea kufanyiwa marekebisho kama huko nyuma ambavyo imekuwa ikifanyiwa marekebisho. Sasa kama ni jambo kubwa namna hii ni lazima tutengeneze dira na tusiwe waoga wa kufikiri mambo makubwa. Hata wenzetu ambao wanakwenda kwenye sayari za *mars* walianza kama sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuweke malengo makubwa, maono makubwa ya kufanya mtaala huu huko unakoenda uweze kujibu matarajio ya mahitaji ya wananchi. Niseme tu mtaala huu u–*focus* mara nyingi tumekuwa na shida ya *career choice* ya watoto wetu. Mwanafunzi anakwenda chuo kikuu hana maono hajui anafika kwenye jambo gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tutumie mfumo wa *co-curriculum* kutazama elimu au mtaala huu tunaotengeneza ukaongezee talanta aliyonayo mtoto. Kuliko kulazimisha mtu hana sifa ya kusoma sheria mradi tu baba yake alisoma sheria tumlazimishe aende huko. Niombe namna ya kutama *career choice* liwe kama somo ambalo linalofundishwa kuanzia kidato cha tano na sita ili watoto waweze kujiandaa wanakwenda kuwa wakina nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na mwonekano na mawazo yaliyoko kwenye mtaala huu mpya unaokwenda sasa kugusa ujuzi. Mheshimiwa Waziri, niombe na nilisema hapa mwaka 2022 eneo hili libaki la kwetu ndani, na hata kama kuna utekelezaji unaohusika tusihangaike sana na hela za watu. *Password* ya maendeleo yetu, *password* ya uwezo wetu wa kufikiri uko kwenye *knowledge* na *skills* za watu wetu. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri tafadhari tazama eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningetamani kugusa, wapo walimu wastaafu, kwa kuwa wewe ndio Baba yao na wewe ndio mlezi wao wengi wamestaafu miaka mingi. Ninafahamu utaratibu wa vikokotoo ulivyo, wao wametumikia Taifa wengine mara baada ya uhuru, wengine wale ambao wachache wamebaki, na wengine miaka ya 50, miaka ya 40 wamestaafu, unakuta wanacholipwa ni kidogo mno. Hapa nina *messages* nyingi wanaomba jamani wakumbukeni, nikuombe sana kaa na Wizara ya TAMISEMI, kaa na Waziri wa Fedha, muone namna ya kuwakumbuka hawa wastaafu ambao wameitumikia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *formula ile* iliyokuwa inatumika wakati ule sambamba na kwa wahadhiri wa vyuo vikuu, *formula* iliyotumika wakati wanastaafu haikuwa rafiki kwao. Pamoja na uchumi wetu bado haujakuwa katika kiwango hicho naomba muwatazame. Unakuta mtu analipwa shilingi 20,000, shilingi 50,000, hebu tutazame viwango hivi pamoja na kwamba ninafahamu kulikuwa na formula ya wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho niombe sana, Wizara ya Afya wametengeneza *guideline* ya wale wauguzi na watoa huduma wa afya wanaojitolea. Hebu na hapa Mheshimiwa Waziri, tafuta utaratibu wa kutengeneza na

wewe *guideline* ya walimu wanaojitolea kwenye shule zetu ili inapofika wakati wa ajira kuwe na *guideline* inayowaongoza.

Mheshimiwa Spika, pia hata kama sio kuajiriwa, kwa maeneo yale ambayo Serikali hatujaweza kufika kwa maana ya kuajiri kuwe na mwongozo *proper* unaowaongoza kuelekea kupata ajira lakini hata kuajiriwa na kulipwa na wazazi kuwe na mwongozo fulani unaowaongoza ili kuepuka mkanganyiko ambao unajitokeza sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho Mheshimiwa Waziri, ninakuomba, zamani tulikuwa na mitaala inayotoa elimu ya ufundi kwa shule za misingi. Kwa mfano; pale kwangu Hai tulikuwa na shule kama nne zinatoa elimu ya ufundi. Zilikuwa zinaitwa shule ya msingi ufundi, shule kadhaa mtaala ule au utaratibu ule umesitishwa na mitihani imesitishwa. Lakini kuna majengo, kuna walimu na kuna rasilimali. Niliwahi kuuliza swali hapa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, akatuambia kwamba hizi shule zimefutwa na sasa tunaelekea *VETA*. Lakini hizi rasilimali zilizoko katika hizi shule nani anazitunza?

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea pale kwangu tumekwishajenga Chuo cha Ufundi cha Rundugai na sasa hivi tunahangaika na Losaa, zile mali na vifaa vile ambavyo vilikuwa kwenye shule hizi za msingi namna ya kuvihamishia viende kwenye vyuo vyetu kuliko kuviacha vitu vinaozea pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna walimu wana taaluma hizi, niombe wawe *allocated* kwenye maeneo ambayo wanaweza kwenda kuisaidia nchi yetu. Ikishindikana, kama maeneo hayana shule basi waingizwe kwenye vyuo vya *VETA* ili wasikae kwenye maeneo ya utoaji wa elimu ambayo wao hawawezi kusaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hivyo naona umewasha nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aloyce Kamamba, jiandae Mheshimiwa Athuman Maige.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Bila kusahau kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuletea fedha kwenye miradi mingi, ametufikia Kakonko, ametufikia Buyungu, tunamshukuu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu lakini bila kusahau watendaji kwa kazi nzuri, hongereni tunawapongeza sana. Lakini nipongeze Wizara kwa hatua nzuri ambayo mmefikia katika kuratibu mpango wa kurekebisha Sera ya elimu na mtaala, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, niipongeze Serikali kwa kupanua wigo wa kutoa huduma ya fedha kwa watoto wa kidato cha tano na sita ambapo takribani bilioni 10.3 zimetengwa kwa ajili ya watoto hawa tunaipongeza sana Serikali. Hii inakwenda sambamba na fedha za wanafunzi kwa ajili ya chakula, tumetoka shilingi 8,500 kwenda shilingi 10,000 si haba ni hatua nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze Serikali imeweza kupeleka miundombinu na imeweza kufanikisjha kwenye uandikishaji awali, Msingi na Sekondari. Lakini hali hii imepelekea upungufu mkubwa sana wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitia kwenye takwimu yetu ambayo imetolewa na *BEST (Basic Education Statistics in Tanzania)* ya mwaka 2021, kwa upande wa elimu ya awali, walimu waliokuwa wanahitajika ni mwalimu mmoja kwa 40 lakini hali ilivyokuwa ni mwalimu mmoja kwa 75. Kwa upande wa elimu ya Msingi waliohitajika ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45 lakini hali ilivyo ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 74. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi ambazo Serikali imeziweka kuajiri walimu 13,130, bado nisisitize Serikali kuhakikisha kwamba inaajiri walimu kwa ajili ya kukidhi mahitaji hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wilaya yangu ya Kakonko, kwa elimu ya awali walimu wnaohitajika ni 224 lakini wako walimu 14 tu upungufu ni walimu 210 upungufu ni sawa na asilimia 93.75 lakini kwa elimu ya Msingi mahitaji ya walimu ni 1189 wako 509 na upungufu ni walimu 680 upungufu sawa na asilimia 57. Nini unategemea katika maeneo kama hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe ufahamu tu kwamba, athari ya mapungufu ya walimu ni tofauti na mapungufu ya Daktari. Daktari asipopatikna leo Vifo vitatokea leo hii lakini athari ya kutokuwepo kwa walimu athari yake ni ya muda mrefu. Niombe sana Serikali ihakikishe kwamba ina ajiri walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nishukuru tumeweza kupangiwa majengo katika maeneo tofauti. Tumetengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule mpya za Kazilamihunda na Nyamtukuza, lakini tumeletewa madarasa katika shule za Msingi, Bukiriilo, Gwarama, Kavungwe, Kigarama na Nyamwilonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu ya awali, tumeletewa fedha kwa ajili ya Shule ya Msingi

Gwarama. Pia tumeletewa fedha kwa ajili ya Shule ya Msingi Bukirilo, Gwarama, Kavungwe, Kigarama na Nyamwilonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeletewa fedha kwa ajili ya nyumba Shule ya Msingi Nyakaviro, hii ni pamoja na *VETA*. Sisi tunaendelea kushukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo nichangie kwa upande wa wanafunzi wanaopata elimu hasa watoto wa kike baada ya kupata ujauzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tungehitaji kujua baada ya kuweka utaratibu huu, ni wanafunzi wangapi sasa wa kike wameweza kupata elimu baada ya Mheshimiwa Rais kutoa nafasi katika eneo hili? Baada ya hapo ni vema tukafahamu je, changamoto zilizosababisha hawa watoto kuweza kupata elimu mpaka wameweza kupata ujauzito na baadae wameweza sasa kurudishwa je, changamoto hizo tumezifanyia kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu Dada alikuwa yuko peke yake, sasa ana mtoto na anahitaji chakula kwa ajili ya mtoto huyu na anahitaji chakula kwa ajili ya mtoto huyu tunamsaidiaje sasa ili aweze kukidhi masomo yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Sera ya elimu, mwanafunzi akiwa nje ya shule awe wa kike au wa kiume kwa siku 90 mfululizo anaondolewa shule. Tunaangalia sasa mwanafunzi huyu wa kike amepata ujauzito ni zaidi ya siku 270 anarudi shule, hapa panahitaji mjadala wa kutosha. Tunamsaidiaje sasa huyu mtoto wa kiume kijana, kwa mujibu wa Sheria hayuko shuleni kwa siku 90 ameondolewa. Kwa Sheria ile maana yake akiondoka ni moja kwa moja, tunamsaidiaje huyu mtoto wa kiume?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hiyo haitoi haki sawa, niombe Wizara ya Elimu iliangalie upya suala hili ili liweze kutoa nafasi sawa kwa watoto wa kike lakini vilevile kwa watoto wa kiume. Hawa Watoto wa kike tumeona changamoto ambayo inawapelekea mpaka wanapata ujauzito lakini mtoto wa kiume nae anakuwa na changamoto mbalimbali katika Maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wanaotoka wanakwenda kwenye boda boda, wapo wengine wankwenda kufanya biashara hali inayopelekea sasa aondolewe nje ya mfumo. Tungetamani nae kwa kuwa mtoto wa kike ameweza kupewa nafasi baada ya kupata ujauzito na huyu mtoto wa kiume pamoja na kwamba kwa mujibu wa Sheria siku 90 zimekwisha na yeye atafutiwe utaratibu ambao utamsaidia kupata elimu baada ya kuwa nje ya mfumo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango mwingine wa kwangu niupeleke kwa wadhibiti ubora. Mdhibiti ubora ndiye jicho la Serikali kwenye upande wa elimu lakini hawajaangaliwa ipaswavyo. Hawajaweza kupewa vitendea kazi vya kutosha ikiwa ni pamoja na fedha za kuweza kufanyia kazi na kuweza kufanya ufuatiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo takwimu ambazo zinaonesha kwamba ukaguzi wa shule haufanyiki kwa zaidi ya asilimia 30. Kwa hiyo, asilimia 70 ukaguzi wa shule zetu haufanyiki. Niombe sana Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ukaguzi wa shule unafanyika ipasavyo na hasa ikizingatiwa kwamba ndilo jicho linaloisaidia Serikali kujua changamoto mbalimbali katika shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ulitolewa waraka ambapo wadhibiti ubora wakuu wa shule wa wilaya walistahili kupewa fedha za madaraka sawa na wakuu wengine katika halmashauri. Nikwambie kwamba waraka huo

haujatekelezwa. Kwa nini hawajapea stahili zao hizo? Niombe sana Serikali iangalie uwezekano wa wadhibiti ubora wa shule kuweza kupewa stahili zao sawa na wakuu wengine wa idara katika halimashauri. Nina uhakika wakiwezeshwa wataweza kufanya zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niombe *UNESCO* kama ambavyo tumeshauri kwenye Kamati liweze kuzingatiwa. Ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, jiandae Mheshimiwa Justine Nyamoga.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mimi kuniruhusu nichangie hii hoja ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa bajeti yao ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitachangia mambo mawili tu, la kwanza, litakuwa lugha ya kufundishia na la pili, elimu ya ufundi. Mambo haya mawili sio mageni humu Bungeni na wala sio mageni Serikali na hasa mimi pia sio mgeni kwenye mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nijiunge na watu wote Wabunge waliochangia kuishukuru Serikali yetu. Serikali hii ya Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya mambo makubwa sana katika kukuza elimu na hasa bajeti pia. Pia tunapata elimu bure, ujenzi wa miundombinu, madarasa, maabara, nyumba za walimu lakini mabweni. Hii inatupunguzia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Pofresa Mkenda na Wizara yake kwa kujituma sana na

kuonesha haya, kuyatekeleza maoni ya Mheshimiwa Rais, kwa vitendo, wote Wizarani nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la lugha kufundishia elimu yetu, najua liko tatizo la watu kupenda mambo ya kigeni, kupenda mambo ya kizungu. Moja kwa lugha lakini pia hata kwa mavazi na kusema mtoto huyu amesoma sana anaongea kingereza kama maji au anaongea kifaransa kama maji. Kwa hiyo, amesoma sana, wanalinganisha elimu na lugha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hapa Tanzania, Serikali ilikuwa na mpango mzuri wa kuendelea kutumia kiswahili kama lugha ya kufundishia na ikachukua muda mrefu, Serikali iligharamia gharama kubwa sana kuandaa vitabu vya kufundishia baada ya Elimu ya darasa la saba Kidato cha kwanza na chapili na wataalamu kule TATAKI Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliandaa vitabu hivyo wakiwa tayari sasa baada ya tafiti nyingi kuonyesha kwamba mtoto ili aelewe maarifa lazima afundishwe kwa lugha ya mama yake, na lugha ya mama hapa Tanzania asilimia 85 ni kiswahili kwa hiyo Serikali ilijikita kufanya tafiti na kupata majibu hayo wakaamua sasa watafute vitabu vya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iligharamia gharama kubwa sana kuandaa vitabu vya kufundishia baada ya elimu ya darasa la saba Kidato cha kwanza na chapili na wataalamu kule TATAKI Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliandaa vitabu hivyo ikiwa tayari sasa baada ya tafiti nyingi kuonyesha kwamba mtoto ili aelewe maarifa lazima afundishwe kwa lugha ya mama yake, na lugha ya mama hapa Tanzania asilimia 85 ni Kiswahili. Kwa hiyo Serikali ilijikita kufanya tafiti na kupata majibu hayo wakaamua sasa watafute vitabu vya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hapa leo nimesikitika sana matokeo ya Tume ya mapitio ya Sera pamoja na

Mitaala kupendekeza kwamba nyuma tutakuwa na lugha mbili za kufundishia kama ilivyokuwa zamani kiingereza na Kiswahili. Hii mimi ninaona kwamba tunarudi hatua kubwa sana nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spoika, mimi hapa nina vitabu. Jiografia kidato cha pili na mwandishi, ni Makunda lakini pia hiostoria kidato cha kwanza na Mwandishi Sago na Jiografia kidata cha kwanza, mwandishisi Makunda huyo. Pia nina kitabu Misingi ya Umeme na Sumaku, mwandishi Almasi Maige. Pia nina kitabu hapa kidato cha kwanza baiolojia mwandishi Isack na mwenzie Mustapha, nina kitabu hapa cha kidato cha kwanza Jifunze Kemia mwandishi Lema na Kimbi, nina kitabu hapa Uraia Kidato cha Kwanza mwandishi Kajigiri lakini nina kitabu hapa Mwandani wa Fundi Umeme mwandishi Almasi Maige, nina kitabu hapa cha Hisabati Kidato cha Kwanza mwandishi Saidi Sima, na nina kitabu hapa cha Fizikia Kidato cha Kwanza mwandishi Thadei na mwenzie Kiiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kimetokea kupiga gia ya kinyume Serikali bila kutoa sababu. Mimi ningefurahi sana Waziri akisimama hapa atoe sababu kwa nini wameamua kurudi nyuma baada ya gharama kubwa hii iliyofanywa na Serikali ya vitabu vyote kidato cha kwanza na cha pili na kuwa tayari nani amesema turudi nyuma?

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna nchi yoyote iliyoendelea kisayansi kwa kutumia lugha ya watu wengine. Wafaransa Kifaransa, Waingereza Kiingereza, Warusi Kirusi, Wajerumani Kijerumani, Wachina Kachina, na kadhalika. Zipo nchi pia za wenzetu, Misri katika Afrika na nchi nyingine kadhaa sisi nini kinatushinda?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Kiswahili kimekua na kutumiwa kote, lakini kinachoendelea kule wanasoma kama somo. Mapendekezo ya mapitio ya sera pamoja na elimu

wanasema na sisi Tanzania tunatumia Kiswahili kama somo. Ndio wenye Kiswahili lakini tunatumia Kiswahili kama somo. Sisi tulitaka, mimi na wenzangu ambao ni wazalendo, wanapenda lugha ya Kiswahili, tuna uthibitisho kwamba mtoto akifundishwa Kiswahili ataelewa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejivua, inasema kwamba wanaotaka sasa kutumia Kiswahili waanzishe shule zao na wanaotaka Kiingereza waanzishe shule zao. Inawezekana, watu hao watakaoanzisha shule zao watapata wapi gharama za kutafsiri vitabu kama hivi vyote viwe vya Kiswahili, watapata wapi walimu hawa wa kufundisha? Hili ni jukumu la Serikali. Serikali inashindwa, Serikali sasa ituambie kwamba sasa jukumu la elimu liwe kwa watu binafsi. Kwa sababu ni nani mtu binafsi ataanzisha shule ya Kiswahili? Haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kukwepa, wanafanya mchepuko kwa sababu ambazo sisi hatuzijui. Mimi sijaelewa kwa nini Serikali isije na msimamo wa kusema hatutaki elimu hii ifundishwe Kiswahili. Na mimi nimekuwa nasema, kwa nini Serikali isianzishe shule ya mfano watoto wakasoma darasa la kwanza mpaka la sita Kiswahili, wakaendelea mpaka sekondari *school* Kiswahili? Labda hadi kidato cha pili cha tatu na cha nne tukaona matokeo yake? Kwa sababu watakuwa wanasoma Kiingereza kuanzia darasa la kwanza watakuwa pia wanajua Kiingereza. Kwa hiyo ikionekana elimu haifundishiki Kiswahili huko mbele hii shule watajiunga Kiingereza. Kwanini Serikali haitaki kufanya hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi wanatushangaa sana Watanzania, sana, nawaambieni. Mimi nasafirisha rangi nchi za nje kule, nikiwaulizia taaluma yetu ifundishweje wanasema kwa nini msitumie Kiswahili kama vile Wachina, Wafaransa, Waingereza na kadhalika? Kwetu ni nini kimetokea? Mimi ninapendekeza Serikali isijivue jukumu la kuendesha shule ya mfano ya Kiingereza, lakini pia nashauri

vilevile pamoja na kuanzisha shule hiyo Serikali ianzishe shule hiyo ya mfano na shule hiyo iangaliwe, ichague wanafunzi wazuri kuanzia darasa la kwanza mpaka shule ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naiongelea Elimu ya ufundi. Ninaipongeza sana Serikali kwa kuja na mfumo ule na kubainisha kwamba kunatakiwa kuwe na mitaala miwili, mmoja unaitwa huu elimu amali au elimu ya ufundi. Wako watu humu ndani tulisoma elimu hiyo ya ufundi, akina *engineer* manyanya. Tuliicha baadaye kwa sababu ilionekana kwamba huko mkimaliza wote mna-*degree* sawa huyo aliyesoma mtaala wa ufundi na aliyesoma mtaala wa kawaida tunapata mishahara tofauti. Mtu aliyesoma kutoka *Dar es Salaam Technical College* akarudi kuwa mhandisi pale anapata mshahara kima cha chini ya mhandisi aliyesoma chuo kikuu, kwa hiyo Elimu hiyo ikafa. Leo tumeona, ninawapongeza sana. Kwamba mitaala yote miwili itaenda sawa na mtu wa mwisho kule, mhandisi wa mwisho kutoka taaluma hii ya amali na ya kawaida wote watakuwa na thamani sawa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** ahsante Mheshimiwa Maige kengele imegonga, Mheshimiwa Justin Nyamoga.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi leo tuweze kuchangia hoja iliyoko mezani. Nianze kwa kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo amei-*support* vizuri sekta ya elimu hususani katika jimbo langu la Kilolo lakini na nchi nzima kwa ujumla.

Tunayo mengi ya kusema lakini tushukuru sana kwanza kwa ahadi yake ya kujenga vyuo vya ufundi *VETA* ambavyo pia Wilaya ya Kilolo ni wanufaika na ujenzi unaendelea hivi tunavyozungumza; tunaona kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nishukuru kwa ujenzi wa shule za wasichana za mikoa ambapo kwa Mkoa wa Iringa itajengwa katika Wilaya ya Kilolo. Ninafahamu kwamba maandalizi yanaendelea na sisi tunaisubiri kwa hamu, tumejiandaa tumejipanga na eneo lipo tayari. Ni kazi tu ya kuanza ujenzi ndiyo inayosubiriwa. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa kazi zinazofanywa na Mheshimiwa Rais na sisi tuko tayari kushirikiana naye na kuendelea kumuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipongeze juhudi zinazofanywa na wizara katika kuboresha mitaala ambayo imekuwa ni kilio chetu muda mrefu humu ndani. Mimi ninaamini majadiliano yanayoendelea yatatupa mtaala bora ambao utaendana na mazingira na hali ilivyo kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao ushauri katika masuala machache ambayo yanaenda kwenye Sera ya Elimu na taratibu mbalimbali, na nianze kwanza na suala la udhibiti ubora. Lakini nizungumzie kidogo kipengele cha mitihani na nizungumze jinsi wasimamizi wa mitihani wanavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanaofundisha shule mbalimbali za sekondari huchukulia kwamba ule usimamiziwa mitihani ni fursa kwao kwa namna mbalimbali kama vile kukua na kujifunza, kusimamia pamoja na kusahihisha. Kukua na kujifunza kuelewa zaidi lakini pia ni fursa kwao kwa sababu ina kipato pia zaidi. Sasa, namna wanavyopatikana hakuna uwazi wa kutosha wa kuwafanya wale ambao hawakuchaguliwa waridhike kwamba na wao hawakuchaguliwa kihalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependekeza kwamba kuwe na utaratibu mzuri wa uchaguzi wa walimu wanaosimamia mitihani na vigezo. Yaani kuwe na mwongozo mzuri unaosema vigezo vya walimu wanaosimamia mitihani namna wanavyopatikana, wale wanaosahihisha mitihani na namna wanavyopatikana, ili kuondoa malalamiko au kuondoa mtu mmoja kuhodhi maamuzi ambayo inawezekana inaweza kupelekea mianya ya rushwa kwa walimu wetu ambao pia vipato vyao si vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni la kwanza, ningependekeza hata tunavyotengeneza sera pia iangalie hicho kipengele, kwamba ni namna gani usimamizi na usahihishaji wa mitihani unafanyika na hao wanaofanya hiyo kazi wanapatikanaje. Ikiwa wazi kwa namna yoyote ile inapunguza malalamiko kwa hiyo linakuwa ni jambo ambalo linauwazi wa kutosha, hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo kisera halijakaa vizuri; wote tunajua kwamba watoto katika shule zote, chekechea, msingi, na sekondari, sasa hivi hizi shule nyingi ni shule za kutwa, liko jambo la chakula cha mchana, sasa jambo la chakula cha mchana limetiwa nguvu sana na umuhimu wa lishe bora kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo jema na wazazi wamelipokea vizuri. Katika mazingira ya elimu bila malipo wanafunzi wengi wanachangia. Lakini nataka nikupe *scenario* moja, unakuta kwenye kata kuna shule mzazi anatakiwa kuleta mahindi debe moja kila mwezi lakini kuna shule mzazi anatakiwa kuleta debe tatu kila mwezi na mwingine anatakiwa kuleta kilo tano kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kawaida sisi wote tuna utaalamu wa kutosha wa kujua *ratio* za chakula kwa sababu tunazo shule za bweni tunajua Watoto wanatakiwa kula nini mchana. Utaratibu ambao ungeweza kuwa mzuri ni

mwongozo wa uchangiaji wa chakula kwenye hizi shule ili kusiwe na mtu anaamua tu. Ndiyo maana wazazi wakati mwingine wanakuwa wagumu kuchangia kwa sababu hakuna kigezo kinachotumika kujua ratio ya mwanafunzi ya chakula lakini yule anayeamua mengi anaweza akawa na nia ovu, inatoa fursa au mwanya kwa mtu ambaye yeye ana mipango yake ya kuchangisha chakula zaidi kwa jambo la kwake yeye aweze kufanya hivyo kama Wizara haikutoa muongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba Wizara ya Elimu fanyeni utafiti njooni na *ratio* ya chakula mtoto anachotakiwa kula ili mzazi aambiwe kwa mujibu wa taratibu unatakiwa kuchangia hiki ili mtoto wako ala chakula cha mchana, na hiyo itapunguza kabisa malalamiko yale yanayojitokeza. Na itapunguza, wakati mwingine unakuta wamekusanya mahindi yamebaki shuleni kwa sababu walichangisha zaidi au wakati mwingine ni majaribu sasa kwa walimu wale kupata majaribu sasa ya kuuza au kufanya jambo lingine ambayo inapelekea mwakani uchangishaji unakuwa mgumu. Suala hili ni la miongozo. Kwa hiyo mshirikiane na TAMISEMI kutoa muongozo mzuri ili hili nalo liweze kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu mikopo ya vyuo vikuu. Kuna changamoto ndogo ambapo mtu ameomba mkopo hakupata. Kimsingi huwa mtoa tu majina hamuwezi kumwambia kwa nini hukupata, na kwa sababu hajui anakata rufaa akikata rufaa majina yanatoka tena hayasemi tena kwa nini rufaa yake haikukubaliwa; mwakani anakata tena rufaa hivyohivyo mpaka akiendelea kujaribisha mpaka atakapopata. Nafikiri mifumo ya rufaa huwa inamrejesho. Kwa sababu ni vibaya kuendelea kumtumainisha huyu mtu kwamba akikata rufaa mwakani atapata. Kwa hiyo kama bodi imeona kuwa huyu mtu hakopesheki imjulishe kwamba wewe hautakopeshwa mpaka utakapomaliza miaka yako

mitatu ili asiendelee kupata shida ya kukata rufaa kukata rufaa wakati kiukweli bodi imesharidhika kwamba huyu mtu hakopesheki na impe majibu kwamba kwa nini hakopesheki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tumelizungumza muda mrefu hapa bungeni; kwa sababu wakati mwingine unakuta huyu ni mtoto kweli wa maskini labda au alisoma shule za kanisa na kwa hiyo pengine au shule hizi za binafsi kwa kulipiwa na mfadhiri na vigezo vingine vingi. Sasa kadiri ambavyo anazidi kukata rufaa anategemea; ni kama bahati nasibu. Mimi nisingependa bodi ya mikopo ifanye kukata rufaa kama bahati nasibu. Kwamba sijui nitapata au sijui sitapata tena; anakata rufaa wakati mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwe na mfumo wa taarifa, yaani wa mrejeshi. Kwamba sababu ambazo zimekufanya usikate ni hizi na kwa hiyo kama hazitarekebishika hautapata, au wewe usiombe tena kwa sababu umekataliwa, au wanaoruhusiwa kukata rufaa watolewe orodha kwamba ninyi mnaweza kukata rufaa. Kwa hiyo hao watu wataona pale kwenye orodha; kwamba hawa ndio mnaoweza kukata rufaa na hawa hawawezi kukata rufaa ili shughuli ziendelee na wale ambao hawastahili kukata rufaa wa sikate rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine la mwisho ambalo ningependa kuzungumza ni namna elimu inavyosimamiwa, na hasa kwenye Vyuo Vikuu. Tunavyo sasa vyuo vikuu ambavyo vinasimamiwa na Wizara moja kwa moja lakini kuna vyuo mbalimbali vinavyosimamiwa na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafikiri hili ni suala la Elimu kwa sababu watoto wote wanaosoma wanatarajia kuingia kwenye soko la ajira kwenye sekta zote. Yaani kama ni kwenye Serikali za mitaa wanatakiwa kuingia kwenye sekta zote. Kama ni kwenye sekta ya fedha wataingia kwenye sekta zote. Kama ni kwenye sekta ya michezo wataingia

kwenye sekta zote kama kila Wizara itaanzisha chuo kwa ajili ya watu wa taaluma yake vile vyuo vikuu vingine vinakosa *relevance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningefikiria kwamba kuwe na mfumo tu mmoja wa vyuo vikuu vyote na viwe vinasimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kwa hiyo watoto wanapomaliza wote wanakwenda kwenye utaratibu wa kutafuta ajira, kunaweza kukawa na vyuo vyenye msisitizo wa jambo fulani. Kwa hiyo kunaweza kukawa na vyuo vya madaktari ambavyo havisimamiwi na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kunaweza kukawa na vyuo vya watumishi wa Serikali za mitaa ambazo hazisimamiwi na TAMISEMI, au vyuo vya michezo ambavyo havisimamiwi na Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kwa sababu mwisho wote wanomaliza wanaingia kwenye soko la ajira moja na kwa hiyo hakuna sababu ya kwamba vyuo hivi visimamiwe na watu wengine. Lakini pia Serikali ni moja; kwa hiyo sualala uratibu wa elimu likiratibiwa na sehemu moja, hasa kwenye hii mitaala tunayoendelea litakuwa jambo zuri kwa sababu uratibu ule utafanyika kwa uzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niwakumbushe tu kwamba kwenye upungufu wa walimu kwa kweli baadhi ya wilaya zilizoko pembezoni zina shida sana, hasa kwa mfano Wilaya ya Kilolo, kuna maeneo kwa kweli ni changamoto, tunaona walimu wawili watatu. Kwa hiyo changamoto ya walimu pia kwa kushirikiana na TAMISEMI inapofika wakati wa kuitatua basi tuangalie pia maeneo ambayo yana changamoto kubwa ili yaweze kuapta kipaumbele katika kupangiwa walimu zaidi na ili hiyo changamoto iweze kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa wachangiaji wetu wa mchana wamekwisha, jioni tutaanza na Mheshimiwa Eric Shigongo, Mheshimiwa Neema Lugangira, Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Yustina Rahhi, na Mheshimiwa Alfred Kimea. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 6.54 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mjadala wa hoja iliyoko mbele yetu, bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Wapo wachangiaji, tunaanza na Mheshimiwa Eric Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangira na Mheshimiwa Kishimba ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mema yote ambayo amelifanyia Jimbo la Buchosha kwa upande wa elimu. Ameleta fedha nyingi sana, tumejenga madarasa mengi, nina uhakika aliyoyafanya Wanabuchosha wote wanamshukuru wakiongozwa na mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na najua anafahamu kabisa kwamba sina mashaka naye hata kidogo. Nimekwishazungumza naye mara nyingi kwamba uadilifu wake na uzalendo wake katika Taifa na namna anavyoipenda elimu, nina hakika kabisa elimu yetu iko kwenye mikono salama. Nimshukuru sana Naibu Waziri, rafiki yangu Kipanga ambaye mara kwa mara tunajadiliana kuhusu elimu ya nchi yetu, hakika anatumika vizuri sana kwa ajili ya Taifa lake, Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara ya Elimu ambao wako hapa nyuma wananisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili suala la elimu, nimekuwa mshabiki mkubwa wa elimu na jambo moja ambalo nimekuwa nikilizingumza sana hapa Bungeni ni kuhusu elimu, kitu ambacho mwenyewe nikiwa kijana mdogo mtoto mdogo nilikikosa. Sikufanikiwa kupata elimu ya kutosha na kwa sababu nimefika kwenye hatua hii na najua umuhimu wa elimu kwa watu wa nchi yangu, nasimama imara siku zote kuhakikisha kwamba elimu ya nchi yangu inakuwa elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nelson Mandela aliwahi kusema na nitamnukuu alisema; "*Education is the most powerful weapon you can use to change the world*". Kwamba elimu ni silaha yenye nguvu mtu yeyote anaweza kuitumia kuibadili dunia. Kwa hiyo tunapojadili elimu inatakiwa tuwe na umakini wa hali ya juu sana kwa sababu kuna uhusiano mkubwa sana kati ya maendeleo ya watu na

elimu. Maendeleo ya watu yanategemeana sana na aina ya elimu ambayo nchi inatoa kwa watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya watu wenye akili sio wenye elimu pekee yake, haiwezi kuwa nyuma kimaendeleo. Ndio maana nasema na narudia kusema na nitaendelea kusema, tuna wajibu wa kuingiza maarifa kwenye akili za watoto wetu. Huo ni wajibu wa Serikali, Serikali ikitimiza wajibu wake sawasawa ika *instill* au kuingiza maarifa kwenye akili za watu wake, hatuna mashaka kuhusu maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo Wizara ambayo Mheshimiwa Mkenda anaiongoza ni Wizara moja muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Kwa sababu kama hatutotimiza wajibu wetu tutakuwa na wananchi, tutakuwa na *human capital* ambayo haina elimu ya kutosha, haitoweza kusukuma maendeleo ya Taifa letu mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote zilizofanya vizuri katika ulimwengu huu watu wake wameelimika vya kutosha na aina ya elimu wanayopewa ndiyo jambo la muhimu zaidi. Sio tu kuwapeleka watoto shule wakasome, lakini aina ya elimu tunayotoa iwe ni elimu ambayo itasaidia kutatua changamoto zetu. Tunapeleka watoto shule tuwaelimishe ili watupe *solution* ya matatizo yetu, ndio lengo. Ninapopeleka mwanangu shule aweze kuja na *solution* kwa matatizo ya familia, *solution* kwa matatizo ya nchi na *solution* kwa matatizo ya dunia. *Otherwise* hapa hakuna sababu ya kupeleka mtoto shule kama tutapeleka watoto wetu shule wakasoma, lakini mwisho wa siku wasitupe *solution* ya matatizo yetu haina sababu ya kupeleka watoto shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lengo letu tunasomesha watoto watupe *solution* ya matatizo yetu. Inaniuma sana, inaniuma sana mara nyingi, ninapokutana na kijana amesoma, amemaliza chuo kikuu, ana *masters,* yuko mtaani hatupi *solution* yoyote kwa Taifa letu. Anazunguka

huku na kule akiwa na bahasha, hana mchango wowote kwa Taifa anageuka mzigo kwa Taifa, mzigo kwa familia yake, sio lengo la elimu yetu, lengo liwe ni kuwaelimisha watu wetu. Sasa tujiulize sisi wenyewe hapa tulipo ni matokeo ya aina ya elimu tuliyopata. Je, tunafurahia tulipo? Je, tungetamani tuwe mahali tofauti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yangu mimi ni kwamba elimu iliyotufikisha hapa haiwezi kutupeleka tunapokwenda. Narudia, elimu iliyotuleta mpaka hapa tulipo, mimi sina furaha sana, nataka aina nyingine ya elimu itakayonitoa hapa kunipeleka kule ninapokwenda kwenye ulimwengu wa kidijitali. *Internet of things, cloud computing* mambo ya *coding* na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri tulizungumza mambo ya *coding* hapa, nimeyakuta kwenye rasimu ya mtaala ambayo nimeisoma. Nimefurahi kwa sababu nina uhakika kwamba rasimu niliyoisoma, watoto tunaokwenda kuwatengeneza kwa rasimu hii watakuwa ni watoto ambao watatusaidia sana tunapokwenda. Kwa hiyo, ninao ushauri kwa Serikali, ushauri wangu kwa Serikali ni mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaotoka kijijini kama mimi mnafahamu huwa tunafyatua matofali kwa kutumia kibao, kile kibao kinaitwa kifyatulio. Kwa hiyo kama kifyatulio ni cha duara matofali yatatoka ya duara, kama kifyatilio ni cha mstatili matofali yatatoka ya mstatili. Hauwezi ukawa na kifyatulio cha mstatili ukapata matofali ya duara. Maana yangu ni nini? Aina ya elimu tunayotoa tujiulize, tunatengeneza watoto wa aina gani huko mbele? Je, tunatengeneza watoto wanaofanya tushinde kwenye ulimwengu ujao? Hili ndilo swali langu la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakuja kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kwangu mimi ni mtaala, mtaala wetu ni lazima uwe ni mtaala ambao utamwandaa mtoto wetu kushindana kwenye ulimwengu ujao. Tusiwajaze watoto wetu *content* pekee yake kichwani isipokuwa tuwape elimu ambayo itawafanya waweze kuwa na *solution* za matatizo. Kwa hiyo, tuupitie mtaala wetu, nimeuona mtaala huu ni mzuri, una maboresho kidogo lakini watoto watakaosomeshwa kwenye mtaala huu wawe majibu ya matatizo kwenye ulimwengu tunaokwenda mbele, sio hapa tulipo hivi leo. Kwa hiyo, mtaala uboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu Mheshimiwa Waziri ni kwamba tusichukue muda mrefu sana kutekeleza mambo. Tunapojadiliana kuhusu mtaala tufanye mambo yetu haraka. Dunia inaenda kwa kasi, unaweza kuwa mjadiliana, mnajadiliana, mnajadiliana kuhusu mtaala, dunia itabadilikia ukajikuta mtaala wako umekwenda *obsolete* kabla hujautekeleza. Kwa hiyo hayo nayo Mheshimiwa Waziri wameshayajadili, wadau wameongea, tuyafanyie utekelezaji kwenye mtaala tuanze kuufanyia kazi mara moja. Kwa hiyo mtaala wetu uboreshwe, uende na ulimwengu ujao, sio ulimwengu tuliotoka wala ulimwengu tuliopo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu; Walimu wetu katika nchi hii wana matatizo sana. Walimu wetu wana shida; huwezi kuwa na elimu bora kwa Walimu wanaolalamika kila siku. Walimu wetu wamejaa mikopo, Walimu wetu wana kila aina ya dhiki, kama tumedhamiria kuboresha elimu ya nchi hii tuanze na Walimu wetu kuboresha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kengele imelia niende katika jambo lingine la muhimu sana ambalo nataka kulisema, wazazi wa nchi hii watimize wajibu wao kwa watoto wao. Kuanzia kwa mama mjamzito, ahakikishe anakula chakula bora, mama mjamzito ajiepushe na matumizi ya dawa au vitu vinavyoathiri akili ya mtoto wake. Udumavu

upigwe vita kwa sababu mtoto aliyedumaa hawezi kujifunza sawasawa tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya vitendo; tupunguze nadharia tuongeze vitendo kwenye elimu yetu. *Medium of instruction,* nilishasema huko nyuma, sikatai kufundisha kwa Kiswahili, lakini wasiwasi wangu ni kwamba mtoto utakayemfundisha Kiswahili kwenye ulimwengu ujao itakuwaje? Asubuhi ya leo wakati nafanya mazoezi, nimekutana na watoto wawili, mmoja amesoma *English medium*, mwingine anasoma shule ya kawaida ya Serikali wote wapo sekondari moja. Nikamuuliza yule aliyetoka shule ya msingi ya kawaida, akaniambia nahangaika sana *form two* kwa sababu nimesoma Kiswahili mpaka darasa la saba, *form one* Kiingereza. Yule mwingine akaniambia mimi sipati shida yoyote kwa sababu nimesoma Kiingereza mwanzo mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu, tuamue kama ni Kiswahili, iwe ni Kiswahili, kama ni Kiingereza iwe ni Kiingereza na kama hilo hawalitaki, basi niwaombe wafundishe mpaka darasa la tatu au la nne Kiswahili, la tano mtu aanze Kiingereza kusudi wajiepushe na suala la mtoto *form one, form two* anajifunza Kiingereza hajakielewa vizuri *form four* umefika mtihani, anafeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza watoto wengi sana. Naomba sana tuamue Wabunge sisi ndio wawakilishi wa wananchi, hebu tuchague tunataka nini, nani kati yetu hapa mtoto wake anasoma Mwananyamala *Primary School*? Nani? Napendekeza huko mbele ikiwezekana Waziri akiteuliwa tu iwe ni sharti kwamba mwanao asome shule ya kawaida. Tukifanya hivyo elimu yetu itabadilika. Sasa hivi tunawadanganya wananchi wetu kwamba tufundishe Kiswahili, watoto wetu hapa wote wanasoma *international schools, that's a lie,* tusiendelee kuwadanganya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na cheti cha *form four*; kansa ya cheti cha *form four* katika nchi yangu. Nilizungumza mara ya mwisho hapa narudia tena. Hivi sasa nina stori ya watoto wamesoma China *medicine*, wamesoma miaka mitano *medicine* China, wamekuja hapa wamekataliwa kufanya *internship* kwa sababu hawana cheti cha *form five* na *six*. Waliondoka hapa kwenda kusoma *medicine* China kwa elimu ya *form four,* hapa wamelazimika kufanya *QT* ya *form five* na *six* ndio wafanye *intership*, *what is wrong with this?* Hebu tufike mahali tuache watu wapate elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mapema, *issue* yangu ya *RPL, Recognition of Para Learning* ambayo ikanifanya mimi nikapata elimu ya chuo kikuu kutoka darasa la saba. Naomba sana Mheshimiwa Waziri anipe majibu ya suala hili, ni lini *RPL* itaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Eric.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ajiandae.

**NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja hii muhimu ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt.

Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoleta mageuzi makubwa katika Sekta hii ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika Bajeti ya Wizara hii ya Elimu, nitajikita katika eneo la lishe na hapa naomba nitambue kwamba eneo la lishe ni moja ya maeneo ya vipaumbele ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tokea akiwa Makamu wa Rais. Vilevile eneo hili la lishe ni moja ya vipaumbele ambavyo vimeainishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, chama changu pendwa ya mwaka 2020 - 2025 ukienda kwenye ukurasa wa saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, naomba nirejee katika Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 ambayo hivi sasa inafanyiwa mapitio. Katika sera hii imeainisha bayana kwamba Serikali itahakikisha inatoa huduma muhimu ikiwemo chakula shuleni. Naamini Serikali ilifanya vile kwa kutambua umuhimu wa chakula na lishe shuleni, lakini kwa bahati mbaya sana utekelezaji wa suala hili umekuwa na changamoto kubwa na hautekelezeki ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kelele nyingi za wazazi pamoja na wadau, niipongeze Wizara ya Elimu ilifanya tafiti na baadaye ikaleta mwongozo. Mwongozo huu hapa ambao ulizinduliwa mwaka 2021 ambao ni Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma wa Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimu ya Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwongozo huu na kutokana na tafiti iliyofanywa na Wizara ya Elimu, ilibaini kwamba katika shule za kutwa asilimia 70 hazitoi huduma ya chakula na lishe shuleni. Kwa msingi huo nifanye rejea ndogo tu, kwamba kwa takwimu za mwaka 2021 za Serikali shule za msingi ambazo tunazo hapa Tanzania ni takribani 18,546 na jumla ya wanafunzi ambao wako kwenye shule hizi za msingi ni takribani milioni 11.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijirejea kwenye ile asilimia 70 ya shule zetu hazitoi chakula na lishe shuleni. Kwa muktadha huo inamaanisha kwa mwaka 2021 jumla ya watoto takribani milioni 7.9 walikuwa wanaenda shule wana shinda na njaa na dunia imeshatambua ikiwemo *WHO, World Bank* na Mataifa ya nje na hata hapa ndani, hapa nchini kwamba chakula na lishe vina mchango mkubwa moja kwa moja katika makuzi ya mtoto pamoja na ufaulu wa darasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata na wenyewe Wizara ya Elimu wametambua na wameiweka humo kwenye mwongozo ambao wameutoa. Sasa nimejaribu kufanya ulinganifu ambao Wizara ya Elimu inaweza ikafanya tafiti nzuri zaidi na kukokotoa kwa kina zaidi. Matokeo ya mwaka 2022 mwaka jana ya mtihani wa kidato cha nne, asilimia 51 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani wa kidato cha nne mwaka jana walipata *division four*. Asilimia 12 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani kwa mwaka 2022 walipata *divison zero*, ukijumlisha hizi asilimia 51 na asilimia 12, unapata asilimia 63, ambayo haipishani sana na ile asilimia 70 ya shule ambazo hazitoi chakula na lishe shuleni. Kwa hiyo kwa muktadha huo unaweza ukaona kwa tafiti na ulinganifu wa haraka haraka kwamba ni dhahiri pamoja na sababu zingine ukosefu wa chakula na lishe shuleni una mchango mkubwa katika ufaulu wa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo linalonisikitisha ni kwamba japokuwa kule kwenye Sera ya Mwaka 2014, Serikali imetambua na kusema kwamba Serikali itahakikisha inatoa huduma muhimu katika shule ikiwemo chakula shuleni. Sasa cha kushangaza katika mwongozo huu wa utoaji wa huduma ya chakula na lishe shuleni, Serikali imejivua jukumu hilo na badala yake imeelekeza kwamba utekelezaji wa mwongozo wa chakula na lishe shuleni ni jukumu la jamii na wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linasikitisha kwa sababu, ni Serikali hii hii kwa kutambua uwezo na uchumi

hafifu wa wananchi na wazazi uliamua kuja na elimu bure ili kumwondolea mzazi mzigo wa kulipa ada na michango mbalimbali lakini Serikali hii hii kwa kutambua wazazi wale wale, sasa imeamua kuwavika wao jukumu la huduma ya chakula na lishe shuleni na yenyewe ikajiondolea jukumu hilo wakati katika Sera ya Elimu ya 2014, inatambua kwamba hilo ni jukumu la msingi la Serikali. Kwa hiyo jambo hili linahitaji liangaliwe kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kuna kitu kinaitwa *human capital development*, rasilimali watu, kwa Taifa kama la Tanzania kama ambavyo linakua kwa kasi inayokua, kwa uwekezaji mkubwa ambao unafanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan tusipowekeza vya kutosha kwenye hii rasilimali watu yetu tutajikuta huko mbeleni tuko kwenye shida. Kwa hiyo, niombe sana Wizara ya Elimu wanapofanya mapitio ya mitaala pamoja na mipango mingine, tutafute namna ya kuhakikisha ya kwamba suala la chakula na lishe shuleni liwe ni suala la msingi kwa sababu si suala la anasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mapendekezo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kwanza, ninaiomba sana Wizara ya Elimu ichakate namna ambavyo chakula na lishe shuleni kinatakiwa kitolewe, kwa sababu hivi sasa hakuna mwongozo. Huu mwongozo uliotolewa ni mzuri lakini mwongozo katika maneno, hakuna mwongozo ambao unasema hicho chakula na lishe ni cha aina gani? Hicho chakula na lishe wastani wa gharama kwa kila mwanafunzi ni kiasi gani kwa mwezi ili wazazi wajue kwanza ni kiwango gani. Maana yake hivi sasa kila shule inajipangia yenyewe kiwango chake lakini pia lazima kuwe kuna uhakika hicho chakula kinachotolewa kweli kina lishe au ni chakula ili mradi tu kushibisha tumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili. Serikali kupitia Wizara ya Elimu itafute namna ya kutokwepa jukumu lake la msingi la kuchangia na kuhakikisha katika shule zetu kuna huduma ya chakula na lishe, hivyo ichangie katika gharama. Serikali inatoa ruzuku kwenye maeneo mengine kupitia *capitation*. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara ione namna gani ambavyo na yenyewe kulingana na ule mwongozo utakaokuwa umenyambulisha gharama za kila mtoto kupata chakula na lishe shuleni, Serikali ichangie walau asilimia 60 na wazazi wachangie asilimia 40 lakini hiyo ionekane wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niipongeze sana Serikali kupitia Wizara ya Elimu. Mwaka jana mwezi wa Tisa, Serikali kupitia Wizara ya Elimu wamejiunga na kitu kinaitwa *School Meals Coalition*. Huu ni mpango wa dunia ambao nchi zinajiunga na moja ya ahadi ambazo wanaweka ni kwamba ifikapo mwaka 2030 kila mtoto katika kila shule atapata walau mlo mmoja wa chakula na lishe kwenye shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa 2030 siyo mbali, hatutaweza kufika kama Wizara ya Elimu itaendelea kutolitilia maanani suala hili na kuanza kuwa na mipango nalo. Kwa hiyo, hapa jambo kubwa ambalo lipo niombe sana Wizara itafute namna ambavyo itapata fedha kwa ajili ya kufanikisha jambo hili na fedha zipo duniani. Yako mashirika ya kimataifa na iko mipango ya kimataifa ambayo tayari inasaidia nchi zingine Barani Afrika kutekeleza ajenda ya chakula na lishe shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo niliwahi kusema katika moja ya michango yangu hapa kwenye bajeti hii hii ni *GPE (Global Partnership for Education)*. Tunayo bahati kubwa kwamba Mwenyekiti wa *GPE* ni Rais Mstaafu wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Kikwete. Sasa tunashindwa nini kutumia fursa hiyo ikiwa wanachangia *GPE* wanasaidia nchi zingine Barani Afrika na sisi pia Tanzania tunaweza tukapata

fursa hiyo, lakini hata Benki ya Dunia hata *IMF, AFDB* zote zinajikita katika kutekeleza katika eneo hili pamoja na *UNICEF*. Kwa hiyo mimi naamini kwamba fursa hizi zipo, ikiwa tu tutaamua kulibeba jambo hili kwa uzito unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha kwa kuiomba sana Serikali kwa kumuomba sana Profesa Adolf Mkenda, kwa sababu natambua anajua umuhimu wa chakula na lishe kwa Watoto, umuhimu wa chakula na lishe katika ufaulu. Tutafanya yote na yote yanaweza yakawa yasiwe na tija inayotakiwa au tija inayotarajiwa endapo tutaendelea kuruhusu watoto wetu asilimia 70 waendelee kuwa wanaenda shule na wanakaa na njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema. Mheshimiwa Jumanne Kishimba atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Rahhi, Mheshimiwa Dokta Alfred Kimea ajiandae.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi naungana na Wabunge wenzangu kuchangia kwenye Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na timu yake nzima kwenye marekebisho makubwa aliyofanya kwenye mitaala ya elimu kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wetu mkubwa ilikuwa ni mtaala mzima wa elimu ambao ulikuwa unaleta shida sana, kwamba mtoto aliyesoma ndiyo anakuwa mgogoro zaidi na taabu ngumu zaidi kwa mzazi kuliko yule ambaye hajasoma. Mzazi anateseka, Serikali inateseka na mpaka mwisho hatupati ufumbuzi, lakini kwa mtaala huu alioleta Mheshimiwa Waziri kama hawakuuchakachua wenzetu

wasomi, unaweza ukatusaidia kutufikisha mahali pazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana sana na Mheshimiwa Shigongo alivyosema. Ni kweli kabisa elimu ya sasa hivi Mheshimiwa Waziri, ilikuwa kama gereza, hauna uhuru nayo wewe mzazi. Sasa hivi kwa mtaala huu tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri katutofautishie sisi wa vijijini na wale wa mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijijini Mheshimiwa Waziri, watoto wetu sisi ni rasilimali ya kuzalisha mali ndiyo baadaye anaanza shule. Ninyi huku mjini Watoto wenu ni watoto wenye gharama. Kwa hiyo, lazima tutofautishane hapo. Sisi wa kwetu akiwa na miaka minne anaanza shughuli za kilimo pale nyumbani na kuchunga mbuzi, anang'oa mbegu za mpunga anakusaidia kupanda. Kwa hiyo, msije tena mkaleta hapo mkasema, aah sisi mambo *human rights,* watoto wanateseka, Hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hawa watoto ndiyo wanaolima huu mchele mnaolia kila siku kwamba umepanda bei. Nani mzee anayeweza kuinama kutwa nzima kwenye tope kama siyo watoto? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba sana kwa kuwa umefungua kwamba mzazi akiwa na shida kesho kwamba ana shida, ana kazi yake nyumbani aje aombe ruhusa shuleni kwamba naomba mwanangu, siku tatu tukafanye naye kazi ili baadaye atakuja shuleni Jumatatu. Itatusaidia sana kwa ukubwa huu ambao umeufungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile elimu hii lazima iwe wazi na iwe nyepesi hasa darasa la kwanza. Afundishwe mtoto kitu chenye faida maana yake unaponiambia mimi nikajitegemee lazima kiwepo kitu kinachonivutia, kwamba unaniambia mimi nilime mahindi lazima unieleze kwamba punje fulani, miche fulani ukimwagilia ndoo moja ya

gharama hii utapata shilingi hii, ili huyu mtoto awe na *interest* ya kwenda kufanya ile kazi akiwa bado mdogo. Itatusaidia tumepiga kelele sana muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi nikifika darasa la nne Mheshimiwa Waziri nikawa mtoro lakini ukanifuata ukanikuta kwenye mahindi nalima mahindi ni kosa? Litakuwa kosa gani? Niruhusu nisome hata jioni kama unaona nashinda kwenye mahindi, nisome jioni nitalipa hiyo gharama kwa sababu hii siyo dini, hata dini ina *option,* kwamba kama hukusali Saa Saba au hukusali Jumapili sala ya asubuhi unaweza kusali ya Saa Saba ili kusudi maisha yaweze kwenda wakati mtoto anasoma na mzazi yuko na mtoto wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *VETA*. *VETA* Mheshimiwa Waziri waongezee mitaala. Tunapoongea hapa *VETA* hana mtaala wa simu, hana mtaala hata wa *television,* hana mtaala wa pikipiki. Leo kuna *market* kubwa sana ya wafanyakazi wa ndani, *VETA* hana mtaala wa wafanyakazi wa ndani. Utajiri wa nchi za Asia ni wafanyakazi wa ndani. Ninyi mnasema mnafundisha *hotel management,* kutenga ugali unahitaji kusoma? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyakazi wa ndani leo hii wote ni mashahidi ukitafuta mfanyakazi wa ndani unampigia Mheshimiwa Jesca kule Iringa unamwambia nitafutie kijana kule mlimani utafikiri unatafuta mbuzi wa mizimu. Yaani ni kazi kweli ni soko kubwa sana. Tulikuwa wote pamoja kwenye mtaala wa elimu, yule jamaa kutoka Philipines alivyosema kwamba utajiri wa Philipines ni wafanyakazi wa ndani ambao wanakwenda nchi za nje. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu weka wafanyakazi wa ndani kwenye mitaala yetu itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwenye suala moja ambalo najua ni gumu sana. Tumeruhusu msichana akipata mimba aendelee na shule lakini wanaopata mimba

wanaweza kuwa wamebakwa labda mbili, asilimia 98 walielewana lakini sheria yetu inasema na huyu atatumikia kifungo cha miaka 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu yetu ambayo mliitoa mwaka jana Wizara ya Elimu, waliopata mimba shule ya msingi walikuwa 3,850, sekondari walikuwa elfu nane na kitu na ninafahamu kabisa hiyo takwimu kwa sababu kuna maelewano mengi sana kule kijijini, inawezekana msingi walikuwa zaidi ya 10,000, sekondari walikuwa zaidi ya 20,000. Sasa Mheshimiwa Waziri ina maana hawa 40,000 watapatikana watoto 40,000, baba zao watakuwa gerezani. Mwakani tena watapata mimba wengine 80,000 lakini tutakuwa na wafungwa tena 80,000. Je, magereza yetu inaweza kuwabeba? Je, hawa watoto watakapokua wakute wazazi wao wako gerezani miaka 30 watamlaumu nani na kosa lao kubwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni swali gumu, ni kazi yetu Wabunge maana yake tunaamka asubuhi ukiamka nyumbani watu watatu unakuta wana mtoto, kwamba baba yake alifungwa au alitoroka na mimi mtoto wa shule nimeruhusiwa kwenda shule lakini na nyanyaswa pale nyumbani. Mnafahamu wote makabila yetu au wenzetu mnatoka Uingereza? Makabila yetu mnayafahamu msichana anapozalia nyumbani hapendwi na kaka kwa sababu kaka alitarajia kupata ng'ombe 40 nae aoe, mzee naye alitarajia kukaa *high table,* naye hampendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu msichana anabaki na mateso, na mume naye ametoroka. Sasa Mheshimiwa Waziri labda tulilete kisheria tuone wale ambao hawakubakwa, huyu mwanaume aozeshwe huyu mtoto, aozeshwe huyu msichana ili huyu msichana aendelee na shule akiwa ameolewa. Maana yake hii shule ni kambi tu wazungu walituletea? Shule ni kambi tu siyo wala kitu chochote. Sisi Waafrika hatukuwa na shule. Hii ni kambi

tumeletewa ikatengenezwa vizuri ndiyo ikawa shule. Sasa kweli watu wapoteze maisha yao baada ya miaka mitano tutakuwa na watoto laki tano hawana baba ila tuna wafungwa laki tano, magereza yetu yatatosha ukiunganisha na wafungwa wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri sisi ambao tunaya-*face* hayo matatizo kule kijijini, maana yake mwenye mtoto wa kiume anakuja kukulilia kwamba mwanangu amepata matatizo amefungwa ana kesi. Mtoto wa kike naye anakuja pia anasema nina watoto wawili kweli nimeruhusiwa kwenda shule lakini hawa watoto sina wa kuwatunza, atawatunza nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni swali gumu ambalo ni lazima Waheshimiwa Wabunge tulifikirie kwa mapana sana. Mimi sikatai sheria ya kwenda shule nakubaliana nayo asilimia 100, kwamba huyu aliyejifungua aendelee na shule lakini huyu mwanaume anaenda wapi sasa? Anaenda gerezani miaka 30. Mheshimiwa Waziri hiki ni kitu ambacho kiko nje ya utaratibu lakini ni dunia tunayokutana nayo, tutafanya namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, familia zingine wamekwenda watu mpaka wanne wapo gerezani lakini hawa wananchi wanakubali hawa waoane na huyu aendelee na shule. Nafikiri tulifikirie kwa mapana sana ili iweze kutunusuru kwenye hili tatizo. Tunaweza kuliona leo ni janga dogo lakini sisi kule vijijini ukiamka asubuhi ni mgogoro kweli. Unashinda kutwa nzima unampigia huku, unaenda gerezani kumuangalia huyu, unamsaidia huyu, mtoto hana baba na kote unakuwa unaendelea na mgogoro, kwa hiyo nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kama utaweza kulifikiria kwa mapana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa Mheshimiwa Waziri niliwahi kuleta hoja hapa kwamba watoto

iwe lazima kuwatunza wazazi siyo wajibu, lakini naona sheria hiyo bado. Mheshimiwa Waziri lazima tuifikirie kwa mapana sana. Mimi nimefanya kazi kubwa na mtoto wangu kutoka akiwa *nursery school* mpaka *form six*. Wewe Serikali umempenda umemuona ana akili umekuja kumchukua, anakuja kukufanyia kazi wewe, unamkopesha wewe na shule anasoma ya kwako, wewe faida unachukua wewe na anakuja kukufanyia kazi na unamkata. Mimi huyu mzazi wala hunisaidii, yaani hakuna chochote chenye *value* kwangu wala huna habari. Ni kweli mbona timu za mpira, mtu anapojua mpira anapocheza mpira si unapata na wewe uliyemtunza au timu iliyomtunza? Itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na ninarudisha pongezi nyingi kwako na shukrani nyingi sana zimuendee Mheshimiwa Rais kwa kuturuhusu kulijadili hili suala la elimu na hadi tulipofikia sasa hivi nashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kishimba. Mheshimiwa Yustina Rahhi atafuatiwa na Mheshimiwa Dokta Alfred Kimea, Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi nafasi nichangie hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza nampongeza Waziri pamoja na timu yake kwa kazi kubwa aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu toka tumepata uhuru tunapigana na maadui watatu ambao ni ujinga, maradhi pamoja na umaskini, lakini unaangalia toka tumepata uhuru sasa tuna miaka 60, ukikaa saa zingine unafikiria hivi tunatumia silaha gani butu namna hii miaka 60 bado tunapigana na ujinga, magonjwa na umaskini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, silaha pekee ya kupambana na hao maadui ni elimu. Sasa tuangalie mfumo wetu wa elimu kweli umetuandaa kupambana na ujinga? Kama tunasema mtoto wa shule ya msingi angalau ajue KKK (K-Tatu), hivi KKK katika ulimwengu wa sasa wa dijitali wa utandawazi ndiyo umemtoa kwenye ujinga? Kwa hiyo, lazima tuangalie hii mifumo yetu inatupeleka wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wameandaliwa kupambana na magonjwa? Jana Waziri wa Afya alikuwa anahitimisha hapo akasema kupambana na magonjwa ni kubadilisha *lifestyle*. Achana na mafuta, sukari, chumvi na pamoja na mazoezi. Sasa ni Watanzania wangapi wanaelewa ni namna gani kwa kuelimika kwao watapambana na magonjwa ili siku moja Tanzania *Malaria* iwe historia kama ilivyo ukoma ni historia, kipindupindu ni historia. Tunahitaji silaha ambayo ni elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ndoto ya kwenda kwenye uchumi wa kati. Tunawategemea hawa vijana watupeleke katika uchumi wa kati. Tunajua demografia nchi yetu asilimia 70 ya vijana ni wana umri kati ya mwaka mmoja mpaka miaka 30. Hao ndiyo tunaowategemea, elimu yetu ni kwa kiasi gani imewaandaa hawa kwenda kujiajiri na kwenda kufanya shughuli ili walipeleke Taifa letu katika uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mama yetu amekumbuka akaliona hili akasema sasa tuangalie upya mitaala pamoja na sera ya elimu ambayo sasa itatupeleka kupambana na hali hiyo ili kijana wa Tanzania sasa aweze kujitegemea, aweze kujiajiri na aweze sasa kuiletea nchi yetu uchumi na tuweze kuvuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napongeza mtaala huu unaonekana utakuwa mtaala mzuri tu, kwa sababu unaonyesha sasa kuanzia *form one* kutakuwa na mikondo

miwili. Kuna mkondo mmoja ambao ni elimu ya jumla hii ambayo wanafunzi wanasoma *form one* mpaka *form four,* pia kuna huo mkondo mwingine wa elimu ya awali ambayo ni elimu ya ufundi, itamsaidia kijana kujifunza ufundi wa namna yoyote ili atakavyofika *form four* aweze kujiajiri na aweze kujitegemea, kwa sababu atakuwa amepata ujuzi na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji maandalizi makubwa. Kwanza wananchi wa Tanzania wenyewe wajiandae kwamba tunavyoenda kwenye mfumo huu ni vitu gani hasa vinatakiwa lakini na vijana tunaowapeleka shuleni wanapaswa kupata elimu. Serikali sasa ndiyo ifikirie tu kwamba tunavyoenda kwenye mfumo huu ambao Mheshimiwa Waziri amesema, ataanza *pilot area* mwakani, mwaka 2024, ni kwa kiasi gani kwa sababu tunahitaji bajeti ya miundombinu, tunahitaji walimu waliobobea. Isije ikawa tena ni elimu ya nadharia, unamtoa mtoto pale *form four,* unamtoa mtoto pale *form six* au hiyo *technical school* bado ni nadharia akawa hajajifunza kitu. Kwa hiyo, ninawaomba Serikali ifikirie kama tunaanza *tentatively* mwakani, japokuwa ni *pilot area* na hili ndiyo tulilokubaliana na ndiyo tunataka sasa tutoke kwenye maadui hawa watatu, basi Serikali itenge pesa za kutosha ili Wizara iweze kujiandaa kwa jambo hili geni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaloliona la kurudisha elimu yetu nyuma isiwe bora sana ni suala la miundombinu. Tulikuwa tunaona zamani tukishindanisha shule zetu, shule za *private,* shule za seminari zilikuwa zikiongoza kwa ufaulu lakini ukiangalia siri ni nini ndani? Mwalimu wa seminari ana wanafunzi 45 tu darasani ukilinganisha na shule za Kata wakati huo mwalimu ana wanafunzi hadi 100 anaowafundisha. Je, anao uwezo wa ku-*monitor* na kufuatilia mtoto huyu anafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi Taifa limefanya kwa nia njema, kwa mfano suala la elimu bure. Elimu bure imeongeza ufaulu kwa shule ya msingi na kuongeza ufaulu katika shule ya msingi ina maana pia imeongeza udahili wa *form one*. Imeongeza udahili kwa asilimia 88. Kwa mfano, tukiona mwaka wa 2021, watoto wa *form one* walikuwa wamedahiliwa 780,376 lakini mwaka jana 2023 wamedahiliwa wanafunzi wa *form one* 1,073,000. Sasa *implication* ya hii ina maana kwa sababu wengi wamedahiliwa bado tunahitaji vyumba vya madarasa, bado tunahitaji matundu ya vyoo, bado tunahitaji vitabu, tunahitaji walimu. Sasa Serikali inavyofanya vitu kwa nia njema, tunasema safari moja inaanzisha nyingine, imejipangaje sasa kuendana na hayo matokeo ambayo tuliyatarajia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kazi kubwa sana kuiweka hii katika historia kama tutakubaliana kama upungufu wa madarasa ambao unaenda kwenye 102,000 na hata ripoti ya *CAG* tumeiona ya mwaka 2021 imeonesha katika Halmashauri 45 imeonesha kuna upungufu wa madawati 158,000, matundu ya vyoo 56,000, nyumba za walimu 35,000, madarasa 27,000 katika Halmashauri hizo 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tu kwamba ni afadhali kuachana na hii kwa sababu kwanza tukiingia kwenye huu mfumo ambao utakuwa na madarasa ya kawaida ya elimu na itakuwa na madarasa ya amali bado tutahitaji madarasa zaidi. *(Makofi)*

Sasa tungeachana na huu upungufu. Kwa vile tunafahamu kwamba darasa moja linajengwa kwa shilingi milioni 20, Serikali ingeongeza bajeti basi katika Wizara hii ili tujenge madarasa *at least* 25 kwa mwaka ambapo itaenda kwenye shilingi bilioni 500 kwa mwaka ili katika historia tutakuwa tumekamilisha upungufu wa madarasa, tukapambana na jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kuangalia Bajeti ya Wizara ya Elimu, naipongeza Wizara kwa sababu bajeti imefika shilingi trilioni 1.6, lakini ninaangalia bajeti iliyoenda kwenye maendeleo ambayo ni shilingi trilioni 1.1, lakini asilimia 67 ya bajeti hii ambayo ni sawasawa na shilingi bilioni 738.7 inaenda kwa mkopo wa elimu ya juu na asilimia 33 ambayo ni sawasawa na shilingi bilioni 363.1, ndiyo inayoenda kwenye *investment*. Sasa najaribu kuangalia, watu wanaweza wakaona kwamba bajeti kubwa ya elimu ya maendeleo imefika Shilingi trilioni moja, lakini fedha za *investment* hapo bado ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuone kama kweli tuna nia njema ya kuboresha elimu, tuangalie kwamba bajeti inayoenda perse kwenye *investment*. Kwa sababu ukiangalia fedha inayoenda kwenye mkopo ambayo pengine wanafunzi watakuja kudaiwa, mimi binafsi najaribu kuona labda iwe *revolving fund* kama siyo hivyo, iwe *capacity building*. Ingefaa zaidi hata iitwe *capacity building,* lakini tukiweka kama ndiyo fedha za maendeleo, kama ndiyo *investment,* kwa vyovyote vile tutakuwa sijui tunajidanganya au tunaiumiza Wizara, kwa sababu uwezo wa kufanya kazi ni mdogo, fedha zinazobaki kwenye *investment* ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inahitaji kufanya mambo mengi, ikiwa ni pamoja na utafiti, kujenga miundombinu. Naona mara nyingi Waheshimiwa Wabunge mkiuliza kujengewa *VETA* kwenye majimbo, mkoani, lakini pesa za Wizara ndiyo hizi, kidogo, pamoja na kuwafundisha walimu na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee pia ruzuku ambayo Serikali inatoa kwa shule ya msingi zaidi, inatoa ruzuku ya shilingi 10,000 kwa mwaka. Katika fedha hiyo, shilingi 4,000 inaenda kwenye vitabu, na shilingi 6,000 ndiyo inaenda shuleni. Ukigawanya hiyo shilingi 6,000 kwa mwaka ina maana kwa mwezi ni shilingi 500 kwa mwanafunzi. Hivi

mwalimu anaweza kufanyaje kwa shilingi 500 kwa mwezi kwa mwanafunzi mmoja? Ruzuku hii ni kidogo. Kuna walimu wanajiongeza. Kuna *clip* moja ilikuwa inatembea, mwalimu anafundisha mambo ya kemikali, ameleta maziwa ya mgando, limao, na kadhalika; hivi mwalimu akitaka ku-*demonstrate,* anataka kufundisha kwa vitendo, ukamwachia shilingi 500 kwa mwezi, anaweza kufanya kitu gani? Kwa hiyo, ruzuku hii ni ndogo, Serikali ifikirie tu kuongeza basi angalau ifike hata shilingi 20,000 au shilingi 25,000 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naona linarudisha nyuma ubora wa elimu ni uhaba na ubora wa walimu. Tumeona uhaba wa walimu ni mkubwa. Kwa shule ya msingi tunaenda kwenye 100,958 na shule ya msingi tunaenda kwenye 74,000, ukijumlisha unapata 175,000. Naipongeza Wizara ya TAMISEMI na Mheshimiwa Rais kwa kutoa kibali hicho cha kuajiri walimu 13,000, lakini kiukweli *speed* hii ni ndogo, mpaka kuja ku-*overcome* hiyo *gap* ya 175,000.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina, muda wako umekwisha.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea, atafatiwa na Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Elimu. Kwanza niwapongeze viongozi

wa Wizara hii ya Elimu. Kwanza Ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Mkenda, kaka yangu Mheshimiwa Omari Kipanga, Katibu Mkuu Profesa Nombo pamoja na Manaibu Katibu Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kuhakikisha wanasimamia sekta hii ya elimu kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda kuishukuru Serikali ya Tanzania ambayo inaongozwa na Rais wetu, Jemadari kabisa, mama jembe, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kunyanyua sekta ya elimu kwenye nchi yetu. Mambo mengi yamefanyika, lakini nitazungumzia machache wala siwezi kuyaongea yote yaliyofanywa kwenye sekta ya elimu hasa kwenye Jimbo langu la Korogwe Mjini. Yamefanywa mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia vyoo, wanafunzi walikuwa wanapata shida lakini tumejengewa vyoo kwenye kila shule ya sekondari na shule ya msingi. Ukizungumzia maabara, kwenye shule zote za sekondari tumejengewa, ukizungumzia mabweni na miundombinu mingi kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, vitu vikubwa ambavyo nataka kuvitaja wananchi wa Korogwe ambao wanatamani kuvisikia Mama Samia amevifanya; moja, katujengea sekondari mpya kabisa kwenye Kata ya Bagamoyo na sasa hivi sekondari nyingine inaendelea kujengwa kwenye Kata ya Mtonga kwenye Kijiji cha Msambiazi. Hayo ni mambo makubwa, lakini hivi tunavyoongea, tayari tumeletewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya msingi na mambo mengine mengi yanafanyika kwenye sekta ya elimu. Kwa hiyo, hatuna budi kumshukuru na kumpongeza mama yetu, jembe kabisa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Kimsingi, baada ya miaka yake 10 ya

uongozi, ataacha historia kubwa kwenye nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, pia nitumie fursa hii kwa ufupi kabisa kuwapongeza viongozi wangu wa Halmashauri ya Korogwe Mji, hasa viongozi kwenye sekta ya elimu, nikizungumzia Afisa Elimu, Walimu pamoja na wadau wengine wa elimu kwenye Jimbo langu la Korogwe Mji. Kwenye Halmashauri yetu tunaongoza kwenye ubora wa elimu kwenye Mkoa wa Tanga. Hivyo, nawapongeza lakini nataka niwatie moyo waendelee kufanya kazi kwa juhudi, tuko pamoja nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo, shukurani na pongezi hizi huwa zina tafsiri yake kwa nyuma kwamba bado tunahitaji vitu vingine. Tunajua vingi vimefanywa lakini bado tuna changamoto chache kwenye shule zetu. Bado tuna upungufu wa baadhi ya madarasa, vyoo na shule nyingine ni chakavu, lakini naamini kabisa kwa kasi hii ya Rais wetu, tutaletewa hivyo vitu na baada ya miaka yetu mitano ya uongozi na Mama Samia akiwa madarakani mambo mengi yatafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa hilo. Hiyo ilikuwa sehemu yangu ya kwanza ya mchango wangu. Sehemu ya pili ni hoja yangu ya msingi kwenye siku ya leo, namwomba Mheshimiwa Prof. Mkenda apate kunisikiliza kwa umakini ili kama Taifa tuweze kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuihi alisimama ndugu yangu Mheshimiwa Maige kuzungumzia lugha ya kufundishwa kwenye shule zetu, lakini muda mchache amesimama ndugu yangu Mheshimiwa Erick Shigongo, nami pia nilikuwa na mchango kama huo huo. Sipingi kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha yetu ya Taifa. Tunaipenda, tunajivunia lugha hii na kila mtu, sio mimi tu, nadhani kila Mtanzania anatamani lugha hii ikapate kuzungumzwa *East*

*Africa* yote, ikapate kuzungumzwa Afrika nzima na hata dunia nzima. Ni lugha yetu, tunaipenda, nitaendelea kuipenda siku zote. Isipokuwa, sisi kama Taifa hatupaswi hata kidogo kupuuzia mchango wa lugha ya Kiingereza kwenye dunia hii na kwenye mchango wa uchumi wa nchi yetu. Sisi kama Taifa hatupaswi kupuuzia hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaeleza kwa uchache faida za lugha ta Kiingereza. Moja, nitaeleza faida kwa mtu binafsi, halafu baadaye nitaeleza faida kama Taifa. Kwenye dunia hii, watafiti wanasema, mtu mwenye uwezo mzuri wa kuweza kuongea vizuri lugha ya Kiingereza, akaweza kuiandika na kuisikia vizuri ana *chance* kubwa ya kuajirika kuliko mtu mwingine yeyote. Huo ndio utafiti unasema hivyo. Sisi kama Taifa hatutakiwi kupuuzia utafiti huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utaungana nami, kwenye nchi yetu, *interview* karibu zote zinafanyika kwenye lugha ya Kiingereza. Kwa hiyo, sisi kama Taifa pia tunafahamu umuhimu wa lugha ya Kiingereza. Pamoja na hilo, ili uajiriwe kwenye makampuni makubwa kwenye dunia hii, nenda *Google,* nenda *Facebook,* nenda *Space*x na makampuni mengine yote, ni lazima uwe na uwezo mkubwa wa kuweza kuongea lugha ya Kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wetu wakimaliza *Form six* wana *option* ya kwenda kusoma kwenye vyuo vikubwa kwenye dunia hii. Kama unataka mtoto kwenda kusoma vyuo vikubwa duniani, iwe *Harvard, Oxford* na vyuo vingine vikubwa kwenye dunia hii, bila ujuzi mzuri wa kuongea, kuandika na kusikia vizuri kugha ya Kiingereza, itakuwa ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, ili mtu aweze kufanya biashara za Kimataifa vizuri, lazima awe na uwezo wa kuongea lugha ya Kiingereza. Utakubaliana nami kwamba mikataba mingi ya kibiashara inaandikwa na inakuwa

*negotiated* kwa lugha ya Kiingereza. Ili uwe *consultant* mzuri kwenye makampuni ya kitaifa na kimataifa, ni lazima uwe na uwezo wa kuongea lugha ya Kiingereza. Pamoja na hayo, hizo ni faida za mtu binafsi lakini nimeamua kufuatilia faida kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwenye Ilani ya CCM, tunasema tunataka kuleta ajira milioni moja kwenye miaka yetu hii mitano ya uongozi. Lugha ya Kiingereza ni sehemu ya ajira. Watu wetu wakiweza kuongea Kiingereza vizuri, watapata ajira nje ya nchi, kwa hiyo, tutapunguza kugombania ajira za ndani ya nchi. Kama tunataka ajira milioni moja, watu 500,000 wakienda nje ya nchi, 500,000 tutawaajiri ndani ya nchi. Ukiachana na ajira, kuna *issue* ya *remittance* kwa *diasporas*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia, nika-*compare remittance,* fedha zinazotumwa na *diaspora* kutoka nje ya nchi kuja Tanzania, na nika-*compare* na zinazotoka nje ya nchi kwenda Kenya. Mtashangaa, kwenye nchi ya Tanzania kwa mwaka tunapokea dola milioni 500 kulinganisha na Dola bilioni nne kwenye nchi ya Kenya. Nikafuatilia sababu, nikaambiwa wananchi wa Kenya wana uwezo mzuri wa kujua Kiingereza, hivyo wanaajiriwa kwenye nchi mbalimbalia hasa Ulaya na Marekani. Hatutakiwi kupuuzia suala la uwezo wa Kiingereza kwenye Taifa hili. Kwenye nchi ya Kenya *remittance* kutoka kwa *diaspora* ndiyo inaongoza kwenye *foreign currency* kwenye nchi yao. Kama Tanzania, hatupaswi kupuuza hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnafahamu wote, nchi ya Kenya inavyotukimbiza na utalii. Watalii muda mwingine wanapenda kutembelea nchi ambayo hawatasumbuka kuongea lugha ya Kiingereza, ndiyo maana Kenya siku zote inatupiga *gap*. Tafiti zinasema, nchi ya India sasa hivi inaongoza kwa *foreign direct investment* kuajiri Wahindi wengi, kwani sasa hivi wana uwezo wa kuongea Kiingereza.

Ukiacha India, nenda Kenya, nenda Ghana, nenda *South Africa*, huwezi kulinganisha na Tanzania. Wawekezaji wengi wanaenda nchi hizo kwa ajili ya uwezo wa kuongea Kiingereza na wananchi wao wanapata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona faida hizo; moja, kwa mtu binafsi; na pili, kwa Taifa, nikaamua sasa kuchimba zaidi, ni wakati gani mtoto wa kitanzania, kwenye umri gani sahihi aweze kujifunza na kuweza kuelewa na kui-*master* lugha ya Kiingereza? Stadi zinatofautiana, lakini asilimia kubwa zinasema, mtoto anatakiwa kufundishwa lugha ya kigeni hasa Kiingereza akiwa na umri kuanzia miaka sita mpaka miaka 10. Baada ya hapo kweli tunaweza tukamfundisha, lakini hawezi kuongea vizuri kama *native speaker*. Hawezi kuongea vizuri kama lugha yake ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, mtoto asipofundishwa lugha hii ya kigeni hasa Kiingereza, kwenye miaka sita mpaka 10, baada ya hapo hawezi kuongea vizuri lugha ya Kiingereza na hawezi kupata hizi faida ambazo nimezielezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujiridhisha kwa hilo pasipo mashaka kabisa, kwamba huo ndiyo umri sahihi, nikaangalia sasa mfumo wetu wa elimu kwenye nchi yetu ya Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja.

**MWENYEKITI:** Malizia sekunde 30.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu wa kitanzania ni mfumo wa kibaguzi sana. Watoto wa kitajiri, watoto wa viongozi, watoto wa wafanyabiashara ndio wanapelekwa kwenye zile shule, wanasoma lugha ya Kiingereza tangu Darasa la Kwanza. Watoto wa kimasikini, watoto wa wapiga kura wa nchi hii wanapelekwa kwenye zile shule ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesho nitasimama na Shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Kabla ya kumwachia Shilingi, aniambie watoto wake wako kwenye shule gani? Baada ya hapo tuchague mfumo gani tunataka kwenda nao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kimea. Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, ajiandae.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wataalam mbalimbali wa elimu na masuala ya maendeleo duniani wamebainisha uhusiano mkubwa wa matatizo mbalimbali katika Taifa yakiwemo ajira na ukosefu wa maendeleo endelevu kuwa na uhusiano mkubwa na elimu duni na pia kuwepo uhusiano mkubwa wa elimu na duni na mitaala duni na uwekezaji mdogo katika elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nampongeza Rais wetu, amezingatia ushauri huu wa wataalamu na sasa tumeona uwekezaji mkubwa kabisa katika elimu. Tunaona mapinduzi na mageuzi makubwa katika mitaala yetu. Kazi hii kubwa ambayo inafanyika, tumeiona na tunaipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kipekee kabisa amesikiliza maoni ya Watanzania. Ni muda mrefu Watanzania walikuja na hoja hii ya uwepo wa mitaala mipya. Kwa mfano, katika *aspect* hii ya 7:4:2:3 na kuendelea, walikuja na maoni. Jambo hili ilianza muda mrefu, toka miaka ya 1985. Wenzetu Kenya walikuwa na mfumo kama huu, toka mwaka 1964 mpaka 1985. Walipofanya mabadiliko haya, kwao katika *aspect* hii wakaenda miaka minane, miaka minne, minne; kwetu Tanzania pia hitaji hili lilianza. Sasa kwa muda wote huo, hakukuwahi kuwepo mabadiliko mpaka wakati huu ambapo Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia amekubalia kufanya mabadiliko haya na tunampongeza sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Serengeti tunamshukuru kwa pesa nyingi ambazo tumepata kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* ambacho tayari sasa kinaendelea. Nawapongeza watumishi wote katika Wizara ya Elimu kuanzia ngazi ya Wizara mpaka kule Wilayani. Kipekee kabisa nampongeza Prof. Adolf Mkenda pamoja na msaidizi wake, Naibu Waziri Mheshimiwa Kipanga. Nimeangalia mitaala ile, uwezo wa kutafsiri *vision* kwenda na kuiweka katika *grounds* vizuri kiasi kile, sisi tunawapongeza sana, tunawaombeeni kazi iendelee vizuri na muimalize vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri mambo machache, kama manne, katika kuchangia bajeti ya Wizara hii. Moja, fedha ile ya *SEQUIP,* fedha ya uboreshaji wa elimu ya sekondari, naomba fedha hii ipelekwe kwa kiasi kikubwa kwenye ujenzi wa shule za ufundi. Nasema hivi kwa sababu, shule hizi za elimu ya jumla, tayari tumekuwa nazo nyingi sana, na tayari sote tunaona shule hizi hazijaweza kutusaidia vizuri. Sasa Serikali inaendelea kujenga shule zile zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Serengeti pia tumepata shule ya Nagusi inajengwa. Shule kama ile tungependekeza ijengwe kuwa shule ya ufundi. Zipo shule nyingine

zinazoendelea kujengwa, tungefika mahali ambapo tungehakikisha walau kila wilaya pamoja na uwepo wa chuo cha *VETA* iwe pia na Shule ya Sekondari ya Ufundi pamoja na Shule za Msingi za Ufundi za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuwa uwepo wa shule hizi za ufundi, zitasaidia sana kwenda kulisaidia Taifa letu kukabiliana na changamoto kubwa hii ya ajira ambayo tunaendelea kukabiliana nayo kwa wakati huu. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu ikishirikiana na Wizara ya TAMISEMI, waone sasa ulazima wa kwenda kupeleka fedha zile katika ujenzi wa shule za ufundi. Kwa kufanya hivi, tutaisaidia Wizara ya Elimu kwenda kufanikisha mtaala huu mpya ambao wanakuja nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala huu kwa ujumla wake umejielekeza sana kuhakikisha tunahamia kwenye elimu ya ufundi na elimu ya vitendo kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo naomba sana hilo la kwanza. La pili, iko fedha ambayo tayari Serikali yetu imeomba *World Bank* na wamefanikiwa na pesa hii ndiyo hii tunaona sasa imeanza kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza hotuba za Mawaziri wengi inaonesha kwamba fedha hii itaenda kutumika na itaendelea kutolewa kwa muda wa miaka mitano. Ushauri wangu, fedha hii tungeiomba Serikali ifanye kila linalowezekana itoke haraka na itumike yote mapema, ikiwezekana tuitumie ndani ya miaka miwili ili tuweze kufanya mageuzi makubwa haya ya elimu ambayo sasa yanaendelea kuinjiniwa katika mtaala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuwa tayari tumechelewa, tayari tuko nyuma, sasa ni vyema tufanye uwekezaji huu mkubwa kwa haraka. Katika uchumi, mradi wowote ukiutekeleza kwa muda mrefu, utaingia gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukumbuke tayari Wizara hii ya Elimu inahitaji uwekezaji mkubwa katika vifaa hizi shule mpya. Shule hizi za mtaala huu mpya ambao una–*focus* zaidi katika ufundi unahitaji vifaa. Tumemsikia Waziri akizungumza habari ya ku–*train* walimu, tumesikia uhitaji wa kuajiri walimu wengine wapya hii yote itawezekana kama tutaruhusu kwenda kutumia fedha hizi nyingi kwa haraka. Tukienda taratibu, tunaenda taratibu mwaka baada ya mwaka kwa miaka mitano, kuna uwezokano tusifikie tija nzuri ambayo tunaikusudia na hasa ambayo wenzetu katika Wizara ya Elimu wanaendelea kuifanya katika mitaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi tutaenda kukabiliana pia na ule upungufu mkubwa wa walimu ambao tunauona upo katika shule zetu. Tayari inaoneka shule nyingi wanafunzi ni wengi sana madarasani, wanafunzi wengi wanakaa katika madarasa yetu wakiwa hata hawawezi kufundishwa na walimu wa kutosha. Wakati mwingine ile *ratio* ya *one to fifty,* kwenye shule za misingi na ile *ratio* ya *one to forty-five* imefika mahali inashindikana. Kwa hiyo, ndiyo maana tunaomba mitaala hii sasa twende kuitekeleza kwa uwepo wa fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo hili kama unavyoliona limejengwa mara mbili, kuna ile *plan* ya *Artech's* pamoja *physical concession*. Sasa wenzetu katika Wizara ya Elimu wanakuja na *plan*, wamekuja na *plan* nzuri ya namna watakavyo *engineer* mabadiliko makubwa ya elimu kwenye nchi yetu. Lakini ile utekelezaji wake, *implementation* ya mitaala hii bila fedha ya kutosha ya haraka, naona mabadiliko haya yanaenda kushindwa. Kwa hiyo, niombe Serikali, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Elimu waone ulazima wa kupeleka fedha hii haraka na tusisubiri miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niombe sana mitaala ile nimeiona Mheshimiwa Waziri, mnafanya vizuri.

Ushauri wangu muangalie, Marx pamoja na Friedrich Engels, katika kitabu chao maarufu kabisa duniani cha *Das Kapital* wanasema *mode of production* ita–*determine* jamii itakuwaje, elimu itakuwaje na mahusiano hata pia yatakuwaje, dini itakuwaje na jamii itakuwaje sasa katika utengenezaji wa mitaala hii ni lazima watengenezaji wa mitaala hii waangalie sana je tunazingatia *context* ipi katika utengenezaji wa mitaala hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho la ushauri wangu, niombe sana Wizara ya Elimu iangalie sasa ufundishaji bora wa kingereza. Iko shida katika namna ambavyo kingereza kinafundishwa wote ni mashahidi hapa hakuna mtu amewekwa darasani akafundishwa kiswahili lakini kwanini kingereza kinakuwa kigumu cha kueleweka? Ni namna ambavyo kinafundishwa *approach* imekuwa siyo sahihi. Nimeona mara nyingi mchina, muhindi akijifunza kingereza ambayo siyo lugha yake ya kwanza anaweza kuongea vizuri, lakini sisi waswahili tukijifunza kingereza iko shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Wizara ya Elimu waangalie *approach* mpya ya kufundisha lugha ya kingereza na mwisho na kabisa niombe Wizara ya Elimu maombi matatu. Moja chuo kikuu cha Mwalimu Nyerere pale Serengeti eneo lipo, naomba mtukumbuke katika ujenzi wa benchi pia shule ya msingi na ufundi Mgumu tunaomba mtukumbuke, iweze kuboreshwa katika mpango wenu na mwisho tunaomba sekondari mpya ufundi pale Serengeti na ikikupendeza tuijenge katika kijiji cha Mesaga kule Ngolemi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar

Ishengoma Kikoyo na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia hii nafasi ili niweze kutoa mchango katika Wizara hii muhimu ambayo ndiyo imebeba maisha yetu. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wote wa Serikali. Lakini nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya katika kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya elimu. Kwa kweli hongreni sana, sote tumeshuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yeyote ili iweze kuendelea inategemea uwezo wa watu wake katika kufikili, inategemea uwezo wa watu wake katika kuwa na maarifa ya kutosha, inategemea uwezo wa watu wake katika kuwa na ujuzi wa kutosha lakini katika kuwa na umahiri wa kuweza kutenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili hayo yaweze kutokea naomba ukisoma vitabu vitakatifu Hosea 4:6 unasema hivi "Watu wangu wana angamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatukumbusha kwamba bila maarifa nchi hii hatuwezi kuendelea, bila maarifa ya kutosha umasikini wetu hauwezi kupungua, hauwezi kuisha, ili tuweze kupambana na umasikini, ili tuondekane na maradhi yaliyoko, ili tujenge uchumi imara, ili tuhakikishe kwamba tunakuwa na sayansi na teknolojia za kutosha hapa nchini tunahitaji maarifa, tunahitaji ujuzi wa kutosha na hii Wizara wamebeba hii dhamana ya kutupeleka huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na timu yake yote na Makatibu Wakuu na wote tunawapongeza kwa mageuzi makubwa ambayo mmekuja nayo katika mwaka huu. Mmekuja na mageuzi makubwa kwanza bajeti imeongezeka na inazidi kuongezeka tumeona madarasa yanajengwa kila aina, vyuo vya ufundi vinajengwa hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya mitaala ndiyo kitu muhimu sana, ambacho mmekibeba na hiki mtaacha *legacy* katika nchi hii. Mabadiliko haya ya mitaala, mitaala yeyote lazima iendane na mahitaji ya nchi na *agenda* ya kitaifa ya nchi. Ajenda ya kitaifa ya nchi yetu sasa hivi ni umasikini uliokithiri, nikujenga uchumi imara ili tuweze kushindana katika nchi yetu hasa haya yote yatawezekana tukifanya mabadiliko makubwa ya mitaala yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara imeanza mabadiliko makubwa na ninawapongeza, juzi tumeshiriki hapa wametufundisha lakini wameleta watu 1,500 kuchangia mawazo kwenye mitaala, haijawahi kutokea mmefanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Lee Kuan Yew wakati ananza kuitawala nchi ya Singapore aliitisha watalam, akasema nataka mniambie kama watalam nifanyaje ili nchi hii iendelee? Na wewe Mheshimiwa Waziri umesema jamani sisi mawazo yetu ni haya, nyinyi mna mawazo gani? Ndiyo maana umeitisha kila aina ya semina na watu kuchangia na sisi hapa tunachangia nakupongeza sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikia waliyochangia kuhusu kiswahili na waliyochangia kuhusu kingereza lakini mimi sitaki kuingia kwenye huo mjadala, nataka nikumbushe tu. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Mwaka 1985 wakati anang'atuka, analihutubia Bunge hili nafikiri ulikuwa mwezi wa nane alisema hivi "kiswahili kimefanya kazi

kubwa ya kuwaunganisha watanzania mpaka hapa tulipofika, akasema lakini kiswahili hakitatuwezesha kufika kule tunakotaka" sasa lazima tuzungumze kiswahili cha dunia, kiswahili kimetufikisha hapa sasa tuzungumze kiswahili cha dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda sitaweza kuyazungumza sana. Lakini kiswahili ni muhimu kimefanya kazi yake, kimetuunganisha watanzania sasa tutafute kiswahili cha dunia, ili tujifunze sayansi na teknolojia, iweze kutusaidi katika kujenga uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mageuzi yanayoendelea Mheshimiwa Waziri ya Mitaala, tunataka tuone kuwe sasa na mageuzi ya namna ya kufundisha. Ufundishaji wetu uendane na mitaala yenyewe tunayoihitaja. Vifaa tunavyovitaka kama ni *competence based,* umahiri lazima tuwe na vifaa vya kuhakikisha kwamba tunawaandaa vijana wetu katika hawa, hawawezi kufikia huko bila kuwa na vifaa vya kufundishia vya kisasa. Tunahitaji kubadilisha fikra, kwa sababu ukiwa na maarifa, ukawa na ujuzi bila kubadilisha tabia bado hatutaweza kufika, tubadilishe tabia maarifa hii itusaidie tuwe na nidhamu tuweze kutekeleza mambo yetu, tuweze kufanya kazi yetu vizuri, naamini hili linawezekana na kila kitu kitawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kazi mnayoifanya nzuri, vyuo vya ufundi, vyuo vya sekondari mnabadilisha manakarabati vya zamani mnakuja na mitaala mipya, mnakuja na vitabu vipya, mmesema mnaanza kufundisha walimu katika ngazi mbalimbali ili wawe ni *competent* hongera. Kwa hiyo, na sisi tutakuunga mkono kwa hali mali ili kuijenga nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mkoa wa Songwe, Mkoa wa Songwe ni Mkoa wa Kilimo na unalima kweli kweli na tunachangia kwa kiwango kikubwa katika Taifa hili. Lakini

tunazo shule za sekondari zaida ya 62 kwenye Wilaya ya Mbozi, Wilaya peke yake ya Mbozi yenye jimbo moja tunazo zaidi ya 62 shule za sekondari. Pamoja na kwamba sisi ni mkoa au ni wilaya ya kilimo lakini hatuna shule hata moja inayofundisha kilimo. Maana yake tunawaandaa wale watoto wasiende kwenye kilimo, kitu ambacho ni kizuri lakini je, kweli? Tuna uwezo wa kuwaondoa wote kwenye kilimo? Sasa hili Mheshimiwa Waziri naomba mliangalie, naomba hili mliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti namshukuru pia katika Mkoa wa Songwe ametuletea Chuo cha *VETA*. Unajenga chuo cha *VETA* sasa na nimeambiwa fedha zimeanza kwenda za kujenga Chuo cha *VETA,* tunapongeza sana kwa hilo, tunafurahia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema hata wakifanya vizuri bado maombi ayaishi, tunaendelea kuomba mkoa wetu ni mchanga ndiyo mkoa wa mwisho kuanzishwa hapa nchini, bado unamapungufu mengi, baada ya *VETA* tunahitaji tawi la chuo kikuu angalau kimoja, sasa hiyo iwe ni kutoka sekta binafsi, iwe ni kutoka wapi, tunahitaji chuo kikuu katika Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo Mheshimiwa Waziri tumeona kazi ya kutoa elimu katika nchi hii ni kazi ya Serikali, lakini na wadau mbalimbali ambao wanachangia katika kutoa hiyo elimu ikiwemo sekta binafsi ambao kuna shule binafsi, kuna vyuo binafsi na kadhalika vyote vinachangia katika kutekeleza jukumu la kimsingi, la kikatiba, la Serikali yetu. Sasa basi vyuo hivi kusiwe na sera ya ubaguzi, hao watekelezaji wote waunganishwe, wanafanyakazi ileile ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi watoto waliyosoma kwenye vyuo, kwenye shule za sekondari za watu binafsi kwenye mikopo wanabaguliwa, wanaambiwa hawana

uwezo hii siyo sahihi. Inatakiwa wale wasaidiwe, inatakiwa nao waungwe mkono ni watanzania, vyuo binafsi ni vyuo vya Tanzania. Kazi yetu sisi ni kuviimarisha, ni kuboresha mitaala vitoe maarifa mazuri, ili vivutie wasomaji na wanafunzi kutoka nchi za nje. Tupate watalii kutoka nchi za nje, waje kusoma Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jitihada tulipofikia hapa, vyuo vyote vilivyoanzishwa hivi vinatakiwa vilindwe kwa sababu vinatoa ajira, vinatoa maarifa, vinachangia katika uchumi wa Taifa letu ili watu wengi kutoka nchi za *SADC* waje kusoma Tanzania, waje kuona Mlima Kilimanjaro, waje kuona bahari na maziwa waje kusoma hapa nchini kwa hiyo, ni muhimu tukaboresha katika hilo eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunahitaji vyuo vyetu sasa viwekeze kwenye kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitalamu. Sasa hivi kwenye vyuo vyetu mkazo uko kwenye kufundisha na kufundisha bado atujafikia kwenye *level* ya *competence based*, bado tunafundisha ya kinadharia zaidi. Sasa wakati tunatoka huko kwenda kwenye *competence based* lakini pia tusisitize kufanya utafi na tusisitize kutoa ushauri wa kitalamu na baada ya kufanya utafiti, tusisitize katika kuandaa machapisho ndiyo yatakayoisaidia nchi hii.

Mheshimiwa Mwwenyekiti, sasa hivi vijana wengi wanafanya *project*, vijana wengi wanafanya *research* nzuri sana unakuta anapata A lakini ukienda unakuta kwamba hiyo *research* aliyoifanya inaenda kuwekwa kwenye makabati badala ya kuichukua na kuona namna inavyoweza kuisaidia nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja, nasisitiza nawaunga kwakweli, tunawapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya na nchi hii tunawategemea, maendeleo ya nchi hii yako mikononi mwenu Mungu awabariki, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo atafuatia na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo na Mheshimiwa Minza Simon Mjika ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipatia fursa ya kuchangia Wizara ya Elimu. Niwapongeze Mheshimiwa Waziri Mkenda, Naibu wake Ndugu yangu Kipanga, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya hasa kwenye sekta ya elimu kwa kuwapatia pesa kubwa na nyingi inadhihirisha nia aliyonayo katika kuboresha elimu yetu. Naomba kutofautiana kidogo na wachangiaji waliyonitangulia, naongelea suala la mtaala ambao uko mbioni kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi tunapotengeneza mtaala kwenye ukachukua maandiko matakatifu yanasema "mvinyo mpya kwenye kiliba cha zamani haifai". Tunayo Sheria Na. 25 ya Elimu ya Mwaka 1978 ilifanyiwa marejeo na Sheria Na. 10 ya Mwaka 1995. Sheria imepitwa na wakati, kama tunataka kuboresha elimu yetu lazima tuanzie huko kwenye sheria ndiyo chimbuko kubwa la kuboresha elimu yetu hata tufanye nini? Tubadilishe mitaala, tufanye nini? Hatutaweza kuboresha elimu. Turudi kwenye chanzo kule, tuboreshe elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Ukiangalia Wizara ya Elimu leo inaendeshwa kwa nyaraka. Zipo nyaraka nyingi sana na hizi nyaraka zinazotolewa na Wizara ya Elimu kila siku ni ishara kwamba kwenye sheria kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye sheria, zipo nyaraka nyingi sana hapa ukisoma unahitaji unaweza

ukafanya *research* ya *PHD*. Kwenye maeneo kumi na tatu mahususi ya elimu zipo nyaraka rukuki kwa mfano ukiangalia nidhamu na malezi zipo nyaraka tisa, ukiangalia kamati ya bodi za shule nyaraka sita, udahili wa wanafunzi nyaraka kumi na saba, ukienda mihula na siku za masomo nyaraka tatu, michezo nyaraka tano, elimu ya ualimu nyaraka tisa, kufukuza kurekebisha na kuamisha wanafunzi nyaraka kumi na moja. Uendeshaji wa mitihani nyaraka kumi na sita, ukienda masharti ya usajili wa shule nyaraka sita, kukuza uzalendo hapo kuna nyaraka moja sijui kwa nini? Nyaraka ya ajira za nje moja, ada na michango nyaraka kumi na nne, taaluma ufaulu na ufundishaji wa rula nyaraka ishirini na nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa ukiangalia hizo nyaraka nane anazitoa kafanya utafiti wapi? Unatoa nyaraka kwa sababu wanataka ku–*supplement* kuna madhaifu makubwa katika Sheria ya Elimu. Sasa nadhani tunapoongelea mitaala tuangalie sera yetu, tuangalie sheria yetu tuweze kuioanisha, tuweze kupata kitu ambacho ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuishauri Wizara ya Elimu, zimetoka nyaraka nyingi sana na juzi juzi hapa ilitoka nyaraka ya watoto wa bweni, *nursery school* wasiende *boarding*, waingie bweni wakiwa darasa la tano. Tunaenda wapi? Tunakwenda mbele, tunarudi nyuma? Hebu tuangalie uchumi wetu, kadiri uchumi unavyokua watu wanavyokuwa na pesa ndivyo watu wanavyo wajibika zaidi kwenye sekta za uzalishaji. Sasa kupanga ni kuchagua, Serikali kazi yake ni kudhibiti ni kufanya kazi ya *regulatory regulations* siyo kupangia watu waishije? Wasomesheje watoto wao? Hiyo siyo kazi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri kadri tunavyotarajia kwenda kwenye uchumi wa kati, ndivyo watu wanavyokwenda kuwajibika zaidi kwenye sekta binafsi na sekta nyinginezo. Sasa mtu anaamua mtoto amwachie nani?

amwachie *maid* hawapatikaniki siku hizi. Kwa hiyo, chaguo halisi ambalo mzazi analiona kwa wakati huo ni kumpeleka shuleni bweni ambako ana uhakika na malezi ya mtoto wake. Niwaombe Wizara ya Elimu tulitafakari hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tena kuishauri Wizara ya Elimu tuiangalie *private sector*. *Private sector* ina shule nyingi, inaajiri watu wengi na imewekeza mitaji kwenye elimu hii lakini kwa macho ambayo unaiangalia *private sector* ni kama mshindani wa Wizara ya Elimu si kweli. *Private sector* ina *supplement* pale ambako Serikali haiwezi kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia *private sector* imewekeza kiasi gani kwenye Wizara hii? Tukiangalia *private sector* inaajiri walimu wangapi katika Taifa hili? Inalipa mishahara walimu wangapi kwenye sekta hii ambao wengekuwa *redundant* kama wasingekuwepo? Nashauri, Mheshimiwa Waziri *private sector* tuichukulie kama ndugu yetu siyo mshindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia mahusiano kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya TAMISEMI, mahusiano yale hayana tija. Ukiangalia kule TAMISEMI tuna wadhibiti ubora mikoani, tuna wadhibiti ubora wilayani, hao wote wanawajibika kwa Waziri wa TAMISEMI, lakini wanafanya kazi ya Waziri wa Elimu. Kuna mpingano, kuna mkorogano hapo katika mahusiano kati ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI. Lazima tuliangalie; na ndiyo maana mimi nashauri badala ya kwenda kwenye mitaala tuangalie kwanza sera na sheria zinasemaje kama tunataka kuleta utulivu kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda huko hata kwenye shule binafsi, unakwenda TAMISEMI wanasema ya kwao, Wizara ya Elimu wanasema ya kwao. Tumefanya hivyo kwenye sekta ya maji, tumefanya hivyo nadhani na sekta ya *TARURA*. Nashauri watendaji wote ambao ni wadhibiti ubora

ambao wako TAMISEMI warudishwe Wizara ya Elimu. Tuwe na Wizara moja ambayo inafanya kazi ya kusimamia elimu na TAMISEMI wabaki na suala la kusimamia miundombinu tu, masuala ya kisera yote yarudi Wizara ya Elimu, vinginevyo tutakuwa tunacheza mdundiko hapa. *(Makofi)*

Mheshimwia Mwenyekiti, yanatoka maagizo, yanatokea TAMISEMI; Wizara ya Elimu hawayakubali. Mengine ya Wizara ya Elimu, TAMISEMI hawayakubali; tunakwenda wapi? Nadhani tunapaswa kuoanisha haya mambo. Serikali ni moja, Taifa ni moja na ni Serikali ya Awamu ya Sita ya mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nawaomba mkae chini mkayangalie haya mambo, tuwe na Wizara moja mahsusi inayo–*regulate* na inayoratibu masuala yote ya elimu kama sera na sheria zinavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nirudi kwenye jimbo langu. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana, tunakushukuru sana hasa Mkoa wa Kagera, na salamu zetu tunaomba umfikishie mama yetu Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; kwa miaka nenda-rudi Mkoa wa Kagera tumepigania kupata chuo kikuu. Tumejaribisha kupitia *private sector* tulishindwa, vikaja vyuo ambavyo vilianzishwa na mashirika ya dini vinajikongoja. Kama mnavyofahamu, Mkoa wa Kagera ni mkoa wa elimu, upende usipende ndivyo ilivyo, ndiyo historia yetu. Kwa kutupatia chuo kikuu chini ya mradi wa *HEET* tunakushukuru sana na tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi niende kwenye Wilaya yangu ya Muleba, Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana, juzi hapa tumepewa taarifa wametupelekea takribani milioni 900 kwa ajili ya chuo chetu cha *VETA*. Kulikuwepo na chuo kidogo hakikuwa na heshima ya Wilaya ya Muleba. Tunakushukuru sana na tunakuomba sasa hicho chuo kijengwe haraka sana. Lakini kama wengine walivyosema, tunapojenga hivi vyuo vya *VETA* na tunavyotoa elimu yetu,

mwaka jana kuna mchangiaji mmoja alichangia hapa, tuangalie tunachofundisha watoto wetu. Walikuwa wanaongelea mambo ya historia, eti tulifundishwa mwanadamu ni *evolution,* alitokea kwenye nyani na bado tunaendelea kufundisha haya mambo kwa watoto wetu. Hivi kwa nini tusikae chini tukatafakari tukaja na mfumo wetu wa elimu wa kuwafundisha watoto wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nilikuwa naangalia kwenye mtaala ambao wameutoa, Mimi naomba nishauri, ukiangalia mpangilio wa yale masomo mliyoyaweka bado tuna *mentality* ile ile ya miaka ya 1960. Mimi nilitarajia tuangalie dunia inakwenda wapi, na uchumi unaelekea wapi. Sasa hivi unapoongelea kufundisha watoto unakwenda kuwafundisha historia zilizopitwa na wakati, haina tija kwa watoto wetu na haina tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani tungeelekeza nguvu zetu kwenye kufundisha TEHAMA, kufundisha *innovation*, *consumer protection* ili watoto wetu wakue wanajua mambo gani ya msingi ya Taifa lao. Taifa letu linasimamia nini? Ukienda nchi za wenzetu unamuuliza mtoto kwa mfano Tanzania inasimamia nini, ukiwauliza watoto wa Kimarekani watakwambia Marekani inasimamia nini miaka 100 ijayo, lakini sisi hapa ukituuliza itategemea tu kama mvua imenyesha, kama kuna maji mito imefurika, tuje na kitu mahususi cha kuwafundisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *VETA* zetu; hivi hizi taasisi zetu ambazo ziko chini ya elimu sijui *SIDO,* sijui nini, zinafundisha nini watoto wetu? Hii mitaala kweli inaendana na hali halisi ya maisha yetu Watanzania? Sioni. *VETA* iko Kagera unawafundisha sijui vitu gani? Badala ya kuwafundisha kutengeneza nyavu, kuwafundisha kuvua samaki, tunafundisha vitu ambavyo tumevi-*import* kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga hoja mkono.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, atafuatiwa na Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza kuchangia, binafsi naona Serikali imefanya kazi kubwa kwenye kuhuisha sera hii, ile ya mwaka 2014 kuileta hili toleo jipya la mwaka 2023, labda kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati, lakini naona wamezingatia kwa kiasi kikubwa maoni na matamanio ya Watanzania kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa hilo niipongeze Serikali, lakini bado ushauri wangu unabakia pale pale tusiishie kwenye kuandika. Kwa kweli ukisoma, ukatulia na ukafuatilia kama kweli yatakwenda kwenye utekelezaji, kama kweli uwekezaji utakuwa namna ile ambayo tunaambiwa, mimi naamini tutakwenda kwenye *step* nyingine.

Kwa hiyo, nitofautiane kidogo na mwenzangu aliyetangulia kwa sababu pale kuna *financial management,* kuna mambo ya *music,* watu wanaopenda *music*, kuna mambo chungu mzima ambayo tulikuwa tunasema kwamba watu wasifanye kwa mazoea. Sasa hivi yamewekwa kwenye sera na kwenye mitaala, na mimi kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati ya Elimu tumepata nafasi mbalimbali za kupitia kushauri na kuelezwa na kuelekezwa ni kitu gani kinakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala la msingi Serikali kweli ikafanyie kazi yale ambayo wameyaweka kwenye maandishi ili kile tulichokikusudia kama nchi tukifikie. Sasa sambamba na hilo, ukisoma ile sera inakwenda zaidi kwenye mambo ya ujuzi, hapo tutapata vyuo vya kati. Lakini sasa wasiwasi wetu ama wasiwasi wangu unakuja hapo kwenye vyuo vya kati ndio inaonekana kuna ugumu wa wanafunzi kusoma kwa sababu ya kukosa mikopo. Serikali sasa itueleze imejipanga vipi ili kuhakikisha wale ambao hawatakwenda kwenye mkondo wa jumla wanakwenda huku kwenye hivi vyuo vya kati kwa ajili ya mafunzo ya amali, wamejipanga vipi kuwawezesha kufikia ndoto zao? Ndio hiyo ninayosema ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vyuo vya *VETA* vinajengwa nchi nzima. Nayo Serikali itueleze imejipanga vipi kuhakikisha wakufunzi wanakuwepo? Sio wakufunzi kwa maana tu wamekaa pale, mkufunzi mwenye sifa stahiki ya kufundisha kile ambacho tumekikusudia mtoto wetu akipate. Serikali ije ieleze kwa undani. Hayo ndiyo mambo ambayo tunataka tuyaone yasiishie kwenye maandishi yaende kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamu, lile suala la kufanya Chuo cha Ualimu Mtwara kawaida kuwa tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam limefikia wapi? Kwa sababu miaka inapita tunaambiwa, natamani Mheshimiwa Waziri atapokuja kuhitimisha atuambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotamani kufahamu; kwenye uandaaji wa mfumo wa usajili wa shule kwa njia ya kielektroniki nao umefikia wapi utekelezaji wake? Pia na hilo natamani nipate kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka nisisitize, mimi kama mwalimu ukiniambia elimu ya awali Mheshimiwa Waziri unasitasita kusema ya lazima au watu wasome tu kwa

kujisikia. Mimi natamani nisikie ya lazima, kwa sababu pale kwenye elimu ya awali watoto wale wadogo ndiyo tunategemea pale wafundishwe namna ya ushirikiano. Unajua tatizo linalokuja tunaona elimu zetu za awali labda kwa sababu zinafundishwa na walimu ambao wengi wao hawajapitia mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana tunaona wanafundisha mambo makubwa tofauti na umri wa watoto. Kwenye elimu ya awali watoto wacheze wakati wanajifunza, watoto wafundishwe namna ya kushirikiana kwa sababu nyumbani mwingine anatoka peke yake hajui kushirikiana na mwenzie, lakini pia wafundishwe zile *language skills* mbalimbali, ndivyo tunavyotegemea viwepo kwenye elimu ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri ukisitasita ilhali tunajua kabisa hapo nyuma kulikuwa na *movement* kwamba kila shule ya msingi kuwe na darasa la awali? Sasa leo kimeingia kizungumkuti gani cha kusema kwamba hii elimu iwe ya lazima? Hapo ndipo ambapo mimi hapo bado nina *question mark* ambayo natamani ukija kuhitimisha utueleze. Ulieleza pale Pius Msekwa, binafsi mimi sikukuelewa, yaani mpaka leo sijakuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme, mchangiaji aliyepita yeye ameongea kwamba shule za *private* zinaajiri walimu, zina wanafunzi na mimi ninakubaliana naye. Mimi nakupeni *data;* leo hivi tunavyoongea kuna walimu 25,926 wako katika shule za msingi za *private;* tuna walimu 21,343 wako katika shule za *private* za sekondari ambapo hizi shule zisingekuwepo hawa walimu wote wangekuwa wako mtaani wanasotea ajira za Serikali. Lakini leo tunapoongea kuna wanafunzi wa shule za msingi 591,005; pia kuna wanafunzi wa shule za sekondari 291,882 wako *private school.* Sasa tujiulize, maana hizi shule leo

zisingekuwepo hawa wote wangekuwa wamerundikana wapi kwenye shule zetu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa ninachotaka kukisema, mimi sina shule wala sina *interest* ya kuanzisha shule, ninachotaka kusema jukumu la kuendeleza au la kutoa elimu kwa wananchi wake ni la Serikali, hii inajulikana kwa asilimia 100. Sasa hawa wawekezaji wanapojitokeza Mheshimiwa Waziri mkae chini, mtatue changamoto kwa amani kwa sababu hawa watoto wanaosoma kule ni watoto wa Kitanzania. Wakielimika wameelimika kwa ajili ya Taifa la Tanzania. Kwa hiyo, yale makandokando mnayoyaona yanaweza upande mmoja yanaleta shida na upande mwingine yanaleta shida, mjitahidi kuyatatua ili tusonge kwa sabaabu hawa ni Watanzania, yaani mtoto akisoma *private* habadiliki kuwa si Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuhusu uhaba wa walimu. Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati yetu alituletea; unajua hapa zinasomwa *data* nyingi, inategemea mtu ameitoa wapi *data* yake. Mimi *data* ninayoongea ni *data* tuliyoletewa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwenye Kamati yetu ya Elimu alisema hivi, uhaba wa walimu. Elimu ya awali, mahitaji ni 61,487; waliopo ni 8,619; uhaba ni 52,868. Elimu ya msingi, mahitaji ni 300,702; waliopo ni 167,245 na upungufu 133,457. Elimu ya sekondari, mahitaji ni 174,632 waliopo ni 84,700, upungufu ni 89,932. Kwa hiyo, mimi ninaachana na hiyo habari ya awali nikachukua tu msingi na sekondari, si kwa maana awali haina mantiki, ina mantiki sana, nimetoka kusema hapa. Upungufu uko 223,389 ukitoa hiyo ajira mpya ambayo imekuja walimu 13,130 upungufu bado unabakia 210,259. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua wahisani wanaweza kutusaidia kujenga miundombinu lakini hawawezi kutusaidia kuajiri walimu. Kama nchi na kama Serikali, hivi vitu inabidi viende sambamba. Kwa maana ipi? Wakati tunasema elimu

bila ada tukumbuke wanafunzi wengi watoto wengi watandikishwa. Tena sasa hivi sera ile inatupeleka mpaka *form four.* Tuone ni kwa namna gani Serikali inajipanga kuajiri walimu wa kutosha, kujenga miundombinu ya kutosha, vitabu huko shuleni ni majanga. Fedha ya ruzuku mpaka leo mtoto wa shule ya msingi anatolewa shilingi 10,000 kwa mwaka, tena 10,000 hiyo 4,000 inabaki Wizarani huko wanasema ya kununua vitabu, na hapo hapo hiyo 6,000 anapoenda shule ukisoma ripoti ya *CAG* anasema mwaka 2021/2022 ilikuwa iende bilioni 33.7 lakini katika hiyo hela haikwenda yote, bilioni tano haikwenda, mnategemea walimu wetu wafanye kazi kwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Serikali iende kwenye utekelezaji wa sera na mitaala mipya ambayo inaanzishwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Minza Saimon Mjika, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mheshimiwa Hamis Tabasam Mwagao ajiandae.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru sana Rais wetu kwa jinsi anavyopambana katika sekta hii ya elimu. Mama anajitahidi ametupa fedha nyingi na amejenga madarasa mengi pia. Lakini vilevile nimshukuru Waziri wa elimu pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ambazo anazifanya, kweli wanapambana na wanaleta maendeleo katika elimu. Nimshukuru pia Katibu wa Elimu pamoja na Manaibu wake kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nasema nishukuru kwa sasa, katika Mkoa wa Simiyu Wilaya ya Meatu

tumepata fedha kwa ajili ya kujenga *VETA,* kwa hiyo nashukuru sana. Mwaka jana nilisimama hapa kuchangia nikaomba hivyo Waziri umetekeleza; wakazi wa Wilaya ya Meatu tunashukuru sana. Lakini vile vile tunashukuru kwa fedha mlizopeleka. Mmepelekea milioni 228, lakini kazi ile ni ya bilioni tatu. Jitahidi sana Waziri kupeleka pesa kule ili yale majengo yajengwe kwa wakati na si kwamba *VETA* ijengwe kwa muda wa miaka mitano, haipendezi. Jitahidi fedha zile ziende na shughuli ziende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kazi nzuri ambazo mnaendelea kuzifanya, mnaelimisha jamii, mnatoa fedha nyingi, tunapata madarasa na madawati pia. Lakini tukumbuke Watanzanjia tuna watoto wengi sana katika shule zetu. Pamoja na kupambana kujenga madarasa miundombinu lakini bado tuna upungufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongea juu ya walimu. Walimu kwa kweli wako katika mazingira ambayo ni magumu sana, lazima niwasemee. Walimu wanahangaika wanafanya kazi katika mazingira magumu. Niliona shule moja hapa, niliwasiliana na Mkuu, shule moja ambayo iko katika Wilaya ya Itilima ina watoto1,200 lakini ina walimu 11, *just imagine,* wale waaalimu wanafanyaje kazi jamani? Mwalimu afundishe kuanzia chekechea, akitoka chekechea ana kipindi cha darasa la kwanza, akitoka kipindi cha darasa la kwanza, ana kipindi cha darasa la tatu yule mwalimu kweli unamuandalia mazingira mazuri hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajikuta mwalimu anachoka, anaongea na wale watoto yaani ukiingia darasani katika Mkoa wetu wa Simiyu nisemee, darasa moja lenye wanafunzi wachache labda ni wanafunzi 125 au 130, mwalimu huyu mmoja. Sasa jiulize, darasa la kwanza mwalimu anaandika kengine kanamfinya; yaani mwalimu unamuweka katika mazingira ambayo ni magumu hata kazi yake anaona kwamba jamani nifanyeje. Lakini bado mwalimu yule

anatoka mbali, umbali wa kilometa tisa mpaka kumi, mwalimu anaendesha baiskeli ama kabebwa kwa boda boda na kwa hela hiyo hiyo tunayoijua. Afike kule mwalimu amechoka, kanyeshewa mvua, yaani ni vitu vya ajabu. Mwalimu tena aingie darasani lakini akifika darasani na penyewe mwalimu anapata shida watoto ni wengi wengine wamekaa chini mwalimu anaandika wanamvuta sketi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usiombe kufundisha darasa la kwanza, na ndiyo maana walimu wengi huwa wanakimbia sana kufundisha darasa la kwanza la pili na la tatu, ni watoto amabo ni wasumbufu mno. Una watoto 140 mwalimu mmoja unafundishaje? Haya wengine wamekaa kwenye madawati, wengine chini, ni vurugu; kanakolia, kanafanya nini, unajikuta mwalimu hafanyi kazi katika mazingira yaliyo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamesema habari ya *private; private* wanajitahidi kweli inabidi Wizara ya Elimu kujiuliza kwamba inakuwaje shule zetu za Serikali zinakuwa na walimu wachache kiasi hicho? na wale wanajitahidi wanakuwa na walimu wengi ambao wanakuwa na mgawanyo mzuri wa masomo, basi mwalimu hata kama amezidiwa namna gani awe na watoto 50; watoto 50 anaweza akajitahidi mwalimu akawafundisha. Mwalimu huyu unampa watoto 130 au 140 lakini atoe maswali 50 kwa kila somo, hasa darasa la saba na la sita, hivi hebu fanya 50 mara 120., atakuwa amesahihisha maswali mangapi? Yule mwalimu akitoka pale atakuwa na hali gani? Waziri wa Elimu naomba ajitahidi sana kwa hilo, atuletee Walimu wa kutosha katika Mkoa wa Simiyu ili tupunguze idadi ya wanafunzi wengi ambao hawaelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine napenda niseme, Serikali imefanya vizuri sana katika kuwapatia Walimu vishkwambi kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia. Tunashukuru kwa hilo Walimu amewasaidia, lakini kuna sababu ya Serikali isaidie upatikanaji wa *wireless internet* ili kurahisisha watoto na

Walimu kusoma kwa kutumia teknolojia mpya hii ya kisasa, Mwalimu asaidiwe. Niliwaona Walimu siku ya Mei Mosi walikuwa wakimwambia mama, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanasema mama tumepewa vishkwambi tunavyo, lakini tunataka tufundishwe jinsi ya kuvitumia. Kwa hiyo, Profesa atumie muda wako apate timu ambayo itawasaidia Walimu ili waweze kufanya kazi katika njia iliyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni upungufu wa miundombinu kwa Walimu. Walimu wengi hawaishi shuleni, wanaishi mbali sana. Angalia mazingira ya kule kwetu, Mwalimu anatoka pale Bukundi anaenda Lukale Shule ya Msingi, ni mbali sana ni kama kilometa kumi na tatu, kumi na nne, anaendesha baiskeli, akifika kule Mwalimu amechoka hawezi kufanya kazi na bado mazingira yetu sisi ni magumu sana kule. Walimu wangepata nyumba, wangefanya kazi vizuri, wakae katika maeneo ya shule ili Mwalimu aweze kutekeleza majukumu yake vizuri. Naomba Waziri alichukue hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona Rais wetu amejitahidi amejenga madarasa mengi sana, basi uwepo na utaratibu wa kujenga nyumba za Walimu ili wakae katika maeneo ya shule, maeneo ya shughuli zao. Walimu wanaishi mbali sana, unakuta anatoka pale Mwanuzi Shule ya Msingi anaenda mbali, umbali wa kilometa kumi na mbili, kumi na tatu, hivyo, Mwalimu anafika amechoka hata ule ufundishaji wake unakuwa uko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka niseme ni changamoto ya madarasa. Madarasa kweli Serikali imejitahidi kujenga, lakini bado kuna upungufu mkubwa. Walimu wanahangaika katika madarasa na watoto wengine wanasoma nje kwa sababu vile vyumba vya madarasa havitoshi. Serikali ilijitahidi kumweka Mwalimu katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine nataka kuzungumzia habari ya hawa watoto wenye mahitaji maalum, watoto hawa wanahangaika sana. Unakuta Mwalimu anafundisha hana darasa la watoto hao, anavamia hapa, yuko hapa, mara yuko nje. Basi Serikali ijitahidi ijenge madarasa maalum kwa wale watoto wenye mahitaji maalum ili nao wasome katika hali nzuri na wajisikie vizuri, pia hata Walimu wawe na mazingira mazuri ya kuwafundisha watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine Mheshimiwa Waziri nataka nishauri juu ya hawa watoto wa MEMKWA. Watoto wa MEMKWA ingependeza nao waandaliwe miundombinu yao, wawe na madarasa yao *special* kwa ajili ya kufundishiwa. Kwamba, hii ni MEMKWA wafundishwe, sio mpaka wasubiri watoto wengine wamalize, wamechelewa, anaingia Mwalimu akiwa amechelewa na ufundishaji wake unakuwa haujakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho napenda niseme, Walimu wetu wanalalamika sana juu ya mafao yao, hasa wanapostaafu. Wanapostaafu inaonekana kwamba, Walimu tunawasahau na tunawatelekeza, lakini wamefanya kazi nzuri sana na kazi ya hali ya juu ya kuinua elimu ya nchi yetu ya Tanzania. Mwalimu anapostaafu *pension* yake inakuwa ni matatizo, wengi wanalia, kila siku napigiwa simu, tusaidie huko. Jamani Mwalimu anapokaribia kustaafu kabla hata ya miezi mitatu mwandalie *pension* yake, apewe hela yake yote aifanyie kazi yeye mwenyewe, sio aanze tena mizunguko ya kuja Dodoma mara mbili, mara tatu, mara nne, hata hela hana, anakopa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuishukuru sana Serikali yangu kwa utendaji mzuri ambao unaendelea. Serikali imefanya vizuri sana kuwapatia Walimu hivyo vishkwambi, kama nilivyosema, lakini hapa kuna *message* nyingi,

wanasema, mwambie Waziri ajitahidi tuelewe vizuri kuvitumia vile vishkwambi. Kwa hiyo, wengi hawaelewi. Waziri apate muda, atafute timu yake, iwafundishe Walimu ili waweze kuvitumia vizuri vile vishkwambi na viwe msaada kwao wao na kwa wanafunzi ambao wanawafundisha, litakuwa ni jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Napenda niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Jasson Samsoni Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamisi Tabasamu Mwagao na Mheshimiwa Dennis Londo ajiandae.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika bajeti ya Wizara ya Elimu. Nimpongeze na kumshukuru Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda; Naibu Waziri, Mheshimiwa Omari Kipanga; Katibu Mkuu na Naibu wake na viongozi wote wa Wizara na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri sana anayoifanya ya kuboresha elimu na hata sekta nyingine anazozisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo pale Bukoba kwangu shule nyingi zimejengwa, madarasa mengi yamejengwa. Pale Mkoa wa Kagera leo tuna Chuo cha *VETA,* chuo kikubwa kizuri sana cha *VETA* kimejengwa, amekifungua mwaka jana yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais na hivi ninavyoongea tunajenga Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, *branch* ya Bukoba. Haya ni maendeleo makubwa ambayo kwa kweli nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huku chini ngazi ya Wizara, Waziri na wasaidizi wake na watendaji wote, naomba tumsaidie Rais kwenye kazi hii, tumsaidie Rais kwa nguvu zote, kwa moyo wote, kwa bidii zote. Wamesema Wabunge hapa leo na siku zote wanasema, amesema msemaji wa mwisho hapa kwa mfano, uhaba wa Walimu ni tatizo kubwa sana kwenye shule zetu. Ni tatizo kubwa sana ambapo shule zimejengwa, madarasa yapo, lakini hakuna Mwalimu, sasa ni kama sifuri, kazi iliyofanyika ni *zero*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina shule pale Bukoba, Shule ya Msingi Musira ina wanafunzi kasoro kumi tu wafike elfu moja, ina Walimu saba. Nina Shule ya Msingi Nakigando ina wanafunzi 840, ina Walimu sita, upungufu wa Walimu kumi na tano. Matokeo yake hawa watoto wanakaa pale, wanashinda wanacheza, hawafundishwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina shule za sekondari, shule nzima haina Mwalimu wa hesabu, shule nzima haina Mwalimu wa kemia. Sasa haya ni matatizo makubwa ambayo nafikiri yako ndani ya uwezo wa Wizara kuyafanyia kazi na kuyatatua angalau kwa kiasi cha kutosha watoto wasome, wapate elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za binafsi zimezungumziwa na Wabunge wengi hapa, Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, Mheshimiwa Tunza, Mheshimiwa Minza amesema, Wizara iache kuziona shule binafsi kama washindani wao. Mheshimiwa Rais ana lengo la kuboresha elimu, elimu iwe na ustawi mzuri, ufanisi uonekane kwenye elimu na shule binafsi zinatoa mchango mkubwa kwenye eneo hili, kwenye kuboresha elimu. Sasa Wizara ya Elimu na Wizara nyingine kama Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinaiona hii sekta kama ni washindani wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye sekta ya shule binafsi, naendesha shule binafsi na ni Mwalimu pia,

nilifundisha huko zamani, kwa hiyo, ninachokisema nakifahamu. Majuzi hapa, mwaka jana, Wizara ilifuta kupanga wanafunzi wa kwanza mpaka wa mwisho, wakafuta kupanga shule ya kwanza mpaka ya mwisho. Kuna Mheshimiwa Mbunge aliuliza swali hapa, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia akajibu vizuri sana, akajieleza vizuri sana watu wakapiga makofi, lakini ukweli uko pale pale, walifuta hiki kitu kwa sababu ya kuogopa shule binafsi, kwamba zinafaulisha zinawazidi, kwa hiyo, ili kuondoa hii noma ya kuwazidi basi angalau kufuta wote tuonekane tunalingana. Huo ndio ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawawezi kusoma bila usindani. Mtoto wa *primary* anasomaje? Hafahamu maana ya kusoma, lakini ile *pride* ya kujivunia kwamba, nimemzidi huyu, nimekuwa wa kwanza, nimekuwa wa kumi, nimewazidi thelathini, arobaini, inamwongezea motisha ya kusoma. Ukitoka mtihani amekuwa wa saba, amekuwa wa ishirini, amewazidi wenzake anaongeza motisha. Sasa wewe unafuta *ranking?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni vita kati ya shule za Serikali na shule za binafsi, hii sio sawa. Kwa kweli, kufuta *ranking* wanaua elimu na ukiua elimu unaua nchi. Mheshimiwa Waziri, Profesa ataingia kwenye rekodi, kwenye historia kwamba, aliua elimu ya Tanzania kwa kufanya hiki kitendo cha kufuta *ranking.* Ushindani ndio kila kitu, hata kwenye maisha huku mtu anataka ajenge nyumba nzuri, avae vizuri kumzidi mwingine na shuleni hivyohivyo, mtoto akifaulu vizuri kumzidi mwenzake anajisikia anaongeza kasi anasoma kila siku anaongeza bidii na nchi inapata ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, kuonesha mapambano yaliyopo kati ya shule za Serikali na za binafsi. Mwaka jana matokeo ya darasa la saba, shule zaidi ya ishirini na kidogo hivi zilifutiwa matokeo kwamba, zimeiba mitihani, zikafutiwa matokeo, zikatangazwa, zikafutiwa vituo vya

mitihani. Shule ya Serikali, Olympio, ilituhumiwa kwamba, imeiba mtihani, ikafutiwa matokeo. Haikutangazwa, haikufutiwa kituo, mpaka leo inaendelea na kituo chake. Sasa haya ni mambo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, za *private* zimetangazwa sana, zimeharibiwa sifa, zimeharibiwa jina, ya Serikali Olympio haikutangazwa, ikaonekana yenyewe haina matatizo, walirudia mtihani kama wengine wote walivyorudia, japo kimya kimya. Sasa haya mapambano ya namna hii kwa kweli, sio kujenga au kuboresha elimu bali ni kupambana na sekta ya binafsi ili kuiondolea uwezo wake na utendaji wake mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyaraka hizi ambazo amezisema Mheshimiwa Kikoyo, amezitaja kwa idadi, amefanya utafiti. Nafikiri baadhi ya nyaraka watoe, watu-*consult* au hawa wahusika na wadau wawashirikishe. Unaposema unafuta mabweni shule ya awali mpaka darasa la nne, hujawauliza wenye shule wanaoendesha, hujawauliza wazazi waliowapeleka kwa hiyari yao, unaboresha unaharibu au unabomoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo Waziri anayemfutia mabweni ameomba kibali kwake kwamba, naenda kujenga shule ya bweni ya awali mpaka darasa la nne. Anampa kibali kwa maandishi, anacho, amekopa pesa benki amenunua vitanda, amejenga majengo, ameweka magodoro, kesho anamfutia kibali, anamfutia bweni, afanyaje? Alipe vipi hilo deni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna njia nyingi za kuzuia ushoga. Kama ni ushoga, hakuna anayeupenda katika nchi hii, nina hakika, ziko njia nyingine nzuri za kuzuia ushoga, sio kufuta mabweni. Weka kamera, weka masharti magumu, idadi ya wanafunzi, toa mafunzo, watu wajifunze namna ya kuendesha shughuli hii bila kufuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule pale Bukoba mwenye shule Kaizirege yeye ni bweni tupu. Ukisema hakuna bweni ina maana shule imefungwa, imekufa hiyo, unataka kuua hizi shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi 18, naona nimepigiwa kengele, sitazisoma zote ningezitaja hapa. Kodi ya mapato, *VAT,* kodi ya ardhi, majengo, leseni, *WCF,* vibali vya wafanyakazi wa nje, kodi ya zimamoto, usalama kazini *OSHA, LATRA,* kodi ya ukaguzi, mitihani ya Taifa ina kodi, ada ya mitihani ya *mock* ya Wilaya, ya kata, ya nini, kuna michango kibao. Matangazo kodi, hata ukiandika kwenye basi lako ukaandika jina la shule unalipia, basi lako mwenyewe uandike jina la shule unalipia *TRA,* yaani mambo ya ajabu sana. Kodi ya *service levy,* sheria inazuia *service levy* kwenye shule wenyewe wanatoza *service levy,* UMISETA, UMITASHUMTA, usipotoa unakipata chamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutafsiri mitihani na yenyewe inalipiwa, tunalipia siku hizi. Kutafsiri kutoka Kiswahili uende Kiingereza sharti ulipie shilingi 8,500 kila mtihani, kila mwanafunzi, yaani hii ni kuumiza wazazi na lengo ni kuua shule. Kwa hiyo, nafikiri ili kutafuta ufumbuzi wa mambo haya, nimesoma taarifa ya Kamati, sio iliyosomwa hapa, ile ni *summary,* ile taarifa kubwa nimeisoma; imependekeza tuunde chombo huru cha kusimamia elimu, chombo huru, tuondoe suala la ukewenza. Huwezi kuwa na wake wanne, halafu uchague mmoja ndiye awe msimamizi wa wenzake. Serikali ina shule na binafsi wana shule, halafu Serikali ndio isimamie shule zote hizi, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ile *TCU* ya vyuo vikuu, Vyuo Vikuu vya Serikali kama Dar es Salaam, vya binafsi, viko chini ya *TCU* au *TCIA* ya ndege, *ATCL* za Serikali, *Precision Air,* ninii, ziko chini ya hiyo, basi na hii elimu iwe na

chombo cha kusimamia shule zote Tanzania ili tuweze kuwa na ufanisi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamisi Tabasam Mwagao, atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Londo.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia eneo hili nyeti sana kwa uchumi wa nchi yetu. Wahengwa wana msemo wao wanasema, kila shida huzaa fursa na kila fursa huzaa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, kila shida yoyote inayompata mtu, inayotokea hapa duniani huzaa fursa na kila fursa unayoipata inakuzalia shida. Sasa nchi yetu imepata fursa ya kuwa na binadamu, kuwa na watu wengi, hii ni fursa, kuna nchi hazina watu. Sasa fursa hii hivi tunavyozungumza inakwenda kutuzalia shida, tunaanza kuhangaika sasa tutafanyaje vijana wetu? Watapataje ajira? Watafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio tunakuja na mtaala mpya. Sasa huu mtaala unaouona huu mtaala ulioanzishwa sasa hivi unaokuja na ndugu yetu Mheshimiwa Profesa Mkenda, namheshimu sana, mtaala huu lazima Serikali ichukue tahadhari kubwa sana. Maneno haya nayasema, mimi ni mdau wa elimu, leo zaidi ya miaka 32. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili nataka niseme maneno mengine makubwa sana ya wanafalsafa wa elimu. Wanasema, kuna watu sita bora sana duniani, watu wote ni bora, lakini kundi la hawa watu sita ni bora sana duniani. Kundi la kwanza la heshima bora duniani ni wazazi wawili; Kundi la pili la heshima duniani ni viongozi wa dini au viongozi

wa kimila; Kundi la tatu la muhimu sana ni Walimu. Mtu anayeitwa Mwalimu ni kundi la tatu la watu wenye heshima duniani; Kundi la nne ni la watu wanaotoa haki, yaani Mahakimu na watu wengine wote wanaosimamia haki; Kundi la tano ni la Matabibu, Waganga, Madaktari; na Kundi la sita la watu muhimu ni watawala, kwa upande mwingine tunasema wanasiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya makundi sita wakikosa uadilifu dunia si mahali salama pa kuishi. Wazazi wasiposimamia nafasi yao kuwa wazazi, basi ni hatari kubwa sana, lakini viongozi wa dini wasipochukua nafasi yao ni hatari kubwa sana. Walimu wasipochukua nafasi yao ni hatari kubwa kote mpaka juu. Sasa leo tunakwenda kubadilisha mtaala na huu mtaala ni sehemu kubwa sana, nafikiri katika mitaala iliyobadilishwa huu unaweza ukawa ni mtaala wa saba au sita katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala wa kwanza ni wa Mjerumani ambao ulikuja kubadilishwa na Mwingereza mwaka 1914. Baada ya hapo tulikaa na mtaala wa Mwingereza mpaka mwaka 1967, zaidi ya miaka 53 na baada ya hapo mtaala ukabadilishwa na Baba wa Taifa mwaka 1967 mpaka mwaka 1977, huu ni mtaala wa tatu. Mtaala wa nne umebadilishwa mwaka 1977 mpaka mwaka 1984 akiwepo baba wa Taifa. Sasa tunakwenda katika mtaala wa tano ambao aliubadilisha Mzee Mwinyi mwaka 1997, baada ya hapo Rais wetu Benjamin Mkapa, marehemu, alibadilisha mtaala ambao umekuja kubadilishwa mwaka 2008. Sasa tumekuja 2014 ukabadilika mtaala, huu tunakwenda mtaala wa saba, tuwe na tahadhari kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeyasema haya? Ni kwamba, wanazuoni waone, wapime, kwamba, tokea mwaka 1905 mpaka 1914, waone Mjerumani alifundishaje, Mwingereza naye hivyohivyo mpaka 67, baada ya hapo sisi

ule mtaala tumekuja kuupokea. Tuwaangalie Waingereza ule mtaala ambao walituletea sisi tukaubadilisha mwaka 1967, je, wameshabadilisha mtaala mara ngapi? Hii ndio tahadhari yangu kubwa. Tusije tukawa abunuwasi, tukawa tuko juu ya mti, tunakata chini tuanguke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani nasema hivyo? Haya masomo ambayo ni ya amali yanayokuja kufundishwa sasa hivi ni kwamba, lazima tuwe tuna tahadhari, tusome masomo yetu. Tuangalie mtaala uliopita na mtaala huu, tusome kuanzia saa moja na nusu mpaka saa nane. Baada ya saa nane tuwe na masomo mengine matatu au mawili kwa masaa haya mawili au matatu, elimu yetu sasa hii ya amali ifundishwe. Vinginevyo tutakataa haya masomo mengine tuje tufute haya masomo, tutakuja kuingia kwenye hatari kubwa sana. Sasa lazima tuchukue tahadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nayasema mimi kama Tabasam lakini natoa ushauri kwa wasomi wetu, hii Mheshimiwa Profesa Mkenda, nakuomba tu, pamoja na kwamba nimeuptia mtaala wako vizuri kabisa kwa heshima, kwa sababu ni lazima tuandae vyuo vya elimu, kwamba tutakuwa tuna vyuo vya elimu kumi vitakavyokwenda kuwafundisha walimu elimu ya amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa na shule ambazo watoto hawa wakitoka wanakwenda kufundishwa walimu kule kwenye zile shule za sekondari wapo pia vyuo vyetu vya ufundi katika kuendelea wapo na utoaji wetu wa *certificate,* tunakwenda na mitaala hii lakini mtu akimaliza *form four* basi apewe *certificate* hata kama hakufaulu lakini ni mjuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi nakupa sasa hivi elimu iliyoko mtaani, kuna mafundi baiskeli, unaileta baiskeli kwenye boksi anakuja anaiunda yule mtu, anaifunga anaiunganisha, hana *certificate,* na huyu mtu hatambuliki kwa sababu hana cheti. Kuna mafundi pikipiki hivyohivyo,

wanakwenda kutengeneza pikipiki, anaiunda inakuwepo lakini hana cheti. Sasa je, Serikali inakwendaje kuwatambua hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamwona Profesa kabisa kama Mheshimiwa Prof. Mkenda anapeleka gari lake mtaani na anayekwenda kulifanyia kazi hana cheti, Profesa Mkenda yuko pale anasubiri, anamwona fundi anamwaga *oil,* anabadilisha tairi, anafanya nini. Je, hawa umewaweka katika upande gani unawapa vyeti lini? Kuna mafundi wanakujengea nyumba wewe mwenyewe, Mheshimiwa Profesa Mkenda na ukenda pale mainjinia wako wanasema hii nyumba iko sawa. Je, huyu naye cheti chake atapata lini? Lazima tuangalie haya makundi yote tumejipangaje kwenda kuwapa vyeti hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wafugaji. Hawa Maprofesa na Madaktari wote mnaowaona wanakwenda kufanya *research* kwa wafugaji, mtu amefuga ng'ombe ana miaka 30, mtu amelima mtama au mpunga ana miaka 30, anayekuja kufanya *research* pale anakuja kumuuliza Mzee hii mbegu yako inatoa magunia mangapi, gunia 30, ukifanya hivi inakuaje, ukiacha maji yanakuwa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mtu akitoka pale anakwenda *SUA* kupata *degree,* lakini amekwenda kumuuliza mkulima wa darasa la pili, ndiyo anajua kabisa kwamba ukipanda mbegu ya karanga ambayo inazaa tatu, itatoa watoto watatu, ukipanda karanga inatoa mbegu mbili utatoa karanga mbili. Haya anayajua Bibi yangu hakwenda hata shule, hana *degree,* sijui unaniulewa vizuri, lakini anayekwenda kufanya *research* mnakuja kumpa *degree.* Sasa lazima muangalie hivi vitu. Tunakwenda katika mitaala tusije tukaacha ya kwetu tukaenda kubeba kila kitu kipya. Sisi tuko vizuri unatuona hapa akina Tabasam, tumesoma mtaala huu unaouona, ulibadilishwa mwaka 1967 tukaenda nao mpaka mwaka 1984 ukaja kubadilishwa, siwezi kulinganishwa

na mtoto sasa hivi unayempeleka akapata *degree SUA*. Atanishinda kuongea Kiingereza tu lakini mambo mengine yote tukiyatunga Kiswahili hanipati ng'oo. Haya nakueleza hapa hapa tu, leteni *paper* tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lugha inayotakiwa kufundishwa ni ile ya kumfanya mtu aelewe, nieleweni vizuri. Kwa sababu utamtoa mtoto huku anasoma Kiswahili halafu ukija ukambadilisha baadae huyu mtoto anakwenda kufeli kwa sababu tu ya kushindwa kujua Lugha ya Kiingereza. Lugha ya Kiingereza itolewe maksi zake na lugha nyingine itolewe maksi zake vilevile kwa sababu yule mtoto ukimfundisha kwa Kiswahili anafaulu ule mtihani, halafu somo la Kiingereza aje alisome ni la muhimu sana kusomeshwa na lenyewe lipate cheti chake, lakini habari ya kutuambia kuitengeneza meza na kupiga msumari mtu aje afanye mtihani wa kiingereza, kutengeneza gari halafu mnasema kwamba amefeli, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabsam, muda wako umeisha naomba umalizie mchango wako.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongeze kidogo tu nimalizie.

**MWENYEKITI:** Haya, sekunde 30 malizia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni suala la usajili wa shule. Suala hili limekwenda kwa Mheshimiwa Prof. Mkenda anajua, mmekuwa mnazifungia hata sekondari zenu za Serikali. Mara hazina kichomea taka, ulipeleka bajeti hiyo? Unazuia

kichomea taka unashindwa kusajili shule, watoto wanakaa 800 darasani. Shule ya Msingi ina watoto mpaka 300. Kuna shule nyingine iko pembeni wamejenga wananchi unaiita shule shikizi unashindwa kuipa usajili. Haya maneno inakuaje upande wa ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani ninyi wenyewe shule ni za kwenu bado mnaziwekea masharti makubwa wakati hamjapeleka bajeti? Hii nchi tunakwenda wapi? Tumsaidie Mama Samia Suluhu Hassan, kule mmeweka Polisi kwenye sehemu ya elimu hata kwenye shule zenu, tukabeni kwenye shule binafsi hivyo lakini siyo shule za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam. Mheshimiwa Dennis Londo ndiye mchangiaji wetu wa mwisho jioni hii.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi pia kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu. Naomba niungane na Wabunge waliotangulia kuchangia kuishukuru Serikali, hasa katika sekta ya elimu. Kuna maboresho makubwa ambayo yamefanyika katika sekta ya elimu na ninaomba nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali ya Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mikumi kuna mambo mengi katika sekta ya elimu, ujenzi wa shule mpya za sekondari, ujenzi wa shule mpya za msingi, kupunguza umbali wa watoto kutoka shuleni mpaka nyumbani au nyumbani kwenda shuleni na kuongeza kiwango cha ufaulu ni maeneo ambayo hayawezi kupita bila kutoa kauli ya pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, naomba nitoe pongezi kwa Serikali kuona umuhimu wa kuboresha

mitaala yetu ni suala ambalo limekuja katika muda muafaka. Ni matumaini yetu kwamba maboresho haya yamekuja kwa sababu ya mapungufu ambayo tumekuwa tukiyashuhudia huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba elimu yetu kimsingi ilikuwa na changamoto nyingi, nyingine zimefanyiwa kazi na nyingine tunaendelea kuzifanyia kazi, lakini bado tunaweza tukakiri kwamba ilishindwa kukidhi matarajio ya wengi kwa sababu ilikuwa imejikita kumjenga kijana wetu kitaaluma zaidi kuliko kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida hii imesababisha vijana wetu wengi kushindwa kukabiliana na mazingira yao, kushindwa kupambana na mazingira yao, kukosa ajira na kukosa ubunifu wa kuwa sehemu ya majibu ya changamoto ambazo zinawakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumaini yangu kwamba mtaala mpya wa Serikali unaenda kujibu changamoto ambazo tumezipitia. Pamoja na hayo, unakwenda kuongeza kasi na umuhimu wa kumtengeneza kijana wa Kitanzania kimaadili na kuwa na hamu ya kutimiza wajibu wake kwa Taifa lake pamoja na ari ya kujituma kupitia mitaala yetu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba mtaala huu mpya unakwenda kuongeza kasi ya Watanzania kupambana kupata ujuzi, maarifa na weledi, mtaala huu unakwenda kujibu changamoto ya mahitaji ya soko la ajira ndani ya Tanzania na soko la kazi katika ulimwengu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba mtaala huu mpya unakwenda kuupunguza umri wa kuanza shule toka miaka saba mpaka sita, lakini tuna mifano huko duniani, kwa mfano nchi kama Finland ambayo imeongoza katika ubora wa elimu, hasa ya msingi na sekondari, mataifa yote

ambayo yameendelea yanakwenda kujifunza Finland, kwa sababu Finland ndiyo nchi pekee katika nchi ambazo zimeendelea mtoto anaingia darasa la kwanza akiwa na miaka saba wakati wengine anakwenda akiwa na miaka mitano mpaka sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini sisi badala ya kuona kwamba hawa wenzetu wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kujenga ari ya mtoto kupenda masomo na kumudu masomo yake akiingia darasa la kwanza akiwa na miaka saba. Kwa nini sisi tumeenda kushusha miaka sita, nini ambacho tunakitarajia kutoka kwa huyu mtoto ambaye tunampeleka shule akiwa na miaka sita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tunafahamu kuna maboresho mengi huko nyuma yamepita. Mengine yamefanikiwa kwa kiasi, mengine yalishindwa. Ukiangalia kwa nini yalishindwa, kwa sababu maboresho mengi yalijikita kwenye kubalisha elimu, mitaala na masomo lakini hayakuweka mkazo kwenye kumuandaa Mwalimu ambaye anakwenda kumudu *skills* za kufundisha watoto ambao tunataka waende kujifunza hayo masomo. Nina wasiwasi hata kwenye huu mtaala mpya hakuna msisitizo wa maandalizi ya Mwalimu ambaye anaenda kuwafundisha watoto wetu katika mtaala mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutawekeza kwa Walimu siyo rahisi kupata matarajio ambayo tunayatarajia. Vyuo vyetu vya ualimu tumeviandaa vipi kukabiliana na mabadiliko ya sera na mtaala, walimu wetu tumewaandaa vipi kukabiliana na haya yote ambayo tunayaita mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini maandalizi mazuri kwa walimu wetu yatatuletea matokeo mazuri, tusipowaandaa walimu wetu kulingana na mahitaji yetu hata kama tutafanya

mabadiliko makubwa ya mtaala wetu, siyo rahisi kupata kile ambacho tunakitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia uhaba wa walimu, lakini huko miaka ya sabini na themanini, masomo mengi yalikuwa yanafundishwa kupitia redio, sasa hivi tuna televisheni, tuna vishkwambi, tuna *YouTube, WhatsApp,* kuna *initiative* gani ambayo inafanyika kuhakikisha kwamba maeneo ambayo yanakosa walimu watoto wanatumia *technology* kupata elimu yote kwa mujibu wa *curriculum* ambayo tumejiwekea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya teknolojia hatuwezi kuyaepuka na yanaweza yakatusaidia siyo tu kufikia wanafunzi ambao wamekosa walimu, lakini yanaweza kutusaidia kupambana na tatizo la uhaba wa walimu hasa katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamesisitizia sana lugha, nami naomba nisisitizie tena suala la lugha, lakini lugha ambazo nasisitiza ni muhimu siyo tu Kiingereza, sasa hivi dunia inakiangalia Kichina, Kifaransa na Kiarabu. Hizi lugha zote ni nzuri kwa mawasiliano kwa ajili ya kufikia watu ambao tunaweza kufanya nao kazi, tukafanya nao biashara, tukaingiliana nao kwa maendeleo ya uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wakati tunatoa kipaumbele kwenye lugha hizi nyingine za mawasiliano ni vizuri tukaangalia kwa mapana yake wapi tunataka kwenda na tunawafikiaje watu katika dunia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia mustakabali wa Taifa letu. Juzi hapa tulikuwa na Sensa Kitaifa, zoezi la sensa lilikuwa kubwa sana. Ninapenda kujua wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha ni Watanzania wangapi ambao hawajui kusoma na kuandika. Tuna mpango gani wa kuwafikia Watanzania hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokujua kusoma na kuandika ni mzigo mkubwa sana katika kizazi hiki na katika jamii tunayoishi. Hasa ukizingatia kwamba takwimu zinaonesha kuna watoto zaidi ya 55,000 ni *drop outs* kutoka shule, lakini tunajua kwamba kuna watoto wengi zaidi ambao wako nje ya mfumo wa shule. Hawa hatuna uhakika kama watajua kusoma na kuandika kesho, na ni jeshi kubwa sana. Tunajiandaaje na kuangalia jinsi gani watoto hawa ambao hawajui kusoma na kuandika wanaingizwa katika mifumo na hii mitaala mipya inakwenda kutumika kama *tool* ya kufikia hawa watoto ili tusiwaache nyuma wakati Taifa linaenda mbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja; ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mwongozo Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Kitila.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Nimesimama kwa Kanuni ya 76, sambamba na Kanuni ya 69(c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema leo asubuhi wakati nawasilisha taarifa ya Kamati yetu, ikiwa dakika ya 15, Kiti kilinizuia kusoma na kutoa shukrani na pongezi kwa Wajumbe wa Kamati ambao walifanya kazi hii. Nami katika wasilisho langu nilikuwa nimefanya bajeti ya muda kwamba ndani ya dakika 30 ambazo zimetolewa kikanuni, ningekamilisha taarifa yangu ikiwemo kuwapongeza Wajumbe wa Kamati yangu kwa kuwasoma majina mmoja baada ya mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, tatizo ni nini? Kama wenzetu upande wa Serikali wanaweza kuwashukuru watu wote ambao wanadhani wamechangia katika kufika hapo walipo, sisi kama Wenyeviti wa Kamati kuna ubaya gani kuwashukuru Wajumbe kwa kumtaja mmoja baada ya mwingine ikiwa ndani ya muda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninataka kupata mwongozo wako kama jambo hili linaruhusiwa au la, kama utaona kwamba haikuwa sahihi, basi nipewe dakika zangu ili niweze kuwasoma na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa Kanuni yetu ya 76, ametupeleka pia Kanuni ya 69(c) akiomba Mwongozo kama jambo lililotokea asubuhi hii ya leo linaruhusiwa au haliruhusiwi.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wangu ni kwamba jambo hili lilishatolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Spika huko nyuma, kwa hiyo ndiyo utaratibu uliopo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana kwa mliopata fursa jioni hii na tunaamini Serikali imepata mapendekezo, maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tunaamini mtayafanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.15 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 17 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*